# Lagano da Sambi kwa Wanhu Wose

The New Testament in Kutu, 2014

# Lagano da Sambi kwa Wanhu Wose
## The New Testament in Kutu, 2014

copyright © 2014 Pioneer Bible Translators and The Word for the World

Language: (Kutu)

Contributor: Pioneer Bible Translators

# The New Testament in Kutu

This translation, published by Pioneer Bible Translators and The Word for the World, was published in 2014.

If you are interested in obtaining a printed copy, please contact www.pioneerbible.org.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-06

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 6 May 2025 from source files dated 6 May 2025
d1e1c737-3fba-57bf-b568-24ce20fef5c5

Contents

Matayo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1
Maluko . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 57
Luka . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 92
Yohana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .151
Sang'hano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .193
Walumi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .246
1 Wakolinto . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .270
2 Wakolinto . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .293
Wagalatia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .308
Waefeso . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .317
Wafilipi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .326
Wakolosai . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .332
1 Wasesalonike . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .338
2 Wasesalonike . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .344
1 Timoseo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .347
2 Timoseo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .354
Tito . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .359
Filimoni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .362
Waebulania . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .364
Yakobo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .382
1 Petulo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .388
2 Petulo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .395
1 Yohana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .399
2 Yohana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .406
3 Yohana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .408
Yuda . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .410
Ugubulo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .413

# Mbuli Inogile ya Yesu Kilisito yandikigwe na Matayo

## Ulongozi

Mbuli Inogile yandikigwe na Matayo ya mumkumbo wa vitabu vine va lagano da sambi, vitabu avo volagusa vija Yesu viyakalile hano mwiisi. Kila kitabu acho chokemigwa, “Injili,” fambulo jake Mbuli Inogile. Vitabu avo vandikigwa ako kumwande na Matayo na Maluko na Luka na Yohana toka Yesu viyafile na kuzilibuka. Wanhu woifunza mbuli hawadijuwile siku diyandikigwe Mbuli Inogile yandikigwe na Matayo, lakini yogesigwa ikala behi na mwaka 60 toka kuvumbuka kwa Kilisito. Vivija ako kuyandikiligwe hakujuwike bule, lakini wanhu wayagwe wogesa yandikiligwa mwiisi ya Palesitina hebu sengine kudibuga da Yelusalemu.

Mwandikaji kakala Matayo yakalile mbokela kodi yang'hali hanakuwa mwanahina wa Yesu. Vivija twaga jake diyagwe dikala Levi. Matayo kakala imoja wa iwatumigwa longo na wabili. Matayo kawandikila Wayahudi, mbuli ino yojuwika kwa vilaguso kubanza 60 vilongigwe mna gamaandiko gang'alile ga lagano da umwaka. Matayo kalonda kulagusa kamba Yesu kakala Kilisito Mkombola, Mulungu kamsagula yawe Mkombola yalaguligwe mbuli zake. Vivija Matayo kandika mbuli nyingi za Undewa wa Mulungu. Wayahudi wagesa Kilisito Mkombola kokuwa Mndewa wa mwiisi ino. Matayo kakulema kutamanila kwao kwa kuwasimulila mbuli za kiloho za Undewa wa Mulungu.

Mbuli Inogile yandikigwe na Matayo acho kitabu kinogile kwa kusongela lagano da sambi, kwavija kina vilaguso vose vilongigwe mna idilagano da umwaka. Kitabu kino cholumbiliza malagano mabili. Wanhu woifunza mbuli, vivija wogesa sengine Matayo kageza kwiga ivitabu vitano vandikigwe na Musa. Vitabu avo, avo vitabu vaichanduso va lagano da umwaka. Yesu viyawapetele wanhu kulugongo (Luka 5-7) yodaha kuigala na Mulungu viyamgwelele Musa malagizo. (Kumbukumbu da Malagizo 19:3-23:33).

**Mbuli zili mkitabu**

Matayo kosonga kwandika Mbuli Inogile kwa kusimulila kuvumbuka kwa Yesu Kilisito na viyasongile sang'hano yake (Sula ya 1-4).

Abaho Matayo kosimulila sang'hano ya Yesu na mafundizo gake mengi (Sula ya 5-25).

Mbuli za kimambukizo za Mbuli Inogile yandikigwe na Matayo zizo zija za sang'hano ng'hulu ya Yesu nayo ayo ifa yake na kuzilibuka kwake (Sula ya 26-28).

*Lukolo lwa Yesu Kilisito*
*Luk 3:23-38*

1 Kitabu cha lukolo lwa Yesu Kilisito mzukulu wa Daudi, mzukulu wa Abulahamu.

2 Abulahamu kamulela Isaka, Isaka kamulela Yakobo, Yakobo kamulela Yuda na ndugu zake.

3 Yuda kamulela Pelesi na Zela, mamao kakala Tamali, Pelesi kamulela Heziloni, Heziloni kamulela Alamu.

4 Alamu kamulela Aminadabu, Aminadabu kamulela Nashoni, Nashoni kamulela Salimoni,

5 Salimoni kamulela Boazi, mamake Boazi kakala Lahabu, Boazi kamulela
Obedi, mamake Obedi kakala Lusi, Obedi kamulela Yese,
6 Yese kamulela Mndewa Daudi.
Daudi kamulela Sulemani, mamake Sulemani kakala mwehe wa Ulia.
7 Sulemani kamulela Lehoboamu, Lehoboamu kamulela Abiya, Abiya
kamulela Asa,
8 Asa kamulela Yehoshafati, Yehoshafati kamulela Yolamu, Yolamu ka-
mulela Uzia,
9 Uzia kamulela Yotamu, Yotamu kamulela Ahazi, Ahazi kamulela
Hezekia,
10 Hezekia kamulela Manase, Manase kamulela Amoni, Amoni kamulela
Yosia,
11 Yosia kamulela Yekonia na ndugu zake, kipindi kija Wayahudi viwa-
hamizigwe kugaligwa Babeli.
12 Viubitile uhamizo wa Babeli, Yekonia kamulela Shealitieli, Shealitieli
kamulela Zelubabeli,
13 Zelubabeli kamulela Abiudi, Abiudi kamulela Eliakimu, Eliakimu ka-
mulela Azoli,
14 Azoli kamulela Sadoki, Sadoki kamulela Akimu, Akimu kamulela Eliudi,
15 Eliudi kamulela Eliazali, Eliazali kamulela Matani, Matani kamulela
Yakobo,
16 Yakobo kamulela Yusufu, mbigalo wake Malia, yamulelile Yesu
yokemigwa Kilisito.
17 Avo kukala na ng'holo longo na nne kulawa Abulahamu mbaka Daudi,
na ng'holo longo na nne kulawa Daudi mbaka Wayahudi viwahamizigwe
Babeli na ng'holo longo na nne toka viwahamizigwe Babeli mbaka kuleleka
kwa Kilisito Mkombola.

### *Kuvumbuka kwa Yesu Kilisito*
*Luk 2:1-7*

18 Kuvumbuka kwa Yesu Kilisito kukala vino, Malia yafungiligwe zengele
na Yusufu, lakini wang'hali hawanakala hamoja kamba mbigalo na mt-
wanzi, Malia koneka kana inda kwa udahi wa Loho Yang'alile.
19 Kwavija Yusufu kakala munhu yotenda ganogile, halondile kumgela
kinyala Malia, avo kalonda kumuleka kinyelegezi.
20 Viyakalile kogelegeza vivo, msenga wa kuulanga wa Mndewa kamu-
lawilila mzinzozi na kamulongela, “Yusufu mzukulu wa Daudi, sekeudumbe
kumsola Malia yawe mwehe wako, kwavija inda yake kaipata kwa udahi wa
Loho Yang'alile.
21 Kolela mwana wa kimbigalo na gweye komgwaa twaga da Yesu, kwavija
kowakombola wanhu zake mzinzambi zao.”
22 Gano gose gatendeka kutenda galongigwe na Mndewa kubitila mtula
ndagu wake galawilile,
23 “Mhambe kogoga inda, na kolela mwana wa kimbigalo, nao womkema
Imanueli,” fambulo jake, “Mulungu kahamoja na tweye.”
24 Avo Yusufu viyalamuke muutulo, kamsola Malia kamba viyalongeligwe
na imsenga wa Mndewa.
25 Lakini hatembele nayo mbaka viyalelile mwana na Yusufu kamgwaa
twaga mwana ayo Yesu.

## 2

### *Wageni walawile mwambu wa kudilawila zuwa*

1 Yesu kavumbuka kudibuga da Beselehemu mwiisi ya Yudea, kipindi Helode viyakalile Mndewa. Aho viyavumbuke wanhu wayagwe wajuwile mbuli za nhondo weza kulawa mwambu wa kudilawila zuwa wavika Yelusalemu.
2 Wauza, “Kakwahi imwana yavumbuke yawe Mndewa wa Wayahudi? Kwavija tuyona nhondo yake kulawa mwambu wa kudilawila zuwa na tweye twiza kumfugamila.”
3 Mndewa Helode viyahulike vivo kanyawanyawa ng'hani na vivija kila munhu yakalile Yelusalemu kanyawanyawa.
4 Kawakema hamoja wakulu wa walava nhosa na wafundiza Malagizo ga Musa kawauza, “Vino Kilisito Mkombola kovumbukila kwahi?”
5 Wamwidika, “Kovumbukila kudibuga da Beselehemu mwiisi ya Yudea, vivo yandike mtula ndagu wa Mulungu,
6 ‘Mweye wanhu wa Beselehemu mwiisi ya Yudea,
buga jenu hadili dodo bule mna gamabuga ga Yuda,
kwavija kumwenu kolawa mulangulizi
yonda yawalongoze wanhu zangu wa Izilaeli.’ ”
7 Avo Helode kawakema kinyelegezi wanhu waja wojuwa mbuli za nhondo kawauza kipindi gani nhondo viyoneke.
8 Abaho kawatuma wachole Beselehemu na kuwalagiza, “Choleni mkazahile goya kuyali imwana, mwahamona nongeleni, nanie vivija nichole nikamfugamile.”
9 Viwamalile kumtegeleza, walawanya, mnzila wayona nhondo iija iwayone mwambu wa kudilawila zuwa, iwalongolela na kwima hanhu aho kuyavumbuke imwana.
10 Viwayone inhondo, wadeng'helela ng'hani.
11 Avo wengila mng'anda, wamona imwana na Malia mamake, wamfugamila na kumtambikila. Abaho wamgwaa nhunza za zahabu, mavumba na mavuta ga bei ng'hulu gokemigwa manemane.
12 Abaho wabwela ukayao kwa kubitila nzila iyagwe, kwavija Mulungu kawazuma mzinzozi sekewabwele kwa Helode.

### *Kukimbililа Misili*

13 Viwasegele msenga wa Mndewa kamulawilila Yusufu mzinzozi kamulongela, “Helode komzahila imwana yamkome. Avo lamuka umsole imwana na mamake mkimbilile Misili, na mukale kuko mbaka vonda nikulongele usegele.”
14 Yusufu kalamuka, kamsola imwana na mamake kasegela ikilo acho na kuchola Misili,
15 kakala ako mbaka Helode viyafile. Gano gatendigwa kutenda acho kiyalongile Mndewa kubitila mtula ndagu kilawilile, “Nimkema mwanangu kulawa Misili.”

### *Kukomigwa kwa wana*

16 Helode viyajuwile kamba wanhu wacholile kumulola Yesu kulawa mwambu wa kudilawila zuwa wamvizila, kagevuzika ng'hani. Kalava lagizo da kuwakoma wana wose wa kimbigalo weli Beselehemu na hiwo weli behi, kusongela wana ving'hele mbaka wana weli na miyaka mibili ino itendigwa kamba viyajuwile kulawa kwa wanhu wacholile kumulola Yesu mna ikipindi viwayone inhondo.
17 Kwa mbuli ino kilawilila kija kiyalongile Yelemia yakalile mtula ndagu wa Mulungu,
18 “Sauti ihulikigwa mwiisi ya Lama,
kulila na kuiyalala ng'hani.

Laheli kowalilila wanage
nayo kolema kuhozigwa,
kwavija wafa."

*Kusegela Misili*

19 Helode viyafile, msenga wa Mndewa kamulawilila Yusufu mzinzozi
mwiisi ya Misili,
20 kamulongela, "Lamuka umsole imwana na mamake, na ubweleganye
mna iisi ya Izilaeli, kwavija wose walondile kumkoma imwana wafa."
21 Avo Yusufu kalamuka, kamsola imwana na mamake na kabweleganya
mwiisi ya Izilaeli.
22 Lakini Yusufu viyahulike Alikelao mwanage Helode, kahala Undewa
wa tatake ako Yudea, kadumba kuchola kuko, kwavija kazumigwa ng'hani
mzinzozi. Avo kachola mwiisi ya Galilaya.
23 Kahamila kudibuga da Nazaleti keka ukazi wake kuko. Avo kilawilile
kija kiwalongile watula ndagu wa Mulungu, "Kokemigwa Mnazaleti."

# 3

*Yohana Mbatizaji kowapetela wanhu*
*Mlk 1:1-8; Luk 3:1-18; Yoh 1:19-28*

1 Mna izisiku azo Yohana Mbatizaji keza kuluwala lwa Yudea, kasonga
kuwapetela wanhu.
2 Kawalongela, "Lekeni nzambi zenu kwavija Undewa wa kuulanga
wammabehi!"
3 Ayo Yohana, ayo munhu yalongigwe na mtula ndagu wa Mulungu Isaya,
"Munhu imoja kokema kuluwala,
'Itandeni nzila ya Mndewa,
goloseni nzila yake yonda yabite!' "
4 Kiwalo cha Yohana kitendigwa kwa mibahila ya ngamiya, na kavala
mkwiji wa ng'hwembe mkigudi chake. Lujo lwake lukala nzige na uki.
5 Wanhu wamcholela kulawa Yelusalemu, na isi yose ya Yudea na kulawa
isi zose zilihabehi na lwanda lwa Yolidani.
6 Watogola hewo watenda nzambi na Yohana kawabatiza muulwanda lwa
Yolidani.
7 Yohana viyawone Mafalisayo na Masadukayo wengi womwizila yawa-
batize, kawalongela, "Mweye mizoka nani yawalongele modaha kuikimbila
nhaguso yonda igaligwe na Mulungu?
8 Musang'hane gaja gonda galaguse muzileka nzambi zenu.
9 Sekemugese kwa kulonga kamba Abulahamu heyo muhenga wetu.
Nowalongela Mulungu kodaha kugasola mabwe gano na kugatenda lukolo
lwa Abulahamu!
10 Shoka ikigwa goya kukanha mibiki mna gamasina. Kila mbiki uleka
kulela matunda ganogile wokanhigwa na kwasigwa muumoto.
11 Niye nowabatiza mweye kwa mazi kulagusa muzileka nzambi zenu.
Lakini yonda yeze kukisogo changu kowabatiza kwa Loho Yang'alile na kwa
moto, heyo ni munhu mkulu kubanza nene, niye sifaya hata kupapa vilatu
vake.
12 Ayo kana lungo lwa kubetela uhule mmakono gake. Nayo kousola
uhemba wake na kuwika kudikanho, lakini koisoma imikumvi muumoto
haufaga."

*Kubatizigwa kwa Yesu*
*Mlk 1:9-11; Luk 3:21-22*

13 Mna izisiku azo Yesu kasegela kulawa Galilaya kachola kuna ulwanda lwa Yolidani yakabatizigwe na Yohana.
14 Lakini Yohana kalonda kumgomesa Yesu, kalonga, “Niye nolondeka nibatizigwe na gweye, habali wiza kumwangu?”
15 Yesu kamwidika, “Leka sambi iwe vivo kwavija kwakutenda vivo togatenda gaja gose golondigwa na Mulungu.” Avo Yohana katogola.
16 Bahaja Yesu viyabatizigwe, kalawa mgamazi, ulanga ugubuka, na kamona Loho wa Mulungu kohumuluka kamba huwa na kakala uchanha yake.
17 Abaho sauti ihulikigwa kulawa kuulanga ilonga, “Ino heyo mwanangu nimnogele, ninogezigwa nayo.”

# 4

*Kugezigwa kwa Yesu*
*Mlk 1:12-13; Luk 4:1-13*

1 Abaho Loho Yang'alile kamulongoza Yesu yachole kuluwala yakagezigwe na Mwenembago.
2 Kakala kuko siku malongo mane imisi na ikilo bila kuja. Viyamambukize siku azo, Yesu kona nzala.
3 Abaho Mwenembago kamcholela kamulongela, “Kamba gweye kwa Mwana wa Mulungu kweli galagize mabwe gano gagaluke magate.”
4 Lakini Yesu kamwidika, “Maandiko Gang'alile golonga, ‘Munhu hawa mgima kwa kuja kwiiyeka, lakini kwa kila mbuli yoolonga Mulungu.’ ”
5 Abaho Mwenembago kamsola Yesu mbaka Yelusalemu buga ding'alile, kamwika mna ikiswili cha Ing'anda ya Mulungu.
6 Abaho kamulongela Yesu, “Kamba kweli gweye kwa Mwana wa Mulungu, ilagaze mwenyego hasi, kwavija Maandiko Gang'alile golonga,
‘Mulungu kowalagiza wasenga zake wa kuulanga mbuli ya gweye,
nao wokusola mmakono gao,
sekeuilumize magulu gako mgamabwe.’ ”
7 Yesu kamwidika, “Vivija Maandiko Gang'alile golonga, ‘Sekeumgeze Mndewa Mulungu wako.’ ”
8 Abaho Mwenembago kamsola Yesu mbaka uchanha ng'hani kuna ulugongo lutali na kamulagusila undewa wa mwiisi yose na unovu wake.
9 Mwenembago kamulongela, “Vino vose nokugwaa, kamba wahanifugamila na kunitambikila.”
10 Yesu kamulongela, “Segela kumwangu Mwenembago! Kwavija Maandiko Gang'alile golonga, ‘Mtambikile Mndewa Mulungu wako, na umsang'hanile heyo yaiyeka!’ ”
11 Baho Mwenembago kamuleka Yesu, na wasenga wa kuulanga weza wamsang'hanila.

*Yesu kosonga sang'hano yake ako Galilaya*
*Mlk 1:14-15; Luk 4:14-15*

12 Yesu viyahulike Yohana Mbatizaji kagodekigwa kukifungo, kachola isi ya Galilaya.
13 Hakalile Nazaleti lakini kachola kukala Kapelinaumu kudibuga dili behi na lamba da Galilaya, kuzimbaka za isi ya Zabuloni na Nafutali.
14 Mbuli ino ilawilila kamba vija viyalongile mtula ndagu wa Mulungu Isaya,
15 “Isi ya Zabuloni na isi ya Nafutali
nzila ya kucholela mbahali, umwambu uyagwe wa lwanda lwa Yolidani

Galilaya, isi ya wanhu haweli Wayahudi!
16 Wanhu wakalile mdiziza
wawona mulenge wa ukombozi wa Mulungu
Waja wose wokala mwiisi ya sisila da ifa
mulenge uwamwemwesela."
17 Kulawa kipindi acho Yesu kasonga kuwapetela usenga wake, "Lekeni
nzambi zenu, kwavija Undewa wa kuulanga wammabehi."

### *Yesu kowakema walowa somba wane*
### *Mlk 1:16-20; Luk 5:1-11*

18 Yesu viyakalile kobita kumgwazo wa lamba da Galilaya, kawavika
munhu na mkulu wake wovuwa somba. Wakala Simoni yakemigwe Petulo
na mdodo wake Andeleya, wakala wovuwa somba mna dilamba na mizavu
yao.
19 Yesu kawalongela, "Nikwelelezeni na niye nowatenda muwe wavuwaji
wa wanhu."
20 Bahaja waileka mizavu yao, wamkweleleza.
21 Kagenda kumwande kawavika wandugu wabili wayagwe. Yakobo na
Yohana wanage Zebedayo. Wakala mwiingalawa hamoja na tatao Zebedayo
woitanda mizavu yao. Yesu kawakema,
22 bahaja waileka ngalawa na tatao, na wamkweleleza Yesu.

### *Yesu kowapetela wanhu na kuwahonya*
### *Luk 6:17-19*

23 Yesu kachola mwiisi yose ya Galilaya, kafundiza mzing'anda za
kumpula Mulungu na kawapetela wanhu Mbuli Inogile ya Undewa wa
Mulungu na baho kawahonya wanhu wakalile na mitamu na magayo gose.
24 Mbuli zake zenela mwiisi yose ya Siliya, avo wanhu wamgalila
wanhu wose wakalile watamu, waja wodununzika na kila utamu, weli na
vinyamkela, na visango na waja waholole na Yesu kawahonya wose.
25 Wanhu wengi wamkweleleza Yesu kulawa Galilaya na Dekapoli,* ku-
lawa Yelusalemu na Yudea na isi ya mwambu uyagwe wa lwanda lwa
Yolidani.

# 5

### *Yesu kowapetela wanhu kulugongo*

1 Yesu viyaluwone lunhu lwa wanhu, kakwela kulugongo, kakala hasi.
Wanahina zake wamcholela,
2 nayo kasonga kuwafundiza.

### *Deng'ho da kweli*
### *Luk 6:20-23*

3 "Wamweda wanhu waja womtamanila Mulungu yaiyeka,
kwavija Undewa wa kuulanga uli wao!
4 Wamweda wanhu waja wonyunyuwala,
kwavija Mulungu kowahoza!
5 Wamweda wanhu waja weli wahole,
kwavija Mulungu kowagwaa isi yose.
6 Wamweda wanhu waja weli na nzala na ng'hilu ya kutenda gaja goyolonda
Mulungu,
kwavija Mulungu kowatenda wegute!
7 Wamweda wanhu waja weli na bazi kwa wayagwe,

---

* **4:25** *Dekapoli* Fambulo jake mabuga longo

kwavija Mulungu nayo kowonela bazi!
8 Wamweda wanhu waja wailavile kwa Mulungu kwa mizoyo yao yose,
kwavija womona Mulungu!
9 Wamweda wanhu waja wotenda wanhu wailumbe,
kwavija wokemigwa wana wa Mulungu!
10 Wamweda wanhu waja wodununzika mbuli ya kutenda gaja goyolonda Mulungu,
kwavija Undewa wa kuulanga uli wao!”

11 “Mmweda mweye muligigwa na kudununzigwa na kulongigwa vihile, kwavija mwa wanahina zangu.

12 Sekeleleni na kudeng'helela, kwavija mwikiligwa nhunza ng'hulu kuulanga. Kwavija vino vivo wadununzigwe watula ndagu wa Mulungu wakalile umwaka, mweye hamunavumbuka.”

### *Mkele na mulenge*
### *Mlk 9:50; Luk 14:34-35*

13 “Mweye mulinga kamba mkele kwa wanhu wose wa mwiisi. Ila kamba mkele wahagiza ukali wake, vino wogeligwa choni mbaka ubweze ukali wake kabili? Haufaya bule, ila wokwasigwa kunze na wanhu woubojoga.”

14 “Mweye muigala na mulenge kwa wanhu wa mwiisi. Buga dizengigwe kulugongo hadidaha kuifisa.

15 Kuduhu munhu yobwinha taa na kuigubika na kikalango, lakini koika kukingolobweda. Baho yomwemwesela kila munhu yeli mng'anda.

16 Vivo ili kumwenu mweye, mulenge wenu uwamwemwesele wanhu wagone gaja ganogile gomtenda muladi wamtogole Tataenu yeli kuulanga.

### *Malagizo ga Musa na mafundizo ga watula ndagu wa Mulungu*

17 “Sekemugese nene niza kugasegeza Malagizo ga Musa hebu mafundizo ga watula ndagu wa Mulungu. Niye niza kutenda Malagizo gago galawilile.

18 Nowalongela ukweli, mbaka ulanga na isi vosegela, kuduhu hata mbuli ndodo ng'hani yonda isegezigwe mna Gamalagizo mbaka gose galongigwe galawilile.

19 Munhu yoyose yolema kukweleleza lagizo dodo mna Gamalagizo gano na kuwafundiza wayagwe watende vivo, munhu ayo kokuwa mdodo mna undewa wa kuulanga. Lakini munhu ija yogagoga Malagizo na kuwafundiza wanhu wayagwe watende vivo, munhu ayo kokuwa mkulu Muundewa wa kuulanga.

20 Nowalongeleni, kamba hamutenda ganogile goyolonda Mulungu kubanza wafundiza Malagizo ga Musa na Mafalisayo, hamwingila ng'o Muundewa wa kuulanga.

### *Yesu kofundiza mbuli ya kugevuzika*
### *Luk 12:57-59*

21 “Muhulika wanhu wa umwaka viwalongeligwe, ‘Sekemukome. Munhu yoyose yonda yakome yatagusigwe.’

22 Lakini niye nowalongeleni munhu yoyose yomwihila ndugu yake kotagusigwa. Munhu yoyose yombeza ndugu yake kolondeka yagaligwe kukitala, na munhu yoyose yomkema ndugu yake, ‘Mbozi!’ ayo kolondeka yengile muumoto wa jehanamu.

23 “Avo kamba wahalonda kumulavila Mulungu nhunza muupango, na kokumbuka mugomba na ndugu yako,

24 tanhu ileke nhunza yako aho hana uupango, chola hima ukailumbe na ndugu yako, na abaho ubwele umulavile Mulungu nhunza yako.

25 “Munhu yahawa na mbuli na gweye na kolonda kukugala mna ikitala,
uilumbe nayo yang'hali hanakugala kukitala. Buleavo yahakugala kukitala,
na kukwika mmakono ga msemi, nayo kokwika mmakono ga wakalizi, na
gweye kogodekigwa mkifungo.
26 Nokulongela kweli, mumo humulawa ng'o mbaka ulipe sente yose.

### *Mbuli ya ugoni*

27 “Muhulika wanhu viwalongeligwe, ‘Sekemutende ugoni.’
28 Lakini niye nowalongela, munhu yoyose yonda yamulole mtwanzi kwa
kumsulukila, munhu ayo katenda ugoni na mtwanzi ayo muumoyo wake.
29 Avo kamba siso jako da mkono wa kudila dahakuhonza utende nzambi,
ding'ole ujase. Kwavija yokuwa vinoga ng'hani gweye wagize kinhu ki-
moja cha lukuli lwako, kubanza lukuli lwako lose lwasigwe muumoto wa
jehanamu.
30 Kamba mkono wako wa kudila wahakuhonza utende nzambi, ukanhe
uwase! Kwavija vinoga ng'hani kumwako wagize kinhu kimoja cha lukuli
lwako kubanza lukuli lwako lose lwasigwe muumoto wa jehanamu.

### *Fundizo da nyasa*
*Mat 19:9; Mlk 10:11-12; Luk 16:18*

31 “Vivija muhulika wanhu viwalongeligwe, ‘Munhu yoyose yomwasa
mwehe wake kolondeka yamgwee kibua cha nyasa.’
32 Lakini niye nowalongeleni, mbigalo sekeyamwase mwehe wake, ila
kamba mtwanzi ayo katenda ugoni. Kwavija kamba yahamwasa, komtenda
yawe mgoni, na mbigalo yonda yamsole mtwanzi ayo yasigwe vivija ko-
tenda ugoni.

### *Fundizo da kuiduila*

33 “Muhulika wanhu wa umwaka viwalongeligwe, ‘Sekeuleke kutenda kija
kiuiduile, ila kolondeka utende mbuli zose ziuiduile kwa Mndewa.’
34 Lakini niye nowalongeleni, sekemuiduile. Sekemuiduile kwa ulanga,
kwavija acho kigoda cha Mulungu,
35 vivija sekemuiduile kwa isi, kwavija aho hanhu ha kwikila magulu gake,
hebu kwa Yelusalemu, kwavija dijo buga da Mndewa mkulu.
36 Vivija sekeuiduile kwa pala jako, kwavija hudaha kulutenda hata luvili
lumoja luwe luzelu hebu lutitu.
37 Wahalonga, ‘Ona’ iwe ‘Ona,’ hebu wahalonga, ‘Bule’ iwe ‘Bule.’ Mbuli
yoyose iyagwe kubanza zino yolawa kwa Mwenembago.

### *Mbuli ya kulipa gehile*
*Luk 6:29-30*

38 “Muhulika viilongigwe, ‘Siso kwa siso, na zino kwa zino.’
39 Lakini niye nowalongeleni, sekeumbwezele munhu yakutendele gehile.
Munhu yahakutowa kanza da mkono wa kudila, muhindusile da kumoso.
40 Kamba munhu yahakugala kukitala kwa kulonda kusola shati jako,
muleke yasole na koti jako.
41 Kamba munhu kokunanahiza umpapile mzigo wake kwa utali wa
kilometa imoja, umpapile kwa kilometa mbili.
42 Munhu yahakupula kinhu mgwee, munhu yahalonda kukukopa sambi-
umulemele.

### *Kuwanogela wakwihile*
*Luk 6:27-28; Luk 6:32-36*

43 “Muhulika wanhu viwalongeligwe, ‘Wanogeleni mbwiga zako, na uwe-
hile waja wakwihile.’

44 Lakini niye nowalongeleni, wanogeleni wanhu wowehila na wapulileni
kwa Mulungu waja wowadununza,
45 baho mokuwa wana wa Tataenu yeli kuulanga. Kwavija heyo
kowamwemwesela zuwa jake wanhu wehile na wanogile, na kowagwaa
mvula waja wotenda gayolonda na waja wotenda gomgevuza.
46 Vino Mulungu kowagwaa nhunza gani kamba muhawanogela waiyeka
wanhu waja wowanogela mweye? Vino hata wabokela kodi hawatenda
vivo?
47 Muhawalamusa mbwiga zenu waiyeka, motenda kilozo gani? Vino hata
wamhazi hawatenda vivo?
48 Molondeka mutelele kamba Tataenu yeli kuulanga viyatelele.

# 6

*Fundizo da kuwataza wakiwa*

1 "Iteganyeni, sekemutende mbuli zinogile mgameso ga wanhu muladi
wanhu wawatogole. Muhatenda avo Tataenu wa kuulanga honda yawag-
wee nhunza yoyose.
2 "Avo kamba komgwaa kinhu munhu mkiwa, sekeutowe mhalati kutenda
wanhu wakijuwe kija kiutenda, kamba viwotenda wanafiki mna izing'anda
za kupulila na mna zinzila muladi wanhu wawatogole. Nowalongeleni
ukweli, awo wabokela mwaka nhunza yao yose.
3 Lakini gweye wahamgwaa kinhu munhu mkiwa, mkono wako wa ku-
moso sekeujuwe kija kitendigwa na mkono wako wa kudila.
4 Tenda avo kwa kinyelegezi. Tatako yolola gotendigwa kinyelegezi
kokugwaa nhunza.

*Fundizo da kumpula Mulungu*
*Luk 11:2-4*

5 "Mwahampula Mulungu, sekemuigale na wanafiki! Kwavija awo
wanogelwa kwima na kumpula Mulungu mna zing'anda za ukupula na
mna zinzila mhanda, muladi wanhu wawalole. Nowalongeleni ukweli, awo
wabokela mwaka nhunza yao yose.
6 Lakini gweye wahampula Mulungu, ingila mdigati jako, hinda
lwivi lwako, umpule Tatako hakoneka. Tatako iyolola gaja gotendigwa
kinyelegezi kokugwaa nhunza.
7 "Mwahampula Mulungu, sekemulonge mbuli nyingi za chaka chaka
kamba viwotenda wamhazi, kwavija wogesa wohulikigwa kwa mbuli zao
nyingi.
8 Sekemuigale nao, kwavija Tataenu kajuwa kija kimulonda mung'hali
hamunampula.
9 Lakini mweye puleni vino,
'Tataetu uli kuulanga,
twaga jako ditogoligwe,
10 undewa wako wize,
goulonda mwiisi gatendigwe, kamba viili kuulanga.
11 Utugwee lelo lujo lwetu lwa kila siku.
12 Uzigele kumgongo nzambi zetu zitutendile,
kamba vija tweye vituzigela kumgongo mbuli za wanhu wayagwe ziwatu-
tendele.
13 Sekeutwingize kuna ukugezigwa,
lakini utuhonye na ija Imdumuka.
[Kwavija siku zose undewa ni wako na inguvu na ukulu. Ona.']

14 “Kamba mwahazigela kumgongo nzambi wanhu ziwawatendele, vivija Tataenu yeli kuulanga kozigela kumgongo nzambi zenu.
15 Lakini kamba hamuzigela bule kumgongo nzambi za wanhu wayagwe, Tataenu yeli kuulanga nayo hazigela bule kumgongo nzambi zenu zimutendile.

### *Fundizo da kufunga kuja*

16 “Mwahafunga kuja, sekemuwe kamba wanafiki, awo wovitenda vihanga vao vigele bazi muladi wakoneke kamba wafunga kuja. Nowalongeleni ukweli, awo wabokela mwaka nhunza yao yose.
17 Lakini gweye wahafunga kuja, sunha kihanga chako na ubunhe mvili zako,
18 muladi wanhu wayagwe sekewakujuwe kamba kufunga kuja ila Tatako yaiyeka yoleka koneka, ayo yonda yajuwe. Nayo Tatako yolola gaja goutenda kinyelegezi kokugwaa nhunza.

### *Ngama ya kuulanga*
*Luk 12:33-34*

19 “Sekemwike ngama zenu mwiisi ino muli na ng'hobo na lungwi luzibananga, na wabavi wokwingila na kwiba.
20 Lakini mwike ngama zenu kuulanga, ako ng'hobo na lungwi havidaha kubananga, na wabavi hawadaha kwingila na kwiba.
21 Kwavija kuko kuili ngama yako, vivija kuko kondauwe moyo wako.

### *Mulenge wa lukuli*
*Luk 11:34-36*

22 “Meso gago taa ya lukuli. Kamba meso gako magima, lukuli lwako lose lokuwa na mulenge,
23 lakini kamba meso gako gabanangika, lukuli lwako lose lokuwa mdiziza. Avo kamba mulenge ulimgati mmwako wahawa ziza, dokuwa ziza totolo!

### *Kumsang'hanila Mulungu na mali*
*Luk 16:13; 12:22-31*

24 “Kuduhu munhu yodaha kuwasang'hanila wakulu wabili, kwavija komwihila imoja na kumnogela iyagwe, hebu koilumba na imoja na kumbeza iyagwe. Hamudaha kumsang'hanila Mulungu hamoja na mali.
25 “Lekaavo nowalongeleni, sekemuugaiye ugima, moja choni na kung'wa choni, hebu ng'huli zenu zovala choni. Vino ugima haunogile bule kubanza lujo? Hebu lukuli halunogile bule kubanza viwalo?
26 Waloleni bondwa, hawahanda, hawasenga, hebu kwika kudikanho, lakini Tataenu yeli kuulanga kowadima. Vino mweye hamunogile ng'hani bule kubanza iwabondwa?
27 Nani kumwenu kwa kuigaza ng'hani kodaha kwengeza hata saa dimoja da ugima wake?
28 “Habali mogaiya viwalo? Loleni maluwa ga kumuhulo vigokula, hagasang'hana hebu kuitendela viwalo.
29 Lakini nowalongeleni, hata mndewa Sulemani mwenyego na utajili wake wose, havalile goya kamba luwa dimoja mna gamaluwa gano.
30 Kamba Mulungu heyo yodivaza jani da kumuhulo, lelo dabahano na mayo dokwasigwa muumoto, vino hondayawavaze ng'hani mweye? Mweye wanhu mutamanila kidogo!
31 “Avo sekemuigaze kwa kulonga, ‘Toja choni?’ hebu, ‘Tong'wa choni?’ hebu, ‘Tovala choni?’

32 Kwavija vinhu vino vivo voogaiya wamhazi. Tataenu yeli kuulanga kojuwa kamba movilonda vinhu vose avo.
33 Lakini tanhu uzahileni Undewa wa Mulungu na gaja goyolonda, na vino vose mogweleligwa.
34 Avo sekemugagaiye ga mayo, kwavija mayo yoigaiya yenyego. Kila siku yoigaiya yenyego.

# 7

*Kuwatagusa wanhu wayagwe*
*Luk 6:37-38, 41-42*

1 "Sekemuwataguse wanhu wayagwe, avo na mweye sekemutagusigwe na Mulungu.
2 Kwavija vimuwatagusa wanhu wayagwe, na mweye motagusigwa vivo. Mulungu kowatendela vivija vimuwatendela wayagwe.
3 Habali kolola kibanzi kili mdisiso da ndugu yako, lakini hulola biki dili mdisiso jako?
4 Hebu kodahaze kumulongela ndugu yako, 'Chonde leka nikulave kibanzi kili mdisiso jako,' na kuno gweye mwenyego mdisiso jako mna biki?
5 Gweye kwa mnafiki! Tanhu lava biki dili mdisiso jako, abaho kodaha kulola goya na kulava kibanzi kili mdisiso da ndugu yako.
6 "Sekemuwagwee umbwa vinhu vilavigwe kwa Mulungu, kwavija wowahinduka na kuwaluma. Hebu sekemuwapigisile nguluwe lulu zenu, kwavija wozibojoga.

*Pula, zahila, gong'onda*
*Luk 11:9-13*

7 "Puleni, na mweye mogweleligwa, zahileni, na mweye movona, gong'ondeni ulwivi, na mweye movugulilwa.
8 Kwavija munhu yoyose yompula Mulungu kogweleligwa, na munhu yoyose yozahila kopata, na munhu yoyose yogong'onda ulwivi kovuguliligwa.
9 Vino kuna munhu yoyose kumwenu mweye kamba mwanage yahampula gate komgwaa dibwe?
10 Hebu yahampula somba komgwaa zoka?
11 Kamba mweye mmemile nzambi mojuwa kuwagwaa wanenu vinhu vinogile, avo Tataenu yeli kuulanga kowagwaa ng'hani vinhu vinogile wanhu waja wompula.
12 "Avo watendeleni wayagwe gaja gose gomulonda mweye kutendeligwa, kwavija dino dijo fambulo da Malagizo ga Musa na mafundizo ga watula ndagu wa Mulungu.

*Lwivi msisili*
*Luk 13:24*

13 "Ingileni kubitila lwivi msisili, kwavija lwivi lwa kwingilila kuna ukupotela lugazi, na nzila ilongoza ako ibuha, na wanhu wengi wobitila nzila ayo.
14 Lakini nzila ilongoza kuugima ni ndodo na sisili, wanhu kidogo awo woyona.

*Mbiki na matunda gake*
*Luk 6:43-44*

15 "Iteganyeni na watula ndagu wa uvizi. Wowezila kwa kukoneka kwa kunze kamba ng'hondolo, lakini mgati mmwao waigala na mbwizi.

16 Mowajuwa kwa sang'hano zao, mkese haudaha kulela fulu na mgude haudaha kulela ngama.
17 Vivija kila mbiki unogile wolela matunda ganogile, na mbiki wihile wolela matunda gehile.
18 Mbiki unogile haulela matunda gehile, na mbiki wihile haulela matunda ganogile.
19 Kila mbiki uleka kulela matunda ganogile wokanhigwa na kwasigwa muumoto.
20 Avo mowajuwa watula ndagu wa uvizi kwa kija kiwosang'hana.

### *Mweye siwajuwile bule*
*Luk 13:25-27*

21 "Siyo kila munhu yong'hema 'Mndewa, Mndewa' kokwingila mna Undewa wa kuulanga, ila waja waiyeka wotenda gaja goyolonda Tatangu yeli kuulanga.
22 Siku ya nhaguso yahavika, wanhu wengi wonongela, 'Mndewa, Mndewa! Kwa twaga jako tuwapetela wanhu usenga wa Mulungu, na kwa twaga jako tuwalava wanhu vinyamkela na kutenda unzonza!'
23 Abaho nowalongela, 'Ka, mweye siwajuwile bule. Segeleni kumwangu, mweye wanhu mutenda gehile!'

### *Wazengaji ng'anda wabili*
*Luk 6:47-49*

24 "Munhu yoyose yohulika mbuli zangu na kuzigoga, ayo kaigala na munhu mbala yazengile ng'anda yake mdibwe kulu.
25 Mvula itowa, vizanda vimema mazi, beho dibuma na kuitowa ng'anda ija, lakini hailagale bule, kwavija chandusilo chake kizengigwa mdibwe.
26 "Lakini munhu yoyose yohulika mbuli zangu na kolema kuzigoga, ayo kaigala na munhu mbozi yazengile ng'anda yake mumsanga.
27 Mvula itowa, vizanda vimema mazi, beho dibuma na kuitowa ng'anda ija, nayo igwa kwa nguvu."

### *Udahi wa Yesu*

28 Yesu viyamambukize kulonga avo, lunhu lose lwa wanhu lukanganywa kwa mafundizo gake,
29 kwavija hafundize kamba wafundiza wao wa Malagizo ga Musa, lakini kafundiza kwa udahi.

## 8

### *Yesu komuhonya munhu yeli na dikulu*
*Mlk 1:40-45; Luk 5:12-16*

1 Yesu viyahumuluke kulawa kukigongo lunhu lwa wanhu lumkweleleza.
2 Munhu imoja yeli na utamu wa dikulu kamgendela Yesu, kamfugamila kalonga, "Go mkulu, wahalonda kodaha kunihonya."
3 Yesu kamgolosela mkono wake, kamkwasa munhu ayo kalonga, "Nolonda, hona!" Bahaja munhu ayo kahona.
4 Abaho Yesu kamulongela, "Tegeleza! Sekeumulongele munhu yoyose, lakini goga inzila mbaka kwa mulava nhosa yakakulolese lolese. Abaho kalave nhosa kamba viyalagize Musa ili kutenda kila munhu yatogole kamba kuhonyigwa."

### *Yesu komuhonya msang'hanaji wa mkulu wa wakalizi wa Lumi*
*Luk 7:1-10*

5 Yesu viyengile Kapelinaumu, mkulu imoja wa wakalizi wa Lumi kamgendela kampula yamtaze.

6 Kalonga, “Go mkulu, msang'hanaji wangu kawasa ukae, kaholola na kolumwa ng'hani.”

7 Yesu kamulongela, “Nochola kumuhonya.”

8 Mkulu ayo kamwidika, “Go mkulu niye sifaya gweye wingile mng'anda yangu. Lakini longa mbuli na msang'hanaji wangu kohona.

9 Naniye vivija na hasi ya udahi wa wakulu na nina wakalizi hasi yangu. Nahamulongela ino ‘Chola!’ nayo kochola, nahamulongela iyagwe ‘Izo!’ nayo kokwiza, vivija nahamulongela msang'hanaji wangu, ‘Tenda vino!’ nayo kotenda vivo.”

10 Yesu viyahulike avo, kakanganya kawalongela waja wamkweleleza, “Nowalongeleni, sinamona munhu yoyose mwiisi ya Izilaeli yotamanila kamba ino.

11 Nowalongeleni ukweli, wanhu wengi wokwiza kulawa mwambu wa kudilawila zuwa na mwambu wa kudihongela, wokala hamoja na Abulahamu na Isaka na Yakobo mna ulujo kuna Uundewa wa kuulanga.

12 Lakini waja wolondeka wawe muundewa wa Mulungu wokwasigwa kunze kudiziza, ako wolila na kudafuna meno.”

13 Abaho Yesu kamulongela mkulu ayo, “Chola ukae, na kija chuupulile chotendigwa.”

Saa iija msang'hanaji wake kahona.

### *Yesu kowahonya wanhu wengi*
*Mlk 1:29-34; Luk 4:38-41*

14 Yesu viyacholile ukayake Petulo, kamvika mkwe wa kitwanzi wa Petulo kawasa mulusazi, kolumwa homa.

15 Yesu kamgoga mkono wake na homa imulawa, nayo kenuka kasonga kuwasang'hanila.

16 Ichungulo viivikile, wanhu wamgalila Yesu wanhu wengi wakalile na vinyamkela. Yesu kawalava vinyamkela kwa kulonga na kawahonya wakalile watamu.

17 Katenda avo muladi kilawilile kija kiyalongile mtula ndagu wa Mulungu Isaya, “Heyo mwenyego kasola magayo getu na kapapa mitamu yetu.”

### *Wanahina wa Yesu viwolondeka kukala*
*Luk 9:57-62*

18 Yesu viyaluwone lunhu lwa wanhu lumzunguluka, kawalagiza wanahina zake waloke mwambu uyagwe wa lamba.

19 Mfundiza Malagizo ga Musa imoja kamcholela kamulongela, “Mfundiza, nokuwinza kokose kuuchola.”

20 Yesu kamwidika, “Vizongo wana mhango na ndege wana mvulu, lakini Mwana wa Munhu kaduhu hanhu ha kubwihila.”

21 Mwanahina wake imoja kamulongela, “Go mkulu, beta tanhu mbweleganye hamzike tatangu.”

22 Lakini Yesu kamulongela, “Nikweleleze, waleke wanhu wafile wawazike wanhu wao wafile.”

### *Yesu kohoza beho*
*Mlk 4:35-41; Luk 8:22-25*

23 Yesu kengila mwiingalawa na wanahina zake wamkweleleza.

24 Bahaja dilawilila beho kulu kudilamba, na mawimbi ga mazi gaitowa ingalawa, mbaka ingalawa ilonda kudidimila. Lakini Yesu kakala yawasile.

25 Wanahina zake wamgendela wamulamusa, wamulongela "Go mkulu, tukombole todidimila!"

26 Yesu kawalongela, "Mweye mutamanila kidogo, habali modumba?" Avo kenuka kadikomhokela beho na ng'humbi ya mazi vinyamale na baho kukala tuluu.

27 Wanhu wakanganya, wauza, "Vino ino munhu gani? Mbaka beho na ng'humbi vomuhulika!"

### *Yesu kowahonya wanhu wabili weli na vinyamkela*
*Mlk 5:1-20; Luk 8:26-39*

28 Yesu viyavikile umwambu, mwiisi ya Gadala, kaiting'hana na wanhu wabili weli na vinyamkela, walawa kuna gamapanga. Wanhu awo wakala wodumbigwa, avo kuduhu munhu yadahile kubita nzila ayo.

29 Bahaja viwamone Yesu waguta mizangi wolonga, "Gweye Mwana wa Mulungu, kotulonda choni? Kwiza kutudununza kipindi king'hali hakinavika?"

30 Behi na hanhu aho hakala na bumbila da nguluwe woja.

31 Avo vinyamkela wampula Yesu, "Wahatulava tuleke twingile mna iwanguluwe."

32 Yesu kawalongela, "Choleni," Avo walawa na wengila mna iwanguluwe. Bumbila jose dihumulukila mna ingema ya dilamba na wose wafa mgamazi.

33 Wasusilaji wa nguluwe awo wakimbila, wachola kudibuga, ako walonga mbuli zose zilawilile na walonga mbuli ya wanhu waja wakalile na vinyamkela.

34 Avo wanhu wose walawa kudibuga dija, wachola kuiting'hana na Yesu. Na viwamone wampula yasegele mwiisi yao.

## 9

### *Yesu komuhonya munhu yaholole*
*Mlk 2:1-12; Luk 5:17-26*

1 Yesu kengila mwiingalawa kaloka umwambu wa lamba kachola kunadibuga diyakalile.

2 Wanhu wayagwe wamgalila munhu yaholole lukuli, yatambalale mulusazi. Yesu viyone kutamanila kwao, kamulongela munhu ayo yaholole, "Mwanangu, gangamala! Nzambi zako zigeligwa kumgongo."

3 Wafundiza Malagizo ga Musa wayagwe wailongela, "Munhu ino komuliga Mulungu!"

4 Yesu kajuwa viwagesile, avo kawalongela, "Habali mogesa gehile mna imizoyo yenu?

5 Vino choni kibuhile kulonga, 'Nzambi zako zigeligwa kumgongo,' hebu kulonga, 'Ima utembele'?

6 Lakini nolonda mujuwe vino, Mwana wa Munhu kana udahi mwiisi wa kuzigela kumgongo nzambi za wanhu." Avo kamulongela munhu ija yaholole, "Ima, papa lusazi lwako, uchole ukayako!"

7 Munhu ija kenuka kachola ukayake.

8 Wanhu viwonile avo, wadumba, wamtogola Mulungu kwa kuwagwaa wanhu udahi awo.

### *Yesu komkema Matayo*
*Mlk 2:13-17; Luk 5:27-32*

9 Yesu kasegela hanhu aho, na viyakalile kochola, kamona mbokela kodi, twaga jake Matayo, kakala hanhu hakulipila kodi. Yesu kamulongela, "Nikweleleze."

Matayo kenuka, kamkweleleza.
10 Yesu viyakalile koja mng'anda ya Matayo, wabokela kodi wengi na wanhu wehile weza, waja hamoja na Yesu na wanahina zake.
11 Mafalisayo wayagwe viwone avo, wawauza wanahina zake, “Habali mfundiza wenu koja hamoja na wanhu wano?”
12 Yesu viyahulike avo, kalonga, “Wanhu wagima hawamulonda mganga, ila wanhu watamu.
13 Lakini choleni mkaifunze mna Gamaandiko Gang'alile, Mulungu kalonga, ‘Kinilonda niye bazi, siyo nhosa.’ Niye sizile kuwakema wanhu wogesa wanoga, lakini niza kuwakema wanhu wene nzambi.”

### *Mbuli ya kufunga kuja*
*Mlk 2:18-22; Luk 5:33-39*

14 Wanahina wa Yohana Mbatizaji wamcholela Yesu wamuuza, “Habali tweye tofunga kuja na Mafalisayo vivija wofunga kuja, lakini wanahina zako hawafunga kuja bule?”
15 Yesu kawedika, “Vino yodahika vilihi wanhu wagonekigwe kuna idizengele wanyunyuwale kipindi munhu yosola kahamoja nao? Haidahika bule! Lakini kipindi chokwiza munhu yosola vonda yasegezigwe kumwao, aho wofunga kuja.”
16 “Kuduhu munhu yokwika kilaka cha sambi mna ikiwalo cha umwaka, yahatenda vivo kilaka cha sambi chokidega kiwalo cha umwaka na aho hadegeke hokongezeka.”
17 “Vivija kuduhu munhu yogida divai ya sambi mna imifuko ya ng'hwembe ya umwaka, kwavija yahatenda avo imifuko ayo yotulika, divai yokwitika na imifuko yobanangika. Ila divai ya sambi yogidigwa mna imifuko ya ng'hwembe ya sambi, vose vokuwa vigima.”

### *Mndele wa mkulu imoja na mtwanzi mtamu*
*Mlk 5:21-43; Luk 8:40-56*

18 Yesu viyakalile kolonga avo, mkulu wa Wayahudi kamgendela kamfugamila kalonga, “Mwanangu kafa, nokupula tuchole ukamwikile makono, nayo kokuwa mgima.”
19 Yesu na wanahina zake wenuka, wachola hamoja nayo.
20 Mtwanzi imoja yakalile na utamu wa kutumika kwa miyaka longo na mibili, kamcholela Yesu kukisogo, kakwasa mhindo ya kiwalo chake.
21 Kailongela mwenyego, “Nahakwasa kiwalo chake, nohona.”
22 Yesu kahinduka, kamona mtwanzi ayo, kamulongela, “Mndele, gangamala! Kutamanila kwako kukuhonya.” Bahaja mtwanzi ija kahona.
23 Yesu viyengile mna ing'anda ya mkulu ija, kawona watowa ving'weng'we va nyila za ndilo na lunhu lwa wanhu lukala lolila.
24 Kawalongela, “Laweni kunze. Imwana hafile bule, ila kawasa!” Nao wamseka.
25 Lunhu lwa wanhu vilulawile kunze, Yesu kengila kudigati da mndele ayo, kamgoga mkono wake, nayo kenuka.
26 Mbuli ayo ibwililika kila hanhu mwiisi ija.

### *Yesu kowahonya wasuwameso wabili*

27 Yesu kasegela hanhu aho, viyakalile kochola wanhu wabili wasuwameso wamkweleleza kuno wokemelela, “Mwana wa Daudi, tonele bazi!”
28 Yesu viyengile mng'anda, wasuwameso waja wabili wamgendela, Yesu kawauza, “Motogola kamba nodaha kuwahonya?”

Wamwidika, “Ona, go mkulu!”
29 Yesu kawakwasa meso gao, kalonga, “Ilawilile kamba vimutogola.”
30 Meso gao galola, Yesu kawazuma ng'hani, “Sekemumulongele munhu
yoyose mbuli ino!”
31 Lakini wao wachola, wazibwililisa mbuli za Yesu mwiisi ija yose.

*Yesu komuhonya munhu halonga*

32 Wanhu viwakalile wosegela, wanhu wayagwe wamgalila Yesu munhu
yakalile halonga, kwavija kakala na kinyamkela.
33 Kinyamkela viyalavigwe, munhu ija yakalile halonga, kasonga kulonga.
Wanhu wakanganya na kulonga, “Hatunachona kinhu kamba kino mwiisi
ya Izilaeli!”
34 Lakini Mafalisayo walonga, “Kana mwenembago ayo yomgwaa udahi
wa kuwalava vinyamkela.”

*Yesu kowonela bazi wanhu*

35 Yesu kachola mna gamabuga gose na ivijiji, kafundiza mna izing'anda
zao za kumpula Mulungu, kawapetela Mbuli Inogile ya Undewa wa Mu-
lungu na kuwahonya wanhu weli na mitamu na magayo.
36 Yesu viyawone wanhu, kawonela bazi kwavija wakala wogaya na
waduhu munhu wa kuwataza, kamba ng'hondolo weliduhu msusilaji.
37 Abaho kawalongela wanahina zake, “Ndiya nyingi, lakini
wasang'hanaji wadodo.
38 Mpuleni Mndewa wa indiya, yawatume wasang'hanaji mumgunda
wake.”

# 10

*Watumigwa longo na wabili*
*Mlk 3:13-19; Luk 6:12-16*

1 Yesu kawakema wanahina zake longo na wabili na kawagwaa udahi wa
kulava vinyamkela, kuhonya mitamu na magayo.
2 Gano gago matwaga ga watumigwa longo na wabili, wa ichanduso
Simoni yakemigwe Petulo na ndugu yake Andeleya, Yakobo na ndugu yake
Yohana wana wa Zebedayo.
3 Filipo na Batulumayo, Tomaso na Matayo mbokela kodi, Yakobo mwana
wa Alufayo, na Tadayo,
4 Simoni Mkananayo, na Yuda Isikaliote, yamuhinduke Yesu.

*Sang'hano ya watumigwa longo na wabili*
*Mlk 6:7-13; Luk 9:1-6*

5 Yesu kawatuma watumigwa wano longo na wabili kawalagiza, “Sekemu-
chole kwa wanhu wamhazi, hebu kwingila mna gamabuga ga Wasamalia.
6 Ila choleni kwa wanhu wa isi ya Izilaeli waigalile na ng'hondolo
wapotele.
7 Mwahachola, wapeteleni usenga uno, ‘Undewa wa kuulanga wa
mmabehi!’
8 Muwahonye watamu, wazilibuleni wafile, muwahonye waja weli na
utamu wa dikulu, muwalave vinyamkela. Mugweleligwa bule, laveni bule.
9 Mna imifuko yenu, sekemusole zahabu hebu shaba hebu sente.
10 Muumwanza wenu, sekemusole mkoba hebu viwalo vibili hebu vilatu
hebu mkongoja. Kwavija msang'hanaji kolondeka yagweleligwe kija kilon-
deka.

11 “Mwahengila mna dibuga jojose hebu mna ikijiji, mumzahile munhu yonda yawabokele, kaleni ukayake mbaka vondamusegele.

12 Mwahengila mng'anda, walamuseni wenekae.

13 Wanhu wa ng'anda ayo wahawabokela goya, tindiwalo jenu dokala nao, kamba wahaleka kuwabokela, tindiwalo jenu dowabweleleni mweye.

14 Munhu yoyose yahalema kuwabokela hebu kuwategeleza, vondamusegele baho kung'huseni matimbwisi mmagulu genu kamba kilaguso cha kuwalema.

15 Nowalongeleni ukweli mna isiku ya nhaguso Mulungu kowonela bazi wanhu wa buga da Sodoma na Gomola kubanza buga dijo.”

*Madununzo gonda geze*
*Mlk 13:9-13; Luk 21:12-17*

16 “Nowatuma kamba ng'hondolo hagati ya mbwizi. Avo muwe wabala kamba zoka na wahole kamba huwa.

17 Muiteganye na wanhu, kwavija wowagala mna ivitala, wowatowa mbalati mna izing'anda za kumpula Mulungu.

18 Mbuli ya niye mogaligwa haulongozi ha wakulu na wandewa, muladi muwalongela wao na wamhazi Mbuli Inogile.

19 Vonda wawagale mkitala, sekemugese gaja gondamulonge, kipindi chahavika mogweleligwa cha kulonga.”

20 Kwavija siyo mweye mondamulonge, lakini Loho wa Tataenu kolonga kubitila mweye.

21 “Munhu komuhinduka ndugu yake too yakomigwe na tata komuhinduka mwanage yakomigwe, na wana wowahinduka tata zao na mama zao wakomigwe.

22 Wanhu wose wowehila mweye mbuli ya twaga jangu. Lakini yoyose yonda yafunge umoyo mbaka kukimambukizo, kokomboligwa.

23 Wahawadununza kudibuga dimoja, kimbilileni kudibuga diyagwe, nowalongeleni ukweli, hamumambukiza sang'hano yenu kuna gamabuga gose ga Izilaeli yang'hali Mwana wa Munhu hanakwiza.

24 “Mwanahina hali mkulu kubanza mfundiza wake, wala mtumwa hambita mndewa wake.

25 Vimnogela mwanahina kuigala na mfundiza wake na mtumwa kuigala na mndewa wake. Kamba mkulu wa ng'anda kakemigwa Belizebuli, vino wanhu wa ng'anda yake honda wakemigwe matwaga gehile ng'hani?”

*Nani wa kumdumba*
*Luk 12:2-7*

26 “Avo sekemuwadumbe wanhu. Chochose kigubikigwe chogubuligwa na chochose kifisigwe chokoneka.

27 Kiniwalongeleni mdiziza, mkilonge imisi, na mbuli imuihulike kwa kinyelegezi, mweye ilongeni mkiswili.

28 Sekemuwadumbe waja iwokoma lukuli, lakini hawadaha kuikoma loho, ila mumdumbe Mulungu yodaha kulukoma lukuli na loho muumoto wa jehanamu.

29 Vino nhongwa wabili hawauzigwa kwa sente imoja? Lakini kuduhu hata imoja wao yofa bila Tata yenu kujuwa.

30 Lakini mweye, hata mvili zili mmapala genu zipetigwa zose.

31 Avo sekemudumbe, mweye munoga ng'hani kubanza nhongwa wengi!”

*Kumtogola na kumulema Kilisito*
*Luk 12:8-9*

32 “Munhu yoyose yonitogola niye mgameso ga wanhu na niye nomtogola
mgameso ga Tatangu yeli kuulanga.
33 Lakini munhu yoyose yonibela niye mgameso ga wanhu na niye
nombela mgameso ga Tatangu yeli kuulanga.”

### *Sizile kugala tindiwalo ila zele*
*Luk 12:51-53; 14:26-27*

34 “Sekemugese kamba niza kugala tindiwalo kwa wanhu wa mwiisi.
Sizile kugala tindiwalo, ila zele.
35 Kwavija niza kuwagola wana na tatazao wandele na mamazao, wandele
na wakwe zao wa kitwanzi.
36 Wehi wa munhu ni wanhu wa mng'anda mmwake.
37 “Munhu yoyose yomnogela tatake hebu mamake kubanza niye hafaya
yawe mwanahina wangu. Na munhu yoyose yowanogela wanage hebu
mndele wake kubanza niye hafaya yawe mwanahina wangu.
38 Munhu yoyose yoleka kupapa msalaba wake na kunikweleleza niye,
hafaya yawe mwanahina wangu.
39 Munhu yougomesa ugima wake kowagiza lakini munhu youlava ugima
wake mbuli ya niye, koupata.

### *Nhunza*
*Mlk 9:41*

40 “Munhu yoyose yowabokela mweye kombokela niye, na munhu yoyose
yombokela niye kombokela ija yanhumile.
41 Munhu yoyose yombokela mtula ndagu wa Mulungu, kwavija ayo mtula
ndagu wa Mulungu, kobokela nhunza ya munhu ayo. Na munhu yoyose
yombokela munhu yanogile, kwavija heyo kanoga kobokela nhunza ya
munhu ayo.
42 Nowalongeleni ukweli, munhu yoyose yomgwaa mwanahina kikasi cha
mazi govega kwavija heyo imoja wa wanahina zangu wadodo, kobokela
nhunza yake.”

## 11

### *Yohana Mbatizaji kowatuma wanahina zake kwa Yesu*
*Luk 7:18-35*

1 Yesu viyamambukize kuwagwaa malagizo gano wanahina zake longo na
wabili, kasegela hanhu aho, kachola kufundiza na kuwapetela wanhu mna
gamabuga ga Galilaya.
2 Yohana Mbatizaji yakalile mkifungo viyahulike gaja gayakalile yotenda
Kilisito, kawatuma wanahina zake kwa Yesu.
3 Wamuuza Yesu, “Vino gweye heyo ija iyalongile Yohana kokwiza, hebu
tumbete iyagwe?”
4 Yesu kawedika, “Bweleni mkamulongele Yohana gaja gomuhulika na
kugona,
5 wasuwameso wolola, mbetembete wotembela, na weli na utamu wa
dikulu wohonyigwa na wanhu hawahulika wohulika, wafile wozilibuka na
wakiwa wopeteligwa Mbuli Inogile.
6 Wamweda waja wose weliduhu shaka na niye!”
7 Wanahina wa Yohana viwakalile wosegela, Yesu kasonga kululongela
lunhu mbuli za Yohana, “Vino vimucholile kuluwala muchola kulola choni?
Muchola kulola lusanze vilutigisigwa na beho?

8 Kumbe muchola kulola choni? Muchola kumulola munhu yavalile
viwalo vinogile? Wanhu wovala kamba avo wokala mna zing'anda za
Wandewa!
9 Nongeleni, vino muchola kulola choni? Muchola kumulola mtula ndagu
wa Mulungu? Ona, lakini mona vingi ng'hani kubanza mtula ndagu wa
Mulungu.
10 Kwavija Yohana ayo yalongigwe mna Gamaandiko Gang'alile, 'Mulungu
kalonga, nomtuma msenga wangu yakulongolele, yaitande nzila yako.'
11 Nowalongeleni ukweli, hanalawilila munhu yoyose yeli munhu mkulu
kubanza Yohana Mbatizaji. Lakini yeli munhu mdodo ng'hani Muundewa
wa kuulanga ni munhu mkulu kubanza Yohana.
12 Kulawa kipindi cha Yohana Mbatizaji mbaka sambi, wanhu waulema
kwa nguvu Undewa wa kuulanga na wanhu wene nguvu wogeza kuuboka.
13 Kwavija Malagizo ga Musa na watula ndagu wa Mulungu, galonga mbuli
ya undewa mbaka kwiza kwa Yohana Mbatizaji.
14 Mwahazitogola mbuli zao, Yohana heyo Eliya yalongigwe kokwiza.
15 Yeli na magwiti yahulike!
16 "Vino wanhu wa lukolo lwa sambi waigala na choni? Waigala na wana
wadodo wakalile mna gamagulilo. Kibumbila kimoja chokemelela kiyagwe,
17 'Tuwatowela gombe sugu, lakini hamuvinile bule! Tuwembila nyila za
kuiyalala, lakini hamulilile bule!'
18 Kwavija Yohana viyezile kafunga kuja na hang'wile divai, nao walonga,
'Kana kinyamkela!'
19 Mwana wa Munhu viyezile, kaja na kung'wa, nao walonga, 'Mululeni
munhu ino! Mmelo na mlevi, mbwiga zake wabokela kodi na wanhu wene
nzambi!' Lakini nzewele ya Mulungu yokoneka inoga kwa sang'hano zake."

### *Mabuga goleka kutogola*
*Luk 10:13-15*

20 Yesu kasonga kuwakomhokela wanhu wa mabuga gayatendile unzonza
mwingi, kwavija wanhu awo hawazilekile bule nzambi zao.
21 "Kogaya, gweye buga da Kolazini! Kogaya gweye buga da Betisaida!
Maza unzonza utendigwe kumwenu mweye, wahatendigwe mna gam-
abuga ga Tilo na Sidoni, wanhu zake wahalekile mwaka nzambi zao na
kuvala magunia na kuibakaza mitozi, kulagusa kamba waleka nzambi zao!
22 Nowalongeleni ukweli, siku ya nhaguso Mulungu kowonela bazi wanhu
wa isi za Tilo na Sidoni kubanza mweye!
23 Vivija na gweye Kapelinaumu! Vino kolonda kuinula mwenyego mbaka
kuulanga? Kohumulusigwa mbaka kowochola wanhu wafile! Maza un-
zonza utendigwe kumwako gweye wahatendigwe Sodoma, isi ayo yahasi-
gale mbaka lelo!
24 Nowalongeleni, mna isiku ya nhaguso Mulungu kowonela bazi wanhu
wa isi ya Sodoma kubanza mweye!"

### *Izoni kumwangu mubwihile*
*Luk 10:21-22*

25 Mna ikipindi acho Yesu kalonga, "Tata, Mndewa wa kuulanga na mwiisi,
nokutogola kwavija kuwafisa mbuli zino wanhu weli na nzewele na ubala,
na kuwagubulila wana wadodo.
26 Ona, Tata, vino vivo viulondile.
27 "Tatangu kanigwaa vinhu vose. Kuduhu munhu yamjuwile Mwana ila
Tata yaiyeka, na kuduhu munhu yamjuwile Tata, ila Mwana yaiyeka na waja
Mwana yawasagule kuwagubulila wamjuwe Tata.

28 “Izoni kumwangu mweye mose mugaya na kulemelwa na mizigo
mikulu, na niye nowatenda mubwihile.
29 Soleni nila yangu muifunze kumwangu, kwavija niye simgaza munhu
hebu kumwehula, na mweye mokala mizoyo iholile.
20 Lakini kipindi chokwiza munhu yosola vonda yasegezigwe kumwao,
baho wofunga kuja.
21 "Kuduhu munhu yokwika kilaka cha kiwalo cha sambi mna kiwalo cha
umwaka. Yahatenda avo, kilaka cha sambi chokidega kiwalo cha umwaka,
na aho hadegeke hokongezeka.
22 Vivija kuduhu munhu yogida divai ya sambi mna mifuko ya ng'hwembe
ya umwaka, kwavija yahatenda avo divai ya sambi yoitula imifuko na divai

yokwitika na imifuko yobanangika. Ila divai ya sambi yogidigwa mna imifuko ya ng'hwembe ya sambi."

*Mbuli ya siku ya Kubwihila*
*Mat 12:1-8; Luk 6:1-5*

23 Siku dimoja da Kubwihila, Yesu na wanahina zake wakala wobita mna imigunda ya uhemba. Viwakalile wobita, wanahina zake wasonga kuhulula uhemba.

24 Mafalisayo wamulongela Yesu, "Lola, wanahina zako wotenda kinhu kigomesigwe kutendigwa kudi siku da Kubwihila!"

25 Yesu kawedika, "Hamusomile kija kiyatendile Daudi kipindi heyo na wayage viwakalile na nzala?

26 Mna ikipindi cha Mkulu wa walava nhosa Abiatali, Daudi kengila mna Ing'anda ya Mulungu na kugaja magate galavigwe nhosa kwa Mulungu. Magate gago golondigwa kudigwa na walava nhosa waiyeka, lakini Daudi kagaja na abaho kawagwaa wayage."

27 Abaho Yesu kawalongela, "Siku ya Kubwihila ikigwa mbuli ya wanhu, na siyo wanhu mbuli ya siku ya Kubwihila.

28 Avo Mwana wa Munhu ayo Mndewa wa siku ya Kubwihila."

# 3

*Munhu yeli na mkono uholole*
*Mat 12:9-14; Luk 6:6-11*

1 Abaho Yesu kachola kabili mng'anda ya kumpula Mulungu. Ako kukala na munhu yakalile na mkono uholole.

2 Wanhu wayagwe wakalile aho walonda kilamuso cha kumtagusila Yesu, avo wamulola bunhuu kamba komuhonya munhu ayo mna isiku ya Kubwihila.

3 Yesu kamulongela munhu ayo yaholole mkono, "Ima hano kuulongozi."

4 Abaho Yesu kawauza wanhu awo, "Vino Malagizo getu gotulonda tutende choni mna isiku ya Kubwihila? Kutenda ganogile hebu kutenda gehile? Kuuhonya ugima wa munhu hebu kuukoma?"

Lakini wao wanyamala huupi.

5 Yesu kawalola wanhu awo kwa kugevuzika, kawonela bazi mbuli ya udala wa mizoyo yao. Abaho kamulongela munhu ayo, "Golosa mkono wako." Nayo kaugolosa mkono wake, na mkono wake uhona.

6 Abaho Mafalisayo walawa kunze mna ing'anda ya kumpula Mulungu, waiting'hana na wanhu wa Helode, wakala kiseto wamkome Yesu.

*Lunhu lomkweleleza Yesu*

7 Yesu na wanahina zake wachola kudilamba da Galilaya, lunhu mkulu lwa wanhu lumkweleleza. Walawa kuzi isi za Galilaya na Yudea,

8 na buga da Yelusalemu, na isi ya Idumeya, na umwambu wa Yolidani, na kulawa mzimbaka zili mmabehi na mabuga ga Tilo na Sidoni. Wanhu wose awo wamcholela Yesu kwavija wahulika mbuli zake ziyakalile kotenda.

9 Kwavija lunhu lukala lukulu, Yesu kawalongela wanahina zake wamtandile ngalawa muladi wanhu sekewamsung'he sung'he.

10 Kwavija Yesu kawahonya wanhu wengi, avo wanhu wose wakalile watamu wakala woisung'ha sung'ha wadahe kumkwasa.

11 Wanhu wakalile na vinyamkela viwamonile Yesu, wamgwila kuulongozi waguta mizangi wolonga, "Gweye kwa Mwana wa Mulungu!"

12 Lakini Yesu kawagomesa vinyamkela sekewamulongele munhu yoyose kamba heyo kakala nani.

### *Yesu kosagula watumigwa longo na wabili*
### *Mat 10:1-4; Luk 6:12-16*

13 Abaho Yesu kakwela kukigongo, kawakema wanhu yawalondile mwenyego, nao wamgendela.
14 Kawasagula wanhu longo na wabili, kawakema watumigwa. Kawalongela, "Niwasagula mweye mukale na niye. Vivija nowagala mkawapetele wanhu Mbuli Inogile,
15 na mweye mokuwa na udahi wa kulava vinyamkela."
16 Wano awo longo na wabili iyawasagule, wakala Simoni, Yesu kamgwaa twaga da Petulo
17 na Yakobo na ndugu yake Yohana, wanage Zebedayo kawagwaa twaga da Boanilige, fambulo jake, "Wana wa Ng'huwa"
18 na Andeleya na Filipo na Batulumayo na Matayo na Tomaso na Yakobo mwana wa Alufayo na Tadayo na Simoni Mkananayo,
19 na Yuda Isikaliote, yamuhinduke Yesu.

### *Yesu na Belizebuli*
### *Mat 12:22-32; Luk 11:14-23; 12:10*

20 Abaho Yesu kachola ukae. Lunhu lwa wanhu luiting'hana kabili mbaka Yesu na wanahina zake walemelwa kuja.
21 Ndugu zake viwahulike avo, wagenda kumsola kwavija wanhu wakala wolonga, "Kana kibozi mbwelela!"
22 Wafundiza Malagizo ga Musa wayagwe walawile Yelusalemu wakala wolonga, "Kana Belizebuli! Ayo mkulu wa vinyamkela yomgwaa udahi wa kuwalava vinyamkela."
23 Yesu kawakema na kawalongela kwa simo, "Vino Mwenembago kodahaze kumulava Mwenembago?
24 Kamba undewa wahaigola wenyego na kuitowa, undewa awo wogwa.
25 Wanhu wa lubuga lumoja wahaigola na kuitowa, lubuga lulo logwa.
26 Avo kamba undewa wa Mwenembago wahaigola wenyego, undewa awo wogwa na kuhelela baho.
27 "Kuduhu munhu yodaha kutula ng'anda ya munhu mwene nguvu na kusola vinhu vake, mbaka yasonge kumgodeka munhu ayo, baho kodaha kusola vinhu vake.
28 "Nowalongela ukweli, nzambi zose ziwatendile wanhu na maligo gao gose, Mulungu kodaha kugela kumgongo.
29 Lakini munhu yoyose yomuliga Loho Yang'alile, maligo gake hondagageligwe kumgongo bule, kwavija katenda nzambi ya mazuwa gose."
30 Yesu kalonga avo kwavija wanhu wakala wolonga, "Kana kinyamkela."

### *Mamake na ndugu zake Yesu*
### *Mat 12:46-50; Luk 8:19-21*

31 Abaho mamake na ndugu zake Yesu weza, wema kunze wamtuma munhu yamkeme Yesu.
32 Lunhu lwa wanhu lukala lumzunguluke Yesu. Nao wamulongela, "Go mkulu, mamako na ndugu zako wa kunze, wokulonda gweye."
33 Yesu kawedika, "Mamangu ayo nani? Na ndugu zangu wao nani?"
34 Baho kawalola wanhu awo wamzunguluke, kawalongela, "Loleni! Wano awo mamangu na ndugu zangu!
35 Munhu yoyose yotenda gaja golondigwa na Mulungu, ayo ndugu yangu na lumbu jangu na mamangu."

# 4

*Lusimo lwa munhu yohanda*
*Mat 13:1-9; Luk 8:4-8*

1 Yesu kasonga kufundiza kabili kumgwazo wa lamba da Galilaya. Lunhu
lwa wanhu lumzunguluka mbaka kengila mwiingalawa na kukala mumo.
Wanhu wose wakala kumgwazo wa lamba.

2 Kawafundiza vinhu vingi kwa simo, kawalongela,

3 “Tegelezeni! Kukala na munhu kachola kuhanda mbeyu.

4 Viyakalile komiza zimbeyu kumgunda, ziyagwe zilagalila mnzila, ndege
weza na kuzija.

5 Ziyagwe zilagalila mgamabwe hakalile na udongo mdodo. Zota
himahima kwavija udongo ukala mdodo.

6 Zuwa vidilawile, diisoma mimeya na kwavija mizizi yake haicholile hasi
ng'hani, inyala.

7 Mbeyu ziyagwe zilagalila mvisolo va miba, visolo avo vikula na kuizonga
mimeya, nayo ilemelwa kulela.

8 Lakini mbeyu ziyagwe zilagalila hanhu heli na udongo unogile. Zota,
zikula na kulela kubanza zija zihandigwe, ziyagwe zilela malongo madatu,
ziyagwe zilela malongo sita, na ziyagwe zilela gana dimoja.”

9 Abaho Yesu kalonga, “Munhu yeli na magwiti, yahulike!”

*Kilamuso cha kulonga kwa simo*
*Mat 13:10-17; Luk 8:9-10*

10 Yesu viyakalile yaiyeka, wanahina zake longo na wabili na wanhu
wayagwe wamulongela yawafambulile simo azo.

11 Yesu kawalongela, “Mweye mugweleligwa kuzijuwa mbuli zifisigwe za
Undewa wa Mulungu, lakini awo weli kunze wohulika mbuli zose kwa simo,

12 muladi,

‘Walole, lakini sekewone,
wategeleze lakini sekewajuwe.
Kwavija wahavijuwa, wodaha kumbwelela Mulungu,
na Mulungu kozigela kumgongo nzambi zao.’ ”

*Yesu kofambula lusimo lwa munhu yohanda*
*Mat 13:18-23; Luk 8:11-15*

13 Abaho Yesu kawauza, “Hamulujuwile vilihi lusimo luno? Vino lelo
molujuwaze lusimo lolose luyagwe?

14 Muhandaji kohanda mbuli ya Mulungu.

15 Wanhu wayagwe waigala na izimbeyu zilagalile mnzila, wahahulika
mbuli, Mwenembago kokwiza na kuisola mbuli ihandigwe mgati mmwao.

16 Wanhu wayagwe waigala na mbeyu zilagalile mna gamabwe. Wahahu-
lika mbuli, bahaja wozibokela kwa kudeng'helela,

17 lakini kwavija waduhu mizizi mgati mmwao, wokala kipindi kidodo.
Wahagaya na kudununzika mbuli ya usenga awo, wobwela kukisogo.

18 Wanhu wayagwe waigala na mbeyu zilagalile mna ivisolo va miba.
Wohulika mbuli,

19 lakini magayo ga ugima uno, kulonda utajili, na kulonda mbuli nyingi
ziyagwe kuizonga mbuli ayo, nayo ilemelwa kulela.

20 Lakini wanhu wayagwe waigala na mbeyu zilagalile muudongo un-
ogile. Wouhulika usenga, woutogola na wolela matunda, wayagwe malongo
madatu wayagwe malongo sita na wayagwe gana dimoja.”

### *Taa igubikigwe*
*Luk 8:16-18*

21 Yesu kagendelela kulonga, “Vino munhu kodaha kubwinha taa
mng'anda na kuigubika na kikalango hebu kuika muuvungu wa lusazi?
Vino haika kukingolobweda?
22 Kwavija kinhu chochose kifisigwe chokoneka na kinhu chochose kigu-
bikigwe chogubuligwa.
23 Yeli na magwiti yahulike!”
24 Vivija kawalongela, “Iteganyeni na gaja gomuhulika! Vija vimuwata-
gusa wayagwe na Mulungu kowatagusa vivo na mokongezeligwa ng'hani.
25 Waja weli na vinhu wokongezelwa, lakini waja waliduhu vinhu
wobokigwa hata vija vidodo viwelinavo.”

### *Lusimo lwa mbeyu ikula*

26 Yesu kagendelela kulonga, “Undewa wa Mulungu uigala na kija kilaw-
ilile kwa munhu yamizile mbeyu mumgunda wake.
27 Ikilo kowasa, imisi kolamuka, mbeyu zota na kukula, lakini heyo
hajuwa choni kigendelela.
28 Udongo wenyego wozitenda mbeyu zikule goya na kulela matunda,
tanhu majani, abaho mada, na womambukiza kwa kuzamiza.
29 Uhemba wahakangala, munhu ayo kosola sengo na kosonga kusenga
kwavija kipindi cha kusenga kivika.”

### *Lusimo lwa mbeyu ndodo ya haladali*
*Mat 13:31-32, 34; Luk 13:18-19*

30 Yesu kalonga kabili, “Vino Undewa wa Mulungu uigala na choni? Vino
tuusimulile kwa lusimo gani?
31 Uigala na kija kilawilile kwa munhu yasolile mbeyu ya haladali mbeyu
ndodo kubanza zose na kuihanda mumgunda.
32 Lakini yahahandigwa, yokula na yokuwa mbiki mkulu kubanza mibiki
yose ihandigwe mumgunda. Yokwika matambi makulu ng'hani mbaka
ndege wozenga mvulu zao mna gamatambi gake.”
33 Yesu kawapetela wanhu usenga wake kwa simo nyingi ziigalile na zino,
kawalongela mbuli nyingi kamba viwadahile kuzijuwa.
34 Halongile nao kinhu chochose bila simo, lakini viwakalile waiyeka na
wanahina zake, kawafambulila vinhu vose.

### *Yesu kohoza beho kulu*
*Mat 8:23-27; Luk 8:22-25*

35 Ichungulo ya siku dijo, Yesu kawalongela wanahina zake, “Tuloke
mwambu wa lamba.”
36 Avo wawaleka wanhu wose, wanahina zake wengila mwiingalawa
yaakalile Yesu na wachola nayo. Vivija kukala na ngalawa ziyagwe hanhu
aho.
37 Bahaja dilawilila nyukwanyukwa kulu da beho na ng'humbi mgamazi
gaizola ija ingalawa mbaka ilonda kumema mazi. 38 Yesu kakala kukisogo
mwiingalawa, kawasa na keka pala jake muna umto. Wanahina zake
wamulamusa na kumulongela, “Mfundiza! Vino gweye hutonga, tweye
tofa?”
39 Yesu kalamuka, kadikomhokela dija dibeho, “Nyamala!” Baho beho
dinyamala tuluu, na kukala poozi.
40 Abaho Yesu kawalongela wanahina zake, “Habali modumba?
Mung'hali mduhu kutamanila?”

41 Wanahina zake wadumba na waiuza wenyego, “Vino ino munhu gani? Mbaka beho na ng'humbi vose vomuhulika!”

# 5

*Yesu komuhonya munhu yeli na vinyamkela*
*Mat 8:28-34; Luk 8:26-39*

1 Yesu na wanahina zake waloka mbaka mwambu wa lamba da Galilaya, mwiisi ya Wagelasi.

2 Baho Yesu viyalawile mwiingalawa, kaiting'hana na munhu yeli na vinyamkela. Munhu ayo kalawa kuna gamapanga.

3 Munhu ayo kakala yokala kuna gamapanga gago, kuduhu munhu yadahile kumgodeka minyololo.

4 Miyanza mingi wageza kumgodeka minyololo mmakono na mmagulu, lakini kakala yozikanha na kuzibena bena mhingu zili mmagulu gake. Kakala na nguvu ng'hani na kuduhu munhu yadahile kumgoga.

5 Imisi na ikilo kakala yokwanga mna gamapanga gaja na kuna ivigongo, kaguta nyangi na kuikanha kanha kwa mabwe.

6 Viyamone Yesu kwa kutali, kamkimbilila na kamfugamila.

7 Kaguta, “Yesu, Mwana wa Mulungu yeli Uchanha Ng'hani! Kolonda choni kumwangu? Iduile kwa twaga da Mulungu kamba hunidununza bule!”

8 Kalonga avo kwavija Yesu kamulongela, “Kinyamkela, mulawe munhu ino!”

9 Yesu kamuuza, “Twaga jako nani?”

Munhu ayo kamwidika, “Twaga jangu Lunhu, kwavija twa wengi!”

10 Kampula Yesu sekeyawagale ivinyamkela kunze ya isi ija.

11 Kukala na bumbila kulu da nguluwe wakala woja kuna umtelemuko wa kigongo.

12 Avo vinyamkela wampula Yesu, “Tugale kwa nguluwe, na utuleke tuwengile wao.”

13 Yesu kawatogolela, avo vinyamkela wamulawa munhu ayo, na wengila mna iwanguluwe. Bumbila jose da nguluwe elufu mbili wahumulukila kudilamba, wose wafila mumo.

14 Wanhu wakalile wowasusila nguluwe awo wakimbila na kuzibwililisa mbuli azo mwiisi na kumigunda. Abaho wanhu wachola kulola kija kilawilile.

15 Viwavikile kwa Yesu, wamona munhu ayo yakalile na vinyamkela kakala aho na kavala goya viwalo, na nzewele zake zimbwelela na wanhu wose wadumba.

16 Wanhu wachone acho kilawilile, wawalongela wayao gaja gampatile munhu ayo yakalile na vinyamkela, na mbuli za nguluwe.

17 Avo wanhu wampula Yesu yasegele mwiisi yao.

18 Yesu viyakalile kokwela mwiingalawa, munhu ayo yakalile na vinyamkela kampula Yesu wachole wose.

19 Lakini Yesu kamulemela, kamulongela, “Bwela ukayako ukawalongele wanhu wa lukolo lwako gaja gose Mndewa gayakutendele, na viyakonele bazi.”

20 Avo munhu ayo kasegela, kachola hanhu hakemigwe Dekapoli, kawalongela wanhu gaja gose Yesu gayamtendele. Wanhu wose wahulike wakanganya.

### *Mndele wa Yailo na mtwanzi yakwasile kiwalo cha Yesu*
### *Mat 9:18-26; Luk 8:40-56*

21 Yesu kabwela mwambu uyagwe wa lamba. Lunhu lwa wanhu lumzun-
guluka kumgwazo wa lamba.
22 Abaho keza mkulu imoja wa ng'anda ya kumpula Mulungu, twaga jake
Yailo. Viyamone Yesu, kaibwanha hasi mmagulu gake,
23 kampula ng'hani, "Mndele wangu kolumwa ng'hani. Nokupula chonde
chonde, wize ukamwikile makono muladi yahone na yawe mgima."
24 Abaho Yesu kachola na Yailo, lunhu mkulu lwa wanhu lumkweleleza
kuno lomsung'ha sung'ha.
25 Baho kukala na mtwanzi yakalile na utamu wa kutumika kwa miyaka
longo na mibili.
26 Mtwanzi ayo kachola kwa waganga wengi na katumia vinhu vose
viyakalile navo, lakini hahonile bule, ila kagendelela kulumwa ng'hani.
27 Viyazihulike mbuli za Yesu, kengila mna ulunhu lwa wanhu, kamc-
holela Yesu kukisogo na kakwasa kiwalo chake.
28 Kailongela mwenyego, "Nahakwasa kiwalo chake, nohona."
29 Viyakwasile kiwalo cha Yesu, bahaja kutumika kuleka, nayo kahulika
kahona utamu wake.
30 Bahaja Yesu kajuwa nguvu zimulawa, avo kahinduka muulunhu na
kuuza, "Nani yanikwasile kiwalo changu?"
31 Wanahina zake wamwidika, "Kowona wanhu viwokusung'ha sung'ha,
abaho kouza nani yakukwasile?"
32 Lakini Yesu kalola mhande zose ili yamone munhu yatendile vivo.
33 Mtwanzi ayo kajuwa kinhu kimulawilile, avo kamgendela Yesu kuno
kodumba na kugwaya. Kamfugamila Yesu, kamulongela fulu ipile.
34 Yesu kamulongela mtwanzi ayo, "Mwanangu, kutamanila kwako
kukuhonya. Genda moyo uholile, kuhona utamu wako."
35 Yesu viyakalile kogendelela kulonga, wasenga kulawa ukayake Yailo
weza na kumulongela Yailo, "Mndele wako kafa. Habali kogendelela
kumgaza Mfundiza?"
36 Yesu viyazihulike mbuli azo zilongigwe na wasenga awo, hazigesile
bule, lakini kamulongela Yailo, "Sekeudumbe, togola tu."
37 Abaho Yesu halondile munhu yoyose iyagwe yamkweleleze, ila Petulo,
Yakobo na Yohana, ndugu yake Yakobo.
38 Viwavikile mng'anda ya Yailo, Yesu kawona wanhu wobwahanhuka
kwa usungu na kuiyalala.
39 Yesu kengila mng'anda kawalongela, "Habali moiyalala na kulila?
Imwana hafile bule, lakini kawasa!"
40 Lakini wamseka, avo Yesu kawalava kunze wose, kamsola tatake na
mamake ija imwana, na waja wanahina zake wadatu. Wengila mna idigati
mulutambalizwe lukuli lwa mwana ayo.
41 Yesu kamgoga mkono, kamulongela, "Talita Kumi!" fambulo jake,
"Mndele, nokulongela lamuka!"
42 Bahaja mndele ayo kenuka na kasonga kugenda. Mndele ayo kakala na
miyaka longo na mibili. Mbuli ino viilawilile, wanhu wakanganya ng'hani.
43 Lakini Yesu kawagomesa ng'hani sekewamulongele munhu yoyose
mbuli ayo ilawilile, abaho kawalongela, "Mgweleleni lujo mndele ino."

# 6

*Yesu kolemigwa ako Nazaleti*
*Mat 13:53-58; Luk 4:16-30*

1 Yesu kasegela hanhu aho kachola kudibuga diyavumbuke, na wanahina zake wamkweleleza.

2 Vidivikile siku da Kubwihila, Yesu kasonga kufundiza mng'anda ya kumpula Mulungu. Wanhu wamuhulike wakanganya ng'hani, waiuza, “Munhu ino kazipata kwahi mbuli zino? Nzewele gani ino mbaka kodaha kutenda unzonza uno?

3 Vino ino siyo ija fundi selemala, mwanage Malia, na ndugu zake Yakobo na Yusufu na Yuda na Simoni? Vino lumbu zake hawakala bahano bule?” Avo wamulema.

4 Yesu kawalongela, “Mtula ndagu kotegelezigwa kila hanhu, lakini hategelezigwa ukayake na kwa ndugu zake, na kwa wanhu wa lukolo lwake mwenyego.”

5 Yesu hatendile unzonza wowose, ila kawekila makono watamu kidogo na kawahonya.

6 Yesu kakanganya ng'hani kwavija wanhu wakala waduhu kutamanila.

*Yesu kowatuma wanahina longo na wabili*
*Mat 10:5-15; Luk 9:1-6*

Abaho Yesu kachola mna ivijiji vili behi, na kasonga kuwafundiza wanhu.

7 Kawakema wanahina longo na wabili, kawatuma wabili wabili, na kawagwaa udahi wa kulava vinyamkela.

8 Kawalongela, “Sekemusole kinhu chochose, ila mkongoja wiiyeka. Sekemusole gate hebu mkoba hebu sente mkibindo.

9 Valeni vilatu, lakini sekemusole kiwalo kiyagwe.

10 Hanhu hohose honda mubokeligwe, kaleni aho mbaka vonda musegele.

11 Mwahavika kudibuga jojose na wanhu wa aho wahalema kuwabokela hebu kuwategeleza, segeleni na kung'huseni matimbwisi geli mmagulu genu muladi iwe kilaguso kamba wawatendela nzambi.”

12 Avo wasegela na kuwapetela wanhu waleke nzambi zao.

13 Wawalava vinyamkela wengi na kuwabakaza mavuta wanhu wengi wakalile watamu na kuwahonya.

*Ifa ya Yohana Mbatizaji*
*Mat 14:1-12; Luk 9:7-9*

14 Mndewa Helode kahulika mbuli azo zose, kwavija twaga da Yesu dikala dijuwike kila hanhu. Wanhu wayagwe wakala wolonga, “Yohana Mbatizaji kazilibuka kulawa kwa wafile, lekaavo kana udahi wa kutenda unzonza.”

15 Wanhu wayagwe walonga, “Ino Eliya.”

Na wanhu wayagwe walonga, “Ino mtula ndagu kaigala na imoja wa watula ndagu wa Mulungu wa kuko umwaka.”

16 Helode viyazihulike mbuli azo, kalonga, “Ino ayo Yohana Mbatizaji inimkanhile pala jake lakini kazilibuka kulawa kwa wafile!”

17 Helode mwenyego kakala yalagize Yohana yagodekigwe nzabi, abaho yekigwe mkifungo. Katenda avo mbuli ya Helodiya iyamsolile, hamoja kakala mwehe wa Filipo, mdodo wake.

18 Yohana Mbatizaji kakala yomulongela Helode, “Malagizo golonga, havinogile bule gweye umsole mwehe wa mdodo wako!”

19 Avo Helodiya kakala komwihila Yohana, na kalonda kumkoma. Lakini hadahile bule,

20 kwavija Helode kakala komdumba Yohana na kajuwa kamba kakala munhu yanogile na yang'alile avo kamkaliza. Kakala konogelwa kumuhulika, hamoja moyo umuluma ng'hani kila viyamalile kumuhulika.

21 Siku dimoja, Helodiya kapata nyafasi mna idisiku da kukumbuka kuvumbuka kwa Helode. Helode kawatendela nyimwili nyimwili ng'hulu wakulu wa mabuga, na wakulu wa wakalizi, na walangulizi wa isi ya Galilaya.

22 Mndele wa Helodiya viyengile kuvina, kamnogeza ng'hani Helode na wageni wagonekigwe kuna inyimwili nyimwili. Avo mndewa Helode kamulongela mndele ayo, "Nipule chochose kiulonda, nokugwaa."

23 Kaiduila, "Noiduila, nokugwaa chochose chondaunipule, hata nusu ya undewa wangu nokugwaa!"

24 Avo mndele ayo kalawa kunze kamuuza mamake, "Nipule choni?"

Nayo kamwidika, "Pula pala da Yohana Mbatizaji."

25 Bahaja mndele ayo kakimbila mbaka kwa mndewa, kamulongela, "Sambi baha nigwelele pala da Yohana Mbatizaji mditanda!"

26 Mndewa kona usungu ng'hani, lakini kwavija kaiduila mgameso ga wanhu wagonekigwe, hadahile kumulemela.

27 Bahaja mndewa kamulagiza mkalizi yadigale pala da Yohana. Mkalizi kagenda mkifungo, kakanha pala da Yohana.

28 Abaho kadika pala dija mditanda, kamgalila mndele ayo, nayo kamgwaa mamake.

29 Wanahina wa Yohana viwahulike mbuli ayo, wachola kulusola lukuli lwa Yohana na kuluzika.

### *Yesu kowagwaa lujo lunhu mkulu lwa wanhu*
### *Mat 14:13-21; Luk 9:10-17; Yoh 6:1-14*

30 Watumigwa wabwela, waiting'hana na Yesu na wamulongela gaja gose gawatendile na kufundiza.

31 Baho kukala na wanhu wengi wakalile wokwiza na kusegela, mbaka Yesu na wanahina zake hawapatile nyafasi ya kuja kinhu. Avo Yesu kawalongela wanahina zake, "Tucholeni twiiyeka hanhu kuduhu wanhu mkabwihile kidogo."

32 Avo wasegela waiyeka mwiingalawa, wachola hanhu kuduhu wanhu.

33 Wanhu viwonile wosegela, bahaja wawajuwa. Avo walawa mna gamabuga gose, wakimbila mbaka wawalongolela kuvika Yesu na wanahina zake.

34 Yesu viyahumuluke mwiingalawa, kaluvika lunhu mkulu lwa wanhu. Kawonela bazi kwavija wakala kamba ng'hondolo weliduhu msusilaji. Avo kasonga kuwafundiza vinhu vingi.

35 Zuwa vidikalile dohonga, wanahina zake wamcholela Yesu, wamulongela, "Hanhu hano hatwili kuduhu wanhu, na sambi zuwa dohonga.

36 Walongele wanhu wachole mna imigunda na vijiji vilibehi muladi wakaigulile vinhu va kuja."

37 Yesu kawedika, "Wagweleleni mweye kinhu cha kuja waje."

Wamuuza, "Vino tuchole tukagule magate ga sente ifaya kumulipa msang'hanaji kwa miezi minane[d] tuwagwee waje?"

38 Yesu kawauza, "Munago magate mangapi? Gendeni mukalole."

Viwagalolile, wamulongela, "Kuna magate matano na somba wabili."

---

d **6:37** ***Sente za miezi minane,*** hebu sente magana mabili.

39 Abaho Yesu kawalongela wanahina zake wawagole wanhu wose mna
ivibumbila bumbila, wakale hasi mna gamajani mabisi.
40 Avo wakala mna ivibumbila va wanhu gana na va wanhu malongo
matano.
41 Abaho Yesu kasola gaja gamagate matano na somba wabili, kalola
uchanha na kamgwaa nhogolwa Mulungu. Abaho kagabanzula gaja gam-
agate, kawagwaa wanahina zake wawagolele wanhu. Vivija kawagolela
wose somba waja wabili.
42 Wanhu wose waja na kwiguta.
43 Abaho wanahina zake wadondola magate gasigale na iwasomba,
wamemeza vigelo longo na vibili.
44 Wambigalo waiyeka wadile wakala gana elufu tano.

### *Yesu kotembela uchanha mgamazi*
### *Mat 14:22-33; Yoh 6:15-21*

45 Bahaja Yesu kawalagiza wanahina zake wakwele mwiingalawa wa-
mulongolele kuchola Betisaida, kuna umwambu uyagwe wa lamba. Heyo
kakala yolulaga lunhu lwa wanhu lusegele.
46 Viyamambukize kuwalaga wanhu, kakwela kuna ikigongo kumpula
Mulungu.
47 Viivikile ichungulo, ngalawa ikala hagati ya lamba, lakini Yesu kakala
yaiyeka mwiisi inyalile.
48 Yesu kawona wanahina zake wolemelwa kutowa ng'hafi, kwavija beho
kulu dikala dowabweza kuwalawile. Nzogolo zikwika, Yesu kawagendela,
kuno kotembela uchanha mgamazi. Kalonda kuwabita,
49 lakini viwamone kotembela uchanha mgamazi, wagizaga mzimu.
Wakemelela kwa bwembwe.
50 Wose viwamone wadumba ng'hani.
Bahaja Yesu kawalongela, “Gangamaleni! Iyo nene! Sekemudumbe!”
51 Abaho Yesu kengila mwiingalawa, na beho dinyamala tuluu. Wanahina
zake wakanganya ng'hani,
52 kwavija wakala hawajuwile fambulo da kuwagwaa lujo wanhu elufu
tano, mizoyo yao ikala midala.

### *Yesu kowahonya watamu ako Genesaleti*
### *Mat 14:34-36*

53 Waloka umwambu, wavika kuna iisi ya Genesaleti, baho waifunga
ngalawa yao.
54 Bahaja viwahumuluke mwiingalawa, wanhu wamjuwa Yesu.
55 Avo wakimbila mwiisi yose, na kila hanhu viwahulike Yesu kabaho
wamgalila watamu watambalale mvisazi vao.
56 Kila hanhu Yesu hayacholile, iwe mna ivijiji, hebu mna gamabuga,
hebu mna imigunda, wanhu wawasola watamu zao na kuwagala kuna
gamagulilo. Wampula Yesu yawatogolele waikwase mhindo ya kiwalo
chake. Wose waikwasile wahona.

## 7

### *Mafundizo ga wahenga*
### *Mat 15:1-9*

1 Mafalisayo na wafundiza Malagizo ga Musa wayagwe wezile kulawa
Yelusalemu waiting'hana haulongozi wa Yesu.
2 Wawona wanahina wayagwe wa Yesu woja bila kusunha makono gao
kamba viilondeka wanhu watende.

3 Mafalisayo na Wayahudi wayagwe wokweleleza mafundizo gawabokele
kwa wahenga zao, hawaja kinhu mbaka wasunhe makono gao ng'hani.
4 Wala hawaja kinhu chochose kulawa kudigulilo mbaka wasunhe, na
wokweleleza mafundizo gayagwe mengi kamba vija mwiko wa kusunha
vikasi na nongo na viya va shaba na gayagwe mengi.
5 Avo Mafalisayo na Wafundiza Malagizo ga Musa wamuuza Yesu, “Habali
wanahina zako hawakweleleza mafundizo gatugoleligwe na wahenga zetu,
lakini woja bila kusunha makono?”
6 Yesu kawedika, “Mweye mwa wanafiki! Kumbe mtula ndagu wa Mu-
lungu Isaya kalagula goya mbuli zenu viyandike,
‘Mulungu kolonga, wanhu wano, wonitegeleza kwa milomo yao,
lakini mizoyo yao yakutali ng'hani na niye.
7 Awo wonitambikila bule,
kwavija wofundiza mafundizo ga wanhu,
na kugatenda kamba galawa kwa Mulungu!’
8 “Mweye mogaleka Malagizo ga Mulungu na mogagoga mafundizo ga
wanhu.”
9 Yesu kagendelela kulonga, “Mweye mwa wabala kwa kulema Malagizo
ga Mulungu na kugagoga mafundizo genu wenyego.
10 Kwavija Musa kawalagiza, ‘Mtegeleze tatako na mamako,’ ‘Munhu
yoyose yonda yamulige tatake hebu mamake kolondeka yakomigwe.’
11 Lakini mweye mofundiza, kamba munhu kana kinhu kodaha kumtaza
tatake hebu mamake lakini kolonga ‘Ino kobani’ fambulo jake kinhu kino
nimulavila Mulungu,
12 munhu ayo halondeka kumtaza tatake hebu mamake.
13 Kwa nzila ino mafundizo genu gomuwagwaa wanhu gosegeza mbuli za
Mulungu. Na gayagwe mengi kamba gano gomutenda.”

### *Vinhu vimgela munhu dikwe*
### *Mat 15:10-20*

14 Abaho Yesu kalukema lunhu lwa wanhu kabili na kalulongela, “Mweye
mose mnitegeleze na mujuwe.
15 Kuduhu kinhu kingila mmulomo wa munhu kulawa kunze kidaha
kumgela munhu dikwe. Lakini, kija kilawa mmulomo wa munhu acho
kimgela munhu dikwe.”
16 Munhu yeli na magwiti yahulike.
17 Yesu na wanahina zake, viwalulekile lunhu lwa wanhu na kwingila
mng'anda, wanahina zake wamuuza yawalongele fambulo da ulonzi uja.
18 Yesu kawalongela, “Vino mweye mduhu nzewele kubanza wanhu
wayagwe? Vino hamujuwile kamba kuduhu kinhu kingila mmulomo wa
munhu kulawa kunze kidaha kumgela munhu dikwe?
19 Kwavija hakingila muumoyo lakini mna iinda na abaho cholawa kunze
ya lukuli.” Kwa ulonzi uno Yesu kavitenda vinhu vose va kuja vinoge
kudigwa.
20 Kagendelela kulonga, “Kinhu kilawa muumoyo wa munhu acho
kimgela munhu dikwe.
21 Kwavija muumoyo wa munhu molawa magesa gehile na kuiwasa chaka
chaka na ubavi na ukomaji,
22 na ugoni na umelo na gehile na uvizi na kusulukila na migongo na
maligo na kuitapa na ubozi.
23 Ago gose gehile golawa mgati mwa munhu na kumgela munhu dikwe.”

### *Kutamanila kwa mtwanzi imoja*
### *Mat 15:21-28*

24 Abaho Yesu kahalawa hanhu aho kachola mwiimbaka ili behi na buga
da Tilo. Kengila mng'anda na halondile munhu yoyose yajuwe kakala aho,
lakini hadahile bule kuifisa.
25 Mtwanzi imoja, yakalile na mndele wake yeli na kinyamkela, viyahulike
mbuli za Yesu, bahaja kamgendela na kamfugamila Yesu.
26 Mtwanzi ayo hakalile Muyahudi, kavumbuka kudibuga da Silofoinike
mwiisi ya Siliya kampula Yesu yamulave mndele wake kinyamkela.
27 Lakini Yesu kamwidika, "Tanhu waleke wana wegute. Kwavija
havinogile bule kusola lujo lwa iwana na kuwapigisila umbwa."
28 Mtwanzi ayo kamwidika, "Ona, go mkulu, lakini hata umbwa weli hasi
mmeza woja kija kisigazigwe na iwana!"
29 Yesu kamulongela mtwanzi ayo, "Kwavija kwidika vivo, bwela ukayako
na komvika mndele wako kinyamkela kamulawa!"
30 Mtwanzi ayo kachola ukayake, viyavikile kamvika mndele wake katambalala mulusazi na kinyamkela kakala yamulawile.

### *Yesu komuhonya munhu hadahile kulonga na kuhulika*

31 Yesu kasegela kachola behi na isi ya Tilo kwa kubitila mwiisi ya
Sidoni mbaka kudilamba da Galilaya kwa kubitila nzila ya mna zimbaka za
Dekapoli.
32 Wanhu wayagwe wamgalila munhu yakalile hahulika na halonga,
wampula Yesu yamwikile makono.
33 Yesu kamsola kamgala hamgwazo hanhu kuduhu wanhu. Yesu kengiza
vidole mna gamagwitwi ga munhu ayo, katema mate kamkwasa lulimi.
34 Abaho Yesu kalola kuulanga, kabweza mhumuzi, kamulongela, "Efata!"
fambulo jake, "Vuguka!"
35 Bahaja munhu ayo magwiti gake gavuguka na kakala yohulika na
kulonga bila kugaya.
36 Abaho Yesu kawagomesa wanhu awo sekewamulongele munhu yoyose
mbuli ayo, lakini Yesu viyagendelele kuwagomesa, vivo viwagendelele
kuibwililisa mbuli ayo.
37 Wanhu wose waihulike mbuli ayo wakanganya. Walonga, "Katenda
goya kila kinhu, kowatenda wanhu hawahulika wahulike na wanhu hawalonga walonge!"

# 8

### *Yesu kowagwaa lujo elufu nne*
### *Mat 15:32-39*

1 Hazibitile siku nyingi lunhu luyagwe lukulu lwa wanhu luiting'hana.
Wanhu viwakalile waduhu kinhu chochose cha kuja Yesu kawakema
wanahina zake kawalongela,
2 "Niye nowonela bazi wanhu wano, kwavija wakala na niye kwa siku
ndatu na waduhu kinhu cha kuja.
3 Nahawalongela wabwele ukayao na nzala, wosinduka mnzila, kwavija
wanhu wayagwe walawa kutali."
4 Wanahina zake wamuuza, "Hano hatwili twa kuluwala, tolupata kwahi
lujo lwa kuwagwaa wanhu wose wano?"
5 Yesu kawauza, "Mna magate mangapi?"
Wamwidika, "Tuna magate saba."

6 Yesu kalulongela lunhu luja lwa wanhu lukale hasi. Abaho kasola gamagate saba, kamgwaa nhogolwa Mulungu, kagabanzula kawagwaa wanahina zake wawagolele wanhu, na wanahina zake watenda vivo.
7 Vivija wakala na visomba kidodo. Yesu kamgwaa nhogolwa Mulungu, vivija kawalongela wanahina zake wawagolele wanhu.
8 Wanhu waja na kwiguta. Abaho wanahina zake wadondola vija visigale na kumemeza vigelo saba.
9 Wambigalo waiyeka wadile wakala elufu nne. Abaho Yesu kawalaga,
10 bahaja Yesu na wanahina zake wakwela mwiingalawa, wachola mwiisi ya Dalimanuta.

*Mafalisayo wolonda vilaguso*
*Mat 12:38-42; 16:1-4*

11 Mafalisayo wayagwe wamcholela Yesu wasonga kuibamilila nayo, walonda kumgeza wampula yatende kilaguso kulawa kuulanga.
12 Lakini Yesu kona usungu, kalonga, “Habali wanhu wa lukolo luno lwa sambi molonda vilaguso? Nowalongeleni ukweli, kuduhu kilaguso chonda mugoleligwe!”
13 Yesu kawaleka, kakwela mwiingalawa kaloka mwambu uyagwe wa dilamba.

*Usasu wa Mafalisayo na Helode*
*Mat 16:5-12*

14 Wanahina zake wakala waisemwile kusola magate, wakala na gate dimoja diiyeka mwiingalawa.
15 Yesu kawazuma wanahina zake kawalongela, “Muiteganye na usasu wa Mafalisayo na usasu wa Helode.”
16 Wanahina zake wasonga kuinyong'onyela, “Ino kolonga vino kwavija twaduhu magate.”
17 Yesu kakijuwa kiwakalile wolonga, kawauza, “Habali moilongela mbuli ya magate? Vino mung'hali hamujuwile? Habali mizoyo yenu midala?
18 Muna meso lakini hamulola, muna magwiti lakini hamuhulika? Vino hamukumbuka bule?
19 Vinibanzule magate matano na kuwagwaa wanhu elufu tano? Vino mmemeza vigelo vingapi kwa avo visigale?”
Wamwidika, “Tumemeza vigelo longo na vibili.”
20 Kawauza kabili, “Vivija vinibanzule gaja magate saba na kuwagwaa wanhu elufu nne, vino mmemeza vigelo vingapi kwa avo visigale?”
Wamwidika, “Tumemeza vigelo saba.”
21 Abaho kawauza, “Mung'hali hamnavijuwa?”

*Yesu komuhonya msuwameso ako Betisaida*

22 Yesu na wanahina zake viwavikile Betisaida, wanhu wayagwe wamgalila Yesu munhu yakalile msuwameso, wampula yamkwase.
23 Yesu kamgoga mkono munhu ayo, kamulava kunze ya kijiji kija. Abaho kamtemela mate mgameso, kamwikila makono, kamuuza, “Vino kokona choni?”
24 Munhu ija kalola, kalonga, “Nowona wanhu, lakini waigala na mibiki itembela.”
25 Yesu kamwikila makono kabili mgameso. Munhu ayo kabunhula meso na meso gake galola, nayo kadaha kulola goya vinhu vose.
26 Yesu kamulongela munhu ayo yachole ukayake, kamzuma, “Sekeyabweleganye mna ikijiji.”

*Petulo kolonga Yesu ayo Mkombola*
*Mat 16:13-20; Luk 9:18-21*

27 Abaho Yesu na wanahina zake wachola kuna ivijiji va Kaisalia ya Filipi,
mnzila Yesu kawauza wanahina zake, “Nongeleni wanhu wolonga niye na
nani?”

28 Wamwidika, “Wanhu wayagwe wolonga gweye kwa Yohana Mbatizaji,
wanhu wayagwe wolonga gweye kwa Eliya, kuno wayagwe wolonga gweye
kwa imoja wa watula ndagu wa Mulungu.”

29 Yesu kawauza, “Na mweye molonga niye na nani?”

Petulo kamwidika, “Gweye kwa Kilisito Mkombola.”

30 Abaho Yesu kawagomesa wanahina zake, “Sekemumulongele munhu
yoyose mbuli zangu.”

*Yesu kolonga mbuli ya madununzo na ifa yake*
*Mat 16:21-28; Luk 9:22-27*

31 Abaho Yesu kasonga kuwafundiza wanahina zake, “Mwana wa Munhu
kolondeka yadununzigwe ng'hani na kulemigwa na wavele na wakulu wa
walava nhosa na wafundiza Malagizo ga Musa. Kokomigwa na siku da
kadatu kozilibuka.”

32 Yesu kawalongela fulu ipile, avo Petulo kamgala Yesu kumgwazo ka-
songa kumkomhokela.

33 Lakini Yesu kahinduka kawalola wanahina zake, kamkomhokela
Petulo, “Segela kumwangu Mwenembago! Kwavija hugesa mbuli za Mu-
lungu lakini kogesa mbuli za kiunhu!”

34 Abaho Yesu kalukema lunhu lwa wanhu na wanahina zake kawa-
longela, “Munhu yoyose yahalonda kunikweleleza, yaileme mwenyego na
kuidikwa msalaba wake yanikweleleze.

35 Kwavija munhu yoyose yahalonda kuukombola ugima wake kowagiza,
na munhu yoyose yowagiza ugima wake mbuli ya niye na kwa Mbuli Inogile
koukombola.

36 Vino munhu kopata choni kamba yahaipata isi yose na kuwagiza ugima
wake?

37 Kuduhu kinhu chonda yalave yaubweze ugima wake.

38 Munhu yoyose yonyonela kinyala niye na mafundizo gangu mna
ulukolo lwa sambi lulekile kumjuwa Mulungu na kutenda gehile, Mwana
wa Munhu nayo komonela kinyala munhu ayo yaheza muukulu wa Tatake
na wasenga zake wang'alile wa kuulanga.”

# 9

1 Yesu kagendelela kulonga, “Nowalongela ukweli, wanhu wayagwe weli
hano hawafa bule mbaka wawone Undewa wa Mulungu ukwiza na nguvu.”

*Yesu kogaluka*
*Mat 17:1-13; Luk 9:28-36*

2 Vizibitile siku sita, Yesu kamsola Petulo, Yakobo na Yohana, kachola nao
waiyeka kuna ulugongo lutali. Viwakalile wolola, Yesu kagaluka.

3 Viwalo vake vikala vizelu chuwee, na kuduhu munhu yoyose mwiisi
yodaha kuvifuwa viwe vizelu kamba vivo.

4 Baho wanahina waja wadatu wamona Eliya na Musa wolonga na Yesu.

5 Petulo kamulongela Yesu, “Mfundiza, vinoga tweye tukale hano!
Tozenga viheha vidatu, kimoja chako gweye, kimoja cha Musa na kimoja cha
Eliya.”

6 Petulo hajuwile cha kulonga kwavija heyo na wayage wakala wodumba.

7 Abaho dilawilila wingu na kuwagubika na sauti ilawa mdiwingu, ilonga, “Ino ayo Mwanangu inimnogele. Mumtegeleze!”

8 Bahaja wawegesela kuno na kuno, lakini hawamonile munhu yoyose iyagwe, ila Yesu yaiyeka hamoja nao.

9 Viwakalile wohumuluka kulugongo Yesu kawazuma, “Sekemumulongele munhu yoyose mbuli zino zimone, mbaka Mwana wa Munhu vonda yazilibuke kulawa kwa wafile.”

10 Watogola kija kiwalongeligwe, lakini wasonga kuiuza, “Kuzilibuka kwa wafile, fambulo jake choni?”

11 Wanahina zake wamuuza Yesu, “Habali wafundiza Malagizo ga Musa wolonga Eliya kolondeka yeze tanhu?”

12 Yesu kawedika, “Ona, Eliya kokwiza tanhu, muladi yakitande goya kila kinhu. Lakini habali Maandiko Gang'alile golonga, Mwana wa Munhu kodununzika ng'hani na kulemigwa?

13 Nowalongeleni, Eliya kamala kwiza na wanhu wamtendela viwalondile, kamba vija Maandiko Gang'alile vigalonga.”

### *Yesu komuhonya mbwanga yeli na kinyamkela*
### *Mat 17:14-21; Luk 9:37-43*

14 Viwawavikile waja wanahina wayagwe, waluwona lunhu lwa wanhu luwazunguluka na wafundiza Malagizo ga Musa wayagwe wakala woibamilila nao.

15 Bahaja wanhu viwamone Yesu wakanganya ng'hani, wamkimbilila, wamulamusa.

16 Yesu kawauza wanahina zake, “Mweye moibamilila nao choni?”

17 Munhu imoja mna ulunhu lwa wanhu kamwidika, “Mfundiza, nikugalila mwanangu, kana kinyamkela yamfungile mulomo.

18 Kinyamkela ayo yahamwizila, komulagaza hasi na kolawa miholovu mumulomo, kodafuna meno na kunyala lukuli lose. Niwalongela wanahina zako wamulave ikinyamkela, lakini hawadahile bule.”

19 Yesu kawalongela, “Mweye wanhu muleka kutamanila! Ng'hale na mweye mbaka lini? Nogela kitumbe kumgongo mbaka lini? Ngalileni hano imbwanga.”

20 Avo wamgala kwa Yesu.

Bahaja kinyamkela viyamone Yesu, kamgela kisango imbwanga ayo, kagwa hasi, kaibimbilisa, kuno kolava mihovu mumulomo.

21 Yesu kamuuza tata wa imbwanga ayo, “Utamu uno umsonga lini?”

Kamwidika, “Umsonga toka haudodo.

22 Miyanza mingi kinyamkela kamgeza kumkoma kwa kumbwanha muumoto na mgamazi. Tonele bazi na ututaze, kamba wahadaha!”

23 Yesu kamulongela, “Kolonga, kamba wahadaha! Kila kinhu chodahika kwa munhu yotamanila.”

24 Bahaja tata wa imbwanga ija kakemelela, “Notamanila, lakini kutamanila kwangu kudodo. Nhaze nitamanile ng'hani!”

25 Yesu viyaluwone lunhu lowamemela, kamkomhokela kinyamkela ayo, “Gweye kinyamkela wa kuleka kulonga na kuhulika, nokulagiza umulawe mbwanga ino, sekeumwingile kabili!”

26 Kinyamkela kaguta, kambwanha hasi mbwanga ayo, kamulawa. Mbwanga ayo koneka kamba munhu yafile, kila munhu kalonga, “Kafa!”

27 Lakini Yesu kamgoga mkono mbwanga ayo kamtaza kwinuka, nayo kenuka.

28 Yesu viyengile mng'anda, wanahina zake wamuuza kinyelegezi, “Habali tweye hatudahile kumulava kinyamkela?”

29 Yesu kawedika, “Kinyamkela kamba ino hadahika kulavigwa kwa nzila yoyose, ila kwa kumpula Mulungu kwiiyeka.”

### *Yesu kolonga kabili mbuli ya ifa yake*
*Mat 17:22-23; Luk 9:43-45*

30 Yesu na wanahina zake wasegela hanhu aho wachola kubitila isi ya Galilaya. Yesu halondile munhu yoyose yajuwe kuyeli,

31 kwavija kakala kowafundiza wanahina zake. Kawalongela, “Mwana wa Munhu kogeligwa mmakono ga wanhu, nao womkoma na siku da kadatu kozilibuka.”

32 Lakini wanahina zake hawadijuwile fambulo da ulonzi awo na wadumba kumuuza.

### *Yeli mkulu nani?*
*Mat 18:1-5; Luk 9:46-48*

33 Wavika Kapelinaumu, viwengile mng'anda, Yesu kawauza wanahina zake, “Mukala muibamilila choni mnzila?”

34 Lakini wanahina zake hawamwidike bule, kwavija mnzila wakala woibamilila nani yeli munhu mkulu viweli.

35 Yesu kakala hasi, kawakema wanahina zake longo na wabili, kawalongela, “Munhu yoyose yolonda kuwa wa ichanduso, kolondeka yawe wa ikimambukizo na yawe msang'hanaji wa wose.”

36 Abaho Yesu kamsola mwana mdodo kamwimiza haulongozi wao, kamuhagatila kawalongela,

37 “Munhu yoyose yombokela mwana mdodo kamba ino kwa twaga jangu, kombokela niye, na munhu yoyose yombokela niye hambokela niye niiyeka vivija kombokela ija yanhumile.”

### *Munhu yoyose hatulema kaubanzi wetu*
*Luk 9:49-50*

38 Yohana kamulongela Yesu, “Mfundiza, tumona munhu imoja kolava vinyamkela kwa twaga jako. Tweye tumgomesa kwavija siyo miyetu.”

39 Yesu kawalongela, “Sekemumgomese, kwavija kuduhu munhu yotenda unzonza kwa twaga jangu na kuno kononga vihile.

40 Kwavija munhu yoyose hatulema kaubanzi wetu.

41 Nowalongela ukweli munhu yoyose yowagwaa kikasi cha mazi ga kung'wa kwa twaga jangu kwavija mweye mwa wanhu wa Kilisito kobokela nhunza yake.

### *Kugezigwa kutenda nzambi*
*Mat 18:6-9; Luk 17:1-2*

42 “Munhu yoyose yomuhonza imoja wa wadodo wano wonitogola yatende nzambi, yokuwa vinoga munhu ayo yagodekigwe dibwe kulu da kudugila msingo na yasigwe mbahali.

43 Kamba mkono wako wahakuhonza utende nzambi, ukanhe! Yokuwa vinoga wingile kuna ugima na mkono umoja, kubanza wingile na makono mabili na abaho uchole jehanamu kuna umoto haufaga.

44 Mumo, ‘Funza wowaja hawafa bule na umoto uwalukuza haufaga.’

45 Kamba mgulu wako wahakuhonza utende nzambi, ukanhe! Yokuwa vinoga wingile kuna ugima na mgulu umoja, kubanza wingile na magulu gose mabili na abaho wasigwe jehanamu.

46 Mumo, ‘Funza wowaja hawafa bule na umoto uwalukuza haufaga.’

47 Kamba siso jako dahakuhonza utende nzambi, ding'ole! Yokuwa vinoga wingile Muundewa wa Mulungu na siso dimoja, kubanza wingile na meso gose mabili na abaho wasigwe jehanamu.
48 Mumo, ‘Funza wowaja hawafa bule na umoto uwalukuza haufaga.’
49 “Kila munhu kotendigwa yatogoligwe na Mulungu kwa moto kamba vija nhosa viitogoligwa na Mulungu kwa mkele.
50 “Mkele unoga, lakini kamba wahagiza ukali wake, vino kodahaze kuubweza kabili?
“Muwe na mkele mgati yenu na mukale kwa tindiwalo na waenu.”

# 10

*Yesu kofundiza mbuli ya nyasa*
*Mat 19:1-12; Luk 16:18*

1 Abaho Yesu kasegela kachola isi ya Yudea, kaloka lwanda lwa Yolidani,
lunhu lwa wanhu lumcholela Yesu kabili, nayo kawafundiza kamba viyatendaga.
2 Mafalisayo wayagwe wamcholela Yesu wamgeza, wamuuza, “Tulongele,
vino vinoga mbigalo kumwasa mwehe wake?”
3 Yesu kawauza, “Vino Musa kawalagiza choni?”
4 Wamwidika, “Musa katulagiza kamba mbigalo kodaha kumgwaa kibua
cha nyasa mwehe wake na kumwasa.”
5 Yesu kawalongela, “Musa kawandikila lagizo dino mbuli ya udala wa
mizoyo yenu.
6 Maandiko Gang'alile golonga kulawa kuna ichanduso, ‘Mulungu
kawaumba mbigalo na mtwanzi.
7 Kwa mbuli ayo mbigalo komuleka tatake na mamake na koilumba na
mwehe wake,
8 na wabili awo wokuwa kinhu kimoja.’ Avo haweli wabili kabili, lakini
kinhu kimoja.
9 Avo kiyalumbilize Mulungu, munhu sekeyakigole.”
10 Viwabwelile mng'anda, wanahina zake wamuuza Yesu mbuli ino.
11 Yesu kawalongela, “Mbigalo yomwasa mwehe wake na kumsola mtwanzi iyagwe, komtendela ugoni mwehe wake.
12 Vivija mtwanzi yomulema mkasano wake na kusoligwa na mbigalo
iyagwe kotenda ugoni.”

*Yesu kowatambikila wana wadodo*
*Mat 19:13-15; Luk 18:15-17*

13 Wanhu wayagwe wamgalila Yesu wana wadodo yawahagatile na
kuwatambikila, lakini wanahina zake wawakomhokela.
14 Yesu viyonile avo, kagevuzika, kawalongela, “Walekeni wana wadodo
weze kumwangu sekemuwagomese kwavija Undewa wa Mulungu ni wa wanhu kamba wana wano.
15 Nowalongeleni ukweli, munhu yoyose yolema kuubokela Undewa wa
Mulungu kamba mwana mdodo, honda yengile ng'o.”
16 Abaho kawahagatila wana waja kawekila makono gake kawatambikila.

*Munhu tajili*
*Mat 19:16-30; Luk 18:18-30*

17 Yesu viyasongile mwanza wake kabili, munhu imoja kamkimbilila,
kamfugamila kamuuza, “Mfundiza Unogile, nhende choni niupate ugima wa mazuwa gose?”

18 Yesu kamuuza, “Habali kong'hema unogile? Kuduhu yanogile, ila
Mulungu yaiyeka.
19 Kugajuwa Malagizo ga Musa, ‘Sekeukome, sekeutende ugoni, sekewibe,
sekeulave usindila wa uvizi, sekeulonge uvizi, wategeleze tatako na ma-
mako.’ ”
20 Munhu ayo kamwidika, “Mfundiza gano gose nigagoga toka haudodo.”
21 Yesu kamulola bunhuu, kamnogela, kamulongela, “Kuhungukilwa
kinhu kimoja. Genda kachuuze vinhu vose viulinavo na uwagwelele
wakiwa zisente na gweye kokuwa na utajili kuulanga. Abaho unikweleleze.”
22 Munhu ija viyahulike avo, kona usungu, kasegela kuno kanyunyuwala
kwavija kakala tajili ng'hani.
23 Yesu kalola mhande zose kawalongela wanahina zake, “Yokuwa vidala
ng'hani kwa munhu tajili kwingila Muundewa wa Mulungu!”
24 Ulonzi uno uwasinhusa wanahina zake, lakini Yesu kagendelela ku-
longa, “Wanangu, vidala ng'hani kwingila Muundewa wa Mulungu!
25 Vibuha kwa ngamiya kubita mna ikizonzo cha sanzia kubanza tajili
kwingila Muundewa wa Mulungu.”
26 Wanahina wakanganya ng'hani waiuza, “Avo lelo nani yonda yadahe
kukomboligwa?”
27 Yesu kawalola bunhuu, kawalongela, “Kwa munhu haidahika lakini
kwa Mulungu haili vivo, gose godahika kwa Mulungu.”
28 Petulo kamulongela, “Lola, tweye tuleka kila kinhu na tukukweleleza
gweye.”
29 Yesu kawedika, “Nowalongela kweli, munhu yoyose yalekile ng'anda
yake hebu ndugu zake hebu lumbu zake hebu mamake hebu tatake hebu
wanage hebu migunda mbuli ya niye na kwa Mbuli Inogile,
30 kobokela vingi ng'hani mna ikipindi cha sambi. Na kobokela ng'hani
miyanza gana, ng'anda na ndugu na lumbu na wana na mama na migunda
na hamoja na madununzo na mna ikipindi chondakize kobokela ugima wa
mazuwa gose.
31 Lakini wanhu wengi weli wa ichanduso wokuwa wa ikimambukizo na
waja wa ikimambukizo wokuwa wa ichanduso.”

### *Yesu kolonga mwanza wa kadatu mbuli ya ifa yake*
### *Mat 20:17-19; Luk 18:31-34*

32 Yesu na wanahina zake wakala mnzila wochola Yelusalemu. Yesu
kawalongolela wanahina zake wakalile wokanganya kuno wanhu wakalile
womkweleleza wadumba. Yesu kainega hamgwazo na wanahina zake
longo na wabili, kawalongela gaja gonda gamulawilile.
33 Yesu kawalongela, “Tegelezeni, tochola Yelusalemu, kuko Mwana wa
Munhu kogeligwa mmakono ga wakulu wa walava nhosa na wafundiza
Malagizo ga Musa. Womtagusa yafe na kogeligwa mmakono ga wanhu
haweli Wayahudi,
34 nao womzeha na womtemela mate na womtowa mbalati na womkoma
lakini siku da kadatu kozilibuka.”

### *Kupula kwa Yakobo na Yohana*
### *Mat 20:20-28*

35 Abaho Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo wamcholela Yesu, wamu-
longela, “Mfundiza, kuna kinhu tolonda ututendele.”
36 Yesu kawauza, “Molonda niwatendele choni?”

37 Wamwidika, “Vondaukale kuna ikigoda chako cha Undewa wako,
tolonda ukale na tweye, imoja mwambu wa mkono wako wa kudila na
iyagwe mwambu wa mkono wako wa kumoso.”
38 Yesu kawalongela, “Hamkijuwile kinhu kimpula. Vino modaha kuk-
ing'wela kikasi cha madununzo chonda niking'wele niye? Na kubatizigwa
ubatizo unibatizigwa?”
39 Wamwidika, “Todaha,”
Yesu kawalongela, “Mong'wela kikasi chonda ning'wele niye na kuba-
tizigwa ubatizo wonda nibatizigwe niye.
40 Lakini niye nabule udahi wa kusagula nani yakale mwambu wa mkono
wangu wa kudila hebu wa kumoso. Mulungu ayo yonda yawagwee hanhu
aho, wanhu waja yawasagule.”
41 Baho wanahina longo viwahulike vivo wawagevuzikila ng'hani Yakobo
na Yohana.
42 Yesu kawakema wose hamoja kawalongela, “Mojuwa kamba waja
wokoneka wakulu wa isi, wowalanguliza wanhu kwa nguvu, na wakulu
wao wana udahi.
43 Lakini haili vivo kumwenu. Munhu yoyose yolonda kuwa munhu
mkulu, yawe msang'hanaji wa wose.
44 Na munhu yoyose yolonda kuwa wa ichanduso, yawe mtumwa wa
wose.
45 Kwavija Mwana wa Munhu hezile kusang'hanilwa, lakini keza
kuwasang'hanila wanhu na kuulava ugima wake kwa kuwakombola
wanhu wengi.”

### *Yesu komuhonya msuwameso*
*Mat 20:29-34; Luk 18:35-43*

46 Wavika Yeliko. Yesu na wanahina zake hamoja na lunhu lwa wanhu
viwakalile wosegela, msuwameso imoja yakalile yopula, twaga jake Batu-
mayo, mwanage Timayo kakala mnzila.
47 Batumayo viyahulike Yesu wa Nazaleti kobita, kasonga kukemelela,
“Yesu, mwanage Daudi nyonele bazi!”
48 Wanhu wengi wamkomhokela, wamulongela yanyamale, lakini heyo
kagendelela kukemelela ng'hani, “Mwana wa Daudi, nyonele bazi!”
49 Yesu kema, kalonga, “Mkemeni.”
Avo wamkema, wamulongela, “Gangamala! Ima, kokukema.”
50 Kawasa mgolole wake, kazumha kamcholela Yesu.
51 Yesu kamuuza, “Kolonda nikutendele choni?”
Munhu ayo kamwidika, “Mfundiza, nolonda kulola.”
52 Yesu kamulongela, “Chola, kutamanila kwako kukuhonya.”
Bahaja kadaha kulola kamkweleleza Yesu mnzila.

## 11

### *Yesu kokwingila Yelusalemu kwa ng'henze*
*Mat 21:1-11; Luk 19:28-40; Yoh 12:12-19*

1 Viwavikile behi na Yelusalemu, habehi na mabuga ga Betifage na Betania
kuna Ulugongo lwa Mizeituni, Yesu kawatuma wanahina zake wabili wamu-
longolele.
2 Kawalongela, “Gendeni kuna ikijiji kili kuulongozi wenu, mwahengila
momvika mwana mhunda kafungigwa, nayo yang'hali hanakweligwa na
munhu. Mfunguleni mumgale hano.
3 Munhu yoyose yahawauza habali motenda avo, mulongeleni Mndewa
komulonda, nayo kombweza sambi baha.”

4 Wanahina waja wachola wamvika mwana mhunda kafungigwa hana
ulwivi lwa ng'anda uilola na nzila. Viwakalile womfungula,
5 wanhu wemile aho wawauza, “Motenda choni, habali momfungula
imhunda?”
6 Wawedika kamba Yesu viyawalongele, wanhu waja wawaleka wachole.
7 Wamgala imwana mhunda ayo kwa Yesu, watandika viwalo vao mum-
gongo wa imhunda, Yesu kakwela uchanha.
8 Wanhu wengi wanzanza viwalo vao mnzila, na wayagwe wabena mi-
bunho wayanzanza mnzila.
9 Wanhu wakalile kukisogo na kuulongozi wa Yesu wakemelela, “Mulungu
yatogolwe! Mndewa Mulungu yamtambikile ayo yokwiza kwa twaga jake!
10 Mulungu yautambikile undewa ukwiza wa mndewa Daudi, muhenga
wetu! Mulungu yeli uchanha ng'hani yatogolwe!”
11 Yesu kavika Yelusalemu, kachola kuna Ing'anda ya Mulungu, kawege-
sela kuno na kuno. Lakini kwavija zuwa dikala dihongile, Yesu kachola
Betania na wanahina zake longo na wabili.

### *Yesu kouduila mbiki wa mtini*
*Mat 21:18-19*

12 Imitondo yake, viwakalile wosegela Betania, Yesu kakala na nzala.
13 Kwa kutali Yesu kawona mbiki wa mtini ukalile na mijani mingi,
avo kaucholela yalole kamba kodaha kupata tunda jojose lakini viyavikile
honile tunda jojose, ila majani gaiyeka, kwavija haukalile msimu wa kulela.
14 Yesu kaulongela mbiki wa mtini, “Munhu sekeyaje tunda jojose
kumwako kabili!”
Wanahina zake wamuhulika viyalongile vivo.

### *Yesu kochola kuna Ing'anda ya Mulungu*
*Mat 21:12-17; Luk 19:45-48; Yoh 2:13-22*

15 Viwavikile Yelusalemu, Yesu kachola kuna Ing'anda ya Mulungu.
Kasonga kuwawinga wanhu wose wakalile wogula na kuchuuza vinhu.
Kazibidula meza za wanhu wakalile wovunja sente na vigoda va wanhu
wakalile wochuuza njiwa.
16 Kawagomesa sekewasole kinhu chochose kubitila kuna Ing'anda ya
Mulungu.
17 Abaho kawafundiza, “Yandikigwa mna Gamaandiko Gang'alile,
‘Ng'anda yangu yokuwa kae ya kupulila kwa wanhu wa isi zose.’ Lakini
mweye moitenda mhango ya wabavi!”
18 Wakulu wa walava nhosa na wafundiza Malagizo ga Musa viwahulike
vivo, wasonga kuzahila nzila ya kumkoma Yesu, lakini wamdumba, kwavija
lunhu lwa wanhu lukanganya mafundizo gake.
19 Viivikile ichungulo, Yesu na wanahina zake wasegela kudibuga.

### *Fundizo da mbiki wa mtini unyalile*
*Mat 21:20-22*

20 Imitootondo yake, viwakalile wobita mnzila wawona mbiki awo wa
mtini unyala gogodaa!
21 Petulo kakumbuka kija kilawilile, kamulongela Yesu, “Mfundiza, lola,
umbiki wa mtini uuduile unyala!”
22 Yesu kawedika, “Mumtogole Mulungu.
23 Nowalongela ukweli, munhu yoyose yahakilongela kigongo kino,
Ng'oka ukayase mbahali na hakona shaka muumoyo wake lakini kotogola
kiyolonga cholawilila, na Mulungu komtendela.

24 Avo nowalongeleni, mwahampula Mulungu kinhu chochose, togoleni kamba mubokela, mogweleligwa chochose chonda mupule.

25 Mwahampula Mulungu geleni kumgongo nzambi ziwawatendele wanhu, muladi Tataenu yeli kuulanga nayo yazigele kumgongo nzambi zenu zimutendile.

26 Kamba hamuzigela kumgongo nzambi za wanhu ziwawatendele, na Tataenu yeli kuulanga honda yazigele kumgongo bule nzambi zenu zimutendile."

*Mbuli ya udahi wa Yesu*
*Mat 21:23-27; Luk 20:1-8*

27 Wavika kabili Yelusalemu, Yesu viyakalile kogenda kuna Ing'anda ya Mulungu, wakulu wa walava nhosa na wafundiza Malagizo ga Musa na wavele wamcholela,

28 wamuuza, "Vino kotenda gano gose kwa udahi gani? Nani yakugwelele udahi wa kutenda gano?"

29 Yesu kawedika, "Na niye nowauza mbuli imoja, mwahanidika, baho nowalongeleni notenda gano kwa udahi gani.

30 Nongeleni, udahi wa Yohana wa kubatiza ulawa kwa Mulungu hebu kwa wanhu?"

31 Wasonga kuilongela, "Twahalonga, 'Ulawa kwa Mulungu,' kotuuza, 'Habali hamumtogole Yohana?'

32 Lakini twahalonga, 'Ulawa kwa wanhu,' " wawadumba wanhu, kwavija wanhu wamtogola Yohana kamba mtula ndagu wa Mulungu.

33 Avo wamwidika, "Tweye hatujuwile."

Yesu kawalongela, "Na niye siwalongela bule kwa udahi gani notenda gano."

# 12

*Lusimo lwa walimaji mumgunda wa mizabibu*
*Mat 21:33-46; Luk 20:9-19*

1 Yesu kalonga nao kwa simo, "Munhu imoja kahanda mizabibu mumgunda wake. Kazungulusila lwigo mumgunda wake, kahimba hanhu ha kukamila zabibu, kazenga lingo. Abaho kawakodisha walimaji, kafunga mwanza kachola.
kwavija vose va mmakono gangu, na niye nodaha kumgwaa munhu yoyose
inimulonda.
7 Nokugwaa vinhu vose vino, kamba wahanitambikila.”
8 Yesu kamwidika, “Maandiko Gang'alile golonga,
‘Mtambikile Mndewa Mulungu wako,
na umsang'hanile heyo yaiyeka!’ ”
9 Abaho Mwenembago kamsola Yesu mbaka Yelusalemu, kamwika
uchanha ng'hani kuna ikiswili cha ing'anda ya Mulungu, abaho kamulon-
gela Yesu, “Kamba gweye kwa Mwana wa Mulungu, ilagaze mwenyego hasi
kulawa hano.
10 Kwavija Maandiko Gang'alile golonga,
‘Mulungu kowalagiza wasenga zake
wa kuulanga wakukalize!’
11 Na vivija golonga,
‘Wokupapa mmakono gao,

sekeuilumize magulu gako mgamabwe!' "
12 Lakini Yesu kamwidika, "Maandiko Gang'alile golonga, 'Sekeumgeze Mndewa Mulungu wako!' "
13 Mwenembago viyamambukize kumgeza Yesu kwa kila nzila, kamuleka mbaka kipindi kiyagwe kinogile.

### *Yesu kosonga sang'hano yake ako Galilaya*
*Mat 4:12-17; Mlk 1:14-15*

14 Abaho Yesu kabwela isi ya Galilaya, nguvu ya Loho Yang'alile ikala hamoja nayo. Mbuli zake zibwililika mziisi zose za mmabehi.
15 Kakala yofundiza mna zing'anda za kumpula Mulungu na kila munhu kamgwaa nhogolwa.

### *Yesu kolemigwa ako Nazaleti*
*Mat 13:53-58; Mlk 6:1-6*

16 Abaho Yesu kachola Nazaleti, hanhu kuyakulile. Mna isiku ya Kubwihila, kengila mng'anda ya kumpula Mulungu kamba viyatendaga. Kema yasome Maandiko Gang'alile.
17 Kagweleligwa kitabu cha mtula ndagu wa Mulungu Isaya, kakifungula na kona hanhu handikigwe,
18 "Loho wa Mndewa Mulungu kamgati mmwangu,
kwavija kanisagula niwagalile wanhu wakiwa Mbuli Inogile.
Kanituma niwapetele wagodekigwe kamba wolekesigwa,
na waja wasuwameso walole,
na kuwakombola waja wadununzigwe,
19 na kuwalongela kamba saa ivika
ya Mndewa kuwakombola wanhu zake."
20 Abaho Yesu kakigubika ikitabu, kakibweza kwa msang'hanaji, abaho kakala hasi. Wanhu wose wakalile mng'anda ya kumpula Mulungu wamulola Yesu bunhuu.
21 Nayo kasonga kuwalongela, "Chandikigwe muno, lelo kilawilila kamba vimuhulike."
22 Wose wamtogola na wakanganya mbuli zake zinogile ziyalongile. Walonga, "Vino ino siyo mwanage Yusufu?."
23 Yesu kawalongela, "Nojuwa monongela ulonzi uno, 'Mganga, ihonye mwenyego! Gose gatuhulike kugatenda ako Kapelinaumu, vivija gatende na hano ukayako.' "
24 Yesu kagendelela kulonga, "Nowalongela ukweli, kuduhu mtula ndagu yotegelezigwa ukayake.
25 "Nhegelezeni, ona kukala na wagane wengi mwiisi ya Izilaeli mna ikipindi cha Eliya. Kipindi acho, mvula haitowile miyaka midatu na nusu, kukala na lufilili lwa nzala mwiisi yose.
26 Lakini Eliya hatumigwe bule kwa munhu yoyose iyagwe mwiisi ya Izilaeli, ila kwa mgane imoja yakalile Selepata, mwiisi ya Sidoni.
27 Vivija mna ikipindi cha mtula ndagu wa Mulungu Elisha, kukala na wanhu wengi wakalile wolumwa utamu wa dikulu mwiisi ya Izilaeli. Lakini kuduhu munhu yoyose iyagwe yahonyigwe, ila Naamani yaiyeka, munhu wa isi ya Siliya."
28 Wanhu wakalile mng'anda ya kumpula Mulungu wagevuzika ng'hani viwahulike avo.
29 Wenuka, wamulava kunze kudibuga jao dizengigwe uchanha kukigongo, wamgala mbaka mwiingema ya kigongo acho, walonda kumpigisa hasi.

30 Lakini Yesu kabita hagati ya lunhu luja, kalawanya.

*Munhu yeli na kinyamkela*
*Mlk 1:21-28*

31 Abaho Yesu kachola kudibuga da Kapelinaumu mwiisi ya Galilaya.
Mwiisiku ya Kubwihila, kakala yofundiza wanhu.
32 Mafundizo gake gawakanganya wanhu wose, kwavija kakala kolonga
kwa udahi.
33 Mng'anda ya kumpula Mulungu kukala na munhu yeli na kinyamkela.
Kalila kwa sauti ng'hulu,
34 "Oii! Kolonda kututenda choni, Yesu wa Nazaleti? Vino kwiza ku-
tukoma? Nokujuwa, Gweye kwa ija Yang'alile wa Mulungu!"
35 Yesu kamkomhokela ikinyamkela ija, "Nyamala! Mulawe munhu ino!"
Kinyamkela kambwanha hasi munhu ija mgameso gao, abaho kamulawa
bila kumulumiza.
36 Wanhu wose wakanganya ng'hani na wailongela, "Mbuli gani zino?
Munhu ino kana nguvu na udahi wa kuwakomhokela vinyamkela, nao
womtegeleza!"
37 Avo mbuli za Yesu zibwililika kila hanhu mwiisi ija.

*Yesu kowahonya wanhu wengi*
*Mat 8:14-17; Mlk 1:29-34*

38 Yesu kalawa kuna ing'anda ya kumpula Mulungu, kachola ukayake
Simoni. Mkwe wa kitwanzi wa Simoni kakala yolumwa homa ng'hali, avo
wamulongela Yesu yamuhonye.
39 Yesu kamcholela, kema behi na lusazi lwa mtwanzi ayo, kaikomhokela
homa imulawe. Homa imulawa, bahaja mtwanzi ija kenuka, kasonga
kuwasang'hanila.
40 Zuwa vidihongile, wanhu wose wakalile na watamu wawagala kwa
Yesu, nayo keka makono gake uchanha mwa kila munhu na kuwahonya
wose.
41 Vinyamkela wawalawa wanhu wengi na kuguta, "Gweye kwa mwana
wa Mulungu!"
Yesu kawakomhokela na kawagomesa kulonga, kwavija wamjuwa kamba
kakala Kilisito.

*Yesu kowapetela wanhu mzing'anda za kumpula Mulungu*
*Mlk 1:35-39*

42 Imitondo yake, Yesu kasegela kudibuga, kachola hanhu kuduhu wanhu.
Wanhu wasonga kumzahila, na viwamone, walonda kumgomesa sekeyac-
hole.
43 Lakini Yesu kawalongela, "Vivija nolondeka kuwapetela wanhu wa
mmabuga gayagwe Mbuli Inogile ya Undewa wa Mulungu, kwavija acho
kiyanhumile Mulungu kukisang'hana."
44 Avo kawapetela wanhu mzing'anda za kumpula Mulungu mwiisi yose
ya Yudea.

# 5

*Yesu kowakema wanahina wa ichanduso*
*Mat 4:18-22; Mlk 1:16-20*

1 Siku dimoja Yesu kakala yemile mumgwazo wa lamba da Genesaleti.
Wanhu wengi wakala woisung'ha sung'ha wategeleza mbuli ya Mulungu.
2 Yesu kazona ngalawa mbili zikalile mwiingema ya lamba, zilekigwe na
wavuwa somba, wakalile wosunha mizavu yao.

[3] Yesu kengila mwiingalawa imoja ikalile ya Simoni, kamulonda Simoni yaikwese mgamazi. Abaho Yesu kakala mwiingalawa, kafundiza lunhu luja.

[4] Viyamambukize kufundiza, kamulongela Simoni, “Kwesa ingalawa mbaka kuna gamazi mengi, abaho gweye na wayago mupigise mizavu yenu muvuwe somba.”

[5] Simoni kamwidika, “Go mkulu, tusang'hana ng'hani kilo kigima lakini hatupatile kinhu bule. Lakini kamba gweye kolonga avo, nogela mizavu yangu mgamazi.”

[6] Wapigisa mizavu yao, somba wengi wanamata mbaka mizavu yao ilonda kudegeka.

[7] Avo wawakema wayao wakalile mwiingalawa iyagwe weze kuwataza. Wayao weza na wazimemeza ngalawa zose mbili, zose zikala zimemile somba mbaka zilonda kudidimila.

[8] Simoni Petulo viyachonile kija kilawilile, kamfugamila Yesu mmagulu, kalonga, “Mndewa, segela haulongozi wangu, niye nimema nzambi!”

[9] Simoni na wayage wakanganya ng'hani mbuli ya somba wengi wawapatile.

[10] Vivija wayage Simoni, Yakobo na Yohana, wanage Zebedayo, nao wakanganya. Yesu kamulongela Simoni, “Sekeudumbe. Kulawa sambi kokuwa mvuwaji wa wanhu.”

[11] Wazilava ngalawa zao kunze mumgwazo, wavileka vinhu vose, wamkweleleza Yesu.

### *Yesu komuhonya munhu yeli na dikulu*
*Mat 8:1-4; Mlk 1:40-45*

[12] Yesu viyakalile kudibuga dimoja, kukala na munhu imoja yakalile na utamu wa dikulu. Viyamonile Yesu, kaibwanha hasi, kampula, “Go mkulu, wahalonda, kodaha kunihonya!”

[13] Yesu kagolosa mkono wake, kamkwasa. Kalonga, “Nolonda, hona!” Bahaja utamu wa dikulu umulawa munhu ija.

[14] Yesu kamulagiza, “Sekeumulongele munhu yoyose, lakini goga inzila mbaka kwa mulava nhosa ukailaguse, abaho kalave nhosa kamba viyalagize Musa ili kutenda kila munhu yatogole kamba kuhonyigwa.”

[15] Lakini mbuli za Yesu zibwililika kila hanhu. Wanhu wengi weza kumtegeleza na kuhonyigwa mitamu yao.

[16] Lakini Yesu kacholaga hanhu kuduhu wanhu na kampula Mulungu.

### *Yesu komuhonya munhu yaholole*
*Mat 9:1-8; Mlk 2:1-12*

[17] Siku dimoja Yesu viyakalile kofundiza, Mafalisayo wayagwe na wafundiza Malagizo ga Musa wakala aho. Wakala walawile kila buga mwiisi ya Galilaya na Yudea na kulawa Yelusalemu. Nguvu ya Mndewa ikala hamoja na Yesu kuwahonya watamu.

[18] Wanhu wayagwe weza kuno wampapa mulusazi munhu yaholole. Wageza kumwingiza mng'anda wamwike haulongozi wa Yesu.

[19] Lakini hawapatile nzila ya kumwingiza mng'anda, kwavija kukala na lunhu lwa wanhu. Avo wamsola mtamu wao, wamgala uchanha kukiswili, watobola zonzo. Abaho wamuhumulusa na lusazi lwake mbaka hagati ya
lunhu lwa wanhu, wamwika haulongozi wa Yesu. [20] Yesu viyone kutamanila
kwao, kamulongela munhu ija, “Mbwigangu, nzambi zako zigeligwa kumgongo.”

[21] Wafundiza Malagizo ga Musa na Mafalisayo wasonga kuiuza, “Munhu gani ino kolonga mbuli za kumuliga Mulungu? Mulungu yaiyeka ayo yodaha kuzigela kumgongo nzambi za wanhu!”

22 Yesu kajuwa viwagesile, avo kawalongela, “Habali mogesa avo?
23 Choni kibuhile, kulonga, ‘Nzambi zako zigeligwa kumgongo,’ hebu kulonga, ‘Ima utembele’?
24 Lakini nolonda mujuwe kamba Mwana wa Munhu kana udahi mwiisi wa kuzigela kumgongo nzambi za wanhu.” Abaho kamulongela munhu ija yaholole, “Nokulongela, ima, papa lusazi lwako, uchole ukayako!”
25 Bahaja munhu ija kenuka mgameso ga wanhu, kapapa lusazi lwake mumo muyatambalale, kachola ukayake kuno komtogola Mulungu.
26 Wanhu wose wakanganya ng'hani na kudumba! Wamtogola Mulungu walonga, “Lelo tona unzonza!”

*Yesu komkema Lawi*
*Mat 9:9-13; Mlk 2:13-17*

27 Abaho Yesu kachola na kamona mbokela kodi yakemigwe Lawi kakala mng'anda ya kusolela kodi. Yesu kamulongela, “Nikweleleze.”
28 Lawi kenuka, kaleka kila kinhu, kamkweleleza.
29 Abaho Lawi kamtendela Yesu nyimwili nyimwili ng'hulu ukayake. Vivija kukala na wabokela kodi wengi na wanhu wayagwe wagonekigwe.
30 Mafalisayo na wafundiza Malagizo ga Musa wayagwe wakalile aho wawauza wanahina wa Yesu, “Habali moja na kung'wa hamoja na wabokela kodi na wanhu wotenda nzambi?”
31 Yesu kawedika, “Wanhu wagima hawalonda mganga, lakini waja weli watamu womulonda mganga.
32 Sizile kuwakema wanhu wogesa wanoga, lakini niza kuwakema waja wene nzambi waleke.”

*Mbuli ya kufunga kuja*
*Mat 9:14-17; Mlk 2:18-22*

33 Wanhu wayagwe wamulongela Yesu, “Wanahina wa Yohana Mbatizaji wofunga kuja miyanza mingi na kumpula Mulungu, na wanahina wa Mafalisayo wotenda vivo, lakini wanahina zako woja na kung'wa.”
34 Yesu kawedika, “Vino mogesa wanhu wagonekigwe kuna idizengele wodaha kufunga kuja kipindi munhu yosola kahamoja nao? Havidahika bule!
35 Lakini kipindi chokwiza, munhu yosola vonda yasegezigwe kumwao, baho wofunga kuja.”
36 Abaho Yesu kawalongela lusimo luno, “Kuduhu munhu yokanha kilaka mkiwalo cha sambi na kukika mkiwalo cha umwaka. Yahatenda avo, kokinanga kija kiwalo cha sambi, na kilaka acho honda kiigale na kiwalo cha umwaka.
37 Vivija kuduhu munhu yogida divai ya sambi mna mifuko ya ng'hwembe ya umwaka. Kwavija yahatenda avo, divai ya sambi yoitula mifuko ayo ya umwaka, divai yokwitika, na mifuko yobanangika.
38 Divai ya sambi yogidigwa mmifuko ya ng'hwembe ya sambi!
39 Kuduhu munhu yolonda divai ya sambi yahamambukiza kung'wa ya umwaka. Kwavija kolonga, ‘Ya umwaka inoga ng'hani.’ ”

# 6

*Mbuli ya siku ya Kubwihila*
*Mat 12:1-8; Mlk 2:23-28*

1 Mna isiku imoja ya Kubwihila, Yesu kakala yobita mmigunda ya uhemba. Wanahina zake wasonga kubena mikungwi ya uhemba, wagafigisa mmakono gao na kuja mhule zake.

2 Mafalisayo wayagwe wawauza, “Habali motenda kinhu kigomesigwe mna isiku ya Kubwihila?”

3 Yesu kawedika, “Vino mweye hamusomile kija kiyatendile Daudi na wayage viwakalile na nzala?

4 Daudi kengila Mng'anda ya Mulungu, kasola magate galavigwe kwa Mulungu, kagaja na vivija kawagwaa wayage. Malagizo gawagomesa wanhu wayagwe kuja magate gago ila kwa walava nhosa waiyeka.”

5 Abaho Yesu kamambukiza kwa kulonga, “Mwana wa Munhu ayo Mndewa wa siku ya Kubwihila.”

*Yesu komuhonya munhu yahololе mkono*
*Mat 12:9-14; Mlk 3:1-6*

6 Mna isiku iyagwe ya Kubwihila, Yesu kengila mng'anda ya kumpula Mulungu na kafundiza. Baho kukala na munhu imoja, mkono wake wa kudila ukala uholole.

7 Wafundiza Malagizo ga Musa na Mafalisayo wayagwe wakala wozahila kilamuso cha kumtagusa Yesu, avo wakala womulola wamone kamba komuhonya munhu mwiisiku ya Kubwihila.

8 Lakini Yesu kawajuwa viwagesile, kamulongela munhu ija yahololе mkono, “Ima wize hano haulongozi.” Munhu ija kenuka na kwima hagati.

9 Abaho Yesu kawalongela, “Nowauza, vino Malagizo getu gotulonda tutende choni mwiisiku ya Kubwihila? Kutenda ganogile hebu kutenda gehile? Kuhonya ugima wa munhu hebu kuukoma?”

10 Yesu kawalola wanhu wose wakalile aho, abaho kamulongela munhu ija, “Golosa mkono wako.” Munhu ija katenda avo, na mkono wake uhona kabili.

11 Lakini wanhu wagevuzika ng'hani na wasonga kuilongela wamtende choni Yesu.

*Yesu kosagula watumigwa longo na wabili*
*Mat 10:1-4; Mlk 3:13-19*

12 Kipindi kija Yesu kachola kuna ikigongo kumpula Mulungu, kakala ako kilo kigima kompula Mulungu.

13 Imitondo yake, kawakema wanahina zake, kawasagula longo na wabili mna idibumbila jao, kawagwaa twaga da watumigwa.

14 Watumigwa awo wakala Simoni, ayo Yesu kamkema Petulo na Andeleya mdodo wake, Yakobo na Yohana, Filipo na Batulumayo,

15 Matayo na Tomaso na Yakobo mwanage Alufayo na Simoni yakemigwe Zelote,

16 Yuda mwanage Yakobo na Yuda Isikaliote yamuhinduke Yesu.

*Yesu kofundiza na kuhonya wanhu*
*Mat 4:23-25*

17 Yesu viyahumuluke kukigongo hamoja na watumigwa zake, kema hanhu hagoloke hamoja na wanahina zake wengi. Lunhu mkulu lwa wanhu lukala aho kulawa isi yose ya Yudea na buga da Yelusalemu, na kulawa mhwani ya isi za Tilo na Sidoni.

18 Weza kumtegeleza Yesu na kuhonyigwa mitamu yao. Vivija wanhu waja wakalile wogazigwa na vinyamkela weza na wahonyigwa.

19 Wanhu wose wageza kumkwasa Yesu, kwavija nguvu ya kuhonya ikala ilawa kumwake na kuwahonya wose.

*Kudeng'helela na kunyunyuwala*
*Mat 5:1-12*

20 Yesu kawalola wanahina zake, kalonga,

“Mmweda mweye muli wakiwa,
kwavija Undewa wa Mulungu uli wenu.
21 Mmweda mweye muli na nzala sambi,
kwavija mokwiguta!
Mmweda mweye mulila sambi,
kwavija modeng'helela!”
22 “Mmweda mweye kamba wanhu womwihilani, wowalema, wowaliga
na kuwalonga vihile kwa mbuli ya Mwana wa Munhu!
23 Deng'heleleni na kuvina vonda galawilile, kwavija mwikiligwa nhunza
ng'hulu kuulanga. Kwavija vivo wahenga zao viwawatendele watula ndagu
wa Mulungu.
24 Lakini mogaya mweye muli matajili sambi,
kwavija mmala kupata deng'ho jenu!
25 Mogaya mweye mwigute sambi,
kwavija mokona nzala!
Mogaya mweye museka sambi,
kwavija moiyalala na kulila!”
26 “Mogaya mweye kamba wanhu wose wowagwaa nhogolwa kwavija
wahenga zao vivija wawatendela vivo watula ndagu wa uvizi.”

*Kuwanogela wakwihile*
*Mat 5:38-48; Mat 7:12*

27 “Lakini nowalongela mweye munitegeleza, wanogeleni wamwihileni,
muwatendele ganogile waja wowatendela gehile.
28 Muwatambikile waja wowaduila, na muwapulile kwa Mulungu waja
womonelani.
29 Munhu yonda yakutowe kanza dimoja, muleke yakutowe kanza
diyagwe vivija, kamba munhu kokuboka koti jako, muleke yasole na shati
jako vivija.
30 Munhu yahakupula kinhu mgwee, na munhu yokuboka vinhu vako,
sekeulonde yakubwezele.
31 Avo watendeleni wayagwe gaja gose gomulonda mweye kutendeligwa.”
32 “Kamba mweye mowanogela wanhu wowanogela mweye waiyeka,
vino motenda kilozo gani? Hata wanhu wene nzambi wowanogela waja
wowanogela hewo!
33 Na kamba mowatendela ganogile waja wowatendela ganogile waiyeka,
vino motenda kilozo gani? Hata wanhu wene nzambi wotenda vivo!
34 Na kamba mowakopesha waja waiyeka mutamanila wodaha kuwab-
wezela, vino motenda kilozo gani? Hata wanhu wene nzambi wowakopesha
wayao wotamanila wodaha kuwabwezela kikija kiwawakopeshe!
35 Lakini mweye wanogeleni waja womwihileni na muwatendele
ganogile, muwakopeshe wanhu bila kutamanila kubwelezeligwa. Abaho
nhunza yenu yokuwa ng'hulu, na mweye mokuwa wana wa Mulungu yeli
Uchanha Ng'hani. Kwavija heyo kanoga kwa waja weliduhu nhogolwa
kumwake na wanhu wotenda nzambi.
36 Muwe na bazi kamba vija Tata yenu viyeli na bazi.”

*Kuwatagusa wayagwe*
*Mat 7:1-5*

37 “Sekemuwataguse wayagwe, Mulungu honda yawataguse mweye.
Sekemuwalaumu wayagwe, na Mulungu honda yawalaumu mweye.
Mugele kumgongo nzambi za wanhu wayagwe, na Mulungu kogela
kumgongo nzambi zenu.

38 Muwagwee wayagwe, na Mulungu kowagwaa mweye. Na mweye
mobokela kibaba kimemile na kusindiligwa mbaka vokwitika mmakono
genu, na vose vonda mudahe kuvigoga. Avo, vija vimuwapimila wayagwe,
Mulungu nayo kowapimila vivo."

39 Abaho Yesu kawalongela lusimo luno, "Msuwameso hadaha kumu-
longoza msuwameso miyage. Yahatenda vivo, wose wabili wolagalila
mdikolombo.
40 Kuduhu mwanahina yombanza mfundiza wake. Lakini kila
mwanahina yahamambukiza mafunzo gake, koigala na mfundiza wake.

41 "Habali kolola kibanzi kili mdisiso da ndugu yako lakini hulola biki dili
mdisiso jako?

42 Hebu kodahaze kumulongela ndugu yako, 'Chonde, leka nikulave
kibanzi kili mdisiso jako,' kuno gweye ung'hali hunajona biki dili mdisiso
jako mwenyego? Gweye kwa mnafiki! Tanhu lava biki dili mdisiso jako,
abaho kodaha kulola goya na kulava kibanzi kili mdisiso da ndugu yako.

### *Mbiki na matunda gake*
*Mat 7:16-20; Mat 12:33-35*

43 "Mbiki unogile haudaha kulela matunda gehile, hebu mbiki wihile
haudaha kulela matunda ganogile.

44 Kila mbiki wojuwika kwa matunda gake goulela, kwavija hudaha
kubawa ngama mumkese hebu kubawa fulu kuna ivisolo va miba.

45 Munhu yanogile kolava ganogile mwiingama yake inogile ili muumoyo
wake, lakini munhu yehile kolava gehile mwiingama yake ihile ili muumoyo
wake. Kwavija munhu kolonga gaja gamemile muumoyo wake.

### *Wazengaji wabili*
*Mat 7:24-27*

46 "Habali monikema, 'Mndewa, Mndewa,' kuno hamugatenda gaja goni-
walongela?

47 Munhu yoyose yokwiza kumwangu na kutegeleza mbuli zangu na
kuzigoga nowalagusila kaigala na choni.

48 Kaigala na munhu yozenga ng'anda yake yahimbile hasi ng'hani, keka
chandusilo chake mdibwe. Mvula ng'hulu viitowile, mazi gaitowa ing'anda,
lakini hagadahile kuitigisa kwavija ikala izengigwe goya.

49 Lakini munhu yoyose yotegeleza mbuli zangu na kolema kuzigoga,
kaigala na munhu yazengile ng'anda yake bila kuhimba chandusilo. Mvula
ng'hulu viitowile, mazi gaitowa ng'anda ija, nayo igwa na kubanangika!"

## 7

### *Yesu komuhonya msang'hanaji wa mkulu imoja wa wakalizi wa Lumi*
*Mat 8:5-13*

1 Yesu viyamambukize kuwafundiza wanhu, kachola Kapelinaumu.

2 Ako kukala na mkulu imoja wa wakalizi gana wa Kilumi yakalile na
msang'hanaji wake mtamu ng'hani, na kalonda kufa. Nayo mkulu ayo
kakala yomnogela ng'hani msang'hanaji ayo. 3 Mkulu ayo viyahulike mbuli
za Yesu, kawatuma wavele wayagwe wa Wayahudi wampule Yesu yeze
kumuhonya msang'hanaji wake.

4 Avo wamcholela Yesu, wampula ng'hani, wamulongela, "Munhu ino
kofaya umtaze.

5 Kowanogela wanhu na vivija katuzengela ng'anda ya kumpula Mu-
lungu."

6 Avo Yesu kachola nao. Viyakalile behi na ng'anda ya mkulu ija, mkulu ija kawatuma mbwiga zake wamulongele Yesu, “Go mkulu, sekeuigaze kwiza ukae, kwavija niye sifaya gweye wingile mng'anda yangu,
7 vivija niiyona sifaya hata kwiza kumwako. Lakini longa mbuli iiyeka, na msang'hanaji wangu kohona.
8 Kwavija naniye vivija na hasi ya udahi wa wakulu na nina wakalizi hasi yangu. Nahamulongela ino, ‘Chola!’ nayo kochola, nahamulongela iyagwe, ‘Izo!’ nayo kokwiza, vivija nahamulongela msang'hanaji wangu, ‘Tenda vino!’ nayo kotenda vivo.”
9 Yesu viyahulike avo kakanganya ng'hani, kahinduka, kalulongela lunhu lwa wanhu lukalile lomkweleleza, “Nowalongela, sinamona munhu yeli na tamanilo kulu kamba dino, hata mwiisi ya Izilaeli!”
10 Wanhu waja watumigwe wabwela kuna ing'anda ya mkulu ija, wamvika msang'hanaji ija kahona.

### *Yesu komzilibula mwana wa mgane*

11 Kumwande, Yesu kachola kudibuga dimoja dikemigwe Naini. Kailon-goza na wanahina zake na lunhu mkulu lwa wanhu.
12 Viyakalile habehi na ulwivi mkulu wa kwingilila kudibuga dijo, wanhu wapapile maiti ga mbwanga wakala wolawa kunze kudibuga, wochola kuzika. Mbwanga ayo yafile kakala mwana yeli yaiyeka wa mtwanzi yakalile mgane. Wanhu wengi wa buga ijo wakala hamoja na mtwanzi ayo.
13 Mndewa Yesu viyamone mtwanzi ayo, kamonela bazi, kamulongela, “Sekeulile.”
14 Abaho kagenda, kalukwasa ulusazi luwaitambalize maiti ya mbwanga ija. Wanhu walupapile ulusazi luja wema. Yesu kalonga, “Mbwanga! Nokulongela, lamuka.”
15 Mbwanga ija yafile kalamuka, kasonga kulonga. Abaho Yesu kamgwaa mama ija mwanage.
16 Wanhu wose wengila bwembwe na wamtogola Mulungu. Walonga, “Mtula ndagu mkulu wa Mulungu katulawilila hamwetu! Mulungu keza kuwakombola wanhu zake!”
17 Mbuli zino za Yesu zenela mwiisi yose ya Yudea na isi zili mmabehi.

### *Wasenga kulawa kwa Yohana Mbatizaji*
*Mat 11:2-19*

18 Wanahina zake Yohana Mbatizaji wamulongela Yohana mbuli zose zino. Nayo kawakema wanahina zake wabili mna iwanahina zake,
19 kawatuma wachole kwa Mndewa wakamuuze, “Vino gweye ayo ija iyalongile Yohana Mbatizaji kokwiza, hebu tumbete iyagwe?”
20 Viwavikile kwa Yesu, wamulongela, “Yohana Mbatizaji katutuma tuku-uze, kamba gweye ayo ija yalongile kokwiza, hebu tumbete iyagwe?”
21 Kipindi kikija Yesu kawahonya wanhu wengi wakalile watamu, wakalile wogaya, wakalile na vinyamkela na kawatenda wanhu wengi wakalile wasuwameso walole.
22 Avo Yesu kawedika, “Bweleni mkamulongele Yohana gaja gomuhu-lika na kugona, wasuwameso wolola, mbetembete wotembela, na weli na utamu wa dikulu wohonyigwa, na wanhu hawahulika wohulika, wafile wozilibuka, na wakiwa wopeteligwa Mbuli Inogile.
23 Kamweda munhu ija yeliduhu shaka na niye!”
24 Wanahina wa Yohana viwasegele, Yesu kasonga kululongela lunhu luja mbuli ya Yohana, “Vino vimucholile kuluwala, muchola kulola choni? Muchola kulola lusanze vilutigisigwa na beho?

25 Vino muchola kulola choni? Muchola kumulola munhu yavalile viwalo vinogile? Wanhu iwovala viwalo vinogile, weli na ugima wa kubwihila wokala mzing'anda za wandewa!

26 Nongeleni, vino muchola kulola choni? Muchola kumulola mtula ndagu wa Mulungu? Ona, lakini mona vingi ng'hani kubanza mtula ndagu wa Mulungu.

27 Kwavija Yohana ayo yalongigwe mna Gamaandiko Gang'alile, ‘Mulungu kalonga, nomtuma msenga wangu yakulongolele, yaitande nzila yako.’ ”

28 Yesu kamambukiza kulonga, “Nowalongela, Yohana ni munhu mkulu kubanza munhu yoyose yakalile mwiisi. Lakini yeli mdodo Muundewa wa Mulungu ni munhu mkulu kubanza Yohana.”

29 Wanhu wose wamuhulike, hata wabokela kodi, wamtogola Mulungu kamba kanoga na wakala wabatizigwe na Yohana.

30 Lakini Mafalisayo na wafundiza Malagizo ga Musa walema kutenda ga Mulungu, kwavija walema kubatizigwa na Yohana.

31 Yesu kagendelela kulonga, “Vino niwasimulile kwa lusimo gani wanhu wa lukolo luno? Vino waigala na choni?

32 Waigala na wana wadodo wakalile mdigulilo. Kibumbila kimoja chokikemelela kibumbila kiyagwe, ‘Tuwatowela gombe sugu, lakini hamuvinile bule! Tuwembila nyila za kuindilo, lakini hamulililile bule!’

33 Yohana Mbatizaji keza, kafunga kuja na hang'wile divai, mweye mulonga, ‘Kana kinyamkela!’

34 Mwana wa Munhu keza, kaja na kung'wa, mweye mulonga, ‘Muloleni munhu ino! Mmelo na mulevi, mbwiga wa wabokela kodi na wanhu waja wotenda nzambi!’

35 Lakini nzewele ya Mulungu yokoneka inoga kwa wanhu waja wose woitogola.”

### *Yesu ukayake Simoni Mfalisayo*

36 Mfalisayo imoja kamgoneka Yesu yakaje nayo lujo lwa ichungulo. Avo Yesu kachola kuna ing'anda ya Mfalisayo, kakala na kuja.

37 Kudibuga dija kukala na mtwanzi imoja yakalile yotenda nzambi. Kahulika kamba Yesu kakala yoja mng'anda ya Mfalisayo ayo, avo kasola nyhupa ya alabasita imemile mavuta gonung'hila goya ga bei ng'hulu.

38 Kema kukisogo, habehi na magulu ga Yesu kolila, mahozi gake galagalila mgamagulu ga Yesu. Abaho kagahangusa magulu ga Yesu kwa mvili zake, kaganonela na kagagidila mavuta.

39 Mfalisayo ija viyone avo, kailongela, “Maza munhu ino yakalile mtula ndagu wa Mulungu, yahamjuwile mtwanzi ino yomgoga kavilihi, yahamjuwile kamema nzambi!”

40 Yesu kamulongela, “Simoni, nina mbuli ya kukulongela.”

Simoni kalonga, “Ona, Mfundiza, nongela.”

41 Yesu kasonga kumulongela, “Kukala na wanhu wabili wakopile sente kwa munhu yokopesha sente. Imoja kakopa sente magana matano, na iyagwe kakopa malongo matano.

42 Wose wabili hawadahile kumulipa, avo munhu ija kawalekelela wose. Vino nani mna iwanhu waja yonda yamnogele ng'hani munhu ija?”

43 Simoni kamwidika, “Vinikona niye kokuwa ija yalekeleligwe sente nyingi.”

Yesu kalonga, “Kulonga goya.”

44 Abaho kamuhindukila mtwanzi ija na kamulongela Simoni, “Komona mtwanzi ino? Niza kuna ikae yako, hungwelele mazi ga kusunha magulu

gangu, lakini mtwanzi ino kagasunha magulu gangu kwa mahozi gake na kagahangusa kwa mvili zake.
45 Gweye hunibokele kwa kuninonela, lakini mtwanzi ino halekile kuganonela magulu gangu tangu vinizile.
46 Hunibakile pala jangu mavuta, lakini mtwanzi ino kambakaza magulu gangu mavuta gonung'hila goya.
47 Nokulongela, nzambi zake nyingi zigeligwa kumgongo, lekaavo kalagusa unogelwa mkulu. Lakini munhu yoyose yeli na nzambi kidogo zigeligwe kumgongo, kolagusa unogelwa mdodo."
48 Abaho Yesu kamulongela mtwanzi ija, "Nzambi zako zigeligwa kumgongo."
49 Wanhu wayagwe wakalile hamoja na Yesu muulujo, wasonga kuilongela, "Ino munhu gani yodaha kuzigela kumgongo nzambi za wanhu?"
50 Lakini Yesu kamulongela mtwanzi ija, "Kutamanila kwako kukukombola. Genda moyo uholile."

# 8

*Watwanzi wacholile na Yesu*

1 Hamwande Yesu kafunga mwanza, kabitila mna gamabuga na vijiji kowapetela wanhu Mbuli Inogile ya Undewa wa Mulungu. Wanahina zake longo na wabili wachola nayo.
2 Watwanzi wayagwe wakalile walavigwe vinyamkela na kuhonyigwa mitamu yao vivija wamkweleleza. Watwanzi awo wakala Malia, yakemigwe Magidalena, ija yalavigwe vinyamkela saba,
3 Yoana mwehe wake Kuza yakalile msang'hanaji mkulu mna ikae ya mndewa Helode, na Suzana, na watwanzi wayagwe wengi. Watwanzi awo wakala wosola vinhu vao na kuwataza Yesu na wanahina zake.

*Lusimo lwa muhandaji*
*Mat 13:1-9; Mlk 4:1-9*

4 Wanhu wagendelela kwiza kwa Yesu kulawa kila buga. Lunhu mkulu viluitig'hane hamoja, Yesu kalulongela lusimo luno.
5 "Kukala na munhu kachola kuhanda mbeyu mumgunda wake. Viyakalile komiza izimbeyu, mbeyu ziyagwe zilagalila mnzila, wanhu wazibojoga, na ndege wazija.
6 Mbeyu ziyagwe zilagalila mdibwe hali na udongo kidogo. Vizotile, zinyala kwavija udongo ukala waduhu unyefu.
7 Mbeyu ziyagwe zilagalila mna ivisolo va miba. Miba ikula na izizonga zimbeyu.
8 Mbeyu ziyagwe zilagalila mna udongo unogile. Zikula na kulela mbeyu nyingi kubanza zija zihandigwe, kila mbeyu ilela miyanza malongo longo."
Yesu viyalongile avo, kalonga kwa sauti ng'hulu, "Munhu yeli na magwiti, yahulike!"

*Simo zotufunza choni*
*Mat 13:10-17; Mlk 4:10-12*

9 Wanahina zake Yesu wamuuza fambulo da lusimo luno.
10 Yesu kawedika, "Mweye mutendigwa kuzijuwa mbuli zifisigwe za Undewa wa Mulungu. Lakini kwa wanhu wayagwe, nolonga kwa simo, muladi walole lakini sekewone, na wategeleze lakini sekewajuwe.

*Yesu kofambula lusimo lwa muhandaji*
*Mat 13:18-23; Mlk 4:13-20*

11 "Dino ijo fambulo da muhandaji, mbeyu ni mbuli ya Mulungu.

12 Zija zilagalile mnzila zolagusa wanhu waja iwohulika mbuli ya Mulungu, lakini Mwenembago kokwiza na kuisola mbuli ayo mmizoyo yao muladi waleke kutogola na kukomboligwa.

13 Mbeyu zilagalile mdibwe zolagusa wanhu waja wohulika mbuli ya Mulungu na kuibokela kwa kudeng'helela, lakini mbuli ayo haika mizizi mgati mmwao. Woitogola kwa kipindi kidodo, lakini wahagezigwa woileka mbuli ayo.

14 Mbeyu zilagalile mvisolo va miba zolagusa wanhu waja wohulika mbuli ya Mulungu, lakini viwogendelela, Mbuli ayo yozongigwa zongigwa na magayo, na utajili, na kudeng'helela vinhu va mwiisi. Wanhu awo hawalela bule matunda gonda gakangale.

15 Lakini mbeyu zilagalile hali na udongo unogile zolagusa wanhu waja iwohulika mbuli ya Mulungu na kuika mmizoyo yao na kuitogola, wofunga umoyo mbaka wolela matunda.

### *Taa kigubikigwe*
### *Mlk 4:21-25*

16 “Wanhu hawabwinha taa kuigubika na kikalango hebu kuika muuvungu wa lusazi. Lakini woika hana ikingolobweda, muladi wanhu viwokwingila wone mulenge.

17 “Kinhu chochose kifisigwe chokwikigwa hanhu hazelu, na kinhu chochose kigubikigwe chojuwika na kugaligwa hana umulenge.

18 “Avo muiteganye na gaja gomuhulika, kwavija munhu yeli na kinhu kokongezeligwa, lakini ija yeliduhu kinhu kobokigwa hata kija kidodo kiyogesa kanacho.”

### *Mamake na ndugu zake Yesu*
### *Mat 12:46-50; Mlk 3:31-35*

19 Mamake na ndugu zake Yesu wamcholela, lakini hawadahile kumvikila habehi mbuli ya lunhu lwa wanhu.

20 Munhu imoja kamulongela Yesu, “Mamako na ndugu zako wema kunze, wolonda kukona.”

21 Yesu kawalongela wanhu wose, “Mamangu na ndugu zangu ni waja woihulika mbuli ya Mulungu na kuitenda.”

### *Yesu kodihoza beho kulu*
### *Mat 8:23-27; Mlk 4:35-41*

22 Siku dimoja Yesu kakwela mwiingalawa hamoja na wanahina zake, kawalongela, “Tuloke umwambu.” Avo wasonga umwanza.

23 Viwakalile muumwanza, Yesu kawasa. Bahaja nyukwanyukwa da beho disonga kubuma mna idilamba, na ngalawa isonga kumema mazi, avo wose wakala mdizumozumo.

24 Wanahina wamgendela Yesu wamulamusa, wamulongela, “Go mkulu! Go mkulu! Tofa!”

Yesu kalamuka, kadikomhokela beho na ng'humbi ya mazi. Vose vinyamala na kukala tuluu.

25 Abaho kawalongela wanahina zake, “Tamanilo jenu da kwahi?”

Lakini awo wakanganya na kudumba, wailongela, “Ino munhu gani? Kodikomhokela beho na ng'humbi, navo vomuhulka!”

### *Yesu komulava munhu vinyamkela*
### *Mat 8:28-34; Mlk 5:1-20*

26 Yesu na wanahina zake wavika kuna imhwani ya isi ya Wagelasi, muumwambu wa lamba kulawa Galilaya.

[27] Viyahumuluke mwiingalawa, kamting'hana munhu imoja yeli na vinyamkela, yalawile kudibuga. Miyaka mingi munhu ayo kakala havala kiwalo wala hasinya ukayake, lakini kakala yokala kuna gamapanga.

[28] Viyamone Yesu, kaibwanha mmagulu ga Yesu, kaguta mizangi yolonga, “Gweye Yesu! Mwana wa Mulungu yeli Uchanha Ng'hani! Kolonda kunitenda choni? Nokupula, sekeunidununze!”

[29] Kalonga avo kwavija Yesu kakala yamulagize ikinyamkela yamulawe munhu ayo. Miyanza mingi kinyamkela ayo kakala yomkumba munhu ayo. Hamoja wanhu wakala womgodeka mng'anda kuno makono gake na magulu gake gagodekigwa minyololo na mhingu, lakini kakala yokanha, na kinyamkela ayo kakala yomkimbiza mbaka kuluwala.

[30] Yesu kamuuza munhu ija, “Twaga jako nani?”

Kamwidika, “Twaga jangu Lunhu.” Kalonga avo kwavija vinyamkela wengi wakala wamkumbile.

[31] Vinyamkela waja wampula Yesu sekeyawagale kuna dikolombo dikulu.

[32] Habehi na aho kukala na bumbila kulu da nguluwe wakalile woja kukigongo. Avo vinyamkela wampula Yesu yawatogolele wawakumbe nguluwe. Yesu kawatogolela.

[33] Vinyamkela wamulawa munhu ija, wawengila nguluwe. Bumbila jose da nguluwe dihumulukila mwiingema ya idilamba, wengila mdilamba, wose wafa mgamazi.

[34] Wanhu wakalile wowadima nguluwe awo wachona acho kilawilile, wakimbila na wazibwililisa mbuli azo kudibuga na mvijiji.

[35] Wanhu wachola kulola kija kilawilile. Viwavikile kwa Yesu, wamona munhu ija yalavigwe vinyamkela kakala mmagulu ga Yesu, kavala viwalo, kana nzewele zake. Wanhu wose wadumba.

[36] Na waja wayonile mbuli ayo, wawalongela wanhu vija munhu ayo yakalile na vinyamkela viyahonyigwe.

[37] Abaho wanhu wose wa isi ija ya Wagelasi wampula Yesu yalawanye, kwavija wakala wadumbile ng'hani. Avo Yesu kakwela mwiingalawa na kulawanya.

[38] Munhu ija yalavigwe vinyamkela kampula Yesu wachole wose.

Lakini Yesu hamtogolele, kamulongela,

[39] “Bwela ukayako ukawalongele wanhu gose gayakutendele Mulungu.”

Avo munhu ija kachola kila hanhu kudibuga dija, kawapetela wanhu mbuli zose ziyatendeligwe na Yesu.

### *Mndele wa Yailo na mtwanzi yakwasile kiwalo cha Yesu*
### *Mat 9:18-26; Mlk 5:21-43*

[40] Yesu viyabwelile mwambu uyagwe wa lamba, wanhu wambokela kwa deng'ho kwavija wose wakala wombeta.

[41] Abaho keza munhu imoja, twaga jake Yailo. Munhu ayo kakala mkulu wa ng'anda ya kumpula Mulungu. Kamfugamila Yesu, kampula yachole ukayake,

[42] kwavija mndele wake yeli yaiyeka kakala mmabehi kufa. Mndele ayo kakala na miyaka longo na mibili.

Yesu viyakalile kochola, wanhu wakala womsung'ha sung'ha kila mwambu.

[43] Mna dibumbila dija da wanhu, kukala na mtwanzi imoja yakalile na utamu wa kutumika kwa miyaka longo na mibili. Kakala yamambukize vinhu vake vose kwa waganga, lakini kuduhu munhu yadahile kumuhonya.

[44] Mtwanzi ija kamcholela Yesu kukisogo, kakwasa mhindo ya kiwalo cha Yesu, bahaja kutumika kuleka.

45 Yesu kauza, “Nani yanikwasile?”
Wanhu wose wabela. Petulo kalonga, “Go mkulu, wanhu wose wakuzun-
guluka na kukusung'ha sung'ha.”
46 Lakini Yesu kalonga, “Kuna munhu kanikwasa, kwavija nihulika nguvu
zinilawa.”
47 Mtwanzi ija viyone hadaha kuifisa, keza yogwaya, kaibwanha mmagulu
ga Yesu. Baho mgameso ga wanhu, kamulongela Yesu habali kakwasa
mhindo ya kiwalo chake, na vija viyahonyigwe bahaja.
48 Yesu kamulongela, “Mwanangu, kutamanila kwako kukuhonya. Chola
moyo uholile.”
49 Yesu viyakalile yang'hali yolonga, msenga kulawa ukayake Yailo keza,
kamulongela Yailo, “Mndele wako kamala kufa, avo sekeumgaze Mfundiza.”
50 Lakini Yesu viyahulike avo, kamulongela Yailo, “Sekeudumbe, gweye
togola tu, mndele wako kohona.”
51 Viyavikile kuna ing'anda ya Yailo, Yesu kawagomesa wanhu
sekewengile hamoja nayo, ila kengila na Petulo na Yohana, na Yakobo
na tatake na mamake mndele ayo.
52 Wanhu wose wakala wolila na kumuyalalila imwana. Yesu kawalon-
gela, “Sekemulile, kwavija imwana hafile bule, kawasa tu!”
53 Wanhu wose wamseka kwavija wakala wajuwile imwana kakala yafile.
54 Lakini Yesu kamgoga mkono, kamulongela, “Mwanangu, lamuka!”
55 Ugima wake umbwelela mndele ija, bahaja kalamuka. Abaho Yesu
kawalagiza wamgwee lujo.
56 Tatake na mamake wakanganya ng'hani, lakini Yesu kawagomesa seke-
wamulongele munhu yoyose kija kilawilile.

# 9

### *Yesu kowatuma wanahina zake longo na wabili*
### *Mat 10:5-15; Mlk 6:7-13*

1 Yesu kawakema hamoja wanahina zake longo na wabili, kawagwaa
nguvu na udahi wa kulava vinyamkela na kuwahonya watamu.
2 Abaho kawatuma wachole wakawapetele wanhu usenga wa Undewa wa
Mulungu na kuhonya watamu.
3 Kawalongela, “Sekemusole kinhu chochose muumwanza wenu. Seke-
musole mkongoja, wala mkoba, wala lujo, wala sente, wala viwalo vibili.
4 Ng'anda yoyose yonda mwingile na kugonekigwa, kaleni mumo mbaka
vonda musegele mna idibuga dijo.
5 Wanhu wahalema kuwabokela, segeleni buga dijo na kung'huseni timb-
wisi dili mmagulu genu kiwe kilaguso kamba wawatendela nzambi.”
6 Wanahina wafunga mwanza, wabitila vijiji vose wowapetela wanhu
Mbuli Inogile na kuwahonya wanhu kila hanhu.

### *Helode konyawanyawa*
### *Mat 14:1-12; Mlk 6:14-29*

7 Helode yakalile mndewa wa Galilaya, kahulika mbuli zose ziyatendile
Yesu. Kanyawanyawa ng'hani, kwavija wanhu wakala wolonga Yohana
Mbatizaji kazilibuka kulawa kwa wafile.
8 Wanhu wayagwe walonga Eliya kalawilila, wayagwe walonga imoja wa
watula ndagu wa Mulungu wa umwaka kazilibuka kulawa kuna iwanhu
wafile.
9 Lakini Helode kalonga, “Yohana nimkanha dipala, vino ino ayo nani
inihulika mbuli zake?” Nayo kalonda kumona Yesu.

### *Yesu kowagwaa lujo wanhu wengi*
*Mat 14:13-21; Mlk 6:30-44; Yoh 6:1-14*

10 Watumigwa waja viwabwelile, wamulongela Yesu kila kinhu waki-
tendile. Yesu kawasola, kachola nao waiyeka kuna dibuga dikemigwe
Betisaida.
11 Lakini wanhu viwajuwile avo, wamkweleleza Yesu. Nayo kawabokela,
kalonga nao mbuli ya Undewa wa Mulungu na kawahonya waja wakalile
watamu.
12 Zuwa vidisongile kuhonga, wanahina longo na wabili wamcholela Yesu,
wamulongela, "Walongele wanhu wachole kuna ivijiji na migunda ilibehi
na hano wakazahile lujo na hanhu ha kuwasa, kwavija hano hatwili twa
kuluwala."
13 Lakini Yesu kawalongela, "Mweye wagweleleni lujo waje."

Lakini wao wamwidika, "Tuna magate matano na somba wabili tu.
Kolonda tuchole tukawagulile lujo lunhu lose luno?"
14 Wambigalo waiyeka wakalile hanhu aho wakala wovika elufu tano.

Yesu kawalongela wanahina zake, "Walongeleni wanhu wakale mna
ivibumbila va wanhu malongo matano."
15 Nao wanahina watenda vivo. Wanhu wose wakala hasi.
16 Abaho Yesu kagasola magate matano na somba wabili, kalola uchanha
kuulanga, kamgwaa nhogolwa Mulungu, kagabanzula gamagate na iwa-
somba, kawagwaa wanahina zake wawagwelele wanhu.
17 Wanhu wose waja na kwiguta. Wanahina zake wasola vigelo longo na
vibili vimemile vinhu visigale.

### *Petulo komtogola Yesu ayo Kilisito*
*Mat 16:13-19; Mlk 8:27-29*

18 Siku dimoja Yesu kakala yaiyeka kompula Mulungu. Wanahina zake
wamcholela, nayo kawauza, "Vino wanhu wolonga niye na nani?"
19 Wamwidika, "Wanhu wayagwe wolonga gweye kwa Yohana Mbatizaji,
wayagwe wolonga kwa Eliya, kuno wayagwe wolonga gweye kwa imoja wa
watula ndagu wa Mulungu wa umwaka yazilibuke kulawa kwa wafile."
20 Yesu kawauza, "Na mweye molonga niye na nani?"

Petulo kamwidika, "Gweye kwa Kilisito, wa Mulungu."
21 Abaho Yesu kawagomesa wanahina zake sekewamulongele munhu
yoyose mbuli ayo.

### *Yesu kolonga mbuli ya ifa yake*
*Mat 16:20-28; Mlk 8:30-9:1*

22 Vivija Yesu kawalongela, "Mwana wa Munhu kolondeka yadununzike
ng'hani, na kulemigwa na wavele na wakulu wa walava nhosa na wafundiza
Malagizo ga Musa. Kokomigwa lakini siku da kadatu kozilibuka."
23 Abaho Yesu kawalongela wanhu wose, "Munhu yoyose yolonda
kunikweleleza, yaileme mwenyego, yaidikwe msalaba wake kila siku,
yanikweleleze.
24 Kwavija munhu yoyose yolonda kuukombola ugima wake mwenyego
kowagiza, lakini munhu yoyose yowagiza ugima wake mbuli ya niye,
koukombola.
25 Vino munhu yahapata kila kinhu mwiisi, lakini kowagiza ugima wake,
munhu ayo kopata choni?
26 Kamba munhu konyonela kinyala niye na mafundizo gangu, Mwana wa
Munhu nayo yaheza muukulu wake na wa Tatake na wasenga wa kuulanga
wang'alile komonela kinyala munhu ayo.

27 Lakini nowalongela ukweli, wanhu wayagwe wemile hano honda wafe
mbaka wawone Undewa wa Mulungu."

*Yesu kogaluka ikihanga*
*Mat 17:1-8; Mlk 9:2-8*

28 Vizibitile siku nane toka yalonge mbuli azo, Yesu kawasola Petulo na
Yohana na Yakobo kachola nao kukigongo kumpula Mulungu.
29 Viyakalile kompula Mulungu, kihanga chake kigaluka, viwalo vake
vikala vizelu chuwee!
30 Bahaja wanhu wabili wakala aho wolonga nayo. Nao wakala Musa na
Eliya,
31 wakoneka muukulu, wakala wolonga na Yesu mbuli ya ifa yake yonda
yaimambukize ako Yelusalemu.
32 Petulo na wayage wakala wokuluza. Viwalamuke, wawona ukulu wa
Yesu na wanhu wabili wemile nayo.
33 Wanhu waja viwakalile wosegela, Petulo kamulongela Yesu, "Go mkulu,
vinoga tweye tukale hano! Tuzenge viheha vidatu, kimoja chako, kimoja cha
Musa na kimoja cha Eliya." Petulo kakala hajuwa bule kija kiyolonga.
34 Petulo yang'hali yolonga, wingu dilawilila, diwagubika na kungugu
jake, wanahina wadumba ng'hani wingu dijo vidiwagubike.
35 Sauti ilonga kulawa mdiwingu, "Ino ayo Mwanangu inimsagule.
Mtegelezeni!"
36 Sauti ayo viinyamale, Yesu kasigala yaiyeka. Wanahina wanyamala
tuluu, na kipindi kija hawamulongele munhu yoyose kija kiwone.

*Yesu komulava mbwanga imoja kinyamkela*
*Mat 17:14-18; Mlk 9:14-27*

37 Imitondo yake Yesu na wanahina zake wadatu wahumuluka kukigongo.
Lunhu mkulu lwa wanhu luiting'hana na Yesu.
38 Munhu imoja mna ulunhu kaguta, "Mfundiza! Nokupula undolele
mwanangu, mwanangu yeli yaiyeka!
39 Kinyamkela komkumba na komtenda yagute nyangi, komgela kisango
kuno kolawa miholovu mumulomo. Kogendelela kumulumiza na hamuleka
hima bule!
40 Niwapula wanahina zako wamulave kinyamkela ayo, lakini
hawadahile bule."
41 Yesu kawalongela, "Mweye lukolo luliduhu kutamanila na lwagile!
Nokala na mweye mbaka lini? Nogela kitumbe kumgongo mbaka lini?"
Abaho kamulongela munhu ija, "Mgale hano mwanago."
42 Mbwanga ija viyakalile komwizila Yesu, kinyamkela kambwanha hasi
na kamgela kisango. Lakini Yesu kamkomhokela kinyamkela, kamuhonya
mbwanga ija, na kamgwaa tatake.
43 Wanhu wose wakanganya kwa udahi mkulu wa Mulungu.

*Yesu kolonga kabili mbuli ya ifa yake*
*Mat 17:22-23; Mlk 9:30-32*

Wanhu viwakalile wang'hali wokanganya mbuli ziyatendile Yesu, Yesu
kawalongela wanahina zake,
44 "Sekemuisemwe mbuli inilonda kuwalongela! Mwana wa Munhu
kogeligwa mmakono ga wanhu."
45 Lakini wanahina zake hawajuwile fambulo da ulonzi awo. Ukala
ufisigwe kumwao avo hawadahile kuujuwa, nao wadumba kumuuza Yesu.

### *Nani yeli munhu mkulu?*
*Mat 18:1-5; Mlk 9:33-37*

46 Wanahina wa Yesu wasonga kuibamilila wao kwa wao nani yeli munhu mkulu viweli.
47 Yesu kakijuwa kiwakalile wogesa, kamsola mwana mdodo, kamwika behi nayo.
48 Abaho kawalongela wanahina zake, “Munhu yoyose yombokela mwana ino kwa twaga jangu, konibokela niye, na munhu yoyose yombokela niye, kombokela ija yanhumile. Kwavija munhu yeli mdodo vimwili, ayo munhu mkulu kubanza wose.”

### *Munhu hamwihilani mweye miyenu*
*Mlk 9:38-40*

49 Yohana kamulongela Yesu, “Mndewa, tumona munhu kolava vinyamkela kwa twaga jako. Tumgomesa kwavija halawa mkibumbila chetu.”
50 Yesu kamulongela Yohana na wanahina wayagwe, “Sekemumgomese, kwavija munhu yoyose hamwihilani mweye miyenu.”

### *Wanhu wa kijiji cha Samalia wolema kumbokela Yesu*

51 Kipindi cha Yesu kugaligwa kuulanga vikikalile mmabehi, kaganga-
mala, kachola Yelusalemu.
52 Kawatuma wasenga wamulongolele wachole kuna ikijiji kili mwiisi ya
Samalia kumtandila kila kinhu.
53 Lakini wanhu wa kijiji cha Samalia hawambokele Yesu, kwavija wa-
juwa kamba kakala kochola Yelusalemu.
54 Wanahina zake, Yakobo na Yohana viwone avo, walonga, “Mndewa,
kolonda tulagize moto kulawa kuulanga uwasakaze wose?”
55 Yesu kahinduka kawakomhokela. Kawalongela, “Hamujuwile bule loho
gani imulinayo, kwavija Mwana wa Munhu hezile kuubananga ugima wa
wanhu lakini keza kuukombola.”
56 Abaho Yesu na wanahina zake wachola kuna ikijiji kiyagwe.

### *Wanhu wofaya kumkweleleza Yesu*
*Mat 8:19-22*

57 Viwakalile mnzila, munhu imoja kamulongela Yesu, “Nokukweleleza
kokose konda uchole.”
58 Yesu kamulongela, “Vizongo wana mhango na ndege wana mvulu,
lakini Mwana wa Munhu kaduhu hanhu ha kubwihila na kutambalala.”
59 Yesu kamulongela munhu iyagwe, “Nikweleleze.”
Lakini munhu ija kalonga, “Go mkulu, beta tanhu mbwele ukae hamzike
tatangu.”
60 Yesu kamwidika, “Waleke wanhu wafile wawazike wanhu wafile
wayao. Lakini gweye chola ukawapetele wanhu Undewa wa Mulungu.”
61 Munhu iyagwe kalonga, “Go mkulu, nokukweleleza, lakini beta tanhu
halulage lukolo lwangu.”
62 Yesu kamulongela, “Munhu yoyose yokwaluka kulima abaho kolola
kukisogo, hafaya Muundewa wa Mulungu.”

## 10

### *Yesu kowatuma wanhu malongo saba na wabili*

1 Abaho Mndewa Yesu kawasagula wanhu wayagwe malongo saba na wabili, kawatuma wabili wabili wamulongolele kila kijiji na kila hanhu kuyalondile kuchola.

2 Kawalongela, “Kuna ndiya nyingi lakini wasang'hanaji wadodo. Mpu-
leni Mndewa wa indiya yawatume wasang'hanaji mumgunda wake.
3 Gendeni! Nowatuma mweye kamba ng'hondolo mna iwambwizi.
4 Sekemusole mfuko hebu mkoba hebu vilatu. Sekemwime na kumula-
musa munhu yoyose mnzila.
5 Ng'anda yoyose yonda mwingile, tanhu mulonge, ‘Tindiwalo dikale
mng'anda ino.’
6 Kamba hana munhu kodinogela tindiwalo, tindiwalo jenu dokala nayo,
kamba kuduhu munhu yodinogela tindiwalo, tindiwalo jenu dowabwelela.
7 Mkale mng'anda ayo, diyeni na kung'wa chochose chonda wawagwelele,
kwavija msang'hanaji kolondeka yapate malipo gake. Sekemuhamehame
kulawa ng'anda imoja kuchola iyagwe.
8 Buga jojose donda mwingile na kubokeligwa, diyeni vija vonda wawag-
welele.
9 Wahonyeni watamu weli kuko, na muwalongele, ‘Undewa wa Mulungu
wa behi yenu.’
10 Lakini buga jojose donda mwingile na wanhu wolema kuwabokela,
laweni mumo, na vimubita kuna zinzila zao, mulonge,
11 ‘Hata matimbwisi ga buga jenu gatunanahile mmagulu getu to-
gakung'husa kiwe kilaguso kumwenu kamba mututendela gehile. Lakini
mujuwe kamba Undewa wa Mulungu wa mmabehi!’
12 Nowalongela ukweli, mna isiku ya nhaguso, Mulungu kolagusa bazi
ng'hani kwa wanhu wa buga da Sodoma kubanza wanhu wa buga dijo!

### *Mabuga golema kutogola*
### *Mat 11:20-24*

13 “Kogaya gweye buga da Kolazini! Kogaya gweye buga da Betisaida!
Maza unzonza utendigwe kumwenu mweye wahatendigwe mna gamabuga
ga Tilo na Sidoni, wanhu zake wahalekile mwaka nzambi zao na kuvala
magunia na kuibakaza mitozi, kulagusa kamba waleka nzambi!
14 Mwiisiku ya nhaguso, Mulungu kolagusa bazi ng'hani kwa wanhu wa
mabuga ga Tilo na Sidoni kubanza mweye.
15 Gweye buga da Kapelinaumu, vino kolonda kuinula mwenyego mbaka
uchanha kuulanga? Mawe! Kohumulusigwa mbaka kowochola wanhu
wafile!”
16 Yesu kawalongela wanahina zake, “Munhu yoyose yowategeleza mw-
eye, konhegeleza niye, na yoyose yowalema mweye, kondema niye. Na
munhu yoyose yondema niye, komulema ija yanhumile.”

### *Kubwela kwa waja malongo saba na wabili*

17 Abaho wanhu waja malongo saba na wabili wabwela kuno
wodeng'helela. Walonga, “Mndewa, hata vinyamkela watutegeleza
vituwakomhokele kwa twaga jako!”
18 Yesu kawedika, “Nimona Mwenembago kolagala kulawa kuulanga
kamba lumwesa.
19 Tegelezeni! Niwagwaa udahi, avo modaha kukanyaga mgendela hasi
na inge na kuzihuma nguvu zose za Mwenembago. Kuduhu kinhu chonda
kiwalumize.
20 Lakini sekemudeng'helele kwavija vinyamkela wowategeleza, ila
deng'heleleni kwavija matwaga genu gandikigwa kuulanga.”

### *Yesu kodeng'helela*
### *Mat 11:25-27; 13:16-17*

21 Kipindi kija Yesu kadeng'helela kwa udahi wa Loho Yang'alile, kalonga,
“Tata, Mndewa wa kuulanga na mwiisi! Nokutogola kwavija kuwafisa
mbuli zino wanhu weli na nzewele na ubala, na kuwagubulila wana
wadodo. Ona, Tata, vino vivo viulondile.
22 “Tatangu kanigwaa vinhu vose. Kuduhu munhu yamjuwile Mwana ila
Tata yaiyeka, na kuduhu munhu yamjuwile Tata ila Mwana na waja wose
Mwana yawasagule kuwagubulila wamjuwe Tata.”
23 Abaho Yesu kawahindukila wanahina zake, kalonga nao kinyelegezi,
“Wamweda wanhu wose wovona vinhu vimona mweye!
24 Nowalongela ukweli, watula ndagu wengi wa Mulungu na wandewa
walonda kuvona vimona mweye, lakini hawavonile bule, na vivija walonda
kuhulika vimuhulika mweye, lakini hawahulike bule.”

### *Lusimo lwa Msamalia yanogile*

25 Munhu imoja yagajuwile goya Malagizo ga Musa, kachola kwa Yesu
yamgeze. Avo kamuuza, “Mfundiza, vino nhende choni niupate ugima wa
mazuwa gose?”
26 Yesu kamwidika, “Vino, Malagizo golongaze na gweye kogajuwaze?”
27 Munhu ija kamwidika, “ ‘Mnogele Mndewa Mulungu wako kwa moyo
wako wose, na kwa loho yako yose, na kwa nguvu zako zose, na kwa nzewele
zako zose,’ na ‘Umnogele miyago kamba viuinogela mwenyego.’ ”
28 Yesu kamwidika, “Kulonga goya, tenda vivo na gweye kokuwa na
ugima.”
29 Lakini munhu ija kalonda kuilagusa kamba kanoga, avo kamuuza Yesu,
“Vino miyangu ayo nani?”
30 Yesu kamwidika, “Munhu imoja kakala kolawa Yelusalemu kochola
Yeliko. Mnzila, wabavi wamgoga, wamboka vinhu vake, na kumtowa,
wamuleka habehi na kufa.
31 Abaho mulava nhosa imoja kakala yohumuluka kubitila nzila iija.
Viyamone, kainega, kabitila kumgwazo.
32 Vivija Mlawi imoja viyavikile aho, kamulola munhu ija, nayo kainega,
kabitila kumgwazo.
33 Lakini Msamalia imoja yakalile muumwanza kavika aho hayakalile
munhu ija. Nayo viyamone, kamonela bazi.
34 Kamcholela, kamgela mavuta na divai mna ivilonda vake na kavifunga
goya. Abaho kamwika uchanha mwa mhunda wake, kamgala mbaka kuna
ing'anda ya wageni na kumulolesa goya.
35 Imitondo yake kalava sente kamgwaa mwene ng'anda, kamulongela,
‘Mulolese goya munhu ino. Chochose chonda umsang'hanile, nahabwela
nokugwaa fungu jako.’ ”
36 Abaho Yesu kamuuza, “Viukona gweye, mna iwanhu awo wadatu, nani
yakalile miyage munhu ija yatoigwe na wabavi?”
37 Munhu ija kamwidika, “Ija yamonele bazi.”
Yesu kamulongela, “Na gweye genda ukatende vivo.”

### *Yesu kowatembelela Mata na Malia*

38 Yesu na wanahina zake viwakalile mnzila, wengila kuna ikijiji kimoja.
Mtwanzi imoja twaga jake Mata kambokela ukayake.
39 Mata kakala na mdodo wake yakemigwe Malia, yakalile hasi behi na
magulu ga Yesu na kutegeleza mafundizo gake.
40 Lakini Mata kakala yohunganika na sang'hano nyingi ziyalondeke
kusang'hana, avo kamcholela Yesu, kamulongela, “Mndewa, vino hutonga

bule kamba mdodo wangu kanilekela sang'hano zose nisang'hane niiyeka? Mulongele yeze yanitaze!”

41 Lakini Mndewa kamwidika, “Gwee Mata gwee! Kohunganika na kugaya kwa vinhu vingi,

42 lakini kimoja kiiyeka kilondeka. Malia kasagula kinhu kinogile, na honda kisegezigwe bule kumwake.”

# 11

*Yesu kofundiza kumpula Mulungu*
*Mat 6:9-13; 7:7-11*

1 Siku dimoja Yesu kakala hanhu kompula Mulungu. Viyamambukize,
mwanahina wake imoja kamulongela, “Mndewa, tufundize kupula, kamba vija Yohana viyawafundize wanahina zake.”

2 Yesu kawalongela, “Mwahampula Mulungu, longeni vino.
‘Tataetu uli kuulanga.
Twaga jako ditogoligwe,
Undewa wako wize.
3 Utugwee lelo lujo lwa kila siku.
4 Uzigele kumgongo nzambi zetu,
kamba vija tweye vituzigela kumgongo nzambi za wanhu.
Sekeutwingize kuna ukugezigwa.’ ”

5 Abaho Yesu kawalongela wanahina zake, “Munhu gani kumwenu yeli na mbwiga yahamcholela kilo kikulu na kumulongela, ‘Mbwigangu, ng'hopeshe magate madatu,

6 kwavija mbwigangu keza, kalawa mwanza, na niye nabule lujo lwa kumgwaa!’

7 na ija yeli mng'anda yamwidike, ‘Sekeunigaze! Lwivi luhindigwa mwaka, na niye na wanangu tuwasa, avo sidaha kulamuka kukugwaa kinhu chochose.’

8 Nowalongela vino, hata yahalema kulamuka na kumgwaa magate kwavija mbwigake, lakini kwavija kaduhu kinyala kugendelela kumpula, kolamuka na kumgwaa kila kinhu kiyopula.

9 “Avo nowalongela, puleni na mweye mogweleligwa, zahileni na mweye movona, gong'ondeni ulwivi na mweye movugulilwa.

10 Kwavija waja wose wompula Mulungu wogweleligwa, na waja wozahila wopata, na lwivi lovuguligwa kwa munhu yoyose yogong'onda.

11 Vino kuna munhu yoyose kumwenu kamba mwanage yahampula somba, heyo komgwaa zoka?

12 Hebu yahampula finga komgwaa inge?

13 Kamba mweye wene nzambi mojuwa kuwagwaa wanenu vinhu vinogile, lakini Tataenu yeli kuulanga kowagwaa ng'hani Loho Yang'alile wanhu waja wompula.”

*Yesu na Belizebuli*
*Mat 12:22-30; Mlk 3:20-27*

14 Siku dimoja Yesu kakala komulava kinyamkela yamtendile munhu imoja yalemelwe kulonga. Kinyamkela ayo viyamulawile, munhu ija kasonga kulonga. Lunhu lwa wanhu lukanganya ng'hani,

15 lakini wanhu wayagwe walonga, “Belizebuli, mkulu wa vinyamkela, ayo yomgwaa udahi wa kulava vinyamkela.”

16 Wanhu wayagwe walonda kumgeza Yesu, avo wampula yatende kilaguso kulawa kuulanga.

17 Lakini Yesu kakijuwa kiwakalile wokigesa, avo kawalongela, “Undewa
wowose wahaigola mna ivibumbila na kuitowa, undewa awo wofa, na
lubuga lumoja lwahaigola, lubuga lulo lofa.
18 Avo kamba undewa wa Mwenembago wahaigola mvibumbila
na kuitowa, undewa awo wokwimaze? Mweye molonga niye nolava
vinyamkela kwavija Belizebuli konigwaa udahi wa kutenda vivo.
19 Kamba nolava vinyamkela kwa udahi wa Belizebuli, avo wanhu wenu
wolava vinyamkela kwa udahi wa nani? Kwa mbuli ayo wanhu wenu
wenyego wowatagusa kamba mobananga!
20 Lakini kamba nowalava vinyamkela kwa udahi wa Mulungu, avo
mujuwe kamba Undewa wa Mulungu uvika mwaka kumwenu.
21 “Munhu mwene nguvu viyokaliza ng'anda yake kwa silaha, vinhu vake
havisoligwa bule.
22 Lakini yaheza munhu mwene nguvu kubanza heyo, komtowa na ku-
muhuma, komboka silaha zake ziyatamanile na koigolela na wayage vija
viyasolile.
23 “Munhu yoyose heli ubanzi wangu konilema, na munhu yoyose yolema
kunitaza kwika hamoja, ayo kopwililisa.

*Kubwela kwa kinyamkela*
*Mat 12:43-45*

24 “Kinyamkela yahamulawa munhu, kochola mwiisi inyalile kuzahila
hanhu ha kubwihila. Yahaswela, koilongela, ‘Nobwela ukayangu kunilaw-
ile.’
25 Yahabwela na kuivika ng'anda ifagiligwa na kila kinhu kikigwa goya,
26 baho kobwela na kuwagala vinyamkela wayagwe saba wehile kubanza
heyo, awo wokwiza na kukala mumo. Avo ugima wa munhu ayo wokuwa
wiha kubanza aho haichanduso.”

*Deng'ho da kweli*

27 Yesu yang'hali yolonga, mtwanzi imoja kulawa kuna ulunhu kamulon-
gela kwa sauti ng'hulu, “Kamweda mtwanzi yakulelile na kukukong'heza!”
28 Lakini Yesu kamwidika, “Wamweda ng'hani wanhu wose wohulika
mbuli ya Mulungu na kuigoga!”

*Wanhu wolonda unzonza*
*Mat 12:38-42*

29 Wanhu viwakalile womsung'ha sung'ha, Yesu kagendelela kulonga,
“Lukolo luno lwa wanhu wotenda nzambi! Lolonda kilaguso, lakini kuduhu
kilaguso chochose chonda wagweleligwe, ila kilaguso cha Yona.
30 Kamba vija mtula ndagu wa Mulungu Yona viyakalile kilaguso kwa
wanhu wa Ninawi, vivo ili kwa Mwana wa Munhu vonda yawe kilaguso kwa
wanhu wa lukolo luno.
31 Mna isiku ya nhaguso, Malikia wa Sheba kokwima na kuwatagusa
mweye kamba mubananga, kwavija heyo kafunga mwanza kulawa mwiisi
yake kachola kumtegeleza Mndewa Sulemani na mafundizo gake geli na
nzewele. Nowalongela, hano hana munhu mkulu kubanza Sulemani.
32 Mna isiku ya nhaguso, wanhu wa Ninawi wokwima na kuwatagusa mw-
eye, kwavija awo waleka nzambi Yona viyawapetele. Lakini nowalongela,
hano hana munhu mkulu kubanza Yona!

*Mulenge wa lukuli*
*Mat 5:15; Mat 6:22-23*

33 “Kuduhu munhu yobwinha taa na kuigubika na kikalango, lakini koika
kukingolobweda, muladi wanhu wokwingila mng'anda wone mulenge.

34 Meso gako mulukuli lwako gaigala na taa. Kamba meso gako magima,
lukuli lwako lose lokuwa na mulenge, lakini meso gako gahabanangika,
lukuli lwako lose lokuwa mdiziza.
35 Muiteganye, mulenge uli mgati mmwenu sekeuwe ziza.
36 Kamba lukuli lwako lose lwahawa na mulenge, na kuduhu hanhu heli
na ziza, lukuli lwako lose lokuwa na lenge eka, kamba vija taa viimwemwesa
mulenge wake.”

### *Yesu kowalonga Mafalisayo na wafundiza Malagizo ga Musa*
*Mat 23:1-36; Mlk 12:38-40*

37 Yesu viyamambukize kulonga, Mfalisayo imoja kamgoneka ukayake
wakaje hamoja, avo Yesu kengila mng'anda, kakala hasi, kasonga kuja.
38 Mfalisayo ayo kakanganya ng'hani viyamone Yesu koja bila kusunha
makono gake.
39 Avo Mndewa kamulongela, “Mweye Mafalisayo mosunha vikasi na
sahani kwa kunze, lakini mgati mmwenu mmema ubokaji na gehile.
40 Mweye mwa wabozi! Vino siyo Mulungu yavitendile va kunze na va
mgati vivija?
41 Lakini laveni vili mgati na muwagwee wakiwa na kila kinhu chonoga
kumwenu.
42 “Mogaya mweye Mafalisayo! Kwavija momgwaa Mulungu fungu da
longo da majani gonung'hila goya kamba vija binzali na kalafuu, na mboga
ziyagwe, lakini moleka kutenda ganogile kwa wanhu na kumnogela Mu-
lungu. Molondeka kutenda gano na sekemugaleke gago gayagwe.
43 “Mogaya mweye Mafalisayo! Kwavija monogelwa kukala kuna ivigoda
va haulongozi mzing'anda za kumpula Mulungu na kulamusigwa mna
gamagulilo.
44 Mogaya mweye! Kwavija muigala na mapanga hagakoneka, wanhu
wobita uchanha bila kugajuwa.”
45 Munhu imoja yagajuwile goya Malagizo ga Musa kamulongela Yesu,
“Mfundiza, wahalonga avo, kotuliga tweye vivija!”
46 Yesu kamwidika, “Vivija mogaya mweye mugajuwile goya Malagizo ga
Musa! Kwavija mowapapiza wanhu mizigo mikulu, lakini mweye wenyego
hamulonda kugolosa makono kuwataza kupapa.
47 Mogaya mweye, kwavija mogazengela goya mapanga ga watula ndagu
wa Mulungu, waja wakomigwe na wahenga zenu.
48 Mweye wenyego mokitogola kija kiwatendile wahenga zenu, kwavija
wao wawakoma watula ndagu wa Mulungu, na mweye mogazengela goya
mapanga gao.
49 Kwa mbuli ayo, nzewele ya Mulungu ilonga, ‘Nowatuma watula
ndagu wa Mulungu na watumigwa, wayagwe wowakoma na wayagwe
wowadununza!’
50 Avo wanhu wa lukolo luno wotagusigwa mbuli ya kuwakoma watula
ndagu wose wa Mulungu, kulawa kuna ichanduso cha isi,
51 toka kukomigwa kwa Habili mbaka kukomigwa kwa Zakalia, ija
yakomigwe hagati ha upango wa kulavila nhosa na Hanhu Hong'ala. Ona,
nowalongela, wanhu wa lukolo luno wotagusigwa kwa kuwakoma wao!”
52 “Mogaya mweye wafundiza Malagizo ga Musa! Kwavija mofisa lu-
vugulo lwa kuvugulila lwivi lwa ng'anda ya kuifunzila. Mweye wenyego
hamwingila bule, abaho muwagomesa waja wakalile wolonda kwingila
sekewengile!”
53 Yesu viyasegele hanhu aho, wafundiza Malagizo ga Musa na Mafalisayo
wasonga kumulonga vihile na kumuuza mbuli nyingi,

54 wageza kumnamata kwa mbuli zake zonda yalonge.

# 12

*Yesu kowazuma wanhu mbuli ya unafiki*
*Mat 10:26-27*

1 Wanhu wengi waiting'hana hamoja mbaka wanhu wakala woikanyaga.
Tanhu Yesu kawalongela wanahina zake, "Iteganyeni na usasu wa Mafal-
isayo, nao ndo unafiki.
2 Kinhu chochose kigubikigwe chogubuligwa, na kija kifisigwe chojuwika.
3 Avo chochose kimulongile mdiziza chohulikigwa mmulenge, na cho-
chose kimunyong'onye mwiiyeka mdigati dihindigwe chopetigwa mkiswili.

*Ija wa kumdumba*
*Mat 10:28-31*

4 "Nowalongela mweye mbwiga zangu, sekemuwadumbe wanhu waja
woukoma lukuli, abaho hawadaha kutenda kinhu kiyagwe chochose kihile.
5 Lakini nowalagusila wa kumdumba, mdumbeni Mulungu, heyo ya-
hakoma, kana udahi wa kumwasa munhu muumoto wa jehanamu. Nowa-
longeleni, mdumbeni ayo!
6 "Vino nhongwa watano hawachuuzigwa kwa sente ndodo mbili? Lakini
kuduhu hata imoja yosemwigwa na Mulungu.
7 Hata mvili zili mmapala genu zipetigwa zose. Avo sekemudumbe.
Mweye munoga ng'hani kubanza nhongwa wengi!

*Kumtogola na kumulema Kilisito*
*Mat 10:32-33; 12:32; 10:19-20*

8 "Nowalongeleni ukweli, munhu yoyose yonitogola niye mgameso ga
wanhu, Mwana wa Munhu nayo komtogola mgameso ga wasenga wa Mu-
lungu.
9 Lakini munhu yoyose yonibela niye mgameso ga wanhu, Mwana wa
Munhu nayo kombela mgameso ga wasenga wa Mulungu.
10 "Munhu yoyose yomulonga vihile Mwana wa Munhu, nzambi zake zo-
geligwa kumgongo, lakini munhu yoyose yomuliga Loho Yang'alile, nzambi
zake honda zigeligwe kumgongo bule.
11 "Wahawagala haulongozi wa ng'anda za kumpula Mulungu, na
mgameso ga wakulu wa isi na wandewa, sekemunyawenyawe vija vonda
mwidike hebu kija chonda mulonge.
12 Kwavija Loho Yang'alile kowafundiza saa iija kimulondeka kulonga."

*Lusimo lwa tajili mbozi*

13 Munhu imoja muulunhu kamulongela Yesu, "Mfundiza, mulongele
ndugu yangu tuigolele uhazi wa tataetu."
14 Yesu kamwidika, "Mbwigangu, nani yanigwelele udahi wa kuwalamula
hebu kuwagolela uhazi wenu?"
15 Abaho kagendelela kuwalongela wose, "Muiteganye na ugila! Kwavija
ugima wa munhu hautamanila wingi wa vinhu viyalinavo."
16 Abaho Yesu kawalongela lusimo luno, "Kukala na munhu imoja yakalile
na mgunda uli na ndiya nyingi.
17 Kasonga kugelegeza mwenyego, 'Nabule hanhu hakwika ndiya yangu
yose. Nhendeze?'
18 Abaho kailongela, 'Notenda vino, nogatula makanho gangu na kuzenga
makulu ng'hani. Mumo nokwika ndiya yangu na vinhu vangu viyagwe.

19 Abaho noilongela, gweye moyo wangu! Kuna vinhu vose vinogile kwa miyaka heleketwaa. Bwihila, diya, ing'wa, na kudeng'helela!'
20 Lakini Mulungu kamulongela, 'Gweye kwa mbozi! Kilo cha lelo noulonda ugima wako, abaho vinhu vose vino viuikile vokuwa va nani?' "
21 Abaho Yesu kamambukiza kulonga, "Vino vivo ili kwa waja woikila vinhu vao wenyego, lakini haweka vinhu vao kwa Mulungu."

### *Kumtamanila Mulungu*
*Mat 6:25-34*

22 Abaho Yesu kawalongela wanahina zake, "Nowalongela, sekemulugaiye lujo lumulonda muladi muwe wagima, hebu viwalo vimulonda kwa ng'huli zenu.
23 Kwavija ugima unoga kubanza lujo, na lukuli lunoga kubanza viwalo.
24 Waloleni bondwa, hawahanda, hawasenga, waduhu makanho, lakini Mulungu kowadima! Vino Mulungu hawanogela ng'hani mweye kubanza iwabondwa?
25 Nani kumwenu kwa kuigaza ng'hani kodaha kwengeza hata saa dimoja da ugima wake?
26 Kumbe hamudaha kutenda mbuli ndodo kamba ino, habali moigaza kwa mbuli ziyagwe?
27 Loleni maluwa vigokula. Hagasang'hana hebu hagaisonela viwalo. Lakini nowalongela kweli, hata mndewa Sulemani, hamoja na utajili wake wose kakala kaduhu viwalo vinogile viigalile na maluwa gano.
28 Kamba Mulungu heyo yodivaza jani da kumuhulo, lelo dabahano na mayo dokwasigwa muumoto, vino hondayawavaze ng'hani mweye? Mweye wanhu mutamanila kidogo!
29 "Avo sekemuigaze moja choni, hebu mong'wa choni.
30 Kwavija vinhu avo, vivo voogaiya wanhu haweli Wayahudi. Tataenu yeli kuulanga kojuwa molonda vinhu vose avo.
31 Lakini uzahileni tanhu Undewa wa Mulungu, nayo kowagwaa vinhu avo.

### *Utajili wa kuulanga*
*Mat 6:19-21*

32 "Sekemudumbe mweye kibumbila kidodo cha wanahina zangu, kwavija Tataenu kanogelwa kuwagwaa mweye Undewa.
33 Chuuzeni vose vimulinavo na muwagwelele wakiwa zisente. Muitendele mikoba hailala, na muikile ngama yenu kuulanga. Ako hondaihunguke, kwavija kuduhu wabavi wodaha kuhavika na kuduhu ng'hobo wodaha kuibananga.
34 Kwavija kuko kuili ngama yako, vivija kuko kondauwe moyo wako.

### *Wasang'hanaji welimeso*

35 "Muitande na kuifunga mikwiji mvigudi, na taa zenu ziwe zokwaka,
36 kamba wasang'hanaji viwombetela mkulu wao yabwele kulawa kuna idizengele. Yahabwela na kugong'onda ulwivi, himahima womvugulila.
37 Wamweda wasang'hanaji waja mkulu wao yahabwela kowavika meso! Nowalongeleni ukweli, mkulu ayo kosaula koti jake, kowalongela wakale hasi muulujo nayo kowasang'hanila.
38 Wamweda wasang'hanaji waja mkulu wao kowavika wang'hali meso, hata kamba yahabwela kilo kikulu hebu nzogolo zikwika!
39 Lakini mujuwe vino, kamba mwene ng'anda yahajuwile saa ya kwiza mbavi, yahakalile meso, na sambi yaileke ng'anda yake ituligwe na mbavi.

40 Na mweye vivija molondeka mwiitande, kwavija Mwana wa Munhu
kokwiza mna isaa hamuigesile.”

### *Msang'hanaji yatamaniligwa na hatamaniligwa*
### *Mat 24:45-51*

41 Petulo kamulongela, “Mndewa, vino lusimo luno kutulongela tweye
twiiyeka, hebu kuwalongela wanhu wose?”
42 Mndewa kamwidika, “Vino msang'hanaji gani yotamaniligwa na yeli na
nzewele? Ayo ija mkulu wake komwika yalolese wasang'hanaji wayagwe,
na yawagwee lujo mna isaa inogile.
43 Kamweda msang'hanaji ija mkulu wake yahabwela komvika
kosang'hana vivo!
44 Nowalongela ukweli, mkulu wake komwika msang'hanaji ayo yawe
mulolesaji wa vinhu vake vose.
45 Lakini msang'hanaji ija yahailongela mwenyego, ‘Mkulu wangu
kokawa ng'hani kubwela.’ Baho kosonga kuwatowa wasang'hanaji
wayagwe, wa kitwanzi na wa kimbigalo, kuno koja na kung'wa mbaka
kokoligwa.
46 Abaho mkulu wake kobwela mna isiku msang'hanaji ija haigesile na
mna isaa haijuwile bule. Mkulu ayo komtowa ng'hani na kumwika hamoja
na wanhu hawatogola.
47 “Msang'hanaji ija yajuwile kija kiyolonda mkulu wake yakisang'hane,
lakini hakisang'hana bule msang'hanaji ayo kotowigwa ng'hani.
48 Lakini msang'hanaji ija hakijuwile kiyolonda mkulu wake, abaho
kotenda kinhu kihile, msang'hanaji ayo kotowigwa kidogo. Munhu yag-
weleligwe vingi kodaigwa vingi, na munhu yagweleligwe vingi ng'hani
kodaigwa vingi ng'hani.

### *Yesu kowatenda wanhu waigole*
### *Mat 10:34-36*

49 “Niza kubwinha moto mwiisi, vinondile niye wahakile mwaka!
50 Nina ubatizo nolondigwa niubokele, na niye nougaiya ng'hani mbaka
umale!
51 Vino mweye mogesa niza kugala tindiwalo mwiisi? Bule! Sizile kugala
tindiwalo, lakini kuwagola wanhu.
52 Kulawa sambi, wanhu watano wa ng'anda imoja woigola, wadatu kwa
wabili, na wabili kwa wadatu.
53 Tata koigola na mwanage, na mwana koigola na tatake. Mama koigola
na mndele wake, na mndele koigola na mamake. Mama mkwe koigola na
mkwe wake wa kitwanzi, na mkwe wa kitwanzi koigola na mama mkwe
wake.”

### *Kujuwa vipindi*
### *Mat 16:2-3*

54 Yesu kawalongela wanhu kabili, “Mwahajona wingu dolawilila
mwambu wa kudihongela zuwa, baho molonga, ‘Mvula kotowa,’ na kweli
kotowa.
55 Na mwahajona beho da kusini nyukwanyukwa molonga, ‘Hokuwa na
joto,’ na yokuwa vivo.
56 Mweye mwa wanafiki! Modaha kulola isi na ulanga na kulagula kamba
mvula kotowa hebu hatowa, habali hamujuwile fambulo da kipindi kino?

### *Ilumbe na munhu yakwihile*
### *Mat 5:25-26*

57 “Habali hamudaha kujuwa wenyego mbuli zinogile za kusang'hana?

58 Kamba munhu kokugala mkitala, vinoga uilumbe nayo mung'hali mnzila. Wahalemelwa, kokugala kwa msemi, nayo msemi kokugala mmakono ga wakalizi, nao wokugodeka mkifungo.
59 Nokulongela, mumo humulawa ng'o, mbaka ulipe sente yose!”

# 13

*Lekeni nzambi buleavo mofa*

1 Kipindi kikija wanhu wayagwe wakala aho, wamulongela Yesu mbuli ya Wagalilaya wakomigwe na Pilato kipindi viwakalile womulavila nhosa Mulungu.
2 Yesu kawedika, “Vino mogesa Wagalilaya awo wakala na nzambi nyingi kubanza Wagalilaya wayagwe lekaavo wadununzika vivo?
3 Bule! Nowalongela kweli, na mweye vivija mwahalema kuleka nzambi zenu, mose mofa kamba awo.
4 Hebu mogesa wanhu waja longo na wanane wafile kwa kulagaliligwa na lingo ako Siloamu wakala na nzambi nyingi kubanza wanhu wose kudibuga da Yelusalemu?
5 Bule! Nowalongela, mwahalema kuleka nzambi, mose mofa kamba awo.”

*Lusimo lwa mbiki wa matunda haulela*

6 Abaho Yesu kawalongela lusimo luno, “Munhu imoja kahanda mbiki wa matunda mumgunda wake wa mizabibu. Kachola kuzahila matunda, lakini hapatile tunda jojose bule.
7 Avo kamulongela msang'hanaji wake, ‘Lola, mwaka uno wa kadatu nokwiza hano kuzahila matunda mumbiki uno, lakini sipata chochose. Ukanhe! Habali ugendelele kuibananga isi?’
8 Lakini msang'hanaji wake kamwidika, ‘Go mkulu, uleke mwaka uno uiyeka, nouhalilila na kuwikila mbolea.
9 Abaho kamba wahalela yokuwa goya, lakini wahaleka kulela, kodaha kuukanha!’ ”

*Yesu komuhonya mtwanzi siku ya Kubwihila*

10 Siku dimoja da Kubwihila, Yesu kakala yofundiza mng'anda ya kumpula Mulungu.
11 Baho kukala na mtwanzi imoja. Mtwanzi ayo kakala na kinyamkela yamtendile yalumwe miyaka longo na nane. Kakala yaveduke mgongo na hadahile kuigolosa bule.
12 Yesu viyamone, kamkema, kamulongela, “Mama, kuhonyigwa utamu wako!”
13 Yesu kamwikila makono, bahaja lukuli lwake lugoloka, nayo kamgwaa nhogolwa Mulungu.
14 Lakini mkulu wa ng'anda ya kumpula Mulungu kagevuzika kwavija Yesu kamuhonya munhu mwiisiku ya Kubwihila. Avo kawalongela wanhu, “Mnazo siku sita za kusang'hana. Mzisiku azo, mwize muhonyigwe, lakini sekemwize kudisiku da Kubwihila!”
15 Mndewa kamwidika, “Mweye mwa wanafiki! Vino, nani kumwenu yoleka kumfungula ng'ombe wake hebu mhunda wake kulawa mdizizi na kumulongoza yachole kung'wa mazi mwiisiku ya Kubwihila?
16 Mtwanzi ino kolawa mulukolo lwa Abulahamu. Nayo kakala yagogigwe na Mwenembago kwa miyaka longo na nane. Vino halondeke kulekesigwa mwiisiku ya Kubwihila?”

[17] Mbuli azo ziyalongile Yesu ziwatenda waja wamwihile wagwe kinyala, lakini wanhu wayagwe wakala wodeng'helela kwa mbuli zose za unzonza ziyasang'hane Yesu.

### *Lusimo lwa mbeyu ndodo ya haladali*
*Mat 13:31-32; Mlk 4:30-32*

[18] Abaho Yesu kawauza, "Vino Undewa wa Mulungu uigala na choni? Vino niusimulile kwa lusimo gani?
[19] Uigala na kija kilawilile kwa munhu yasolile mbeyu ndodo ya haladali na kuihanda mumgunda wake. Mbeyu ayo yota na kuwa mbiki mkulu, na ndege wazenga mvulu zao mna gamatambi gake."

### *Lusimo lwa mela*
*Mat 13:33*

[20] Yesu kawauza kabili, "Vino Undewa wa Mulungu uigala na choni?
[21] Uigala na kija kilawilile kwa mtwanzi yasolile mela na kuditibwiliza hamoja na madebe mabili ga usage, abaho usage wose ugongomoka."

### *Mulango msisili*
*Mat 7:13-14, 21-23*

[22] Yesu kagendelela na mwanza wake kuchola Yelusalemu, kubitila kuna gamabuga na vijiji kowapetela wanhu.
[23] Munhu imoja kamuuza, "Go mkulu, vino wonda wakomboligwe wanhu wadodo waiyeka?"
Yesu kawedika,
[24] "Gangamaleni mwingile kubitila ulwivi msisili, kwavija wanhu wengi wolonda kwingila lakini honda wadahe bule.
[25] Mwene ng'anda kokwinuka na kuhinda ulwivi. Mweye mokwima kunze na kusonga kugong'onda ulwivi molonga, 'Mndewa, tuvugulile!' Nayo kowedika, 'Sikujuwile kumulawa!'
[26] Mweye momwidika, 'Tuja na kung'wa hamoja na gweye, na gweye kutufundiza kudibuga jetu!'
[27] Lakini heyo kolonga kabili, 'Sikujuwile kumulawa! Segeleni kumwangu, mweye mose mutenda nzambi!'
[28] Baho molila na kudafuna meno mwahawona Abulahamu na Isaka na Yakobo na watula ndagu wose wa Mulungu muundewa wa Mulungu, kuno mweye wenyego mwasigwa kunze!
[29] Wanhu wokwiza kulawa mwambu wa kudilawila zuwa na mwambu wa kudihongela zuwa, kulawa mwambu wa kasikazini na mwambu wa kusini, wokala hasi muulujo muundewa wa Mulungu.
[30] Abaho wanhu waja weli wa ikimambukizo sambi wokuwa wa ichanduso, na waja weli wa ichanduso sambi wokuwa wa ikimambukizo."

### *Yesu koinogela Yelusalemu*
*Mat 23:37-39*

[31] Kipindi kikija Mafalisayo wayagwe wamcholela Yesu, wamulongela, "Segela hanhu hano uchole hanhu hayagwe, kwavija Helode kolonda kukukoma."
[32] Yesu kawedika, "Gendeni mkamulongele vino ija kizongo, 'Nolava vinyamkela na kuhonya watamu lelo na mayo, na siku da kadatu nomambukiza sang'hano yangu!'
[33] Hata avo lelo, mayo, na kisindo nogendelela na mwanza wangu, kwavija hailondeka mtula ndagu wa Mulungu yafile kunze ya buga Yelusalemu.
[34] "Gweye Yelusalemu! Gweye Yelusalemu! Kowakoma watula ndagu wa Mulungu na kuwatowa kwa mabwe waja Mulungu yawatumile kumwako!

Miyanza mingapi nilonda kuwahagata wanago kwa makono gangu, kamba vija nguku viyovihagata vinziya vake mna gamabawa gake, lakini hulondile bule!

35 Sambi lola, Ng'anda yenu ya Mulungu ilekigwa vihame! Na niye nowalongela, hondamumbone kabili mbaka siku dija vondamulonge, ‘Mulungu yamtambikile ija yokwiza kwa twaga da Mndewa!’ ”

# 14

*Yesu komuhonya munhu mtamu*

1 Mwiisiku imoja ya Kubwihila, Yesu kachola kuja lujo mng'anda ya mkulu imoja wa Mafalisayo, wanhu wakala womulola goya Yesu.

2 Munhu imoja yakalile na utamu wa kuvimba lukuli keza kwa Yesu.

3 Yesu kawauza wafundiza Malagizo ga Musa na Mafalisayo, “Vino, vinoga kumuhonya munhu mwiisiku ya Kubwihila hebu havinogile bule?”

4 Lakini wao hawalongile mbuli yoyose bule. Yesu kamsola mtamu ija, kamuhonya, abaho kamuleka yachole.

5 Abaho kawauza, “Vino nani kumwenu yeli na mwana hebu ng'ombe, yahadumbukila mdikolombo mwiisiku ya Kubwihila, hamulava mwiisiku ayo?”

6 Lakini wao hawadahile kumwidika mbuli ino.

*Uhole na moyo unogile*

7 Yesu kawona wanhu waja wagonekigwe viwakalile wosagula vigoda va kuulongozi. Avo kawalongela wose lusimo luno,

8 “Munhu yahakugoneka kuna idizengele, sekeukale mvigoda va haulongozi, kwavija kodaha kwiza munhu yagonekigwe yeli munhu mkulu kubanza gweye,

9 na munhu yawagoneke mose wabili kokwizila na kukulongela, ‘Segela aho haukalile umulekele miyago.’ Baho kogwa kinyala mgameso ga wanhu na kobwela kukala kuna ivigoda va kukisogo.

10 Lakini wahagonekigwa kuna ulujo, genda ukakale kuna ivigoda va kukisogo, muladi munhu yakugoneke yaheza yakulongele, ‘Mbwigangu, izo ukale kuna ivigoda va haulongozi.’ Baho kopata nhogolwa mgameso ga wanhu wose wagonekigwe.

11 Kwavija waja wose woitenda wenyego wanhu wakulu wotendigwa wanhu wadodo, na waja woitenda wenyego wanhu wadodo wotendigwa wanhu wakulu.”

12 Abaho Yesu kamulongela ija yamgoneke, “Kamba kowatanda wanhu lujo lwa imisi hebu lwa ichungulo, sekeuwagoneke mbwiga zako, hebu ndugu zako, hebu matajili hebu wanhu welibehi na gweye. Kwavija wahatenda avo, wao nao wokugoneka na avo wokulipa vija viuwatendele wao.

13 Lakini kamba wahatenda nyimwili nyimwili, wagoneke wakiwa,, mbetembete, waholole, na waja wasuwameso,

14 na gweye kotambikiligwa, kwavija awo hawadaha kukulipa. Mulungu kokulipa mwiisiku ya kuzilibuligwa kwa wanhu wanogile.”

*Lusimo lwa nyimwili nyimwili ng'hulu*
*Mat 22:1-10*

15 Munhu imoja mna iwaja wakalile muulujo viyahulike avo, kamulongela Yesu, “Wamweda waja wonda waje lujo lwa nyimwili nyimwili muundewa wa Mulungu!”

16 Yesu kamulongela, “Munhu imoja katenda nyimwili nyimwili ng'hulu, kawagoneka wanhu wengi.

17 Viivikile saa ya nyimwili nyimwili, kamtuma msang'hanaji wake
yakawalongele wanhu wagonekigwe weze, kwavija kila kinhu kitandigwa.
18 Lakini kila munhu kalava kitala chake. Munhu wa ichanduso kamulon-
gela msang'hanaji ija, ‘Nigula mgunda, avo nolondeka nikaulole. Chonde,
ndeka nyhole.’
19 Iyagwe kalonga, ‘Nigula ng'ombe longo wa kulimila, avo vino na
muumwanza, nochola kuwageza. Chonde, ndeka nyhole.’
20 Iyagwe kalonga, ‘Sambi sambi nisola mwehe, avo sidaha kwiza.’
21 “Msang'hanaji ija kabwela na kumulongela mbuli zose zino mkulu
wake. Mkulu wake kagevuzika ng'hani, kamulongela msang'hanaji wake,
‘Lopola ugende mzinzila mhanda na mna gamabuga, uwagale hano wanhu
wakiwa, waholole, wasuwameso na mbetembete.’
22 Bahaja msang'hanaji ija kamulongela, ‘Go mkulu, gago gose
gasang'hanigwa, lakini kuna gati disigala.’
23 Avo mkulu ija kamulongela msang'hanaji wake, ‘Lawa kunze uchole
mzinzila na mna gamakulugumbi ukawalongele wanhu weze, muladi
ng'anda yangu imeme.
24 Nowalongela kweli, kuduhu hata munhu imoja mna iwaja wag-
onekigwe walemile kwiza yonda yalanze lujo lwangu!’ ”

### *Kudununzika sama ya kuwa mwanahina*
*Mat 10:37-38*

25 Baho lunhu lwa wanhu vilukalile lomkweleleza, Yesu kahinduka, kawa-
longela,
26 “Munhu yoyose yokwiza kumwangu na kuno kowanogela ng'hani
tatake na mamake na mwehe wake na wanage na lumbu zake na ndugu
zake na vivija kamba kounogela ng'hani ugima wake mwenyego kubanza
kumnogela Kilisito, hadaha kuwa mwanahina wangu.
27 Na munhu yoyose haupapa msalaba wake na kunikweleleza, hadaha
kuwa mwanahina wangu.
28 “Vino nani kumwenu yahalonda kuzenga lingo, tanhu hakala hasi
na kugelegeza sente za kudizengela, muladi yajuwe kamba kana sente za
kumambukiza sang'hano yake?
29 Buleavo, yahamambukiza kuzenga chandusilo, kolemelwa kumambuk-
iza kuzenga dilingo, na wose wachone acho kilawilile womseka,
30 wolonga, ‘Munhu ino kasonga kuzenga, lakini kalemelwa kumambuk-
iza sang'hano yake!’
31 “Hebu mndewa gani yahaitanda kuchola kuitowa na mndewa iyagwe,
tanhu hakala hasi na kugelegeza kamba heyo na wakalizi zake elufu kumi
kodaha kuitowa na mndewa miyage yeli na wakalizi elufu ishilini?
32 Kamba yahona hadaha, kowatuma wasenga zake wakaiting'hane na
mndewa iyagwe, wampule wailumbe yang'hali kutali.”
33 Yesu kamambukiza kulonga, “Vivo ili kumwenu, kuduhu munhu yo-
daha kuwa mwanahina wangu mbaka yaleke kila kinhu kiyali nacho.

### *Mkele ubanangike*
*Mat 5:13; Mlk 9:50*

34 “Mkele unoga, lakini wahagiza ukali wake, kuduhu nzila ya kuubweza
kabili.
35 Haufaya kwa isi hebu mna imbolea, lakini wokwasigwa. Yeli na magwiti
yahulike!”

# 15

*Lusimo lwa ng'hondolo yapotele*
*Mat 18:12-14*

1 Siku dimoja wabokela kodi wengi na wanhu wayagwe wotenda nzambi
wachola kumtegeleza Yesu.

2 Mafalisayo na wafundiza Malagizo ga Musa wasonga kunung'unika,
“Munhu ino kowabokela wanhu wotenda nzambi na kuja nao!”

3 Avo Yesu kawalongela lusimo luno.

4 “Vino kamba imoja wenu kana ng'hondolo gana, abaho ng'hondolo
imoja kapotela, vino kotenda choni? Kowaleka waja malongo tisa na tisa
kuluwala, na kuchola kumzahila ija yapotele mbaka yampate.

5 Yahampata, kodeng'helela na kumwika mmaega gake,

6 na kumgala ukae. Abaho kowakema hamoja mbwiga zake na wanhu
weli behi nayo na kowalongela, ‘Miyenu nodeng'helela kwavija nimpata
ng'hondolo wangu yapotele. Avo tudeng'helele hamoja!’

7 Nowalongela, avo vondaiwe, hokuwa na ndeng'helelo ng'hulu kuulanga
mbuli ya munhu imoja mwene nzambi yahaleka nzambi zake, kubanza
waja malongo tisa na tisa wogesa wanoga na hawalonda kuzileka nzambi
zao.”

*Lusimo lwa sente ipotele*

8 “Hebu mtwanzi yeli na sente longo yahagiza imoja, kotendaze? Kob-
winha taa, kofagila ng'anda yake, na kulola goya kila hanhu mbaka yaipate.

9 Yahaipata, kowakema hamoja mbwiga zake na wanhu weli behi yake,
kowalongela, ‘Nodeng'helela ng'hani kwavija niipata sente yangu ipotele.
Avo tudeng'helele hamoja!’

10 Vivija nowalongela, wasenga wa Mulungu wodeng'helela mbuli ya
munhu imoja mwene nzambi yahaleka nzambi zake.”

*Lusimo lwa mwana yapotele*

11 Yesu kagendelela kulonga, “Kukala na munhu imoja yakalile na wana
wabili.

12 Ija imdodo kamulongela tatake, ‘Tata, nigwelele uhazi wangu sambi.’
Avo munhu ija kawagolela uhazi wao wanage awo wabili.

13 Hazibitile siku nyingi, ija imdodo kachuuza uhazi wake. Abaho kafunga
mwanza na sente ziyapatile, kachola isi ya kutali, ako kazinanga sente zose
ziyapatile.

14 Kamambukiza kila kinhu kiyakalile nacho. Abaho lufilili lwa nzala
lulawilila mwiisi ija, nayo kakala kaduhu kinhu chochose kisigale.

15 Avo kachola kusang'hana kibaluwa kwa munhu imoja wa isi ija, munhu
ayo kamtuma mumgunda wake yasusile nguluwe.

16 Kakala kosulukila kuja maganda gawadile nguluwe, lakini kuduhu
munhu yamgwelele kinhu chochose cha kuja.

17 Abaho kagelegeza na kulonga, ‘Tatangu kana wasang'hanaji wengi,
woja mbaka wosigaza na niye hano nofa na nzala!

18 Nosegela na kuchola kwa tatangu na kumulongela, Tata, nimtenda
Mulungu nzambi, na vivija nikutendela gweye nzambi.

19 Sifaya kukemigwa mwanago. Nhende kamba imoja wa wasang'hanaji
zako.’

20 Avo kafunga mwanza wa kubwela kwa tatake.

“Viyakalile yang'hali kutali, tatake kamona. Kamonela bazi mwanage, avo
kamkimbilila, kamuhagatila na kamnonela.

21 Mwanage kamulongela, ‘Tata, nimtenda Mulungu nzambi, na vivija nikutendela gweye. Sifaya kukemigwa mwanago.’
22 Lakini tatake kawakema wasang'hanaji zake. Kawalongela, ‘Lopoleni! Galeni kiwalo kinogile mumvaze. Mvazeni pete mkidole chake na vilatu mmagulu gake.
23 Abaho choleni mumgale bofu da ng'ombe dinonile mudichinje, wose tuje na kudeng'helela!
24 Kwavija mwanangu ino kakala yafile lakini sambi mgima. Kakala yapotele lakini sambi koneka.’ Avo wasonga kudeng'helela.
25 “Kipindi acho mwanage imkulu kakala kumgunda. Viyakalile behi na ing'anda, kahulika nyila na wanhu wovina.
26 Avo kamkema msang'hanaji imoja, kamuuza, ‘Ako kuna choni?’
27 Msang'hanaji ayo kamwidika, ‘Mdodo wako kabwela ukae, na tatako kamchinjila bofu da ng'ombe dinonile, kwavija kabwela mgima!’
28 “Ija imwana mkulu kagevuzika ng'hani, avo kalema kwingila mng'anda. Tatake kalawa kunze na kumpula yengile mng'anda.
29 Lakini kamwidika tatake, ‘Lola, miyaka yose ino niye nokusang'hanila kamba msang'hanaji, na silemile lagizo jako jojose. Kungwaa choni? Hunigwelele hata mbuzi nideng'helele na mbwiga zangu!
30 Lakini mwanago ino kananga vinhu vako mbuli ya ugoni, na viyabwelile ukae kumchinjila bofu da ng'ombe dinonile!’
31 Tatake kamwidika, ‘Mwanangu, kipindi chose kukala na niye, na vinhu vose vinilinavo vako.
32 Lakini tulondeka tudeng'helele na kusekelela, kwavija mdodo wako kakala yafile lakini sambi mgima, kakala yapotele lakini sambi koneka!’ ”

# 16

*Lusimo lwa mulolesaji mbala*

1 Yesu kawalongela wanahina zake, “Kukala na tajili imoja yakalile na mulolesaji wa vinhu vake. Tajili ayo kalongeligwa kamba mulolesaji ayo konanga sente zake.
2 Avo kamkema mng'anda, kamuuza, ‘Mbuli gani zimhulika kumwako? Mhetela vinhu vose viubokele na vija viulavile, kwavija hudaha kuwa mulolesaji wa vinhu vangu kabili.’
3 Mulolesaji ija kailongela, ‘Mkulu wangu konilekesa usang'hano. Notenda choni? Kulima sidahile bule, na kupula nokona kinyala.
4 Sambi nojuwa choni chonda nhende muladi nahalavigwa mna isang'hano, niwe na mbwiga wa kunibokela mzikae zao!’
5 “Avo kawakema wanhu wose wakalile wodaigwa na mkulu wake. Kamuuza wa ichanduso, ‘Kodaigwa choni na mkulu wangu?’
6 Nayo kamwidika, ‘Madebe gana ga mavuta.’ Mulolesaji ija kamulongela, ‘Sola cheti chako, kala hasi, lopola wandike malongo matano.’
7 Abaho kamuuza iyagwe, ‘Na gweye kodaigwa choni?’ Nayo kamwidika, ‘Viloba gana va ngano.’ Mulolesaji ija kamulongela, ‘Sola cheti chako, wandike malongo nane.’
8 “Mkulu wa ija mulolesaji mbala kamtogola kwavija katenda vinhu kwa ubala. Kwavija wanhu wa mwiisi ino wabala ng'hani mna zimbuli zao kubanza wanhu wa kumulenge.”
9 Yesu kagendelela kulonga, “Avo nowalongeleni, itendeleni umbwiga kubitila vinhu va mwiisi, muladi vahamala mudahe kubokeligwa kuna ikae ya ugima wa mazuwa gose.

10 Munhu yoyose yotamaniligwa mna ivinhu vidodo, kotamaniligwa mna ivinhu vikulu. Na munhu yoyose hatamaniligwa mna ivinhu vidodo, vivija hatamaniligwa mna ivinhu vikulu.

11 Avo kamba mweye hamutamaniligwa kulolesa mali za mwiisi, modahaze kutamaniligwa kulolesa mali za kuulanga?

12 Na kamba hutamaniligwa kulolesa vinhu va munhu iyagwe, nani yonda yakugwee vinhu vako mwenyego?

13 “Kuduhu msang'hanaji yodaha kuwasang'hanila wakulu wabili. Kwavija komwihila imoja na kumnogela iyagwe, hebu koilumba na imoja na kumbeza iyagwe. Hamudaha kumsang'hanila Mulungu hamoja na mali.”

### *Ulonzi uyagwe wa Yesu*
### *Mat 11:12-13; 5:31-32; Mlk 10:11-12*

14 Mafalisayo viwazihulike mbuli zino zose, wamzeha Yesu, kwavija wakala wanogelwa na sente.

15 Yesu kawalongela, “Mweye awo wanhu muitenda munoga mgameso ga wanhu, lakini Mulungu kaijuwa mizoyo yenu. Kwavija vinhu vikoneka vinoga ng'hani kwa wanhu, mgameso ga Mulungu vokoneka viha.

16 “Malagizo ga Musa na maandiko ga watula ndagu wa Mulungu vikala vipetigwa mbaka kipindi cha Yohana Mbatizaji. Kusongela aho, Mbuli Inogile ya Undewa wa Mulungu yopetigwa, na kila munhu kowamba kokwingila.

17 Lakini vibuha ng'hani kwa ulanga na isi kupotela, kubanza kinhu kidodo ng'hani kupotela mna Gamalagizo.

18 “Mbigalo yoyose yomwasa mwehe wake na kusola mtwanzi iyagwe, kotenda ugoni. Na mbigalo yomsola mtwanzi ija yasigwe, nayo kotenda ugoni vivija.

### *Munhu tajili na Lazalo*

19 “Kukala na tajili imoja yavalile viwalo va sente nyingi ng'hani na kuja goya kila siku.

20 Vivija kukala na munhu imoja mkiwa yakemigwe Lazalo, kamema vilonda lukuli lose, kakala yokwikigwa muulwivi lwa tajili ija.

21 Lazalo kakala yosulukila kuja vilagale muimeza ya tajili ayo. Na umbwa wakala wokwiza na kumulambita mvilonda vake.

22 “Abaho mkiwa ija kafa na kasoligwa na wasenga wa kuulanga mbaka behi ya Abulahamu. Tajili ayo nayo kafa na kazikigwa.

23 Ako kowochola wanhu wafile, kakala kodununzika ng'hani. Kenula meso gake, kamona Abulahamu kwa kutali na Lazalo kakala behi yake.

24 Avo kamkema kwa sauti ng'hulu, ‘Tata Abulahamu! Nyonele bazi! Mtume Lazalo yazabike kidole chake mgamazi, yaluhoze lulimi lwangu, kwavija nogaya ng'hani muumoto uno!’

25 “Lakini Abulahamu kamulongela, ‘Mwanangu, kumbuka muugima wako kubokela vinhu vinogile, nayo Lazalo kabokela vihile. Lakini sambi Lazalo kobwihila, na gweye kodununzika.

26 Hata avo, hagati yetu tweye na mweye hekigwa kolombo kulu, muladi munhu yolonda kuloka kulawa kuno kwiza kumwenu sekeyadahe, hebu munhu yoyose kulawa kumwenu sekeyaloke kwiza kumwetu!’

27 Tajili ija kalonga, ‘Nokupula gweye, tata Abulahamu, umtume Lazalo kuna ikae ya tatangu,

28 ako kuna ndugu zangu watano. Muleke yachole yakawazume muladi sekeweze hanhu hano ha kudununzika!’

29 “Abulahamu kalonga, ‘Ndugu zako wanago maandiko ga Musa na ga watula ndagu wa Mulungu ga kuwazuma. Wawategeleze wao kiwolonga!’
30 Tajili ija kamwidika, ‘Bule tata Abulahamu! Lakini kamba munhu yahazilibuka kulawa kwa wafile na kuwacholela, baho wozileka nzambi zao!’
31 Lakini Abulahamu kamulongela, ‘Kamba hawagagoga maandiko ga Musa na watula ndagu wa Mulungu, honda wategeleze hata kamba munhu yahazilibuka kulawa kwa wafile!’ ”

# 17

*Nzambi*
*Mat 18:6-7, 21-22; Mlk 9:42*

1 Yesu kawalongela wanahina zake, “Vinhu vondaviwatende wanhu watende nzambi volawilila, lakini kogaya munhu ija yovitenda vilawilile!
2 Yokuwa vinoga kwa munhu ayo yagodekigwe dibwe kulu da kudugila msingo na yasigwe mbahali, kubanza kumuhonza imoja wa wadodo wano yatende nzambi.
3 Avo iteganyeni!
“Ndugu yako yahakutendela nzambi, umzume. Yahatogola, gela kumgongo.
4 Yahakutendela nzambi miyanza saba kwa siku dimoja, na kila yaheza kumwako kolonga, ‘Ng'hosa,’ kolondeka ugele kumgongo.”

*Tamanilo*

5 Watumigwa wamulongela Mndewa, “Twengezele tamanilo.”
6 Mndewa kawedika, “Maza tamanilo jenu dahakuwile dodo kamba mbeyu ndodo ya haladali, mwahadahile kuulongela mbiki uno wa mkuyu, ‘Ng'oka ukaihande mbahali!’ nao wahawatogolele.

*Sang'hano ya msang'hanaji*

7 “Vino nani kumwenu yeli na msang'hanaji yomulimila hebu kosusila ng'hondolo, yahabwela kumgunda, komulongela yalopole kuja lujo lwake?
8 Bule. Lakini komulongela, ‘Uitande, nitandile lujo lwangu, unisang'hanile mbaka ng'homeleze kuja na kung'wa, abaho na gweye koja na kung'wa.’
9 Vino komgwaa nhogolwa msang'hanaji ayo kwavija kasang'hana gaja galagilizigwe?
10 Vivo ili kumwenu mweye, mwahatenda vose vimulagilizigwe, longeni, ‘Tweye twa wasang'hanaji wadodo, tusang'hana kija kitulondigwe kusang'hana!’ ”

*Yesu kowahonya wanhu longo*

11 Yesu viyakalile mnzila kochola Yelusalemu, kabitila mzimbaka za vijiji va Samalia na Galilaya.
12 Viyakalile kokwingila mna ikijiji kimoja, mumo kukala na wanhu longo wakalile na utamu wa dikulu, wemile kutali.
13 Waguta, “Go mkulu! Yesu! Tonele bazi!”
14 Yesu kawona, kawalongela, “Gendeni mkailaguse kwa walava nhosa.”
Viwakalile mnzila wochola, wahona.
15 Imoja wao viyone kahona, kabweleganya kwa Yesu kuno komgwaa nhogolwa Mulungu kwa sauti ng'hulu.
16 Kamgwila Yesu mmagulu kingubanguba, kamtogola. Munhu ayo kakala Msamalia.

17 Yesu kalonga, “Vino hawakalile wanhu longo wahonyigwe? Wayagwe
tisa wa kwahi?
18 Vino kuduhu iyagwe yabwelile kumgwaa nhogolwa Mulungu, ila
munhu ino hali muyahudi?”
19 Abaho Yesu kamulongela munhu ija, “Ima na uchole. Kutamanila
kwako kukuhonya.”

### *Kwiza kwa Undewa wa Mulungu*
*Mat 24:23-28, 37-41*

20 Mafalisayo wayagwe wamuuza Yesu Undewa wa Mulungu vondawize.
Yesu kawedika, “Undewa wa Mulungu hawiza kwa kukoneka kwa meso.
21 Kuduhu munhu yonda yalonge, ‘Lola, uno hano!’ hebu ‘Uja haja!’
Kwavija Undewa wa Mulungu wa mgati mmwenu.”
22 Abaho kawalongela wanahina zake, “Kipindi chokwiza vonda mulonde
kuyona siku imoja mwiizisiku za Mwana wa Munhu, lakini hondamuyone
bule.
23 Baho wanhu wowalongela, ‘Loleni kakuja!’ hebu ‘Loleni, kahano!’
Sekemuwakweleleze.
24 Kwavija kamba vija lumwesa vilulawilila kuulanga na kumwemwesa
kulawa mwambu umoja mbaka mwambu uyagwe, vivo vondayawe Mwana
wa Munhu mwiisiku yake.
25 Lakini tanhu kolondeka yadununzike ng'hani na kulemigwa na wanhu
wa lukolo luno.
26 Kamba viikalile mna ikipindi cha Nuhu, vivo vondaiwe mzisiku za
Mwana wa Munhu.
27 Kila munhu kakala koja na kung'wa, kusola na kusoligwa mbaka siku
ija Nuhu viyengile mdisafina. Mvula ng'hulu itowa na kuwakoma wanhu
wose.
28 Vivija kamba viilawilile mna ikipindi cha Lutu. Wanhu wagendelela
kuja na kung'wa, kugula na kuchuuza, kuhanda na kuzenga.
29 Lakini siku ija Lutu viyasegele Sodoma, moto na mabwe gokwaka
vilagala hasi na kuwakoma wose.
30 Vivo vondaiwe mwiisiku Mwana wa Munhu vonda yagubuligwe.
31 “Mwiisiku ayo, munhu yeli mkiswili cha ng'anda yake sekeyahumuluke
mng'anda kusola vinhu vake, vivija munhu yeli kumgunda sekeyabwele
ukayake.
32 Kumbukeni gampatile mwehe wake Lutu.
33 Munhu yoyose yolonda kuukombola ugima wake mwenyego, kowagiza,
na yoyose yowagiza ugima wake, koukombola.
34 Nowalongela, kilo acho wanhu wabili wawasile mulusazi lumoja, imoja
kosoligwa na iyagwe kolekigwa.
35 Watwanzi wabili woduga sembe hamoja, imoja kosoligwa na iyagwe
kolekigwa.
36 Wanhu wabili wokuwa kumgunda, imoja kosoligwa na iyagwe
kolekigwa.”
37 Wanahina zake wamuuza, “Vino, kwahi Mndewa?”
Yesu kawedika, “Kokose kuli na mzoga, baho honda waiting'hane
mhungu.”

## 18

### *Lusimo lwa mgane na msemi*

1 Abaho Yesu kawafundiza wanahina zake kwa lusimo kamba siku zose
wolondeka kumpula Mulungu na sekewadonhe.
2 Kalonga, “Kudibuga dimoja kukala na msemi yakalile hamdumba Mu-
lungu hebu kuwatonga wanhu.
3 Vivija kudibuga dijo, kukala na mgane imoja yakalile komgendela msemi
ayo baho kwa baho, kampula, ‘Ngwelele haki yangu kulawa kwa munhu
yanitendele gehile.’
4 Siku nyingi msemi ayo hamtegeleze mgane ayo, lakini kumwande kai-
longela, ‘Hata kamba simdumba Mulungu hebu kuwatonga wanhu,
5 lakini kwavija mgane ino konigaza, nomgwaa haki yake, kwavija na-
haleka, kogendelela kwiza hano na kunigaza!’ ”
6 Abaho Mndewa kagendelela kulonga, “Tegelezeni kiyalongile msemi ija
yehile.
7 Vino, Mulungu honda yawagwee haki wanhu zake yawasagule, wom-
ulilila imisi na ikilo? Vino kokawa kuwategeleza?
8 Nowalongela, kowagwaa haki yao himahima. Lakini Mwana wa Munhu
vondayeze, vino kodivika tamanilo mwiisi?”

### *Lusimo lwa Mfalisayo na mbokela kodi*

9 Abaho Yesu kawalongela lusimo luno wanhu waja wakalile woitapa
wanoga na kuwabeza wayagwe.
10 “Kukala na wanhu wabili wacholile kumpula Mulungu kuna Ing'anda
ya Mulungu. Imoja kakala Mfalisayo na iyagwe kakala mbokela kodi.
11 “Mfalisayo ayo kainega kumgwazo na kumpula Mulungu, ‘Go Mulungu,
nokugwaa nhogolwa kwavija niye sili kamba wanhu wayagwe, wabokaji,
wotenda gehile, hebu wagoni. Wala sili kamba ino mbokela kodi.
12 Niye nofunga kuja miyanza mibili mzisiku saba, na nolava fungu da
longo da vinhu vangu vose vinipata!’
13 “Lakini ija mbokela kodi kema kutali, hadahile hata kwinula meso
gake kuulanga, lakini kaitowa mhambaga yake kwa usungu, kalonga, ‘Go
Mulungu, nyonele bazi, niye notenda nzambi!’
14 Nowalongela, mbokela kodi ija kachola ukayake kuno katendigwa
kanoga mgameso Mulungu kubanza ija Mfalisayo. Kwavija wose woi-
tenda wanhu wakulu wohumulusigwa, na waja woihumulusa wotendigwa
wanhu wakulu.”

### *Yesu kowatambikila wana wadodo*
### *Mat 19:13-15; Mlk 10:13-16*

15 Wanhu wayagwe wamgalila Yesu wana wadodo yawekile makono.
Wanahina viwone avo, wawakomhokela.
16 Lakini Yesu kawakema iwana, kalonga, “Walekeni wana wadodo weze
kumwangu, sekemuwagomese, kwavija Undewa wa Mulungu wa wanhu
kamba wano.
17 Nowalongeleni ukweli! Munhu yoyose yolema kuubokela Undewa wa
Mulungu kamba mwana mdodo, honda yengile ng'o!”

### *Munhu tajili*
### *Mat 19:16-30; Mlk 10:17-31*

18 Mkulu imoja kamuuza Yesu, “Mfundiza Unogile, nhende choni niupate
ugima wa mazuwa gose?”
19 Yesu kamuuza, “Habali kong'hema, ‘unogile’? Kuduhu yanogile, ila
Mulungu yaiyeka.
20 Kugajuwa Malagizo, ‘Sekeutende ugoni, sekeukome, sekewibe, sekeu-
longe uvizi, wategeleze tatako na mamako.’ ”

21 Munhu ija kedika, “Gago gose nigagoga toka haudodo.”
22 Yesu viyahulike avo, kamulongela, “Kuhungukiligwa na kinhu kimoja.
Chuuza vose viulinavo, uwagwee sente wanhu wakiwa, na gweye kokuwa
na ngama yako kuulanga. Abaho wize unikweleleze.”
23 Lakini munhu ayo viyahulike avo, kanyunyuwala kwavija kakala tajili
ng'hani.
24 Yesu viyamone kanyunyuwala, kalonga, “Vino avo vonda iwe vidala
kwa wanhu matajili kwingila Muundewa wa Mulungu!
25 Kwavija vibuha kwa ngamiya kubita mna ikizonzo cha sanzia, kubanza
tajili kwingila muundewa wa Mulungu.”
26 Wanhu wamuhulike, wamuuza, “Avo lelo nani yonda yadahe kukom-
boligwa?”
27 Yesu kawedika, “Vinhu havidahika kwa wanhu, kwa Mulungu vo-
dahika.”
28 Abaho Petulo kalonga, “Lola! Tweye tuvileka vinhu vetu vose, tukuk-
weleleza gweye.”
29 Yesu kawalongela, “Nowalongela kweli, munhu yoyose yoleka kae yake
hebu mwehe wake hebu ndugu zake hebu tatake na mamake hebu wanage
mbuli ya Undewa wa Mulungu,
30 kobokela vinhu vingi ng'hani mna ikipindi kino na kobokela ugima wa
mazuwa gose mna ikipindi chonda kize.”

*Yesu kolonga lwakadatu mbuli ya ifa yake*
*Mat 20:17-19; Mlk 10:32-34*

31 Yesu kawagala hamgwazo wanahina zake longo na wabili, kawalon-
gela, “Tegelezeni! Tochola Yelusalemu. Kuko kila kinhu chandikigwe na
watula ndagu wa Mulungu mbuli ya Mwana wa Munhu cholawilila.
32 Kwavija kogeligwa mmakono ga wanhu haweli Wayahudi, nao
womzeha, womuliga, na womtemela mate.
33 Womtowa mbalati na kumkoma, lakini siku da kadatu kozilibuka.”
34 Lakini wanahina hawazijuwile bule mbuli azo, kwavija wakala
wafisigwe na hawakijuwile kija kiyakalile yokilonga Yesu.

*Yesu komuhonya msuwameso*
*Mat 20:29-34; Mlk 10:46-52*

35 Yesu viyakalile behi na kuvika Yeliko, munhu imoja yakalile
msuwameso kakala hamgwazo mnzila, kopula.
36 Munhu ayo viyahulike lunhu lwa wanhu lobita, kauza, “Kuna choni?”
37 Wanhu wamulongela, “Yesu wa Nazaleti kobita.”
38 Nayo kakemelela, “Yesu! Mwana wa Daudi! Nyonele bazi!”
39 Wanhu walongole wamkomhokela, wamulongela yanyamale. Lakini
heyo kagendelela kukemelela ng'hani, “Mwana wa Daudi! Nyonele bazi!”
40 Avo Yesu kema, kalagiza munhu ija yagaligwe kumwake. Viyavikile
behi, Yesu kamuuza,
41 “Kolonda nikutendele choni?”
Nayo kamwidika, “Go mkulu, nolonda kulola.”
42 Yesu kamulongela, “Lola! Kutamanila kwako kukuhonya.”
43 Bahaja munhu ija kadaha kulola, kamkweleleza Yesu kuno komgwaa
nhogolwa Mulungu. Wanhu wose viwone avo, wamgwaa nhogolwa Mu-
lungu.

# 19

*Yesu na Zakayo*

1 Yesu kachola kudibuga da Yeliko, na kakala yobita mzinzila za buga dijo.
2 Kuko kukala na mkulu imoja wa wabokela kodi yakemigwe Zakayo, nayo
kakala tajili.
3 Kakala kolonda kumona Yesu, lakini hadahile mbuli ya lunhu lwa wanhu
na kwavija kakala mguhi.
4 Avo kakimbila haulongozi wa lunhu luja, kakwela mumbiki wa mkuyu
muladi yamone Yesu, yakalile yochola kubitila nzila ija.
5 Yesu viyavikile hanhu aho, kalola uchanha, kamulongela, "Zakayo,
himahima humuluka hasi, kwavija lelo nolondeka kukala mng'anda yako."
6 Zakayo kahumuluka himahima, kamgoneka Yesu kwa kudeng'helela.
7 Wanhu wose wagone ago, wasonga kunung'unika, walonga, "Munhu ino
kachola kukala mng'anda ya munhu mwene nzambi!"
8 Zakayo kema, kamulongela Yesu, "Go Mkulu, tegeleza! Nowagwaa
wakiwa nusu ya vinhu vangu, na kamba nimboka munhu yoyose kinhu,
nombwezela miyanza mine."
9 Yesu kamulongela, "Lelo ukombozi uvika kwa wanhu wa lubuga luno,
kwavija munhu ino nayo kolawa mulukolo lwa Abulahamu.
10 Kwavija Mwana wa Munhu keza kuwazahila na kuwakombola waja
wapotele."

### *Lusimo lwa wasang'hanaji longo*
*Mat 25:14-30*

11 Wanhu viwakalile wotegeleza gago, Yesu kagendelela kuwalongela
lusimo. Baho kakala mmabehi na Yelusalemu, nao wagesa kamba Undewa
wa Mulungu wa mmabehi kulawilila.
12 Avo kawalongela, "Kukala na munhu imoja wa lukolo lwa kindewa
yafungile mwanza kuchola isi ya kutali yakatendigwe mndewa, abaho
yabwele ukayake.
13 Avo yang'hali hanasegela, kawakema wasang'hanaji zake longo, kila
imoja kamgwaa sente sawa, abaho kawalongela, 'Tendeni biashala mbaka
vondambwele.'
14 Lakini wanhu wa isi yake wakala wamwihile. Avo wawatuma wasenga
wagende kwa wanhu waja wakalonge, 'Hatumulonda munhu ino yawe
mndewa wetu.'
15 "Munhu ija kaupata undewa, kabwela ukayake. Baho kawalagiza
wasang'hanaji zake yawagwelele sente wachole kumwake yapate kujuwa
kija kiwapatile.
16 Msang'hanaji wa ichanduso keza, kalonga, 'Go mkulu, sente zako ziu-
nigwelele zilela miyanza longo.'
17 Kamulongela, 'Kutenda goya msang'hanaji unogile! Kwavija kutenda
vinogile kulolesa mna ivinhu vidodo, nokutenda uwe munhu mkulu wa
mabuga longo.'
18 Msang'hanaji wa kabili keza, kalonga, 'Go mkulu, sente zako ziunig-
welele zilela miyanza mitano.'
19 Nayo kamulongela, 'Kokuwa munhu mkulu wa mabuga matano.'
20 "Msang'hanaji iyagwe keza, kalonga, 'Go mkulu, sola sente zako. Nikala
nizifungile goya mkikumbi.
21 Nikudumba, kwavija kuna gahigahi. Kosola vinhu va wayago kwa uvizi
na kosenga vija huvihandile.'
22 Mkulu ija kamulongela, 'Gweye kwa msang'hanaji yehile! Nokutagusa
kwa mbuli zako mwenyego! Kunijuwa nina gahigahi, nisolaga vinhu va
wayangu na kusenga vija sivihandile.

23 Habali huzikile sente zangu kwa wanhu wokwika sente muladi vimbwelile nyambulile zongezeke?’

24 “Abaho kawalongela waja wemile aho, ‘Mbokeni ayo zisente, mumgwelele msang'hanaji ija yapatile sente miyanza longo ya zija ziyagweleligwe.’

25 Lakini wao wamulongela, ‘Go mkulu, lakini heyo kanazo sente miyanza longo!’

26 Nayo kawedika, ‘Munhu yeli na kinhu kokongezelwa, lakini ija yeliduhu kinhu, kobokigwa hata kija kidodo kiyelinacho.

27 Na sambi, waja wanihile, wondema niye niwe mndewa wao, wagaleni hano, muwakome bahano mgameso gangu!’ ”

*Yesu kokwingila Yelusalemu kwa deng'ho*
*Mat 21:1-11; Mlk 11:1-11; Yoh 12:12-19*

28 Yesu viyamambukize kulonga avo, kawalongolela kuchola Yelusalemu.

29 Viyakalile behi na kuvika Betifage na Betania, habehi na Lugongo lwa Mizeituni, kawatuma wanahina zake wabili,

30 kawalongela, “Gendeni kuna ikijiji kili kuulongozi wenu. Mwahengila,
momvika mwana mhunda kafungigwa, nayo yang'hali hanakweligwa na
munhu. Mfunguleni mumgale hano.
31 Munhu yoyose yahawauza habali
momfungula, mulongeleni, ‘Mndewa komulonda.’ ”

32 Wanahina waja wachola, wamvika kamba vija Yesu viyawalongele.

33 Viwakalile womfungula imwana mhunda, wenyego wawauza, “Habali momfungula?”

34 Nao wawedika, “Mndewa komulonda.”

35 Wamgala imwana mhunda kwa Yesu. Abaho watandika viwalo vao mumgongo wa imwana mhunda, na wamtaza Yesu kukwela.

36 Yesu viyakalile kochola, wanhu wanzanza viwalo vao mnzila.

37 Viyakalile behi na kuvika Yelusalemu, hanhu hali na mtelemuko wa Lugongo lwa Mizeituni, lunhu mkulu lwa wanahina zake lusonga kudeng'helela na kumgwaa nhogolwa Mulungu kwa sauti ng'hulu mbuli ya unzonza wauwonile.

38 Walonga, “Mulungu yamtambikile Mndewa yokwiza kwa twaga da Mulungu, tindiwalo kuulanga na ukulu kwa Mulungu!”

39 Baho Mafalisayo wayagwe wakalile muulunhu wamulongela Yesu, “Mfundiza, walagize wanahina zako wanyamale!”

40 Yesu kawedika, “Nowalongeleni, wahanyamala wano, mabwe goguta.”

*Yesu kowalilila wanhu wa buga da Yelusalemu*

41 Yesu viyavikile behi na buga da Yelusalemu na viyawone wanhu wa buga dijo, kawalilila,

42 kalonga, “Maza lelo mwahajuwile mbuli zilondeka kugala tindiwalo! Lakini sambi zifisigwa mgameso genu!

43 Kwavija kipindi chokwiza, wanhu wakwihile vonda wakuzengele luwa, wokuzunguluka na kukusung'ha sung'ha kila mwambu.

44 Wokuhondahonda gweye na wanhu zako weli muuluwa wako. Kuduhu hata dibwe dimoja donda disigazigwe uchanha ya diyagwe, kwavija hukijuwile kipindi kiyezile Mulungu kukukombola!”

*Yesu kokwingila Mng'anda ya Mulungu*
*Mat 21:12-17; Mlk 11:15-19; Yoh 2:13-22*

45 Abaho Yesu kengila Mng'anda ya Mulungu, kasonga kuwawinga wanhu wakalile wochuuza vinhu,

46 kawalongela, “Yandikigwa mna Gamaandiko Gang'alile, Mulungu kalonga, ‘Ng'anda yangu yokuwa ng'anda ya kupulila.’ Lakini mweye muitenda mhango ya wabavi!”
47 Kila siku Yesu kakala kofundiza Mng'anda ya Mulungu. Wakulu wa walava nhosa, wafundiza Malagizo ga Musa, na walangulizi wa wanhu walonda kumkoma,
48 lakini hawadahile bule kutenda avo, kwavija wanhu wose wakala womtegeleza goya, hawalondile kuswela mbuli.

# 20

*Mbuli ya udahi wa Yesu*
*Mat 21:23-27; Mlk 11:27-33*

1 Siku dimoja Yesu kakala Mng'anda ya Mulungu kowafundiza wanhu na
kuwapetela Mbuli Inogile. Wakulu wa walava nhosa na wafundiza Malagizo
ga Musa hamoja na wavele weza,
2 wamulongela, “Tulongele, vino kotenda mbuli zino kwa udahi wa nani?
Nani yakugwelele udahi uno?”
3 Yesu kawedika, “Beteni na niye niwauze mbuli imoja. Nongeleni,
4 vino udahi wa Yohana wa kubatiza ulawa kuulanga hebu kwa wanhu?”
5 Wagesa, “Tulonge choni? Twahalonga, ‘Ulawa kuulanga,’ kotuuza,
‘Habali, hamumtogole Yohana?’
6 Na twahalonga, ‘Ulawa kwa wanhu,’ lunhu lose luno lotutowa mabwe,
kwavija wose wotogola kamba Yohana kakala mtula ndagu wa Mulungu.”
7 Avo wamwidika, “Hatujuwile kuulawile.”
8 Yesu kawalongela, “Na niye siwalongela bule notenda mbuli zino kwa
udahi wa nani.”

*Lusimo lwa walimaji mumgunda wa mizabibu*
*Mat 21:33-46; Mlk 12:1-12*

9 Abaho Yesu kawalongela wanhu lusimo luno, “Kukala na munhu imoja
yahandile mizabibu mumgunda wake. Kawakodisha walimaji, abaho kachola mwiisi iyagwe na kakala siku nyingi.
10 Msimu wa kubawa zabibu viuvikile, munhu ija kamtuma msang'hanaji
wake yachole kwa walimaji wamgwelele zabibu. Lakini walimaji waja
wamtowa msang'hanaji ija, wamuwinga makono gaiyeka.
11 Avo kamtuma msang'hanaji iyagwe, lakini walimaji wamtowa vivija na
kumuliga, wamuwinga makono gaiyeka.
12 Abaho kamtuma msang'hanaji wa kadatu. Ino nayo walimaji wamulumiza, wamwasa kunze.
13 Abaho mwene mgunda ija kalonga, ‘Nhende choni? Nomtuma
mwanangu nimnogele. Lamda ino womtegeleza!’
14 Lakini walimaji viwamone, wailongela, ‘Ino ayo muhazi wake.
Tumkome na uhazi wake wokuwa wetu.’
15 Avo wamulava kunze ya mgunda uja, wamkoma.”
Yesu kawauza, “Vino, mwene mgunda kowatenda choni waja walimaji?
16 Kokwiza na kuwakoma walimaji wose awo na kowakodisha walimaji
wayagwe mgunda awo wa mizabibu.”
Wanhu viwahulike mbuli ayo, walonga, “Bule! Sekeilawilile avo!”
17 Lakini Yesu kawalola, kawauza, “Vino, ulonzi uno fambulo jake choni?
‘Dibwe wadilemile wazengaji kamba hadifaya,
digalamuka dibwe kulu da kutamanila kubanza gose!’

[18] Munhu yoyose yonda yaikwale mdibwe ajo kobeneka beneka munhu donda dimulagalile domuhonda tipitipi."

### *Mbuli ya kulipa kodi*
*Mat 22:15-22; Mlk 12:13-17*

[19] Wafundiza Malagizo ga Musa na wakulu wa walava nhosa wajuwa kamba lusimo ulo kakala kowafumbila wao. Avo bahaja walonda kumgoga Yesu, lakini wawadumba wanhu.
[20] Avo wazahila kipindi kinogile. Wawahonga wanhu wayagwe waitende wanoga, wawatuma wamgeze Yesu kwa kumuuza, muladi wadahe kumgoga na kumgala kwa mkulu wa Lumi.
53 Bahaja tata ayo kakumbuka ikala kipindi acho Yesu viyamulongele, “Mwanago kohona.” Avo heyo na wanhu wa mng'anda yake wamtogola Yesu.
54 Uno ukala unzonza wakabili yautendile Yesu viyalawile isi ya Yudea kwiza isi ya Galilaya.

# 5

### *Yesu komuhonya mtamu hana dikolombo*

1 Vigabitile gano, Yesu kachola kudibuga da Yelusalemu kuna inyimwili nyimwili ya Wayahudi.
2 Ako Yelusalemu behi na mulango ukemigwe Mulango wa Ng'hondolo kukala na kolombo dikemigwe kwa Kiebulania Betisaza. Mumgwazo wa kolombo dijo kukala na vihelengo vitano.
3 Lunhu mkulu lwa wanhu wolumwa lukala lutambalala mvihelengo vivo, wanhu wasuwameso, mbetembete na wanhu waholole. Wakala wobetela mazi gatibuligwe,
4 kwavija kuna kipindi msenga wa kuulanga kezaga na kugatibula gaja gamazi geli kudikolombo, na mtamu yoyose yahalongola kwingila mazi gahamala kutibuligwa, kohona utamu wowose uyali nao.
5 Aho kukala na munhu imoja mtamu kwa miyaka malongo madatu na nane.
6 Yesu viyamone katambalala aho, kajuwa kamba munhu ayo kana utamu wa siku nyingi, avo Yesu kamuuza, “Kolonda kuhona?”
7 Mtamu ayo kamwidika, “Go mkulu. Kuduhu munhu wa kuningiza kudikolombo mazi gahatibuligwa. Kila vinigeza kwingila, munhu iyagwe konilongolela.”
8 Abaho Yesu kamulongela, “Winuke, papa mkeka wako, utembele.”
9 Bahaja munhu ayo kahona, kapapa mkeka wake, kasonga kutembela.
Mbuli ino ilawilila mwiisiku ya Kubwihila,
10 avo wakulu wa Wayahudi wamulongela munhu ija yahonyigwe, “Lelo ni siku ya Kubwihila, Malagizo getu gogomesa gweye sekeupape mkeka wako.”
11 Munhu ayo yahonyigwe kawedika, “Munhu heyo yanihonyile kanilongela nipape mkeka wangu nigende.”
12 Wamuuza, “Munhu gani heyo yakulongele utende vivo?”
13 Lakini munhu ayo yahonyigwe kakala hamjuwile Yesu viyali, kwavija hanhu aho kukala na lunhu, na Yesu kakala yasegele.
14 Abaho, Yesu kamvika munhu ayo yamuhonyile Mwiig'anda ya Mulungu. Kamulongela, “Tegeleza, gweye sambi kuhona. Sekeutende nzambi kabili, muladi sekegakupate gehile kubanza gano.”
15 Abaho munhu ayo kasegela, kachola kwa iwakulu wa Wayahudi, kawalongela, “Yesu ayo yanihonyile.”
16 Abaho Wayahudi wasonga kumwihila Yesu kwavija kamuhonya munhu siku ya Kubwihila.
17 Yesu kawedika, “Tatangu kosang'hana siku zose, na niye vivija nosang'hana.”
18 Ulonzi uno uwatenda wakulu wa Wayahudi wazahile nzila kwa nguvu zose wadahe kumkoma Yesu. Watenda avo siyo kwavija kabena lagizo da siku ya Kubwihila diiyeka, lakini vivija kamkema Mulungu Tatake, avo kaitenda kamba kaigala na Mulungu.

### *Udahi wa Mwana wa Mulungu*

19 Yesu kawedika, “Nowalongeleni ukweli, Mwana hatenda mbuli yoyose heyo mwenyego, kotenda gaja goyomona Tatake kotenda. Gaja goyotenda Tata, Mwana nayo kotenda.
20 Avo Tata komnogela Mwanage na komulagusila gaja gose goyotenda mwenyego. Komulagusila mbuli ng'hulu ng'hani kubanza zino, na mweye mose mokanganya.
21 Kamba vija Tata viyowazilibula wanhu wafile na kuwagwaa ugima, vivo ili kwa Mwana nayo kowagwaa ugima waja wose yawalondile.
22 Tata hamtagusa munhu yoyose. Kamgwelela Mwanage udahi wose wa kutagusa,
23 avo wanhu wose wamtegeleze Mwana, kamba vija viwomtegeleza Tata. Munhu yoyose yolema kumtegeleza Mwana kolema kumtegeleza Tata yamtumile.”
24 “Nowalongeleni ukweli, wanhu wose wozihulika mbuli zangu na kumtogola heyo yanhumile wanao ugima wa mazuwa gose. Awo honda watagusigwe bule, kwavija wamala kubita mkufa kwiza muugima.
25 Nowalongeleni ukweli, kipindi chokwiza tena kipindi kimala kwiza, baho waja wafile woihulika sauti ya Mwana wa Mulungu, na waja woihulika wokuwa wagima.
26 Kamba Tata mwenyego viyali chanduso cha ugima, vivo ili kwa Mwanage, kamtenda yawe chanduso cha ugima.
27 Kamgwelela Mwana udahi wa kutagusa, kwavija heyo ayo Mwana wa Munhu.
28 Sekemuikanganye mbuli ino, kipindi chokwiza baho waja wose wafile woihulika sauti yake
29 na wolawa mna gamapanga gao. Waja wose watendile ganogile wozilibuka na kupata ugima, na waja watendile gehile wozilibuka ili watagusigwe.”

### *Ukweli mbuli ya Yesu*

30 “Niye mwenyego sitenda mbuli yoyose kwa udahi wangu, lakini notagusa kamba Mulungu viyonongela, avo notagusa goya, kwavija sitenda kija kinonda, lakini kija kiyolonda heyo yanhumile.”
31 “Nahalonga mbuli zangu mwenyego, ulonzi wangu wokuwa wa uvizi.
32 Lakini kabaho imoja yosindila mbuli ya niye, naniye nojuwa gaja goyolonga ga ukweli.
33 Mweye mutuma wasenga kwa Yohana, na mbuli ziyalongile mbuli yangu ni za ukweli.
34 Siulonda usindila wa munhu, lakini nonga vino ili mukomboligwe.
35 Yohana kakala kamba kiwenge kikwaka yangaduu, na mweye muudeng'helela mulenge wake kwa kipindi kidodo.
36 Lakini niye mwenyego ninao usindila mkulu kubanza wa Yohana, kija kinhenda acho kiyanigwelele Tatangu nikitende, gano gose golagusa kamba Tata ayo yanhumile.
37 Tata mwenyego yanhumile, vivija kosindila mbuli ya niye. Mweye hamunaihulika sauti yake hebu kuchona kihanga chake,
38 na mweye muilema mbuli yake kwavija hamumtogole ija iyamtumile.
39 Mogasoma Maandiko Gang'alile kwavija mogesa kulawa mumo moupata ugima wa mazuwa gose. Na kuno Maandiko gago gago gandika mbuli zangu!
40 Lakini hamulonda kwiza kumwangu mupate ugima.

41 “Sizahila nhogolwa kulawa kwa wanhu.

42 Lakini niye niwajuwa. Nojuwa mna imizoyo yenu hamumnogela
Mulungu.

43 Niza kwa twaga da Tatangu, lakini hamunibokele, ila munhu iyagwe
yaheza kwa twaga jake mwenyego, mombokela.

44 Munogelwa kubokela nhogolwa kulawa mweye kwa mweye, lakini
hamulonda kupata nhogolwa kulawa kwa heyo yeli Mulungu yaiyeka, vino
modahaze kunhogola niye?

45 Sekemugese nowalongeleza kwa Tatangu, lakini Musa, yumumta-
manila ayo yonda yawalongeleze.

46 Kamba kweli mumtogola Musa, mwahanhogole na niye, kwavija Musa
kandika mbuli zangu.

47 Kamba hamgatogole gaja gayandike Musa, modahaze kutogola gano
gonilonga?”

# 6

*Yesu kowagwaa lujo lunhu mkulu*
*Mat 14:13-21; Mlk 6:30-44; Luk 9:10-17*

1 Abaho, Yesu kaloka mwambu wa lamba da Galilaya, vivija dokemigwa
Lamba da Tibelia.

2 Lunhu mkulu lumkweleleza, kwavija luwona unzonza wake wa kuho-
nya watamu.

3 Yesu kakwela mbaka uchanha kukigongo kakala hasi na wanahina zake.

4 Kipindi cha nyimwili nyimwili ya Wayahudi ikemigwe Pasaka kikala
behi.

5 Yesu viyalolile kaluwona lunhu mkulu lomwizila, avo kamuuza Filipo,
“Tukagule kwahi vinhu vingi vakuja muladi wanhu wano wose waje?”

6 Yesu kalonga vino kumgeza Filipo kwavija kakala yajuwile kinhu gani
chonda yatende.

7 Filipo kamwidika, “Sente magana mabili hazidaha kugula magate kwa
wanhu wose wano!”

8 Imoja wa wanahina zake Yesu yakemigwe Andeleya, ndugu yake Simoni
Petulo, kalonga,

9 “Kabahano mbwanga kana magate matano ga ngano na somba wabili,
lakini sikinhu chochose kwa lunhu lulihano.”

10 Yesu kawalongela wanahina zake, “Walongeleni wanhu wakale hasi.”
Kwavija hanhu aho hakala na mijani, wanhu wose wakala hasi. Kukala na
wambigalo kamba elufu tano.

11 Yesu kasola gaja gamagate, kamgwaa nhogolwa Mulungu, kawagolela
wanhu wose wakalile aho. Katenda vivo kwa waja iwasomba, kila munhu
kapata viyalondile.

12 Viwamambukize kuja, Yesu kawalongela wanahina zake, “Dondoleni
vihande visigale. Sekemuleke hata kimoja.”

13 Avo wanahina wadondola na kumemeza vigelo longo na vibili kulawa
kuna gamagate matano gawadile wanhu.

14 Viwauwonile unzonza uno yautendile Yesu, wanhu walonga, “Kweli ino
ayo mtula ndagu wa Mulungu yalondeke kwiza mwiisi!”

15 Yesu kajuwa kamba walonda kumgoga kwa nguvu na kumtenda mn-
dewa wao, avo kabweleganya kuvigongo yaiyeka.

*Yesu kotembela uchanha mgamazi*
*Mat 14:22-23; Mlk 6:45-52*

16 Viivikile ichungulo, wanahina wa Yesu wahumuluka kudilamba,
17 wakwela mwiingalawa, na kubwela umwambu wa lamba mwambu wa
Kapelinaumu. Ikilo ivika lakini Yesu kakala yang'hali hanachola kumwao.
18 Beho kulu dibuma na kugatibula ga mazi.
19 Wanahina zake viwacholile utali wa kilometa tano mbaka sita, wamona
Yesu kotembela uchanha mgamazi, kokwiza mwambu wao kuili ngalawa,
wadumba ng'hani.
20 Yesu kawalongela, “Sekemudumbe. Iyo niye!”
21 Wanahina zake walonda kumsola Yesu mwiingalawa, bahaja wavika
mwiisi kuwakalile wochola.

### *Wanhu womzahila Yesu*

22 Imitondo iyagwe lunhu mkulu lukala lukalile mwambu uyagwe wa
lamba wona aho hakala na ngalawa imoja iiyeka. Wao wajuwa kamba Yesu
hacholile hamoja na wanahina zake, lakini wasegela waiyeka.
23 Ngalawa ziyagwe zilawile Tibelia zivika mbaka behi na hanhu hawadile
magate Mndewa viyamambukize kumgwaa nhogolwa Mulungu.
24 Wanhu viwajuwile Yesu kahaduhu hanhu aho, hebu wanahina zake,
wakwela mzingalawa na kuchola Kapelinaumu, kumzahila.

### *Yesu ayo lujo lwa ugima*

25 Wanhu viwamvikile Yesu umwambu uyagwe wa lamba, wamuuza,
“Mfundiza, vino hano kwiza lini?”
26 Yesu kawedika, “Nowalongeleni ukweli, monizahila niye kwavija muja
magate mwiguta, siyo kwavija mona unzonza wangu.
27 Sekemulusang'hanile lujo lunangika, lakini mulusang'hanile lujo lugala
ugima wa mazuwa gose. Uno awo lujo londa yawagwee Mwana wa Munhu,
kwavija Mulungu Tata kamsagula.”
28 Avo wamuuza, “Vino kinhu gani tutende tudahe kugatenda goyolonda
Mulungu?”
29 Yesu kawedika, “Kinhu choolonda Mulungu mweye mutende, mumto-
gole ija yamtumile.”
30 Wamwidika, “Vino unzonza gani wonda utende ili tuwone na kukuto-
gola? Choni chonda utende?
31 Wahenga zetu waja lujo lukemigwa Mana kuluwala, kamba Maandiko
Gang'alile vigalonga, ‘Kawagwelela lujo luhumuluke kuulanga.’ ”
32 Yesu kawalongela, “Nowalongeleni ukweli, siyo Musa yawagwelele
lujo lwa kuulanga, lakini Tatangu ayo yowagwaa lujo lwa ukweli kulawa
kuulanga.
33 Lujo loowagwaa Mulungu ayo heyo yezile hasi kulawa kuulanga na
kowagwaa ugima wanhu wa mwiisi.”
34 Wamulongela, “Go mkulu, tugwee lujo lulo siku zose.”
35 Yesu kawalongela, “Niye ayo lujo lugala ugima. Wose wonda weze
kumwangu honda wone nzala, na waja wose wonhogola honda wone
ng'hilu.
36 Niwalongeleni kamba munyona lakini hamtogola.
37 Wose iwonigwelela Tatangu wokwiza kumwangu. Na niye simwasa
kunze munhu yoyose yokwiza kumwangu,
38 kwavija sizile hasi kulawa kuulanga kutenda gaja gonilonda lakini
goyolonda Tata yanhumile.
39 Gano gago goyolonda ija yanhumile sekenimwagize hata imoja mna
iwaja wose yangwelele, lakini nolondeka niwazilibule wose na kuwagwaa
ugima siku ya kimambukizo.

40 Kwavija kiyolonda Tatangu acho kino, kila munhu yomulola Mwana na kumtogola heyo yawe na ugima wa mazuwa gose. Na niye nomzilibula munhu ayo mna isiku ya uhelelo."

41 Avo, Wayahudi wasonga kumnung'unikila Yesu kwavija kalonga, "Niye ayo lujo luhumuluke kuulanga."

42 Avo walonga, "Vino ino siyo Yesu mwanage Yusufu? Tumjuwa tatake na mamake. Yokuwaze kabili kolonga kahumuluka kuulanga?"

43 Yesu kawedika, "Lekeni kuinung'unikila.

44 Kuduhu munhu yodaha kwiza kumwangu bila kugaligwa na Tata yanhumile, na niye nomzilibula munhu ayo mna isiku ya uhelelo.

45 Watula ndagu wa Mulungu wandika, 'Kila munhu kofundizigwa na Mulungu.' Munhu yoyose yomtegeleza Tata na kuifunza kumwake kokwiza kumwangu.

46 Kuduhu munhu yoyose yamonile Tata, heyo yalawile kwa Mulungu ayo heyo yaiyeka yamonile Tata.

47 Nowalongeleni ukweli, heyo yotogola kanao ugima wa mazuwa gose.

48 Niye ayo lujo lugala ugima.

49 Wahenga zenu waja lujo Mana kuluwala, lakini wafa.

50 Lakini munhu yoyose yoluja lujo luhumuluke kuulanga honda yafe bule.

51 Niye ayo lujo lugala ugima luhumuluke kuulanga. Munhu yoyose yoja lujo luno, kokuwa mgima siku zose. Lujo londa nimgwee munhu ayo ni lukuli lwangu, awo uniwagwelela wanhu wa mwiisi ili wawe wagima."

52 Mbuli ino iwatenda Wayahudi waibamilile. Waiuza, "Vino munhu ino kodahaze kutugwaa lukuli lwake tuluje?"

53 Yesu kawalongela, "Nowalongeleni ukweli, kamba hamuluja lukuli lwa Mwana wa Munhu na kuing'wa damu yake, honda muwe na ugima mgati mmwenu.

54 Munhu yoluja lukuli lwangu na kuing'wa damu yangu kanao ugima wa mazuwa gose, na niye nomzilibula mna isiku ya uhelelo.

55 Kwavija lukuli lwangu ulo lujo lwa kweli, na damu yangu acho king'waji cha kweli.

56 Wanhu woluja lukuli lwangu na kuing'wa damu yangu wokala mgati mmwangu, na niye nokala mgati mmwao.

57 Tata yeli mgima yanhumile, na kwa mbuli yake niye na vivija mgima. Vivo vonda iwe munhu yoyose yoluja lukuli lwangu kokuwa mgima mbuli ya niye.

58 Uno awo lujo luhumuluke kuulanga, haluigalile na lujo luja luwadile wahenga zenu, abaho wafa. Lakini yoyose yoluja lujo luno kokuwa mgima siku zose."

59 Yesu kalonga mbuli zino viyakalile kofundiza mna ing'anda ya kumpula Mulungu ako Kapelinaumu.

### *Mbuli zigala ugima wa mazuwa gose*

60 Wanhu zake wengi wamkweleleze waihulika mbuli ino na kulonga, "Mafundizo gano madala ng'hani. Nani yodaha kugatogola?"

61 Bila kulongeligwa, Yesu kajuwa kamba wanhu zake wamkweleleze wakala woinung'unikila mbuli ino, avo kawalongela, "Vino mbuli ino yolonda kuwatenda mulemelwe?

62 Vino yokuwaze, mwahamona Mwana wa Munhu kobwela uchanha kuja kuyakalile ichanduso?

63 Loho wa Mulungu ayo yomgwaa munhu ugima, nguvu za munhu hazidaha kinhu chochose. Mbuli ziniwalongeleni ni za Loho wa Mulungu na zogala ugima.

64 Lakini wayagwe wenu hawatogola.” Yesu kawajuwa toka mwaka waja hawamtogola na kamjuwa ija yonda yamuhinduke.

65 Abaho kalonga, “Lekaavo niwalongeleni kuduhu munhu yodaha kwiza kumwangu bila Tata kutenda idahike kwa munhu ayo kutenda vivo.”

66 Kwa ulonzi uno, wanhu wengi wamkweleleze wabweleganya kukisogo na hawadahile kabili kuchola nayo.

67 Avo Yesu kawauza wanahina zake longo na wabili, “Na mweye vivija molonda kusegela?”

68 Simoni Petulo kamwidika, “Mndewa, tweye tuchole kwa nani? Gweye kunazo mbuli zigala ugima wa mazuwa gose.

69 Sambi tweye totogola na tojuwa kamba gweye ayo Yang'alile ija yalawile kwa Mulungu.”

70 Yesu kedika, “Vino siwasagule mweye longo na wabili? Lakini imoja wenu Mwenembago!”

71 Yesu kakala yolonga mbuli ya Yuda, mwanage Simoni Isikaliote. Yuda kakala imoja wa wanahina longo na wabili, ayo yonda yamuhinduke Yesu.

# 7

*Yesu na ndugu zake*

1 Vigabitile gano, Yesu kachola mwiisi ya Galilaya, halondile kuchola isi ya Yudea kwavija wakulu wa Wayahudi wakala wolonda kumkoma.

2 Siku ya nyimwili nyimwili ya Wayahudi ya viheha ikala behi,

3 avo ndugu zake Yesu wamulongela, “Segela hanhu hano uchole isi ya Yudea, muladi wanhu zako wokukweleleza wazone mbuli ziutenda.

4 Kuduhu munhu yofisa kija kiyotenda kamba yahalonda wanhu wamjuwe goya. Kwavija gweye kotenda mbuli zino, leka wanhu wose wamwiisi wakujuwe.”

5 Yesu hatogoligwe hata na ndugu zake.

6 Yesu kawalongela, “Kipindi changu niye hakinavika. Lakini kipindi chochose kinoga kumwenu.

7 Wanhu wa mwiisi hawawehila mweye, lakini wonihila niye, kwavija siku zose nowalongela gaja goyotenda ganyolodoka.

8 Mweye choleni kuna inyimwili nyimwili. Niye sichola bule, kwavija kipindi changu hakinavika.”

9 Yesu kalonga vino, abaho kagendelela kukala mwiisi ya Galilaya.

*Yesu kuna inyimwili nyimwili ya viheha*

10 Ndugu zake Yesu viwacholile kuna inyimwili nyimwili, Yesu nayo kachola. Hacholile kunze kunze lakini kachola kinyelegezi.

11 Wakulu wa Wayahudi wakala womzahila Yesu hana inyimwili nyimwili. Walonga, “Munhu ija ka kwahi?”

12 Hakala na minong'ono hana ulunhu mbuli ya Yesu. Wanhu wayagwe walonga, “Kanoga,” lakini wayagwe walonga, “Bule, kokwagiza wanhu.”

13 Lakini kuduhu munhu yokala yolonga mbuli ya Yesu chaka chaka, kwavija wakala wowadumba wakulu wa Wayahudi.

14 Nyimwili nyimwili viikalile hagatigati, Yesu kengila Mng'anda ya Mulungu kasonga kufundiza.

15 Wakulu wa Wayahudi wakanganya ng'hani na kulonga, “Yokuwaze munhu ino kojuwa vinhu vingi na kuno haifunzile kokose?”

16 Yesu kawedika, “Mafundizo gano gonifundiza siyo gangu, lakini golawa kwa Mulungu yanhumile.

17 Munhu yoyose yolonda kutenda goyolonda Mulungu kojuwa gano gonifundiza golawa kwa Mulungu hebu nolonga gaja gonilonda.

18 Munhu ija yolonga mbuli zake kozahila nhogolwa yake mwenyego. Lakini heyo yozahila nhogolwa kumwake ija yamtumile munhu ayo mkweli, mduhu uvizi mumulomo mmwake.

19 Vino Musa hawagwelele Malagizo? Lakini kuduhu hata munhu imoja yogagoga. Vino habali molonda kung'homa?”

20 Lunhu lwa wanhu lumwidika, “Gweye kuna kinyamkela. Nani yolonda kukukoma?”

21 Yesu kawedika, “Nhenda unzonza umoja, mweye mose mukanganya.

22 Musa kawalagiza muwengize kumbi wanenu hamoja siyo Musa lakini wahenga zenu awo wasongile, na mweye momwingiza kumbi mwana mna isiku ya Kubwihila.

23 Kamba mwana kokwingizigwa kumbi mna isiku ya Kubwihila muladi sekemubene Malagizo ga Musa, habali monigevuzikila kwavija nimuhonya munhu mna isiku ya Kubwihila?

24 Lekeni kutagusa kwa meso, lakini mutaguse kwa ukweli.”

*Ayuno iyo Kilisito Mkombola?*

25 Wanhu wayagwe wa Yelusalemu walonga, “Vino ino siyo munhu ija iwakulu wolonda kumkoma?

26 Loleni! Kolonga kunze kunze na hawamulongela mbuli yoyose! Vino iwakulu wamjuwa ayo Kilisito Mkombola?

27 Lakini Kilisito Mkombola yaheza, kuduhu munhu yonda yajuwe kolawa kwahi, lakini tweye tukujuwa koolawa munhu ino.”

28 Yesu viyakalile kofundiza Mng'anda ya Mulungu, kalonga kwa sauti ng'hulu, “Vino mweye munjuwa goya niye na mukujuwa kuja kundawa? Sizile kwa udahi wangu mwenyego, heyo yanhumile, ni mkweli. Mweye hamumjuwile,

29 lakini niye nimjuwa, kwavija nolawa kumwake, nayo kanhuma.”

30 Abaho walonda kumgoga, lakini kuduhu hata munhu imoja yamgolosele mkono, kwavija saa yake ikala hainavika.

31 Lakini wanhu wengi hana ulunhu wamtogola na kulonga, “Vino Kilisito Mkombola yaheza, kotenda unzonza mkulu kubanza yautendile munhu ino?”

*Wakalizi watumigwa kumgoga Yesu*

32 Mafalisayo waluhulika lunhu lonyong'onya mbuli ya Yesu, avo wao na iwakulu wa walava nhosa wawatuma wakalizi wamgoge.

33 Yesu kalonga, “Nokala na mweye kipindi kidodo, na abaho nochola kumwake ija yanhumile.

34 Monizahila, lakini honda munyone, kwavija hamudaha kwiza hanhu hanili.”

35 Wakulu wa Wayahudi wailongela, “Vino munhu ino kochola kwahi mbaka seketumone? Vino kochola kunagamabuga ga Wagiliki kuko kookala wanhu zetu na kuwafundiza Wagiliki?

36 Vino kofambula choni viyolonga, tomzahila lakini honda tumone, na hatudaha kuchola kuko konda yawe?”

### *Vizanda va mazi ga ugima*

37 Mna isiku ya uhelelo na siku ng'hulu ya inyimwili nyimwili, Yesu kema kakemelela, “Munhu yoyose yokona ng'hilu yeze kumwangu yang'we.

38 Kamba Maandiko Gang'alile vigalonga, ‘Munhu yonhogola niye, vizanda va mazi gogala ugima vokilima muumoyo wake.’ ”

39 Yesu kalonga vino mbuli ya Loho Yang'alile, ija wanhu wose womtogola wombokela. Kipindi acho Loho Yang'alile kakala yang'hali hanakwiza, kwavija Yesu kakala hanakwinuligwa muukulu.

### *Kuigola kwa wanhu*

40 Wanhu wayagwe mna ulunhu wamuhulika viyalongile avo na walonga, “Kweli munhu ino mtula ndagu wa Mulungu!”

41 Wanhu wayagwe walonga, “Heyo ayo Kilisito Mkombola!”

Lakini wayagwe walonga, “Kilisito Mkombola hadaha kulawa mwiisi ya Galilaya!

42 Maandiko Gang'alile golonga kamba Kilisito Mkombola kolawa mulukolo lwa Daudi na kovumbukila Beselehemu kudibuga diyakalile Daudi.”

43 Avo lunhu luigola mbuli ya Yesu.

44 Wanhu wayagwe walonda kumgoga Yesu, lakini kuduhu hata munhu imoja yamgolosele mkono.

### *Kuleka kutogola kwa wakulu wa Wayahudi*

45 Wakalizi viwabwelile, wakulu wa walava nhosa na Mafalisayo wawauza, “Habali hamumgalile?”

46 Wakalizi wawedika, “Kuduhu munhu yolonga kamba munhu ayo!”

47 Mafalisayo wawauza, “Vino na mweye vivija muviziligwa?”

48 “Mumjuwa mkulu yoyose hebu Mfalisayo yomtogola?

49 Lunhu luno halugajuwile Malagizo ga Musa, avo waduiligwa na Mulungu!”

50 Nikodemo kakala imoja wa Mafalisayo wakalile aho, ayo yacholile kumulola Yesu ichanduso. Kawalongela wayage,

51 “Vino Malagizo getu godaha kumtagusa munhu yoyose bila tanhu kumuhulika na kukijuwa kija kiyatendile?”

52 Wamwidika, “Vino na gweye vivija kolawa mwiisi ya Galilaya? Gasome Maandiko Gang'alile na koifunza, kuduhu mtula ndagu wa Mulungu yalawile mwiisi ya Galilaya.”

53 Abaho kila munhu kachola ukayake.

## 8

### *Mtwanzi yagogigwe ugoni*

1 Yesu kachola kuna Ulugongo lwa Mizeituni.

2 Imitootondo ng'hani Yesu kabwela kuna Ing'anda ya Mulungu. Wanhu wose wamzunguluka, nayo kakala hasi kasonga kuwafundiza.

3 Wafundiza Malagizo ga Musa na Mafalisayo wamgala mtwanzi yagogigwe ugoni, wamwika haulongozi wa wanhu wose.

4 Wamulongela Yesu, “Mfundiza, mtwanzi ino kagogigwa ugoni.

5 Muna ga Malagizo getu Musa katulagiza kamba mtwanzi kamba ino yatoigwe mabwe mbaka yafe. Lelo gweye kolongaze?”

6 Walonga vino ili wamgoge Yesu kwa mbuli zake, muladi wapate kumtagusa. Lakini Yesu kainama kandika hasi kwa kidole chake.

7 Viwagendelele kwima aho kuno womuuza, Yesu kenuka kawalongela, "Munhu yoyose hatendile nzambi yasonge kumpigisila dibwe."
8 Abaho Yesu kainama kabili kandika hasi.
9 Viwahulike avo, wose wasegela imoja imoja, wasonga iwavele. Yesu kalekigwa yaiyeka, na mtwanzi ija yang'hali yemile aho.
10 Yesu kenuka na kumulongela mtwanzi ija, "Wa kwahi wanhu waja? Kuduhu munhu yoyose yakutaguse?"
11 Mtwanzi ija kalonga, "Go mkulu, kahaduhu."
Yesu kalonga, "Vinoga. Na niye vivija sikutagusa. Genda lakini sekeutende nzambi kabili."

### *Yesu yuyo mulenge wa isi*

12 Yesu kawalongela Mafalisayo kabili, "Niye ayo mulenge wa isi. Munhu yoyose yonikweleleza kokuwa na mulenge wa ugima na honda yagende mdiziza bule."
13 Mafalisayo wamulongela, "Gweye koisindila mwenyego, avo gago goulonga hagatogoligwa kamba kweli."
14 Yesu kawedika, "Aka, hata kamba nahaisindila mwenyego, gaja gonilonga ga ukweli kwavija nikujuwa kundawile na kuja kunichola. Mweye hamukujuwile kuja kundawile hebu kuja kunichola.
15 Mweye motagusa kwa nzila zoyotagusa wanhu, niye simtagusa munhu yoyose.
16 Lakini hata nahatagusa, notagusa goya kwavija sili niiyeka bule, nahamoja na Tata yanhumile.
17 Yandikigwa mna ga Malagizo genu kamba usindila wa wanhu wabili wahailumba, gaja gowolonga ga ukweli.
18 Niye noisindila mwenyego, na Tata yanhumile vivija konisindila."
19 Wamuuza, "Tatako kakwahi?"
Yesu kawedika, "Hamnijuwile niye hebu Tatangu. Maza munijuwile niye, vivija mwahamjuwile Tatangu."
20 Yesu kalonga gano gose viyakalile kofundiza Mng'anda ya Mulungu, mdigati hakikigwe kiya cha kulavila sadaka. Kuduhu munhu yamgogile, kwavija saa yake ikala hainavika.

### *Hamudaha kuchola kuja kunyhola*

21 Yesu kawalongela kabili, "Niye nosegela, mweye monizahila, lakini mofa na nzambi zenu. Hamudaha kuchola kuja kunyhola."
22 Avo wakulu wa Wayahudi wauza, "Kolonga hatudaha kuchola hanhu kuyochola. Vino kolonda kuikoma mwenyego?"
23 Yesu kawedika, "Mweye mwa wanhu wa mwiisi ino, lakini niye nolawa kuulanga. Mweye molawa mumuno mwiisi, lakini niye silawa mwiisi bule.
24 Lekaavo niwalongeleni mofa na nzambi zenu. Mofa na nzambi zenu kamba hamulonda kutogola kamba 'Niye ayo Heyo.' "
25 Wamuuza, "Gweye kwa nani?"
Yesu kawedika, "Niwalongeleni haichanduso.
26 Ninazo mbuli nyingi za kulonga kumwenu, nyingi za kuwatagusa. Hata ivo ija yanhumile ni mkweli, na niye nowalongela wanhu wa mwiisi kija kimhulike kumwake."
27 Wakala hawajuwile kamba Yesu kakala kolonga mbuli ya Tata.
28 Avo kawalongela, "Mwahamwinula uchanha Mwana wa Munhu, mojuwa kamba, 'Niye ayo Heyo,' abaho mojuwa kamba sitenda mbuli yoyose kwa udahi wangu, lakini nolonga kija kiyanilagize Tata nonge.

29 Na heyo yanhumile kahamoja na nene, handekile niiyeka bule kwavija siku zose notenda kija kimnogele."
30 Wanhu wengi wamuhulike Yesu yolonga mbuli zino wamtogola.

### *Yesu kowatenda mulekesigwe*

31 Avo Yesu kawalongela Wayahudi waja wamtogole, "Kamba mwahatogola mafundizo gangu, mwa wanahina zangu kweli.
32 Avo moijuwa kweli, na kweli yowatenda mulekesigwe."
33 Wamwidika, "Tweye twa lukolo lwa Abulahamu na hatunakuwa watumwa wa munhu yoyose. Habali kotulongela 'Tolekesigwa'?"
34 Yesu kawalongela, "Nowalongeleni ukweli, munhu yoyose yotenda nzambi mtumwa wa nzambi.
35 Mtumwa hali munhu wa lukolo siku zose, lakini mwana ayo munhu wa lukolo siku zose.
36 Kamba Mwana yahawalekesa, na mweye molekesigwa kweli.
37 Nojuwa mwa lukolo lwa Abulahamu. Lakini molonda kunikoma, kwavija hamgatogola mafundizo gangu.
38 Nowalongela kija kiyanilagusile Tatangu, lakini mweye motenda kija kimulongeligwe na tata yenu."
39 Wamwidika, "Tata yetu Abulahamu."

Yesu kawedika, "Maza mukalile wana wa Abulahamu, mwahatendile mbuli zizija ziyatendile heyo.
40 Niwalongela ukweli umhulike kwa Mulungu, lakini molonda kunikoma. Abulahamu hatendile kamba vivo!
41 Motenda kiyatendile tata yenu."

Wamwidika, "Mulungu yaiyeka ayo Tata itwilinayo hatuli wana wa kuvikila, tweye twa wanage too."
42 Yesu kawalongela, "Maza Mulungu yakalile Tata yenu, mwahaninogele, kwavija niza kulawa kwa Mulungu na sambi nabahano. Sizile kwa udahi wangu mwenyego, lakini kanhuma.
43 Habali hamjuwa kinonga? Kwavija hamudaha kutegeleza usenga wangu.
44 Mweye mwa wana wa tataenu, Mwenembago, na mweye molonda kukweleleza kusulukila kwa tataenu. Kusongela mwaka kakala mkomaji na hemile muna ikweli, kwavija mduhu kweli mgati mmwake. Yahalonga uvizi, kolagusa viyali, kwavija heyo ni mvizi na tata wa uvizi.
45 Lakini nowalongeleni ukweli, lekaavo hamnitogola bule.
46 Nani imoja wenu yodaha kulagusa kamba nibananga? Kamba nolonga ukweli, habali hamunhogola?
47 Munhu wa Mulungu kotegeleza mbuli za Mulungu. Hata ivo, mweye hamuli wa Mulungu, lekaavo hamnitegeleza."

### *Yesu kakala kuko Abulahamu yang'hali hanavumbuka*

48 Wayahudi wamuliga Yesu walonga, "Hatulongile goya kamba gweye kwa Msamalia na kuna kinyamkela?"
49 Yesu kawedika, "Nabule kinyamkela. Nomtegeleza Tatangu lakini mweye monibeza.
50 Sizahila nhogolwa yangu mwenyego. Lakini kabaho imoja yoizahila, heyo ayo yotagusa.
51 Nowalongeleni ukweli, munhu yoyose yotogola mafundizo gangu honda yafe bule."

52 Avo, Wayahudi wamulongela, “Sambi tojuwa kamba gweye kuna
kinyamkela! Abulahamu kafa, na watula ndagu wa Mulungu wafa, abaho
gweye kolonga yoyose yotogola mafundizo gako honda yafe bule.
53 Vino gweye kwa mkulu kubanza tata yetu Abulahamu? Heyo kafa, na
watula ndagu wa Mulungu vivija wafa. Kogesa gweye kwa nani?”
54 Yesu kawedika, “Nahaitogola mwenyego, nhogolwa ayo mduhu kinhu.
Ija yonitogola niye ni Tatangu yumulonga Mulungu wenu.
55 Mweye hamumjuwile bule, lakini niye nimjuwa. Nahalonga simjuwile,
nokuwa mvizi kamba mweye. Lakini nimjuwa, na nozigoga mbuli zake.
56 Tata yenu Abulahamu kadeng'helela viyachonile kipindi changu chak-
wiza, kachona na kadeng'helela.”
57 Wayahudi wamulongela Yesu, “Vino gweye hunapata hata miyaka
malongo matano, kumonaze Abulahamu?”
58 Yesu kawedika, “Nowalongeleni ukweli, Abulahamu yang'hali hana
vumbuka, niye nabaha.”
59 Abaho wadondola mabwe wampigisile, lakini Yesu kaifisa kalawanya
Mng'anda ya Mulungu.

# 9

*Yesu komuhonya munhu yavumbuke msuwameso*

1 Yesu viyakalile kogenda, kamona munhu yavumbuke msuwameso.
2 Wanahina zake wamuuza, “Mfundiza, nzambi gani imtendile munhu ino
yavumbuke msuwameso? Vino heyo ayo yaitendile nzambi ayo hebu tatake
na mamake?”
3 Yesu kawedika, “Ino hailawilile kwavija heyo katenda nzambi hebu
tatake na mamake watenda nzambi. Lakini kavumbuka msuwameso mu-
ladi udahi wa Mulungu woneke kumwake.
4 Kwavija ing'hali imisi, tolondeka tusang'hane sang'hano ya ija yanhu-
mile. Ikilo yovika, baho kuduhu munhu yodaha kusang'hana.
5 Kipindi ning'hali mwiisi, niye na mulenge wa isi yose.”
6 Viyamambukize kulonga vino, Yesu katema mate hasi, kabuluga nhope
kwa mate gaja, abaho kambaka mgameso munhu ija msuwameso.
7 Yesu kamulongela, “Genda kasunhe kihanga chako hana dilamba da
Siloamu.” Siloamu fambulo jake “Yatumigwe.” Avo munhu ija kachola,
kasunha kihanga chake, kabwela yolola.
8 Wanhu weli mmabehi nayo, na wanhu wamonile aho umwaka yopula,
ing'hali hainalawililа mbuli ino, wauza, “Vino ino siyo munhu ija yakalile
na kupula?”
9 Wanhu wayagwe walonga, “Iyo heyo,” lakini wayagwe walonga, “Aka,
siyo heyo, kaigala nayo.”
Avo munhu ija kalonga mwenyego, “Iyo niye.”
10 Wamuuza, “Vino kudahaze kulola?”
11 Kawedika, “Munhu yokemigwa Yesu katenda nhope, kanibaka
mgameso gangu, kanilongela nigenda Siloamu nikasunhe kihanga changu.
Avo nichola, na bahaja vinisunhile nidaha kulola.”
12 Wamuuza, “Munhu ayo kakwahi?”
Kawedika, “Mmhane.”

*Mafalisayo wozahila munhu msuwameso kahonyigwa vilihi*

13 Abaho wamgala kwa Mafalisayo munhu ayo yakalile msuwameso.
14 Yesu viyatendile nhope na kumuhonya munhu ayo yakalile
msuwameso ikala siku ya Kubwihila.

15 Abaho Mafalisayo wamuuza kabili munhu ayo viyadahile kulola. Kawalongela, “Kanibaka nhope mgameso gangu, nisunha kihanga changu, na sambi nodaha kulola.”

16 Mafalisayo wayagwe walonga, “Munhu yatendile mbuli ino halawa kwa Mulungu bule, kwavija hadigoga lagizo da siku ya Kubwihila.”

Lakini wayagwe walonga, “Vino munhu yotenda nzambi kodahaze kutenda unzonza kamba uno?” Avo, wakala waigolile.

17 Avo Mafalisayo wabwelela kumuuza munhu ayo, “Kulonga kakuhonya usuwameso wako. Gweye kolongaze mbuli ya munhu ayo?”

Munhu ayo kawedika, “Mtula ndagu wa Mulungu.”

18 Hata ivo wakulu wa Wayahudi hawalondile kutogola kamba kakala msuwameso na sambi kodaha kulola. Avo wawakema tatake na mamake,

19 Wayahudi wawauza, “Vino ino ayo mwanenu? Yumulonga kavumbuka msuwameso, lelo kadahaze kulola?”

20 Tatake na mamake wawedika, “Tojuwa kamba heyo ayo mwanetu, na tojuwa kamba kavumbuka msuwameso.

21 Lakini hatujuwile sambi viyadahile kulola, wala hatumjuwile munhu yamuhonyile. Muuzeni mwenyego, heyo mkulu goya, kodaha kuwedika!”

22 Tatake na mamake walonga vino kwavija wakala wowadumba wakulu wa Wayahudi, kwavija Wayahudi walonga munhu yoyose yolonga komtogola Yesu kamba ayo Kilisito Mkombola kowingigwa mng'anda ya kumpula Mulungu.

23 Lekaavo tatake na mamake walonga, “Heyo mkulu goya, muuzeni!”

24 Mwanza wa kabili wamkema munhu ija yavumbuke msuwameso, wamulongela, “Iduile kwa Mulungu kamba kolonga ukweli! Tojuwa kamba munhu ino yakuhonyile kotenda nzambi.”

25 Munhu ayo kawedika, “Mmhane kamba munhu ayo kotenda nzambi hebu hatenda bule. Kinhu kimoja kinjuwile, ng'hala silola, sambi nolola.”

26 Wamuuza, “Vino kakutendela choni? Kakuhonyaze usuwameso wako?”

27 Kawedika, “Nimala kuwalongela, lakini hamulonda kutegeleza. Vino habali molonda kuihulika kabili? Hebu na mweye vivija molonda kuwa wanahina zake?”

28 Wamuliga na kumulongela, “Gweye kwa mwanahina wa munhu ayo! Tweye twa wanahina wa Musa.

29 Tojuwa kamba Mulungu kalonga na Musa, lakini kwa munhu ayo, hatujuwile kolawa kwahi!”

30 Munhu ija kawedika, “Mweye monyazanya! Hamkujuwile kuyalawile, lakini kanitenda nidahe kulola!

31 Tojuwa kamba Mulungu hawategeleza wanhu wotenda nzambi, lakini kowategeleza wanhu waja womtegeleza heyo na kusang'hana gaja goyolonda.

32 Tangu chanduso cha isi yose kuduhu munhu yahulike kamba munhu yoyose kamuhonya munhu yavumbuke msuwameso.

33 Maza munhu ino halawile kwa Mulungu, sambi yadahe kutenda mbuli ino.”

34 Wamwidika, “Gweye kuvumbuka na kukulila mzizambi abaho kolonda kutufunza tweye?” Avo wamuwinga mna ing'anda ya kumpula Mulungu.

### *Usuwameso wa loho*

35 Yesu viyahulike kamba wamuwinga mng'anda ya kumpula Mulungu, kamona munhu ayo kamuuza, “Vino gweye komtogola Mwana wa Munhu?”

36 Munhu ayo kamwidika, “Go mkulu, nongela ayo nani, mhate kumtogola!”

37 Yesu kamulongela, “Kumona, ayo heyo yolonga na gweye sambi.”

38 Munhu ayo kalonga, “Notogola Mndewa.” Abaho kamfugamila Yesu.

39 Yesu kalonga, “Niza mwiisi ino kuwatagusa wanhu, avo waja hawalola walole na waja wogesa wolola waleke kulola.”

40 Mafalisayo wayagwe wakalile hamoja na Yesu viwamuhulike kolonga avo, wamuuza, “Vino kolonga na tweye vivija hatulola?”

41 Yesu kawedika, “Maza mkalile hamulola, sambi mutende nzambi. Lakini kwavija molonga mulola, avo mung'hali motenda nzambi.”

# 10

### *Lusimo lwa msusilaji*

1 Yesu kalonga, “Nowalongela ukweli, munhu yoyose yoleka kubitila hana ulwivi lwa ng'hondolo, lakini kokwela na kubitila nzila iyagwe, munhu ayo mbavi na mbokaji.

2 Munhu ija yobitila hana ulwivi ayo msusilaji wa ng'hondolo.

3 Mkalizi wa ulwivi komvugulila ulwivi, ng'hondolo wokihulika kifengwa cha msusilaji viyowakema ng'hondolo zake kwa matwaga gao, kowalava kunze.

4 Yahawalava kunze kowalongolela, na ng'hondolo womkweleleza kwavija wakijuwa kifengwa chake.

5 Honda wamkweleleze munhu yoyose iyagwe, lakini womkimbila munhu ayo kwavija hawakijuwile kifengwa chake.”

6 Yesu kawalongela lusimo luno lakini hawajuwile fambulo jake.

### *Yesu ayo msusilaji yanogile*

7 Avo Yesu kalonga kabili, “Nowalongeleni ukweli, niye ayo lwivi lwa ng'hondolo.

8 Wose wayagwe wezile kukisogo changu wabavi na wabokaji, lakini ng'hondolo hawawategeleze bule.

9 Niye ayo lwivi. Munhu yoyose yobitila kumwangu kokomboligwa, kokwingila na kulawa kuzahila chakuja.

10 Mbavi kokwiza muladi yebe, yakome, na kunanga. Niye niza muladi muwe na ugima, ugima umemile.

11 “Niye ayo msusilaji yanogile. Msusilaji yanogile koulava ugima wake mbuli ya ng'hondolo.

12 Munhu wa kulipigwa yeli siyo msusilaji na ng'hondolo haweli wake, yahamona mbwizi kokwiza, kowaleka ng'hondolo na kukimbila. Avo mbwizi kogoga imoja na wayagwe wopwililika.

13 Munhu wa kulipigwa kokimbila kwavija heyo munhu wa kulipigwa kwiiyeka, na hawatonga bule ng'hondolo.

14 Niye ayo msusilaji yanogile. Niwajuwa ng'hondolo zangu na wao wonijuwa niye,

15 kamba Tata viyonjuwa niye, na niye vinimjuwa Tata. Na niye nodaha kufa mbuli yao.

16 Abaho ninao ng'hondolo wayagwe siyo wa mdizizi dino. Vivija nolondeka niwagale, wokihulika kifengwa changu, nao wokuwa bumbila dimoja da msusilaji imoja.

17 “Tata koninogela kwavija noulava ugima wangu kwa kulonda mwenyego, muladi nidahe kuubweza kabili.

18 Kuduhu munhu youlava ugima wangu. Niye noulava kwa kulonda mwenyego. Ninao udahi wa kuulava, na udahi wa kuubweza kabili. Vino vivo viyanilagize Tata nhende."

19 Mbuli zino za Yesu ziwatenda Wayahudi waigole kabili.

20 Wanhu wengi wakala wolonga, "Kana kinyamkela, vivija kana kibozi mbwelela! Habali mumtegeleza?"

21 Lakini wanhu wayagwe wakala wolonga, "Munhu yeli na kinyamkela hadaha kulonga kamba vino! Vino kinyamkela kodahaze kuwahonya wasuwameso?"

### *Yesu kolemigwa*

22 Ako Yelusalemu kukala na nyimwili nyimwili ya kulavigwa kwa Ng'anda ya Mulungu kwa Mulungu. Kikala kipindi cha kihuhwe.

23 Yesu kakala kotembela mna uluhelengo lwa Sulemani hana Ing'anda ya Mulungu,

24 Wayahudi wamzunguluka, wamuuza, "Vino gweye kotugaza mbaka lini? Tulongele fulu ipile, gweye kwa Kilisito Mkombola?"

25 Yesu kawedika, "Nimala kuwalongeleni, lakini hamnhogola. Mbuli zinhenda kwa udahi wa Tatangu zonilagusa,

26 lakini honda mtogole, kwavija hamuli ng'hondolo zangu.

27 Ng'hondolo zangu woihulika sauti yangu, niye niwajuwa na wao wong'holeleza.

28 Nowagwaa ugima wa mazuwa gose, na honda wafe bule. Kuduhu munhu yonda yawasole mmakono gangu.

29 Tatangu yanigwelele awo ayo mkulu kubanza wose, na kuduhu yodaha kuwasola mmakono ga Tata.

30 Niye na Tata twa wamoja."

31 Abaho Wayahudi wadondola mabwe kabili wamtowe Yesu.

32 Yesu kawalongela, "Nhenda mbuli nyingi zinogile mgameso genu zija ziyanigwelele Tata nhende, kwa mbuli gani molonda kunhowa mabwe?"

33 Wayahudi wamwidika, "Hatulonda kukutowa na mabwe mbuli ya mbuli yoyose inogile, lakini mbuli ya ukuduzi wako! Gweye kwa munhu, lakini koitenda mwenyego kwa Mulungu!"

34 Yesu kawedika, "Vino hayandikigwe mna Ikitabu chenu cha malagizo kamba Mulungu kalonga, 'Mweye mwa walungu?'

35 Mulungu kawakema 'walungu' wanhu waja wagweleligwe usenga wake, na tweye tojuwa kamba Maandiko Gang'alile golonga ukweli siku zose.

36 Kamba viili kumwangu, Tata kanisagula na kanhuma mwiisi. Yokuwaze kabili mweye molonga nomkudula kwavija nonga niye na Mwana wa Mulungu?

37 Kamba sitenda gaja goyolonda Tatangu nhende, sekemunhogole.

38 Lakini kamba nogatenda, hata kamba hamnitogola niye, molondeka mutogole gaja ganisang'hane, muladi mujuwe kamba Tata kokala mgati mmwangu na niye nokala mgati mwa Tata."

39 Bahaja walonda kumgoga Yesu, lakini kawalawa mmakono gao.

40 Abaho Yesu kabwela kabili mwambu wa lwanda lwa Yolidani mbaka aho haakalile Yohana yobatiza wanhu, kakala kuko.

41 Wanhu wengi wamcholela, walonga, "Yohana hatendile unzonza, lakini kila kinhu kiyalongile mbuli ya munhu ino cha ukweli."

42 Wanhu wengi wa ako wamtogola Yesu.

# 11

### *Kufa kwa Lazalo*

1 Munhu yakemigwe Lazalo yakalile kudibuga da Betania kakala mtamu.
Betania dijo buga diwakalile Malia na mkulu wake Mata.
2 Malia ino ayo yambakaze Mndewa mavuta gonung'hila goya mmagulu
na kuhangusa kwa mvili zake. Lazalo lumbu jake ayo yakalile mtamu.
3 Avo lumbu zake Lazalo wamgalila Yesu usenga, "Mndewa, mbwigako
yuumnogele mtamu."
4 Yesu viyahulike avo, kalonga, "Utamu awo honda ugale ifa. Uno ulawilila
kugala nhogolwa kwa Mulungu, na vivo vonda iwe kwa Mwana wa Munhu
kobokela nhogolwa."
5 Yesu kawanogela Mata na mdodo wake Malia na lumbu jao Lazalo.
6 Viyabokele usenga uno kamba Lazalo kakala mtamu, Yesu kongeza siku
mbili kukala aho haakalile.
7 Abaho Yesu kawalongela wanahina zake, "Tubweleni Yudea."
8 Wanahina wamwidika, "Mfundiza, sambi sambi Wayahudi wa aho
walonda kukutowa mabwe, abaho kofunga mwanza ubwele kuko?"
9 Yesu kalonga, "Vino imisi yaduhu masaa longo na mabili? Avo wanhu
wogenda imisi hawaikwala, kwavija wowona mulenge wa mwiisi ino.
10 Lakini kamba wahagenda ikilo woikwala kwavija waduhu mulenge."
11 Yesu viyamambukize kulonga avo, kalonga, "Mbwigaetu Lazalo
kawasa, lakini nochola kumulamusa."
12 Wanahina wamwidika, "Mndewa, kamba kawasa kohona."
13 Yesu kakala yofambula kamba Lazalo kafa, lakini wanahina zake
wagesa kakala yolonga kuwasa utulo.
14 Avo Yesu kawalongela fulu ipile, "Lazalo kafa,
15 lakini nodeng'helela mbuli yenu kwavija sikalile nayo muladi mutogole.
Leka tucholeni kumwake."
16 Tomaso yakemigwe Pacha kawalongela wanahina wayage, "Tucholeni
hiko hamoja na Mfundiza, tukafe nayo!"

### *Yesu ayo uzilibuko na ugima*

17 Yesu viyavikile ako, kaluvika lukuli lwa Lazalo lwa mdipanga siku nne.
18 Betania ikala utali wa kamba kilometa ndatu kulawa Yelusalemu,
19 Wayahudi wengi weza kuwalola Mata na Malia na kuwagoga makono
mbuli ya ifa ya lumbu jao.
20 Mata viyahulike kamba Yesu kakala yokwiza, kalawa kunze kumbokela,
lakini Malia kasigala mng'anda.
21 Mata kamulongela Yesu, "Mndewa, maza ukalile baha lumbu jangu
sambi yafe bule!
22 Lakini hata sambi nojuwa kamba Mulungu kokugwaa kinhu chochose
kiumpula."
23 Yesu kamulongela, "Lumbu jako kozilibuka."
24 Mata kedika, "Nojuwa kamba kozilibuka mna isiku ya uhelelo."
25 Yesu kamulongela, "Niye ayo uzilibuko na ugima. Wanhu wose won-
hogola wokuwa wagima, hata wahafa,
26 na wanhu wose weli wagima na wonhogola niye honda wafe bule.
Kozitogola mbuli zino?"
27 Mata kedika, "Ona Mndewa, notogola kamba gweye ayo Kilisito Mkom-
bola, Mwana wa Mulungu ija yezile mwiisi."

*Yesu kolila*

28 Mata viyalongile avo, kabweleganya mng'anda, kamkema mkulu wake Malia kinyelegezi. Kamulongela, “Mfundiza kabaha, kokukema gweye.”

29 Malia viyahulike avo, kenuka himahima kamcholela Yesu.

30 Yesu kakala yang'hali hanavika mkijiji, lakini kakala hanhu aho haamting'hane Mata.

31 Avo, Wayahudi wakalile mng'anda na Malia womgoga makono, wamkweleleza viwamone kenuka himahima na kuchola kunze. Wagesa kochola kudipanga kulila.

32 Malia kavika aho haakalile Yesu, bahaja viyamone, kamfugamila, kalonga, “Mndewa, maza ukalile baha, lumbu jangu sambi yafe bule!”

33 Yesu viyamone Malia kolila, na Wayahudi wakalile nayo wolila vivija, kona usungu na kanyunyuwala muumoyo.

34 Yesu kawauza, “Mumzikila kwahi?”

Wamwidika, “Mndewa izo ulole.”

35 Yesu kalila.

36 Wayahudi walonga, “Loleni viyamnogele Lazalo.”

37 Lakini wanhu wayagwe walonga, “Kamuhonya munhu msuwameso, hadahile vilihi kumtenda Lazalo sekeyafe?”

*Lazalo kozilibuka*

38 Yesu viyakalile yang'hali konyunyuwala muumoyo, kachola kudipanga, dikalile mhango igubikigwe na dibwe.

39 Yesu kawalagiza, “Segezeni idibwe!”

Mata, lumbu wa munhu ija yafile, kedika, “Mndewa, kwiza honung'ha bundo, kwavija kana siku nne toka yazikigwe!”

40 Yesu kamulongela, “Vino sikulongele bule wahatogola kouwona ukulu wa Mulungu?”

41 Wadikwesa hamgwazo idibwe, Yesu kalola uchanha kalonga, “Nokugwaa nhogolwa gweye Tata, kwavija konhegeleza.

42 Nojuwa kamba siku zose konhegeleza, lakini nolonga vino mbuli ya wanhu weli hano, ili watogole gweye kunhuma.”

43 Viyamambukize kulonga avo, kakemelela, “Lazalo, lawa kunze!”

44 Lazalo kalawa kunze kuno makono gake na magulu gake gazingilizigwa sitili, na leso mkihanga chake. Yesu kawalongela, “Mfunguleni mulekeni yachole.”

*Kiseto cha kumkoma Yesu*

*Mat 26:1-5; Mlk 14:1-2; Luk 22:1-2*

45 Wayahudi wengi wacholile kumtembelela Malia wachona kiyatendile Yesu, wamtogola.

46 Lakini wanhu wayagwe wabwela kwa Mafalisayo, wawalongela kija kiyatendile Yesu.

47 Avo Mafalisayo na wakulu wa walava nhosa waiting'hana na wanhu wa
mkitala waiuza, “Vino tutende choni? Loleni mbuli za unzonza ziyotenda
munhu ino! 48 Kamba twahamuleka yagendelele vivo, kila munhu komto-
gola, na wakulu wa Walumi wokwiza na kuinanga Ng'anda yetu ya Mulungu
na isi yetu!”

49 Imoja wao, yakemigwe Kayafa, yakalile Mkulu wa walava nhosa, kalonga, “Mweye mwa wabozi!

50 Vino hamona kamba vinoga ng'hani kumwenu munhu imoja yafe mbuli ya wanhu, kubanza isi yose inangigwe?”

51 Halongile vino kwa kugesa mwenyego, lakini kwavija kakala Mkulu
wa walava nhosa mwaka awo, kakala yolagula kamba Yesu kofa mbuli ya
Wayahudi,
52 na siyo kwa Wayahudi waiyeka, lakini vivija kuwagala hamoja wanhu
wa Mulungu wapwililike wawe wamoja.
53 Kulawa siku dijo wakulu wa Wayahudi wamkalila kiseto Yesu
wamkome.
54 Avo Yesu hacholile kunze kunze mwiisi ya Yudea, lakini kasegela
kachola behi na luwala, kunadibuga dikemigwe Efulahimu, kakala kuko na
wanahina zake.
55 Kipindi cha nyimwili nyimwili ya Pasaka ya Wayahudi kikala behi
kuvika, avo wanhu wengi wachola Yelusalemu ili waisunhe, nyimwili ny-
imwili ing'hali hainavika.
56 Wakala womzahila Yesu, na viwaiting'hane Mng'anda ya Mulungu,
waiuza, "Vino mogesaze? Hambe Yesu honda yeze mwiinyimwili ny-
imwili?"
57 Wakulu wa walava nhosa na Mafalisayo walagiza kamba munhu yoyose
kakujuwa kuyali Yesu yalonge, ili wamgoge.

# 12

*Yesu kobakigwa mavuta ako Betania*
*Mat 26:6-13; Mlk 14:3-9*

1 Zing'hali siku sita kuvika nyimwili nyimwili ya Pasaka, Yesu kachola
Betania, ukayake Lazalo, ayo iyamzilibule kulawa kwa wafile.
2 Wanhu wamtandila lujo lwa ichungulo baho, Mata ayo yakalile yomtaza
kugola. Lazalo kakala imoja mna iwanhu wakalile woja na Yesu.
3 Abaho Malia kasola nusu lita ya mavuta gonung'hila goya ga bei ng'hulu
ng'hani, kambakaza Yesu mmagulu, kagahangusa kwa mvili zake. Ng'anda
yose ikala bwiki bwiki mbuli ya gaja gamavuta gonung'hila goya.
4 Yuda Isikaliote imoja wa wanahina zake Yesu, ayo yonda yamuhinduke
Yesu, kalonga,
5 "Vino habali mavuta gano hagauzigwe kwa sente magana madatu, na
sente azo wagweleligwe wanhu wakiwa?"
6 Kalonga vino siyo kwavija kakala yowatonga wakiwa, lakini kwavija
kakala mbavi. Kakala mpapaji wa mkoba wa zisente, na miyanza mingi
kakala yosola sente.
7 Lakini Yesu kalonga, "Sekemumgaze! Mulekeni yatende vivo mbuli ya
siku yangu ya kuzikigwa.
8 Wanhu wakiwa mokala nao siku zose, lakini hamkala na niye siku zose."

*Kiseto cha kumkoma Lazalo*

9 Wayahudi wengi wahulika kamba Yesu kakala Betania, avo wachola
kuko, siyo mbuli ya Yesu yaiyeka lakini vivija kumona Lazalo, ayo
iyamzilibule.
10 Avo wakulu wa walava nhosa wakala kiseto cha kumkoma Lazalo vivija,
11 kwavija mbuli ya Lazalo Wayahudi wengi wakala wowalema na kum-
togola Yesu.

*Yesu kokwingila Yelusalemu kwa ng'henze*
*Mat 21:1-11; Mlk 11:1-11; Luk 19:28-40*

12 Imitondo yake lunhu mkulu lwizile kuna inyimwili nyimwili ya Pasaka
luhulika kamba Yesu kakala yokwiza Yelusalemu.

13 Avo wabena mibunho ya mbiki wa mtende na wachola kumbokela, wakemelela,
“Mulungu yatogolwe!
Mulungu yamtambikile munhu ayo yokwiza kwa twaga da Mndewa!
Mulungu yamtambikile Mndewa wa Izilaeli!”
14 Yesu kamona mwana mhunda, kamkwela mumgongo, kamba Maandiko Gang'alile vigalonga,
15 “Sekeudumbe, isi ya Sayuni!
Hano kokwiza Mndewa wako,
yakwelile mumgongo wa mwana mhunda.”
16 Kipindi acho wanahina zake hawaijuwile mbuli ino. Lakini Yesu viyenuligwe muukulu, wakumbuka kamba Maandiko Gang'alile galonga mbuli ino na wamtendela kamba vivo.
17 Wanhu wakalile na Yesu kipindi viyamkemile Lazalo kulawa mdipanga na kumzilibula kulawa kwa wafile, wakala wogabwililisa gaja galawilile.
18 Lekaavo lunhu lwa wanhu luchola kumbokela, kwavija luhulika unzonza uno uyatendile.
19 Abaho Mafalisayo wailongela, “Mona, hatudaha kutenda chochose! Loleni wanhu wose wa mwiisi womkweleleza!”

### *Wagiliki wolonda kulonga na Yesu*

20 Wagiliki wayagwe wakala mumo mna iwanhu wacholile Yelusalemu kutambika mna ikipindi cha nyimwili nyimwili ya Pasaka.
21 Wachola kwa Filipo mwenekae wa Betisaida mwiisi ya Galilaya walonga, “Go mkulu, tolonda tumone Yesu.”
22 Filipo kachola na kumulongela Andeleya, abaho wose wabili wachola kumulongela Yesu.
23 Yesu kawedika, “Sambi kipindi kivika cha Mwana wa Munhu kubokela ukulu.
24 Nowalongeleni ukweli, mhule ya uhemba yosigala imoja siku zose mbaka ilagale hasi ife. Ila yahafa baho yolela na kuwa mhule nyingi.
25 Munhu yoyose younogela ugima wake kowagiza, lakini munhu yoyose yowihila ugima wake mwiisi ino kowika kwa ugima wa mazuwa gose.
26 Munhu yoyose yolonda kuwa msang'hanaji wangu kolondeka yanikweleleze, avo msang'hanaji wangu kokuwa na niye aho honda niwe. Tatangu komgwaa nhogolwa munhu yoyose yonisang'hanila.

### *Yesu kolonga mbuli ya ifa yake*

27 “Sambi loho yangu yoluma, vino nongeze? Nonge, ‘Tata, sambiutende kipindi kino kivike kumwangu’? Lakini lekaavo niza ili nibite kipindi kino cha madununzo.
28 Tata, uditogole twaga jako!”
Abaho sauti ihulikigwa kulawa kuulanga, “Niditogola, na notenda vivo kabili.”
29 Lunhu lwimile aho luihulika sauti ayo, na wanhu wayagwe walonga, “Mulungu kaduma.” Kuno wayagwe walonga, “Msenga wa kuulanga kalonga nayo!”
30 Lakini Yesu kawalongela, “Sauti ino haihulikigwe mbuli ya niye, lakini mbuli yenu.
31 Sambi acho kipindi cha wanhu wa mwiisi ino kutagusigwa, na Mwenembago mkulu wa mwiisi ino kokwasigwa.
32 Kipindi nahenuligwa uchanha kulawa hasi, nomkwega kila munhu kumwangu.”

33 Kwa ulonzi uno Yesu kalagusa ifa yonda yafe.
34 Lunhu lwa wanhu lumwidika, “Malagizo getu gotulongela kamba Kil-
isito Mkombola kokuwa mgima siku zose. Habali kabili gweye kolonga
Mwana wa Munhu kolondeka yenuligwe uchanha? Vino ino Mwana wa
Munhu ayo nani?”
35 Yesu kawedika, “Mulenge wokala na mweye kwa kipindi kidodo.
Gendeleleni na mwanza kung'hali na mulenge muladi ziza sekediwezile,
kwavija munhu yotembela mdiziza hajuwa kuja kuyochola.
36 Utogoleni mulenge baho mulinao muladi muwe wanhu wa mulenge.”

### *Wanhu wolema kumtogola Yesu*

Yesu viyamambukize kulonga avo, kasegela, wanhu hawamonile.
37 Hamoja Yesu kasang'hana unzonza mgameso gao, lakini hawamtogole
bule.
38 Avo kiyalongile mtula ndagu wa Mulungu Isaya kilawilile.
“Mndewa, nani yatogole usenga wetu utulongile?
Vino Mulungu kalagusa udahi wake kwa nani?”
39 Avo hawadahile kutogola, kwavija Isaya vivija kalonga,
40 “Mulungu kagafumba meso gao
kazifunga nzewele zao,
muladi meso gao sekegadahe kulola,
na nzewele zao sekezidahe kujuwa.
Sekewanibwelele niye, Mulungu kolonga,
na niye nidahe kuwahonya.”
41 Isaya kalonga vino kwavija kawona ukulu wa Yesu na kalonga mbuli
yake.
42 Avo wakulu wengi wa Wayahudi wamtogola Yesu, lakini mbuli ya
Mafalisayo hawadahile kulonga mbuli zake kunze kunze, kwavija wad-
umba kuwingigwa mna ing'anda ya kumpula Mulungu.
43 Kwavija walonda nhogolwa za wanhu kubanza nhogolwa za Mulungu.

### *Mbuli ya Yesu yotagusa wanhu*

44 Yesu kakemelela, “Munhu yoyose yonhogola niye, hanhogola niye
niiyeka lakini vivija komtogola ija yanhumile.
45 Yoyose yonyona niye vivija komona ija yanhumile.
46 Niye niza mwiisi niwe mulenge, ili munhu yoyose yonhogola sekeyasi-
gale mdiziza.
47 Munhu yoyose youhulika usenga wangu na halonda kuutogola, niye
simtagusa bule, kwavija sizile kuwatagusa wanhu wa mwiisi, ila kuwakom-
bola.
48 Wose wonilema niye na kuulema usenga wangu kabaho imoja yonda
yawataguse. Mbuli zinongile zowatagusa mwiisiku ya uhelelo!
49 Kwavija silongile kwa udahi wangu, lakini Tata yanhumile kanilagiza
vinondeka kulonga.
50 Na niye nojuwa kamba lagizo jake dogala ugima wa mazuwa gose. Avo
nolonga gaja gayanilongele Tata nonge.”

## 13

### *Yesu kowasunha magulu wanahina zake*

1 Dikala ding'hali siku dimoja kuvikila nyimwili nyimwili ya Pasaka. Yesu
kajuwa kamba kipindi chake kivika cha kusegela mwiisi ino na kuchola
kwa Tatake. Yesu kakala yawanogele ng'hani wanhu zake weli mwiisi,
kawanogela siku zose.

2 Yesu na wanahina zake wakala muulujo lwa ichungulo. Mwenembago kakala yamalile kwingila muumoyo wa Yuda mwanage Simoni Isikaliote, yamuhinduke Yesu.

3 Yesu kajuwa kamba Tata kamgwaa vinhu vose mmakono gake. Na kajuwa kamba kalawa kwa Mulungu na kochola kwa Mulungu.

4 Avo kenuka muulujo, keka hamgwazo mgolole wake, kasola kikumbi, kaifunga mkigudi.

5 Abaho kagida mazi mwiinongo, kasonga kuwasunha magulu wanahina zake na kuwahangusa kwa kija kikumbi kiyaifungile mkigudi.

6 Yesu kavika kwa Simoni Petulo, lakini Petulo kamuuza, “Mndewa, vino gweye kolonda kunisunha magulu niye?”

7 Yesu kamwidika, “Kinhenda sambi gweye hukijuwa bule, lakini baho kumwande kokijuwa.”

8 Petulo kalonga, “Aka, gweye hunisunha magulu gangu hata siku dimoja!”

Yesu kamwidika, “Kamba sikusunha magulu gako, honda uwe mwanahina wangu bule.”

1 Siku dimoja saa tisa ya imisi kipindi cha kumpula Mulungu, Petulo na Yohana wakala wochola kuna Ing'anda ya Mulungu.
2 Kipindi acho wanhu wakala wampapile munhu imoja mbetembete toka viyavumbuke. Kila siku wakala womwika munhu ayo hana ulwivi lwa Ng'anda ya Mulungu lukemigwe, “Lwivi lunogile” muladi yapule sente kwa wanhu wakalile wokwingila Mng'anda ya Mulungu.
3 Viyawone Petulo na Yohana wokwingila Mng'anda ya Mulungu, kawapula wamgwee kinhu chochose.
4 Nao wamulola munhu ayo bunhuu. Petulo kamulongela, “Tulole tweye!”
5 Avo kawalola bunhuu, kuno kotamanila kupata kinhu chochose kulawa kumwao.
6 Lakini Petulo kamulongela, “Nabule sente, ila nokugwaa kija kinilinacho, kwa twaga da Yesu Kilisito wa Nazaleti, nokulagiza ima wima utembele!”

7 Abaho kamgoga kwa mkono wake wa kudila kamwinula. Na bahaja mige ya magulu gake igangamala.

8 Kenuka, kema kwa magulu gake, kasonga kutembela. Abaho kengila Mng'anda ya Mulungu hamoja nao, kuno kozumha zumha na kumtogola Mulungu.

9 Wanhu wose viwamone kotembela na komtogola Mulungu,

10 wamjuwa kamba heyo yakalile yopula hana, “Ulwivi Lunogile,” avo wose wakanganya kija kimulawilile munhu ayo.

### *Usenga wa Petulo Mng'anda ya Mulungu*

11 Kuno munhu ayo yang'hali kowawinza Petulo na Yohana hana, “Uluhelengo lwa Sulemani,” kamba vilukemigwe, wanhu wose wakanganya na wasonga kuwakimbilila.

12 Petulo viyawone wanhu, kawalongela, “Ndugu zangu wa Izilaeli, habali moikanganya mbuli ino, habali motubunhulila meso? Vino mogelegeza mbuli ino ilawilila kwa udahi wetu kumtenda munhu ino yatembele hebu kwavija tweye tomtambikila Mulungu?

13 Mulungu wa Abulahamu na Isaka na Yakobo na Mulungu wa wahenga zetu, kamgwaa ukulu mtumigwa wake Yesu. Lakini mumgela mmakono ga iwakulu, mumulema haulongozi ha Pilato, hata Pilato viyalondile kumulekesa.

14 Kakala yang'alile na yanogile, lakini mweye mumulema, mumpula Pilato yawatendele vimulonda, yawafungulile munhu mkomaji.

15 Mumkoma ayo yakalile chanduso cha ugima, lakini Mulungu kamzilibula kulawa kwa wafile na tweye tuyona mbuli ayo.

16 Udahi wa twaga da Yesu awo umgwelele nguvu munhu ino mbetembete. Kino kimona na kukijuwa kitendigwa kwa kutamanila kwa twaga jake. Kumtamanila Yesu ako kumtendile munhu ino yahonyigwe, kamba mose vimona.

17 “Sambi, ndugu zangu, nojuwa kija kimumtendele Yesu mweye na wakulu zenu mukala hamkijuwile.

18 Mulungu kalonga mbuli ino toka mwaka ilawilile kubitila watula ndagu zake wose, kamba Kilisito wake Mkombola kolondeka yadununzike, na vino vivo ili.

19 Lelo lekeni nzambi zenu mumbwelele Mulungu, muladi Mulungu yazigele kumgongo nzambi zenu.

20 Mwahatenda avo, kipindi cha kuhozigwa moyo chokwiza kulawa kwa Mndewa, na komtuma Yesu, yeli Kilisito Mkombola yasaguligwe mbuli yenu.

21 Kolondeka yasigale kuulanga mbaka kipindi kivike cha kugatenda gose gawe ga sambi, kamba viyalongile Mulungu kubitila watula ndagu zake wang'alile wakalile kuko umwaka.

22 Kwavija Musa kalonga, ‘Mndewa Mulungu wenu kowagalileni mtula ndagu wake, kamba viyanhumile niye, kokuwa imoja wa wanhu zenu. Mutogole chochose chonda yawalongeleni.

23 Munhu yoyose yolema kumtegeleza mtula ndagu ayo wa Mulungu kobaguligwa mna iwanhu wa Mulungu na kokomigwa.’

24 Na watula ndagu wa Mulungu wose wakalile na usenga, kusongela Samweli na wayagwe wezile kumwande, vivija walonga vinhu vilawilila mzisiku zino.

25 Lagano da Mulungu kubitila watula ndagu zake ni jenu, na mweye mwamgati mna idilagano da Mulungu yaditendile kwa wahenga zenu.

Kamba viyalongile kwa Abulahamu, ‘Kubitila lukolo lwako nowatenda wanhu wose wa mwiisi wamwede.’
26 Avo Mulungu viyamzilibule mtumigwa wake, tanhu kamtuma kumwenu, mumwede na kuwatenda mweye muleke nzambi zenu.”

# 4

*Petulo na Yohana wogaligwa mkitala cha Wayahudi*

1 Petulo na Yohana viwakalile wang'hali wolonga na wanhu, walava nhosa, wakulu wa wakalizi wa Ng'anda ya Mulungu, na Masadukayo wayagwe wavika.
2 Wagevuzika ng'hani kwavija watumigwa wao wabili wakala wowafundiza wanhu kuwa Yesu kazilibuka kwa wafile, na ino ilagusa kamba wafile wozilibuka.
3 Avo wawagoga na kuwagodeka mkifungo mbaka imitondo yake, kwavija zuwa dikala dihongile.
4 Lakini wanhu wengi wauhulike usenga watogola, na wambigalo wongezeka mbaka gana malongo matano.
5 Siku diyagwe wakulu wa Wayahudi, wavele, na wafundiza Malagizo ga Musa waiting'hana Yelusalemu.
6 Waiting'hana na Anasi mulava nhosa mkulu, na Kayafa na Yohana na Alekizanda, na wanhu wayagwe wa lubuga lwa mulava nhosa mkulu.
7 Waweka Petulo na Yohana haulongozi wao, wawauza, “Vino mweye mutendaze? Nguvu gani yumpatile hebu mosang'hana kwa twaga da nani?”
8 Petulo kuno kamema Loho Yang'alile, kawedika, “Walangulizi wa wanhu na wavele!
9 Kamba lelo touzigwa mbuli ya kija kinogile kitendigwe kwa munhu yabemendeke magulu na vija viyahonyigwe,
10 avo molondeka mose mujuwe, na wanhu wose wa Izilaeli mujuwe, kamba munhu ino yemile haulongozi wenu kahona kwa twaga da Yesu Kilisito wa Nazaleti, ayo yummuwambile mumsalaba na Mulungu kamzilibula kulawa kwa wafile.
11 Yesu iyo yolongigwa mna Gamaandiko Gang'alile,
‘Dibwe dilemigwe na mweye wazengaji
digalamuka dibwe da kutamanila kubanza gose.’
12 Ukombozi haupatikana kwa munhu yoyose iyagwe, kwavija mwiisi yose kuduhu twaga diyagwe diyatugwee Mulungu donda tukomboligwe najo.”
13 Wakulu wa mkitala wakanganya kona vija Petulo na Yohana viwagangamale, kwavija wawajuwa kamba hawaifunzile ubala wowose. Abaho wajuwa kamba wakala mbwiga zake Yesu.
14 Lakini viwamone munhu ayo yahonyigwe kema hamoja na Petulo na Yohana, hawadahile kulonga mbuli.
15 Avo wawalongela walawe mdigati da ikitala, abaho wakulu wa mkitala wasonga kuilongela wenyego.
16 Wakulu wa mkitala waiuza, “Tuwatende choni wanhu wano? Kila munhu mwiisi ya Yelusalemu kojuwa kamba unzonza uno mkulu utendigwa na hewo, na tweye hatudaha kuibela bule mbuli ino.
17 Lakini kutenda mbuli ino sekeibwililike ng'hani kwa wanhu, leka tuwazume wanhu wano waleke kulonga kwa munhu yoyose kwa twaga da Yesu.”
18 Avo wawakema kabili mng'anda, wawazuma sekewalonge hebu kufundiza kwa twaga da Yesu.

19 Lakini Petulo na Yohana wawedika, “Mweye wenyego taguseni choni kinogile mgameso ga Mulungu, kuwategeleza mweye hebu kumtegeleza Mulungu.
20 Kwavija hatudaha kuleka kulonga kija kituwone na tukihulike tweye wenyego.”
21 Avo wanhu wa mkitala wawazuma ng'hani abaho wawalekesa. Hawadahile kuwatagusa, kwavija wanhu wose wakala womgwaa nhogolwa Mulungu mbuli ya kija kilawilile.
22 Munhu yatendiligwe unzonza uno wa kuhonyigwa kakala na miyaka kubanza malongo mane.

### *Wanhu wamtogole Yesu wompula Mulungu yawagangamize*

23 Bahaja Petulo na Yohana viwalekesigwe, wabwela kuna ikibumbila chao na kuwalongela kija kilongigwe na wakulu wa walava nhosa na wavele.
24 Wanhu wamtogole Yesu viwahulike avo, wailumba hamoja mna ukumpula Mulungu, walonga, “Mndewa gweye kuumba ulanga, isi, bahali na vose vilimgati mmwake!
25 Kulonga kubitila muhenga wetu Daudi, mtumigwa wako, kwa udahi wa Loho Yang'alile. Viyalongile,
‘Habali wanhu wa mwiisi yose wagevuzika?
Habali wanhu wokala kiseto cha kibozi?
26 Wandewa wa mwiisi waitanda wenyego,
walangulizi waiting'hana hamoja
kumbiduka Mndewa na Mkombola ayo yaamsagule.’
27 Kwavija Helode na Pontio Pilato waiting'hana hamoja mna idibuga dino da wanhu haweli Wayahudi na wanhu wa Izilaeli kumbiduka Yesu, Mtumigwa wako Yang'alile, Kilisito Mkombola yuumsagule.
28 Watenda mbuli zija ziulondile toka mwaka zilawilile kwa udahi wako.
29 Sambi, gweye Mndewa, ulole mbuli zao zakugela bwembwe ziwatendile. Tutaze tweye wasang'hanaji zako seketudumbe kuwapetela wanhu usenga wako.
30 Golosa mkono wako uwahonye wanhu. Tenda vifukuzi na unzonza kwa twaga da Yesu mtumigwa wako yang'alile.”
31 Viwamambukize kumpula Mulungu, aho hawakalile waiting'hane hatigisika. Wose wamemezigwa Loho Yang'alile na wagendelela kuwapetela wanhu usenga wa Mulungu bila kudumba.

### *Wanhu wamtogole Yesu wokala kamba wanhu wa lubuga lumoja*

32 Kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu wakala na moyo umoja. Kuduhu imoja wao yalongile vija viyakalile navo vikala vake, lakini waigolela na wayao kila kinhu kiwakalile nacho.
33 Watumigwa wawapetela wanhu mbuli ya kuzilibuka kwa Mndewa Yesu kwa nguvu ng'hulu, na Mulungu kawagwaa wanhu ng'hekewa ng'hani.
34 Kukala kuduhu munhu yoyose mkibumbila yakalile bila kinhu. Wanhu wayagwe wakalile na migunda hebu ng'anda wakala wochuuza, na kugala zisente ziwapatile,
35 na wawagwaa watumigwa, na zisente izo zigoligwa kwa kila munhu kamba viyalondile.
36 Kukala na Mulawi imoja twaga jake Yusufu, mwenekae wa Kupulo, ayo watumigwa wamkema Balinaba, fambulo jake, “Munhu yogangamiza wanhu,”
37 kachuuza mgunda wake, kawagwaa zisente watumigwa.

# 5

*Anania na Safila*

1 Kukala na munhu imoja yakemigwe Anania na mwehe wake Safila, nao vivija wachuuza mgunda wao.
2 Anania kailumba na mwehe wake, kabagula sente ziyagwe na zisigale kawagwaa watumigwa.
3 Petulo kamuuza, “Anania, habali kumtogolela Mwenembago yakulongoze umvizile Loho Yang'alile kwa kufisa sente ziyagwe ziupatile kwa kuchuuza mgunda wako?
4 Viukalile ung'hali hunachuuza umgunda ukala wako, na viumambukize kuchuuza, sente zikala zako. Lelo, habali kutenda mbuli ayo? Humvizile munhu bule ila kumvizila Mulungu!”
5 Bahaja Anania viyaihulike mbuli ayo, kagwa hasi kafa. Wanhu wose waihulike mbuli ayo wadumba ng'hani.
6 Wabwanga weza waluvaza sitili lukuli lwake walulava kunze waluzika.
7 Vigabitile masaa madatu mwehe wake Anania keza, kengila mng'anda, lakini hajuwile gaja gampatile mkasano wake.
8 Petulo kamuuza, “Nongele, zino izo sente zose zimpatile gweye na mkasano wako kwa kuchuuza mgunda wenu?”
Kamwidika, “Ona, zizo.”
9 Avo Petulo kamulongela, “Vino habali gweye na mbigalo wako muilumba kumgeza Loho wa Mndewa? Wanhu wamzikile mkasano wako sambi wa hamulango na gweye wokusola vivija!”
10 Bahaja kagwa hasi mmagulu ga Petulo kafa. Wabwanga viwengile wamvika kafa, avo wamulava kunze na wamzika behi na mbigalo wake.
11 Wanhu wose wamtogole Yesu na wose wayagwe waihulike mbuli ayo wadumba ng'hani.

*Unzonza na vifukuzi*

12 Watumigwa watenda mbuli nyingi za unzonza na vifukuzi mna iwanhu. Wanhu wose wamtogole Yesu waiting'hana hamoja muluhelengo lwa Sulemani.
13 Kuduhu wanhu wayagwe kulawa kunze wagezile kuilumba na wanhu wamtogole Yesu, hamoja wanhu wawagwaa nhogolwa.
14 Lunhu lwa wambigalo na watwanzi wamtogole Mndewa wongezeka mkibumbila.
15 Mbuli ya unzonza uwakalile wotenda watumigwa, wanhu wawagala watamu mvisazi na mmikeka, muladi sisila da Petulo diwakwase wanhu wayagwe viyakalile kobita.
16 Lunhu lwa wanhu lwiza kulawa mmabuga geli behi na Yelusalemu, na kuwagala wanhu wose wakalile wolumwa hebu wakalile na vinyamkela, na wose wahonyigwa.

*Watumigwa wodununzigwa*

17 Abaho mulava nhosa mkulu na wayage wose, na wanhu wa kibumbila cha Masadukayo, wawonela migongo ng'hani watumigwa, avo wasonga kuwehila.
18 Wawagoga watumigwa na kuwagodeka mkifungo.
19 Lakini ikilo msenga wa kuulanga wa Mndewa kafungula nyivi za ikifungo, kawalava kunze iwatumigwa, kawalongela,
20 “Gendeni mkeme Mng'anda ya Mulungu, walongeleni wanhu mbuli ya ugima uno.”

21 Watumigwa watogola, na imitootondo wengila Mng'anda ya Mulungu na wasonga kufundiza.

Mulava nhosa mkulu na wayage wawakema hamoja wavele wose wa Izilaeli mkitala, abaho walagiza watumigwa walavigwe mkifungo na wa-galigwe haulongozi wao.

22 Lakini wakulu wa wakalizi wa Ng'anda ya Mulungu viwacholile, hawawavikile iwatumigwa mkifungo, avo wabwela mkitala na kulonga,

23 “Vituvikile mkifungo, tukivika kihindigwa na wakalizi wose wokaliza zinyivi, lakini vitufungule zinyivi, hatumvikile munhu bule mgati!”

24 Wakulu wa walava nhosa na wakulu wa wakalizi wa Ng'anda ya Mulungu viwahulike avo, wakanganya kija kiwalawilile watumigwa.

25 Abaho munhu imoja keza kawalongela, “Tegelezeni! Wanhu wa-muwagodeke mkifungo wa Mng'anda ya Mulungu wofundiza wanhu!”

26 Avo mkulu wa wakalizi wa Ng'anda ya Mulungu kachola hamoja na wanhu zake wawagoga iwatumigwa. Hawawagogile kwa nguvu, kwavija wawadumba wanhu sekewawatowe mabwe.

27 Wawagala iwatumigwa mgati, na wawemiza haulongozi wa mkitala, na mulava nhosa mkulu kawalongela,

28 “Tuwagomesa sekemufundize kwa twaga da munhu ino, lakini loleni kimtendile! Mugabwililisa mafundizo genu mwiisi yose ya Yelusalemu, na molonga tweye wao kilamuso cha ifa yake!”

29 Petulo na watumigwa wayagwe wedika, “Tolondeka tumtegeleze Mu-lungu siyo wanhu.

30 Mweye mumkoma kwa kumuwamba mumsalaba, lakini Mulungu wa wahenga zetu kamzilibula Yesu kulawa kwa wafile.

31 Mulungu kamwinula mbaka mwambu wa mkono wake wa kudila kamtenda Mulangulizi na Mkombola, kuwatenda wanhu wa Izilaeli waleke nzambi zao na Mulungu yazigele kumgongo.

32 Tweye tuzona mbuli azo, tweye na Loho Yang'alile, yeli nhunza ya Mulungu kwa wose womtogola.”

33 Wanhu wa mkitala viwahulike avo, wagevuzika ng'hani walonda kuwakoma iwatumigwa.

34 Lakini imoja wao, Mfalisayo yakemigwe Gamalieli yakalile mfundiza Malagizo ga Musa yadumbigwe ng'hani na wanhu wose, kema aho mkitala. Kawalongela watumigwa walavigwe kunze kidogo,

35 abaho kawalongela wanhu wa mkitala, “Waizilaeli wayangu, ite-ganyeni ng'hani na kija kimulonda kuwatendela wanhu wano!

36 Baho umwaka kukala na munhu yakemigwe Teuda, kaitenda munhu mkulu, na wanhu gana na nne wailumba nayo. Lakini kakomigwa na wanhu zake wamkweleleze waimwaga na mbuli zake zihelela baho.

37 Abaho, Yuda mwenekae wa Galilaya kalawilila mna ikipindi cha kuwapeta wanhu, na heyo vivija kakala na lunhu mkulu, lakini vivija kakomigwa, na wanhu zake wose wamkweleleze waimwaga.

38 Lelo, nowalongeleni, sekemuwatendele mbuli yoyose wanhu wano. Walekeni! Kamba kija kiwaitogolele kutenda cholawa kumwao wenyego, hondakitendeke bule,

39 lakini kamba cholawa kwa Mulungu, hondamuwahume bule. Baho mogomba na Mulungu!”

Wanhu wa mkitala wakweleleza mbuli za Gamalieli.

40 Wawakema iwatumigwa mkitala, wawatowa mbalati, na wawalagiza sekewalonge kabili kwa twaga da Yesu, abaho wawalekesa.

41 Watumigwa viwasegele mkitala, wakala na deng'ho kwavija Mulungu
katogola wageligwe kinyala mbuli ya twaga da Yesu.
42 Kila siku wagendelela kufundiza na kuwapetela wanhu Mng'anda ya
Mulungu na mzikae za wanhu, kamba Yesu Kilisito iyo Mkombola.

# 6

*Watazaji saba*

1 Siku vizigendelele wanahina viwakalile wokongezeka, kukala na nd-
wagi mna Iwayahudi wolonga Kigiliki na waja iwolonga Kiebulania.
Wayahudi iwolonga Kigiliki walonga kamba wagane wakiwa weli kumwao
wasemwigwa muna ukugoleligwa sente kila siku.
2 Avo iwatumigwa longo na wabili wawakema wanahina wose wawa-
longela, “Havinogile bule kumwetu kuleka kuwapetela wanhu mbuli ya
Mulungu na kuwagolela lujo.
3 Avo, ndugu zangu, saguleni wanhu saba kumwenu wajuwike kamba
wamema Loho Yang'alile na nzewele, na toweka wawe wakulu wa mbuli
ino.
4 Lakini tweye tompula Mulungu na kuwapetela wanhu mbuli ya Mu-
lungu kipindi chetu chose.”
5 Wanhu wose wanogelwa na mbuli za watumigwa, avo wamsagula
Sitefano munhu yamemile kutamanila na Loho Yang'alile, hamoja na Filipo
na Polokolo na Nikanoli, Timona na Palimena na Nikolasi munhu hali
Muyahudi kulawa Antiokia iyo yakalile yengile mwiidini ya Kiyahudi.
6 Abaho wanhu wao wose wagaligwa kwa iwatumigwa, wao wampula
Mulungu na kuwekila makono.
7 Avo mbuli za Mulungu zigendelela kwenela. Wanahina wongezeka
ng'hani ako Yelusalemu na walava nhosa wengi wamtogola Yesu.

*Sitefano kogogigwa*

8 Mulungu kamgwaa ng'hekewa na nguvu Sitefano, nayo kadaha kutenda
unzonza na vifukuzi mna iwanhu.
9 Lakini kalemigwa na wanhu wayagwe wakalile wanhu wa ng'anda ya
kumpula Mulungu, ikemigwe, “Ng'anda ya kumpula Mulungu ya wanhu
Walekesigwe,” wanhu awo walawa Kilene na Alekizandilia. Wayagwe
walawa isi za Kilikia na Asiya.
10 Lakini Loho Yang'alile kamgwaa nzewele Sitefano viyakalile kolonga,
mbaka walemelwa kumuhuma.
11 Avo wawahonga wanhu walonge, “Tumuhulika komulonga vihile Musa
na Mulungu!”
12 Kwa ulonzi uno wawading'hula wanhu, wavele na wafundiza Malagizo
ga Musa. Wamgoga Sitefano na kumgala mkitala cha Wayahudi.
13 Abaho wawagala wanhu wayagwe walonge uvizi mbuli yake, walonga,
“Siku zose munhu ino koilonga vihile Ng'anda ya Mulungu na Malagizo ga
Musa.
14 Tumuhulika kolonga kamba Yesu wa Nazaleti koibomola Ng'anda ya
Mulungu na kugalusa vihendo vetu vitugweleligwe na Musa!”
15 Wanhu wose wakalile mkitala wambunhulila meso Sitefano, wachona
kihanga chake kiigala na kihanga cha msenga wa kuulanga.

# 7

*Sitefano kolonga na wanhu wa mkitala*

1 Mulava nhosa mkulu kamuuza Sitefano, “Mbuli zino za ukweli?”

2 Sitefano kawedika, “Tata zangu na ndugu zangu, nhegelezeni! Muhenga
wetu Abulahamu yang'hali hanachola kukala isi ya Halani, Mulungu wa
ukulu kamulawilila mwiisi ya Mesopotamia.
3 Mulungu kamulongela, ‘Segela mwiisi yako, waleke wanhu wa lubuga
lwako uchole isi yonda nikulagusile.’
4 Avo kalawanya mwiisi ya Wakalidayo kachola kukala kudibuga da
Halani. Tatake Abulahamu viyafile, Mulungu kamulongela Abulahamu
yeze mwiisi ino yumukala sambi.
5 Mulungu hamgwelele Abulahamu hata kimhongwe kidodo kiwe chake
mwenyego, lakini Mulungu kamulongela komgwaa, iwe yake na lukolo
lwake. Mulungu viyamulongele avo, Abulahamu kakala kaduhu wana.
6 Vino vivo Mulungu viyamulongele Abulahamu, ‘Lukolo lwako lokala
mwiisi ya ugeni, ako wokuwa watumwa na wotendigwa vihile kwa miyaka
magana mane.
7 Lakini nowatagusa wanhu wondawawatende watumwa. Abaho lukolo
lwako lolawa mwiisi iyo na wonigwaa ukulu niye hanhu hano.’
8 Abaho Mulungu kamgwaa Abulahamu kihendo cha kwingila kumbi
kamba kilaguso cha lagano. Avo Abulahamu kamwingiza kumbi Isaka siku
ya nane toka viyavumbuke. Vivija Isaka kamwingiza kumbi mwanage,
yakemigwe Yakobo, na Yakobo kawengiza kumbi waja wahenga zetu longo
na wabili.”
9 “Wanage Yakobo wamonela migongo mdodo wao Yusufu na wamchuuza
yawe mtumwa mwiisi ya Misili. Lakini Mulungu kakala hamoja nayo,
10 kamuhonya na magayo gake. Yusufu viyagaligwe kwa Falao mndewa
wa Misili, Mulungu kamtenda yanogeligwe, na nzewele zake zoneka, avo
mndewa wa Misili kamtenda yawe mkulu wa wakulu wa Isi, na mkulu wa
wasang'hanaji wa mng'anda.
11 Abaho kukala na lufilili lwa nzala mwiisi yose ya Misili na Kanaani,
itendile wanhu wadununzike. Wahenga zetu hawapatile lujo bule.
12 Yakobo viyahulike ako Misili kukala na ndiya, kawatuma wanage,
wahenga zetu, mwanza wa ichanduso kuvika ako.
13 Viwacholile mwanza wa kabili, Yusufu kailagusa kwa ndugu zake, na
mndewa Falao kalujuwa lukolo lwa Yusufu.
14 Avo Yusufu kawatuma wasenga kwa tatake Yakobo, wamulongele heyo
na lukolo lose weze Misili, wose kwa wose wakala malongo saba na tano.
15 Abaho Yakobo kachola Misili, ako heyo na wanage wafa.
16 Ng'huli zao zigaligwa Shekemu, ako wazikigwa mna gamapanga gayag-
ulile Abulahamu kwa sente kulawa kuna ulukolo lwa Hamoli.”
17 “Kipindi cha Mulungu kutenda gayamulongele Abulahamu vikikalile
behi, wanhu zetu wongezeka ng'hani mwiisi ya Misili.
18 Abaho mndewa iyagwe yalekile kumjuwa Yusufu kasonga kutawala
mwiisi ya Misili.
19 Kawatendela usede wahenga zetu na kuwatenda vihile, kawalagiza
waweke kunze wanao ving'hele, muladi wafe.
20 Musa kavumbuka mna ikipindi acho, kakala mwana yanogile.
Kaleligwa na mamake kwa miezi midatu,
21 na viyekigwe kutali na ukae, mndele wa Falao kamsola na kamulela
kamba mwanage.
22 Musa kafundizigwa ubala wose wa Wamisili na kawa munhu mkulu
kwa kulonga na sang'hano.”
23 “Musa viyavikize miyaka malongo mane, kachola kuwalola ndugu zake
Waizilaeli.

24 Kamona imoja wao kotendiligwa vihile na Mmisili, avo kachola kumtaza Mwiizilaeli kwa kumulipa gehile Mmisili kwa kumkoma.

25 Kagesa ndugu zake Waizilaeli wahajuwile kamba Mulungu yahawakombole kubitila heyo, lakini wao hawajuwile.

26 Imitondo yake kawona Waizilaeli wabili woitowa, kageza kuwagombeleza kawalongela, ‘Nhegelezeni mweye mwa ndugu habali moitowa kamba avo?’

27 Lakini ayo yakalile yomtowa miyage kamsung'ha Musa kumgwazo. Kamuuza, ‘Nani yakutendile mulangulizi na mulamuzi wetu?

28 Hebu kolonda kunikoma kamba viumkomile ija Mmisili jana?’

29 Musa viyahulike avo, kalawanya mwiisi ya Misili kachola mwiisi ya Midiani. Ako kapata wana wabili.”

30 “Viibitile miyaka malongo mane, msenga wa kuulanga kamulawilila Musa kuna ikisolo kikalile chokwaka kuluwala behi na lugongo lwa Sinai.

31 Musa kakanganya ng'hani kija kiyone, kachola behi ya kisolo yalole goya. Lakini kahulika sauti ya Mndewa,

32 ‘Niye na Mulungu wa wahenga zako, Mulungu wa Abulahamu na Mulungu wa Isaka na Mulungu wa Yakobo.’ Musa kagwaya kwa bwembwe na hagezile kulola kabili.

33 Mndewa kamulongela, ‘Vula vilatu vako, kwavija hanhu aho hawimile hang'ala.

34 Niwona wanhu zangu viwodununzigwa mwiisi ya Misili. Nihulika viwogutilila, nihumuluka niwahonye. Avo sambi nokutuma uchole Misili.’
”

35 “Musa iyo yalemigwe na wanhu wa Izilaeli, viwamulongile, ‘Nani yakutendile mulangulizi na mulamuzi kumwetu?’ Musa iyo yatumigwe na Mulungu kuwalanguliza wanhu na kuwakombola kubitila msenga wa kuulanga yamulawilile hana ikisolo kikwaka.

36 Kawalongoza wanhu walawe Misili, kwa kutenda unzonza na vilaguso mwiisi ya Misili na hana Ibahali ya shamu kwa miyaka malongo mane kuluwala.

37 Musa iyo yawalongele wanhu wa Izilaeli, ‘Mulungu kowasagulileni mtula ndagu wake, kamba viyanhumile niye na kokuwa imoja wa wanhu zenu.’

38 Musa iyo yakalile na lung'husesa lwa wanhu wa Izilaeli kuluwala, kakala ako na wahenga zetu na msenga wa kuulanga yalongile nayo hana Ulugongo lwa Sinai, na kabokela mbuli za ugima wa Mulungu yatugwelele tweye.”

39 “Lakini wahenga zetu walema kumtogola, wamsung'ha kumgwazo na walonga yahanogile kumwao wahabweleganye Misili.

40 Avo wamulongela Haluni, ‘Tutendele mulungu yonda yatulongoze. Hatujuwa kinhu gani kimulawilile Musa, yatulavile Misili.’

41 Avo watenda kinyago cha ng'ombe, wakigwaa ukulu, watenda nyimwili nyimwili kudeng'helela kija kiwatendile.

42 Mulungu kawaleka na kawatenda wazigwee ukulu nhondo za kuulanga, kamba viyandikigwe mna ikitabu cha watula ndagu wa Mulungu.”

“Mweye wanhu wa Izilaeli! Si niye bule yumunichinjile wanyama na kundavila nhosa

kwa miyaka malongo mane kuja kuluwala?

43 Mweye mkipapa kiheha cha mulungu Moleki,

na kinyago cha nhondo ya mulungu wenu Lefani,

vinyago vimutendile vivo vimvitambikile, avo nowahamizila mwiisi ya Babeli."
44 "Wahenga zetu wakala na kiheha kilagusa kamba Mulungu kabaho
ako kuluwala. Kitendigwa kamba Mulungu viyamulongele Musa yakitende,
kiigalile na kija kiyaone.
45 Abaho, wahenga zetu wakibokele acho ikiheha kwa wahenga zao.
Wakipapa viwacholile hamoja na Yoshua na wachola nacho mna ziisi
ziyawabitize Mulungu. Kikala kuko mbaka kipindi cha Daudi.
46 Daudi kanogeligwa na Mulungu na kampula Mulungu yamtogolele
yatende hanhu hakukala Mulungu wa Yakobo.
47 Lakini Sulemani iyo yamzengele Mulungu ng'anda."
48 Lakini Mulungu yeli Uchanha Ng'hani hakala mng'anda izengigwe kwa
makono ga wanhu, kamba mtula ndagu wa Mulungu viyolonga,
49 "Ulanga acho kigoda changu
na isi iyo inikile magulu gangu.
Ng'anda ya gani yonda munizengele niye?
Hanhu gani hondanikale niye?
50 Niye mwenyego iyo nhendile vinhu vose vino."
51 Abaho Sitefano kalonga, "Mweye muli na mizoyo midala, na mulekile
kumjuwa Mulungu, mweye musitile magwiti genu kutegeleza usenga wa
Mulungu! Mwiigala na wahenga zenu na mweye vivija momulema Loho
Yang'alile!
52 Vino hana mtula ndagu yoyose wa Mulungu wahenga zenu wamulekile
kumdununza? Wawakoma wasenga wa Mulungu wao kulawa umwaka
walongile kwiza kwa Msang'hanaji wake Yanogile. Na sambi mumuhinduka
na kumkoma.
53 Mweye wao mubokele malagizo ga Mulungu, gamgweleligwe na
wasenga wa kuulanga, lakini hamgagogile bule!"

### *Sitefano kotoigwa mabwe*

54 Wanhu wa mkitala viwamtegeleze Sitefano, wagevuzika ng'hani, wada-
funa meno gao.
55 Lakini Sitefano kuno kamema Loho Yang'alile, kalola uchanha kuu-
langa kawona ukulu wa Mulungu na Yesu kema mwambu wa mkono wa
kudila wa Mulungu.
56 Kalonga, "Loleni, nouwona ulanga ugubuka na Mwana wa Munhu kema
mwambu wa mkono wa kudila wa Mulungu!"
57 Kwa nyangi wanhu wa mkitala wasita magwiti gao. Bahaja wanhu wose
wamzumhila Sitefano,
58 wamulava kunze ya buga, wamtowa mabwe. Waja wakalile womtowa
mabwe waleka viwalo vao kwa mbwanga imoja twaga jake Sauli.
59 Viwakalile womtowa mabwe Sitefano kapula, "Mndewa Yesu, ibokele
loho yangu!" 60 Kafugama kaguta, "Mndewa! ugele kumgongo nzambi yao
ino!" Viyalongile avo kafa.

# 8

1 Nayo Sauli kona vinoga kukomigwa kwa Sitefano.

### *Sauli kowadununza wanhu wamtogole Yesu*

Mna izisiku azo wanhu wamtogole Yesu ako Yelusalemu wasonga
kudununzigwa vihile. Wanhu wose wamtogole Yesu, wahaleka watumigwa,
wakala wapwililike mwiisi iyo ya Yudea na Samalia.
2 Wanhu wanogile wamzika Sitefano na wamulilila ng'hani.

3 Lakini Sauli kalonda kuwadununza wanhu wamtogole Yesu. Kachola ng'anda mbaka ng'anda, kawalava kunze wanhu wamtogole Yesu, wambigalo kwa watwanzi, na kaweka mvifungo.

### *Mbuli Inogile yopetigwa ako Samalia*

4 Wanhu wamtogole Yesu wapwililike wachola kila hanhu kuwapetela wanhu Mbuli Inogile.
5 Filipo kachola kudibuga da Samalia na kawapetela wanhu mbuli ya Kilisito Mkombola.
6 Lunhu lwa wanhu lumtegeleza goya Filipo viyalongile na kuwona unzonza uyatendile.
7 Vinyamkela wawalawa wanhu kwa kulila, na wanhu wengi waholole na mbetembete wahonyigwa.
8 Avo kukala na deng'ho kulu kudibuga dija.
9 Munhu imoja twaga jake Simoni kakala yokala mumo, kawazanya Wasamalia kwa uhawi wake. Kaitenda kamba kakala munhu mkulu.
10 Wanhu wose kudibuga dija, wakulu kwa wadodo wamtegeleza ng'hani, walonga, “Munhu ino kana udahi wa Mulungu ukemigwa, ‘Udahi Mkulu’.”
11 Wamtegeleza ng'hani kwavija kwa miyaka mingi kawazanya kwa uhawi wake.
12 Lakini viwautogole usenga wa Filipo, usenga wa Mbuli Inogile ya Undewa wa Mulungu na mbuli ya twaga da Yesu Kilisito, wose wabatizigwa, wambigalo kwa watwanzi.
13 Simoni nayo katogola, viyamambukize kubatizigwa kakala yokwanga na Filipo na kakanganya viyone unzonza na vilaguso vikalile vitendigwa.
14 Watumigwa wakalile Yelusalemu wahulika wanhu wa Samalia waibokela mbuli ya Mulungu, avo wawatuma Petulo na Yohana kumwao.
15 Viwavikile, wawapulila kwa Mulungu wanhu wamtogole Yesu wambokele Loho Yang'alile.
16 Kwavija Loho Yang'alile kakala yang'hali hanamuhulumukila munhu yoyose kumwao, wakala wabatizigwe kwa twaga da Mndewa Yesu diiyeka.
17 Abaho Petulo na Yohana wawekila makono, wabokela Loho Yang'alile.
18 Simoni kona wanhu wamtogole Yesu wambokela Loho Yang'alile viwekiligwe makono na watumigwa. Avo kalonda kuwagwaa sente Petulo na Yohana,
19 kalonga, “Naniye nigweleleni udahi uno, muladi munhu yoyose yonda nimwikile makono gangu yabokele Loho Yang'alile.”
20 Lakini Petulo kamwidika, “Upotele kutali gweye na sente zako, kwa kugesa kodaha kugula kwa sente nhunza ya Mulungu!
21 Kuduhu hanhu hohose mwiisang'hano yetu, kwavija moyo wako haugesa ganogile mgameso ga Mulungu.
22 Avo leka nzambi zako, na magesa gako gehile na mpule Mndewa yagele kumgongo.
23 Kwavija nokona kumema migongo na kwa mfungwa wa nzambi.”
24 Simoni kamulongela Petulo na Yohana, “Mhulileni kwa Mndewa, gano gamulongile sekegandawilile.”
25 Viwamambukize kulonga gaja gawone na kuwapetela wanhu usenga wa Mndewa, Petulo na Yohana wabwela Yelusalemu. Mnzila wawapetela Mbuli Inogile wanhu wa mvijiji va Samalia.

### *Filipo na mkulu wa Isiyopiya*

26 Msenga wa kuulanga wa Mndewa kamulongela Filipo, “Itande uchole
kusini kubitila nzila ilawa Yelusalemu kuchola Gaza.” Nzila ino sambi
haitumika.
27 Avo Filipo kaitanda na kuchola. Muisiopiya yeliduhu kimbigalo,
yakalile munhu mkulu mna ingama ya Kandake mndewa wa kitwanzi wa
Isiopiya kakala mnzila ya kuchola ukayake. Kakala Yelusalemu komtambik-
ila Mulungu na kakala yobwela ukayake na mtuka wa kubulula.
28 Viyakalile mnzila kakala yosoma kitabu cha mtula ndagu wa Mulungu
Isaya.
29 Avo Loho Yang'alile kamulongela Filipo, “Genda kakale behi na mtuka
uja.”
30 Baho Filipo kakimbila behi na mtuka kamuhulika munhu ayo kosoma
kitabu cha mtula ndagu wa Mulungu Isaya. Filipo kamuuza, “Vino kogajuwa
gago gousoma?”
31 Mkulu ayo kedika, “Nodahaze kugajuwa bila munhu kunifambulila?”
Avo kamgoneka Filipo yakwele mumtuka na yakale hamoja nayo.
32 Munhu ayo kakala yosoma hanhu hano mna Gamaandiko Gang'alile,
“Kakala kamba ng'hondolo yogaligwa kuchinjigwa,
kamba mwana ng'hondolo yanyamale huupi viyokanhigwa mibahila,
halongile mbuli.
33 Kageligwa kinyala na koneligwa.
Kuduhu munhu yodaha kulonga mbuli za lukolo lwake,
kwavija ugima wake mwiisi uvika kuuhelelo.”
34 Mkulu iyo kamuuza Filipo, “Nongele mtula ndagu wa Mulungu kolonga
mbuli ya nani? Mbuli yake mwenyego hebu ya munhu iyagwe?”
35 Filipo kasonga kulonga, kasongela hanhu hano ha Maandiko Gang'alile,
kamulongela Mbuli Inogile ya Yesu.
36 Viwakalile wogendelela na mwanza, wavika hanhu hakalile na mazi,
mkulu ayo kalonga, “Hano hana mazi. Kinhu gani kingomesa ndeke kuba-
tizigwa?” 37 Filipo kamulongela, “Kodaha kubatizigwa kamba wahatogola
kwa moyo wako wose. Mkulu ayo kamwidika, ‘Notogola kamba Yesu Kilisito
iyo Mwana wa Mulungu’.”
38 Mkulu ayo kalagiza mtuka wime. Filipo na mkulu iyo wahumulukila
mgamazi, Filipo kambatiza.
39 Viwalawile mgamazi, Loho wa Mndewa kamsegeza Filipo. Mkulu ayo
hamonile kabili, lakini kagendelela na mwanza kuno kamema deng'ho.
40 Filipo kasinhukila ka Azoto, kachola isi ya Kaisalia na mnzila
kawapetela wanhu Mbuli Inogile kila buga.

# 9

*Sauli komtogola Yesu*
*Sang'h 22:6-16; 26:12-18*

1 Mna ikipindi acho Sauli kagendelela kuwehila na kuwakoma wanahina
wa Mndewa. Kachola kwa mulava nhosa mkulu,
2 kapula baluwa ya kujuwika mng'anda ya kumpula Mulungu ako Dame-
siki, muladi yahamvika munhu yoyose mtwanzi hebu mbigalo kotogola
nzila ya Mndewa yamgoge yamgale Yelusalemu.
3 Sauli viyakalile mnzila behi na kuvika Damesiki, bahaja mulenge kulawa
kuulanga ummwemwesela banzi zose.
4 Kagwa hasi na kahulika sauti yomulongela, “Sauli, Sauli! Habali
konidununza?”
5 Sauli kauza, “Mndewa, gweye kwa nani?”

Kedika, “Niye na Yesu yuunidununza.
6 Lakini inuka uchole kudibuga, ako kolongeligwa cha kusang'hana.”
7 Wanhu wakalile mwanza umoja na Sauli wema, hawalongile mbuli,
sauti waihulika lakini hawamonile munhu.
8 Sauli kenuka, kabenzula meso gake, lakini hachonile kinhu. Avo
wamgoga mkono wamulongoza Damesiki.
9 Kwa siku ndatu hadahile kulola, na kipindi chose acho hadile na
hang'wile kinhu chochose.
10 Kukala na mwanahina wa Yesu kuko Damesiki twaga jake Anania.
Mulungu kamulagusila kinhu mzinzozi, Mndewa kamkema, “Anania!”
Anania kedika, “Aino baha Mndewa.”
11 Mndewa kamulongela, “Winuke uchole Mnzila Igoloke. Kuna ing'anda
ya Yuda muuze munhu yokemigwa Sauli kulawa Taliso. Heyo kompula
Mulungu,
12 Mulungu kamulagusila kinhu, kamona munhu yakemigwe Anania keza
na kumwikila makono gake yadahe kulola kabili.”
13 Lakini Anania kamwidika, “Mndewa wanhu wengi wanongela mbuli
zake munhu ino na gaja gose gayawatendele wanhu zako wa mwiisi ya
Yelusalemu.
14 Nayo keza Damesiki kwa udahi kulawa kwa wakulu wa walava nhosa
kuwagoga wanhu wose wokugwaa ukulu gweye.”
15 Mndewa kamulongela, “Genda kwavija nimsagula yanisang'hanile,
kutenda twaga jangu dijuwike na wanhu haweli Wayahudi na wandewa
wao na wanhu wa Izilaeli.
16 Niye mwenyego nomulagusila vonda yadununzike mbuli yangu.”
17 Avo Anania kachola kengila mng'anda iyakalile Sauli, kamwikila
makono, kalonga, “Ndugu yangu Sauli, Mndewa kanhuma, Yesu mwenyego
yakulawilile gweye mnzila viukalile kokwiza hano. Kanhuma muladi udahe
kulola kabili na umemezigwe Loho Yang'alile.
18 Bahaja vinhu kamba vibale vilagala mgameso ga Sauli, na kadaha
kulola kabili, kenuka na kabatizigwa,
19 viyamambukize kuja, nguvu zake zimbwelela.”

### *Sauli kowapetela wanhu ako Damesiki*

Sauli kakala siku ndodo na wanahina wa Yesu ako Damesiki.
20 Baho kasonga kuwapetela wanhu mzing'anda za kumpula Mulungu
kamba Yesu iyo Mwana wa Mulungu.
21 Wanhu wose wamuhulike wakanganya wauza, “Vino ino siyo heyo
yawakomile wanhu wamgwelele ukulu Yesu mwiisi ya Yelusalemu. Hezile
hano mbuli ya kuwagoga wanhu wao na kuwagala kwa wakulu wa walava
nhosa?”
22 Lakini Sauli kawapetela wanhu kwa udahi mkulu, na kulonga kwake
kamba Yesu Kilisito kakala Mkombola kuwatenda Wayahudi wakalile
Damesiki walemelwe kumwidika.
23 Vizibitile siku nyingi, Wayahudi waiting'hana na wakala kiseto cha
kumkoma Sauli.
24 Lakini kalongeligwa mbuli iyo, imisi na ikilo wakaliza hana ulwivi lwa
kwingila kudibuga muladi wamkome.
25 Lakini ikilo kimoja wanahina wakalile na Sauli wamsola, wamuhumu-
lusa mdigelo kulu kubitila zonzo dikalile muuluwa uzunguluke dibuga.

### *Sauli ako Yelusalemu*

26 Sauli kachola Yelusalemu kalonda kuilumba na wanahina. Lakini wose
wamdumba, kwavija hawatogole kamba Sauli nayo kakala mwanahina.

27 Abaho Balinaba keza kumtaza Sauli, na kamgala kwa watumigwa. Kawasimulila vija Sauli viyamonile Mndewa mnzila na Mndewa kalonga nayo. Vivija kawalongela vija Sauli viyawapetele wanhu wa Damesiki kwa twaga da Yesu.
28 Avo Sauli kakala nao na kachola kudibuga jose da Yelusalemu, kawapetela wanhu wa Damesiki kwa twaga da Mndewa kwa kugangamala.
29 Vivija kalonga na kuibamilila na Wayahudi wolonga Kigiliki, lakini hewo walonda kumkoma.
30 Wanhu wamtogole Yesu viwone vivo, wamgala Sauli mbaka kudibuga da Kaisalia na wamuleka yachole Taliso.
31 Avo kipindi acho vibumbila va wanhu wamtogole Yesu vikala moyo hole kila hanhu kuko Yudea na Galilaya na Samalia. Kubitila Loho Yang'alile yakalile yowagangamiza wanhu, wanhu wongezeka ng'hani viwakalile wokala kwa kumdumba Mndewa.

### *Petulo kotenda unzonza kudibuga da Ludia na Yopa*

32 Petulo kagenda kila hanhu, siku dimoja kachola kuwatembelela wanhu wamtogole Yesu wakalile ako Ludia.
33 Ako kamting'hana munhu yakemigwe Enea, yakalile yaholole na hadahile kwinuka mulusazi kwa miyaka minane.
34 Petulo kamulongela, "Enea, Yesu Kilisito kokuhonya. Lamuka mulusazi lwako tandika lusazi lwako." Bahaja Enea kenuka.
35 Wanhu wose wakalile Ludia na Saloni wamona Enea, nao wamtogola Mndewa.
36 Ako Yopa kukala na mtwanzi yakemigwe Tabita yakalile mwanahina wa Yesu, Twaga jake kwa Kigiliki Dolikasi, fambulo jake, "Mhala," Mtwanzi ayo kakala yotenda ganogile na kuwataza wakiwa.
37 Kipindi acho mtwanzi ayo kalumwa, abaho kafa. Lukuli lwake lusun-higwa lwikigwa mdigati da uchanha.
38 Buga da Yopa hadikalile kutali ng'hani na buga da Ludia. Wanahina wa Yesu ako Yopa viwahulike kamba Petulo kakala kuko Ludia, wawatuma wanhu wabili na usenga uno, "Tokupula ulopole wize kumwetu."
39 Avo Petulo kachola nao. Viyavikile kagaligwa mdigati da uchanha ako wagane wose wamzunguluka kuno wolila na kumulagusila viwalo vose viyasonile Dolikasi viyakalile yang'hali mgima.
40 Petulo kavilava kunze, kafugama mavindi kampula Mulungu, abaho kaluhindukila lukuli lwa mtwanzi ayo yafile, kalonga, "Tabita, lamuka!" Nayo kabenzula meso gake, viyamonile Petulo, kagandamuka.
41 Petulo kamgoga mkono kamtaza kwinuka. Abaho kawakema wanhu wose wamtogole Yesu, wayagwe wakala wagane kamwika haulongozi wa hewo, kuno ka mgima.
42 Mbuli ino ibwililika kudibuga jose da Yopa na wanhu wengi wamtogola Mndewa.
43 Petulo kagendelela kukala ako Yopa kwa siku nyingi mwiikae ya munhu yakalile yowamba ng'hwembe yakemigwe Simoni.

# 10

### *Petulo na Kolinelio*

1 Kukala na munhu imoja mwiisi ya Kaisalia yakemigwe Kolinelio, kalala mkulu wa kibumbila cha wakalizi gana wa Kilumi kikemigwe, "Kibumbila cha Italia."

2 Kakala munhu yomdumba Mulungu, heyo na wanhu wose wa mulubuga lwake wamgwaa ukulu Mulungu. Vivija kasang'hana ng'hani kuwataza wanhu wakiwa na kakala yompula Mulungu siku zose.

3 Siku dimoja saa tisa imisi, Mulungu kamulagusila kinhu, kamona msenga wa kuulanga wa Mulungu kamwizila kamulongela, “Kolinelio!”

4 Kolinelio kamulola bunhuu msenga ayo wa kuulanga kwa bwembwe kamulongela, “Go mkulu, kuna choni?”

Msenga wa kuulanga kamwidika, “Mulungu kanogelwa kumpula kwako na sang'hano ya kuwataza wakiwa, nayo hakusemwa bule.

5 Watume wanhu sambi baha, wachole Yopa kwa munhu imoja yokemigwa Simoni Petulo.

6 Heyo mgeni mna ikae ya munhu yokemigwa Simoni, muwamba ng'hwembe, kokala behi ya Bahali.”

7 Abaho msenga ayo wa kuulanga kasegela, Kolinelio kawakema wasang'hanaji zake wabili na mkalizi wake imoja wa iwasang'hanaji zake, yomdumba Mulungu.

8 Kawalongela kija kilawilile, abaho kawatuma wachole Yopa.

9 Siku diyagwe viwakalile mnzila behi na Yopa, imisi Petulo kachola kudigati da uchanha kumpula Mulungu.

10 Kona nzala na kalonda kuja kinhu chochose, lujo vilukalile lotandigwa, Mulungu kamulagusila kinhu.

11 Kona ulanga ugubuka na kona kinhu kamba mgolole mkulu uwambigwe mhande zake nne wohumulusigwa hasi.

12 Mgati yake kukala na wanyama wose na wang'onyo wotambala na ndege.

13 Kahulika sauti yomulongela, “Petulo, lamuka uchinje uje!”

14 Lakini Petulo kalonga, “Aka, Mndewa, sinakuja bule kinhu kigomigwe hebu kihile.”

15 Sauti imulongela kabili, “Sekeuvikeme viha vinhu viyatendile Mulungu vinoge.”

16 Mbuli ino ilawilila miyanza midatu, abaho kinhu acho kigaligwa kuulanga.

17 Petulo viyakalile kokanganya fambulo da kinhu acho, wanhu watumigwe na Kolinelio wavika hana ing'anda ya Simoni, na wakala wemile haulongozi wa ulwivi.

18 Wakema, wauza, “Vino hano hana mgeni yoyose yokemigwa Simoni Petulo?”

19 Petulo kakala yang'hali yogelegeza fambulo da kinhu acho, baho Loho Yang'alile kamulongela, “Tegeleza! Kuna wanhu wadatu wokuzahila.

20 Avo sekeunyawenyawe, itande uchole nao, kwavija niye iyo niwatumile.”

21 Avo Petulo kahumuluka kawalongela wanhu wao, “Niye iyo yumumzahila. Muwinza choni?”

22 Wamwidika, “Mkulu Kolinelio katutuma. Munhu ayo kanoga na komdumba Mulungu na katogoligwa ng'hani na Wayahudi. Msenga yang'alile wa kuulanga kamulongela yakugoneke gweye ukayake. Muladi yahulike chondaulonge.”

23 Petulo kawagoneka wanhu awo kumwake, ikilo acho kawagwaa hanhu ha kuwasa.

Imitondo yake kaitanda kachola nao na wanhu wayagwe wamtogole Yesu kulawa Yopa wachola nayo.

24 Imitondo yake wavika mwiisi ya Kaisalia. Kolinelio kakala kowabeta,
hamoja na ndugu na mbwiga zake wa behi yawagoneke.
25 Petulo viyakalile behi kuvika, Kolinelio kenuka kamcholela, kagwa
kingubanguba kamtambikila.
26 Petulo kamwinula, kamulongela, “Inuka, niye mwenyego na munhu
kamba gweye.”
27 Petulo kagendelela kulonga na Kolinelio viyakalile kokwingila
mng'anda, mumo kawavika wanhu wengi waiting'hana.
28 Petulo kawalongela, “Mweye wenyego mujuwa goya kamba Muyahudi
kagomigwa na malagizo gake sekeyamtembelele hebu kuilumba na munhu
hali Muyahudi. Lakini Mulungu kandagusila sekenimkeme munhu yoyose
keha hebu hafaya.
29 Na viundagize, silemile bule niza, avo nokuuza kabili kung'hemela
choni?”
30 Kolinelio kalonga, “Siku ndatu zibitile mna isaa kamba ino, saa tisa
imisi, ng'hala nimpula Mulungu mng'anda yangu. Bahaja munhu yavalile
viwalo vizelu chuwee, kema haulongozi wangu,
31 kalonga, ‘Kolinelio! Mulungu kahulika viumpulile na kazitogola
sang'hano zako za kuwataza wanhu wakiwa.
32 Mtume munhu yachole Yopa kwa munhu yokemigwa Simoni Petulo.
Kokala mwiikae ya Simoni muwamba ng'hwembe, kokala behi na Bahali.’
33 Avo bahaja niwatuma wanhu kumwako, na kutenda goya viwizile.
Sambi wose twabaha haulongozi wa Mulungu, tobetela kuhulika mbuli
yoyose yakulagize Mndewa ulonge.”

### *Ulonzi wa Petulo*

34 Baho Petulo kasonga kulonga, “Sambi nojuwa kweli Mulungu hambag-
ula munhu yoyose.
35 Wose womgwaa ukulu na kutenda ganogile kowatogola, hatonga
wolawa isi gani.
36 Muujuwa usenga uyaugalile kwa wanhu wa Izilaeli, kuwapetela wanhu
Mbuli Inogile igala tindiwalo kubitila Yesu Kilisito yeli Mndewa wa wanhu
wose.
37 Muzijuwa mbuli ng'hulu zitendeke mwiisi yose ya Wayahudi, kusongela
Galilaya, Yohana viyamalile kuwapetela wanhu usenga wake wa ubatizo.
38 Mumjuwa Mulungu viyamsagule Yesu wa Nazaleti kwa kumgwaa Loho
Yang'alile na udahi. Kila hanhu hayacholile katenda ganogile na kuwaho-
nya wanhu wose wakalile mmakono ga Mwenembago, kwavija Mulungu
kakala nayo.
39 Tweye tuchona kila kinhu kiyatendile mwiisi ya Wayahudi na
Yelusalemu. Abaho wamkoma kwa kumuwamba mumsalaba.
40 Lakini siku ya kadatu Mulungu kamzilibula kulawa kwa wafile na
kamtenda yaoneke,
41 siyo kwa kila munhu, lakini kwa waja wazonile mbuli azo, wasag-
uligwe mwaka na Mulungu, wao tweye tudile na kung'wa hamoja nayo
viyazilibuke kulawa kwa wafile.
42 Katulagiza tuwapetela wanhu Mbuli Inogile na kuwalongela kamba
Yesu iyo yasaguligwe na Mulungu kuwatagusa wanhu wagima na wafile.
43 Watula ndagu wose wa Mulungu walonga mbuli yake, walonga wanhu
wose womtogola nzambi zao zogeligwa kumgongo kwa udahi wa twaga da
Yesu.”

### *Wanhu haweli Wayahudi wombokela Loho Yang'alile*

44 Petulo viyakalile yang'hali yolonga, Loho Yang'alile kawahumulukila wanhu wose wakalile womtegeleza.
45 Wayahudi wamtogole Yesu wezile kulawa Yopa hamoja na Petulo wakanganya viwone Mulungu vivija kawagwaa wanhu haweli Wayahudi nhunza ya Loho Yang'alile.
46 Kwavija wawahulika wolonga kwa ulonzi wa sambi na kuutogola ukulu wa Mulungu. Petulo kawalongela,
47 "Wanhu wano wambokela Loho Yang'alile, kamba vitumbokele tweye. Vino munhu yoyose kodaha kuwagomesa sekewabatizigwe kwa mazi?"
48 Avo kalagiza wabatizigwe kwa twaga da Yesu Kilisito. Abaho wampula yakale nao kwa siku ndodo.

# 11

*Petulo kowasimulila wanhu wamtogole Yesu ako Yelusalemu*

1 Watumigwa na wanhu wayagwe wamtogole Yesu ako Yudea wahulika kamba wanhu haweli Wayahudi vivija wabokela mbuli ya Mulungu.
2 Petulo viyacholile Yelusalemu, wanhu wolonda wanhu haweli Wayahudi wengile kumbi, wambeza Petulo,
3 walonga, "Gweye kukala mzikae za wanhu haweli Wayahudi hawengile kumbi na vivija kuja nao!"
4 Avo Petulo kawalongela fulu ipile kija kilawilile kusongela kuna ichanduso.
5 "Vinikalile nompula Mulungu kudibuga da Yopa, Mulungu kandagusila kinhu. Nyona kinhu chokwiza hasi kiigala na mgolole mkulu uhumulusigwa kwa mhande zake nne kulawa kuulanga, wima behi yangu.
6 Ndola goya mgati yake nyona wanyama wose, wang'onyo wotambala na ndege.
7 Abaho mhulika sauti yonongela, 'Petulo, lamuka uchinje uje!'
8 Lakini nonga, 'Mndewa bule! Kuduhu kinhu kihile hebu kigomesigwe kingile mumulomo wangu.'
9 Sauti ilonga kabili kulawa kuulanga, 'Sekeuvikeme viha vinhu viyatendile Mulungu vinoge.'
10 Mbuli ayo ilawilila miyanza midatu, kukikomelezo kinhu kija kibwelezigwa kuulanga.
11 Bahaja wanhu wadatu watumigwe kumwangu kulawa Kaisalia wavika mng'anda ing'alile.
12 Loho kanilongela nichole nao sekeninyawenyawe. Ndugu wano sita kulawa Yopa wachola na niye Kaisalia na wose twingila mng'anda ya Kolinelio.
13 Kolinelio katulongela vija viyamonile msenga kulawa kuulanga kema mng'anda yake. Kamulongela, 'Mtume munhu yachole Yopa kwa munhu yokemigwa Simoni Petulo.
14 Kowalongeleni mbuli zondaziwatende gweye na wanhu wa mulubuga lwako mukomboligwe.'
15 Vinisongile kulonga, Loho Yang'alile keza kumwao kamba viyezile kumwetu kuna ichanduso.
16 Abaho nikumbuka kija kiyalongile Mndewa, 'Yohana kawabatiza wanhu kwa mazi, lakini mweye mobatizigwa kwa Loho Yang'alile.'
17 Vivo ili Mulungu kawagwaa wanhu haweli Wayahudi nhunza iija iyatugwelele tweye vitumtogole Mndewa Yesu Kilisito Mkombola, niye na nani, mbaka nimgomese Mulungu?"

18 Viwahulike avo, waleka kumulonga na wamtogola Mulungu, walonga,
“Vivija Mulungu kawagwaa wanhu haweli Wayahudi nyafasi ya kuleka
nzambi na kubokela ugima wa mazuwa gose!”

*Wanhu wamtogole Yesu ako Antiokia*

19 Wanhu wayagwe wamtogole Yesu wakalile wapwililike mbuli ya
madununzo galawilile viyakomigwe Sitefano, wachola mbaka Foinike,
Kupulo na Antiokia, kuwapetela Wayahudi waiyeka usenga uno.
20 Lakini wanhu wayagwe wamtogole Yesu, walawile Kupulo na Kilene,
wachola Antiokia kuwapetela wanhu haweli Wayahudi usenga wa Mbuli
Inogile ya Mndewa Yesu.
21 Udahi wa Mndewa ukala hamoja nao, na wanhu wengi watogola na
wambwelela Mndewa.
22 Mbuli ino iwavikila wanhu wamtogole Yesu ako Yelusalemu, avo
wamtuma Balinaba yachole Antiokia.
23 Viyavikile na kona vija Mulungu viyawagwelele ng'hekewa,
kadeng'helela na kawapula wagendelele kumtamanila Mndewa kwa
mizoyo yao yose.
24 Balinaba kakala munhu yanogile, kamema Loho Yang'alile na kuta-
manila, na wanhu wengi wambwelela Mndewa.
25 Abaho Balinaba kachola Taliso kumzahila Sauli.
26 Viyamonile, kamgala Antiokia, mwaka mgima waiting'hana na wanhu
wamtogole Yesu na wawafundiza wanhu wengi. Ako Antiokia, kuko
wanahina wa wasonga kukemigwa Wakilisito.
27 Mna ikipindi acho watula ndagu wayagwe wa Mulungu wasegela
Yelusalemu wachola Antiokia.
28 Imoja wao yakemigwe Agabo, kema na kwa udahi wa Loho Yang'alile
kalagula kamba hokuwa na lufilili lwa nzala mwiisi yose. Ilawilila kipindi
cha utawala wa Kilaudio.
29 Wanahina wa Yesu waitogolela kila munhu yagale chochose kiyakalile
nacho, kuwataza wayao wamtogole Yesu wakalile Yudea.
30 Watenda avo, abaho wawagwaa sente Balinaba na Sauli wazigale kwa
wavele wa wanhu wamtogole Yesu.

# 12

*Madununzo makulu*

1 Mna ikipindi kikija Mndewa Helode kasonga kuwadununza wanhu
wayagwe wamtogole Yesu.
2 Kalagiza Yakobo mkulu wake Yohana yakomigwe kwa panga.
3 Helode viyonile mbuli ino iwanogela Wayahudi, kagendelela, kamgoga
Petulo. Mbuli ino ilawilila mna ikipindi cha Magate hagageligwe usasu.
4 Viwamgogile Petulo wamgodeka mkifungo, wamwika mmakono ga
wakalizi wakalile vibumbila vine kila kibumbila kikala na wakalizi wane.
Helode kalonda kumulava Petulo haulongozi wa wanhu yahamala Ny-
imwili nyimwili ya Pasaka.
5 Avo Petulo viyakalile yang'hali kagodekigwa, wanhu wamtogole Yesu
wampulila ng'hani kwa Mulungu.

*Petulo kolekesigwa kulawa mkifungo*

6 Mna ikilo cha siku ayo iyalondile Helode yamgale Petulo haulongozi
wa wanhu, Petulo kakala yawasile hagati ya wakalizi wabili. Kakala
yagodekigwe kwa minyololo mibili. Hana ulwivi lwa kifungo hakala na
wakalizi wakalile wokaliza.

7 Bahaja msenga wa kuulanga wa Mndewa kema, mulenge umwemwesa mdigati dija. Msenga wa kuulanga kamtigisa Petulo mdiega, kamulongela, lamuka, “Lopola, inuka!” Bahaja minyololo ilagala kulawa mmakono ga Petulo.
8 Abaho msenga ayo wa kuulanga kamulongela, “Ifunge mkwiji wako na uvale vilatu vako.” Petulo katenda vivo, na msenga wa kuulanga kamulongela, “Vala kiwalo chako uniwinze.”
9 Petulo kamkweleleza kunze ya kifungo, lakini hajuwile kamba msenga wa kuulanga kakala yotenda vivo kweli, kagiza kakala yolota nzonzi.
10 Wabita kibumbila cha ichanduso cha wakalizi abaho cha kabili, na kukimambukizo kibumbila cha wakalizi wa lwivi lwa kwingilila kudibuga. Lwivi luwavugukila lwenyego na wao walawa kunze, wagenda mnzila bahaja msenga wa kuulanga kamuleka Petulo.
11 Abaho Petulo kajuwa gamulawilile kalonga, “Sambi nojuwa kweli! Mndewa kamtuma msenga wake wa kuulanga yamhonye mmakono ga Helode na kulawa kwa kija kiwalondile kutenda Wayahudi.”
12 Viyajuwile avo kachola ukae kwa Malia mamake Yohana yakemigwe Maluko, ako wanhu wengi wakala waiting'hane na wakala wompula Mulungu.
13 Petulo kagong'onda lwivi lwa kunze, na mtumigwa wa kitwanzi yakemigwe Loda kachola kulola nani yogong'onda.
14 Viyajuwile ikala sauti ya Petulo, kadeng'helela kaleka kuvugula ulwivi kabweleganya mng'anda, kawalongela, “Yemile kunze Petulo!”
15 Wamulongela, “Gweye kuna kibozi mbwelela.” Lakini kagangamiza kamba ikala kweli. Avo wamwidika, “Sengine msenga wake kulawa kuulanga.”
16 Mna ikipindi acho Petulo kagendelela kugong'onda ulwivi, kukimambukizo wamvugulila, na viwamone wakanganya.
17 Petulo kenula mkono kulagusa wanyamale, kawalongela vija Mndewa viyamulavile mkifungo. Kawalongela, “Mulongeleni Yakobo mbuli ino na wanhu wayagwe wamtogole Yesu,” abaho kachola hanhu hayagwe.
18 Viivikile imitondo, wakalizi wakala wonyawanyawa kwa kija kimulawilile Petulo.
19 Helode kalagiza wamzahile Petulo, lakini hawamonile bule. Avo kalagiza waja wakalizi wauzigwe na kalagiza wakomigwe.
Abaho, Helode kasegela mwiisi ya Yudea kachola kukala mwiisi ya Kaisalia.

### *Ifa ya Helode*

20 Helode kawagevuzikila ng'hani wanhu wa Tilo na Sidoni, avo wamgendela hamoja. Tanhu wamtewenza Bulasto, mkalizi wa ng'anda ya Mndewa yawataze. Abaho wachola kwa Helode kumpula kuwe na tindiwalo, kwavija isi yao itamanila lujo kulawa mwiisi ya Mndewa.
21 Mna disiku disaguligwe Helode kavala viwalo vake va undewa, kakala mkigoda chake cha undewa, kalonga na wanhu.
22 Wanhu wakemelela, “Ino sauti ya Mulungu, siyo ya munhu.”
23 Bahaja msenga wa kuulanga kambwanha hasi Helode, kwavija hamgwelele Mulungu ukulu. Kahomigwa na msango kafa.
24 Lakini mbuli ya Mulungu igendelela kwenela.
25 Balinaba na Sauli viwamambukize sang'hano yao, wabwela Yelusalemu hamoja na Yohana Maluko.

# 13

### *Sauli na Balinaba wosaguligwa na kutumigwa*

1 Mna iwanhu wamtogole Yesu ako Antiokia, kukala na watula ndagu wa Mulungu na wafundiza, Balinaba na Sauli na Simeoni yakemigwe Mtitu na Lukio yalawile Kilene, Manaeni yakulile hamoja na Mndewa Helode.

2 Viwakalile womgwaa ukulu Mndewa na kufunga kuja, Loho Yang'alile kawalongela, “Mbagulileni Balinaba na Sauli wasang'hane sang'hano iniwakemele.”

3 Wafunga kuja na kumpula Mulungu, wawekila makono wawatuma wachole.

### *Sauli na Balinaba wowapetela wanhu ako Kupulo*

viyokomigwa na kukaliza viwalo va wanhu wakalile womkoma.’
21 Mndewa kanongela, ‘Genda, kwavija nokugala kutali kwa wanhu
haweli Wayahudi.’ ”
22 Wanhu wamtegeleza Paulo mbaka viyalongile vino, lakini wasonga
kuguta nyangi, “Msegezeni! Mkomeni! Holondigwa yawe mgima!”
23 Wagendelela kuguta nyangi kuno wopunga viwalo vao, wagevuzika na
kupigisa timbwisi uchanha.
24 Mkulu wa wakalizi kawalagiza wanhu zake wamgale Paulo
kuing'hambi, kawalongela wamtowe mbalati muladi wajuwe habali
Wayahudi woguta nyangi kamba avo mbuli yake.
25 Lakini viwamgodeke na kulonda kumtowa mbalati, Paulo kamulongela
mkulu yemile aho, “Vino malagizo gotogola kumtowa mwenekae wa Lumi
ing'hali hainajuwika mbuli gani ihile iyaitendile?”
26 Mkulu ayo viyahulike vivo kachola kwa mkulu wa wakalizi kamuuza,
“Kolonda kutenda choni? Munhu ayo mwenekae wa Lumi!”
27 Avo mkulu wa wakalizi kamcholela Paulo kamuuza, “Nongele, gweye
kwa mwenekae wa Lumi?”
Paulo kamwidika, “Ona.”
28 Mkulu wa wakalizi kamulongela, “Niye niwa mwenekae wa Lumi kwa
kulipa sente nyingi.”
Lakini Paulo kamwidika, “Niye na mwenekae wa Lumi kwa kuleligwa,”

29 Bahaja wanhu walondile kumsola Paulo walawanya. Na ayo mkulu wa wakalizi kadumba ng'hani viyajuwile Paulo kakala mwenekae wa Lumi na kuno kamgodeka nzabi.

### *Paulo kamkitala cha Wayahudi*

30 Mkulu wa wakalizi kalonda kujuwa habali Wayahudi wamtagusa Paulo. Avo imitondo yake kamfungula Paulo iminyololo na kuwalagiza wakulu wa walava nhosa na wanhu wose wa mkitala waiting'hane. Abaho kamsola Paulo na kumwika haulongozi wao.

# 23

1 Paulo kawalola bunhuu wanhu wa mkitala, kalonga, “Waizilaeli wayangu! Mbaka lelo nosang'hana goyolonda Mulungu kwa moyo uleka kunitagusa kamba nibananga.”
2 Baho Anania Mulava nhosa mkulu kawalagiza waja wakalile behi na Paulo wamtowe kofi mumulomo.
3 Paulo kamulongela, “Mulungu kokutowa kofi gweye mwenyego uigalile na kando dibakigwe uzelu! Kwima baho muladi unitaguse kwa Malagizo, kuno gweye mwenyego kobena Malagizo kwa kulagiza nhoweke!”
4 Wanhu wemile behi na Paulo wamulongela, “Gweye komuliga mulava nhosa mkulu wa Mulungu!”
5 Paulo kedika, “Waizilaeli wayangu, sijuwile bule kamba kakala mulava nhosa mkulu. Kwavija Maandiko Gang'alile golonga, ‘Sekeumulonge vihile mulangulizi wa wanhu zako.’ ”
6 Paulo viyone bumbila diyagwe wakala Masadukayo na wayagwe wakala Mafalisayo, kakemelela mkitala, “Waizilaeli wayangu! Niye na Mfalisayo, mwanage Mfalisayo. Niye ngaligwa hano mkitala kwavija notogola kamba wanhu wafile wozilibuka!”
7 Bahaja viyalongile avo, Mafalisayo na Masadukayo wasonga kuihasanya, na bumbila diigola.
8 Kwavija Masadukayo wolonga kuduhu kuzilibuka kwa wafile na kuduhu wasenga wa kuulanga hebu loho, lakini Mafalisayo wogatogola gose madatu.
9 Wakemelela ng'hani, wafundiza Malagizo ga Musa wayagwe wa kibumbila cha Mafalisayo wenuka walonga kwa nguvu, “Hatuona kiyabanange munhu ino! Yodahika loho hebu msenga wa kuulanga kalonga nayo kweli!”
10 Bwato dikala kulu mbaka mkulu wa wakalizi kengila bwembwe kamba Paulo yahakanhigwe vihande vihande. Avo kawalagiza wakalizi zake wahumuluke kuna dibumbila, wamsegeze Paulo wamgale kuna ing'hambi.
11 Kilo acho Mndewa kema behi ya Paulo, kamulongela, “Sekeudumbe! Kamba viuwalongele mbuli zangu hano Yelusalemu, vivija kolondeka utende vivo kudibuga da Lumi.”

### *Wayahudi wolonda kumkoma Paulo*

12 Imitondo yake wayahudi wayagwe waiting'hana hamoja na kutenda ubala. Waiduila honda waje hebu kung'wa mazi mbaka vonda wamkome Paulo.
13 Wanhu waitogolele kutenda avo wakala wanhu kubanza malongo mane.
14 Abaho wachola kwa wakulu wa walava nhosa na wavele, walonga, “Tuiduila hamoja kamba hatuja kinhu mbaka vonda tumkome Paulo.

15 Avo, gweye na wanhu wa mkitala galeni usenga kwa mkulu wa wakalizi yamgale Paulo kumwetu, kuno moitenda molonda kujuwa goya mbuli zake. Na tweye toitanda kumkoma yang'hali hanavika hano."

16 Lakini mwana wa lumbu jake Paulo kahulika kiseto chao, avo kachola kuna ing'hambi kamulongela Paulo.

17 Abaho Paulo kamkema mkulu imoja wa wakalizi, kamulongela, "Mgale mbwanga ino kwa mkulu wa wakalizi, kana mbuli ya kumulongela."

18 Mkulu ayo kamsola, kamulongoza mbaka kwa mkulu wa wakalizi, kamulongela, "Ayo Paulo yagodekigwe, kang'hema na kunipula nimgale mbwanga ino kumwako, kwavija kana mbuli kolonda kukulongela."

19 Mkulu wa wakalizi kamgoga mkono, kamgala hamgwazo waiyeka, kamuuza, "Kolonda kunongela choni?"

20 Kamulongela, "Wakulu wa Wayahudi wailumba mayo wakupule wamsole Paulo kuna ikitala, kuno woitenda wanhu wa mkitala wolonda kujuwa goya mbuli zake.

21 Lakini sekeuwatogolele, kwavija kuna wanhu kubanza malongo mane awo waifisa wombeta. Waiduila hawaja kinhu hebu kung'wa mbaka vonda wamkome. Wao sambi waitanda kutenda avo na wobetela vonda ulonge."

22 Mkulu wa wakalizi kalonga, "Sekeumulongele munhu yoyose kamba kunongela mbuli ino." Abaho kamuleka imbwanga yachole.

### *Paulo kogaligwa kwa mkulu wa isi ya Yudea*

23 Abaho mkulu wa wakalizi kawakema wakulu zake wabili, kawalongela, "Watandeni wakalizi magana mabili wachole Kaisalia, hamoja na wakwela falasi malongo saba na wakalizi magana mabili wa migoha, na muitande kusegela saa ndatu lelo ikilo.

24 Mtandeni falasi wa Paulo, na mumvikize mgima kwa Felikisi mtawala wa Kilumi wa isi ya Yudea."

25 Abaho mkulu wa wakalizi kandika baluwa ilonga vino,

26 Go mkulu, zihoze, "Niye Kilaudio Lusia, nokwandikila gweye, mkulu Felikisi.

27 Wayahudi wamgoga munhu ino na walonda kumkoma, lakini vimbonile kakala mwenekae wa Lumi, avo nhyola na wakalizi zangu kumuhonya.

28 Nilonda kujuwa kilamuso cha kumtagusila, avo nimgala mkitala chao.

29 Lakini nyona kuduhu mbuli yoyose iyatendile kumtenda yafe hebu kugodekigwa mkifungo. Nhaguso yao kumwake ikala mbuli ya Malagizo gao wenyego.

30 Na vinongeligwe kuna kiseto cha kumkoma, ndopola kumgala kumwako. Niwalongela wanhu wamtaguse wagale vitala vao kumwako."

31 Avo wakalizi wao wamsola Paulo kamba viwalagizigwe. Wamgala ikilo acho mbaka Antipatili.

32 Imitondo yake wakalizi wa magulu wabwela kuna ing'hambi, wawaleka waja wakalizi wa falasi wagendelele na mwanza hamoja na Paulo.

33 Viwavikile Kaisalia wamgwaa ija ibaluwa mkulu wa isi ayo na kumwika Paulo mmakono gake.

34 Mkulu ayo viyaisomile ibaluwa kamuuza Paulo kalawa isi gani. Viyajuwile kalawa isi ya Kilikia,

35 kamulongela, “Nokutegeleza kipindi wanhu wakutaguse wahavika.” Abaho kalagiza Paulo yekigwe muukalizi, mng'anda ya Helode imkulu wa isi.

# 24

### *Paulo kamkitala kwa Felikisi*

1 Vizibitile siku tano, Anania mulava nhosa mkulu hamoja na wavele na munhu yagajuwile malagizo yakemigwe Telutulo, wachola kwa Felikisi wamulongela vitala vao mbuli ya Paulo.

2 Abaho Paulo kakemigwa, na Telutulo kasonga kulava kitala chake vino,

“Go mkulu Felikisi! Ulangulizi wako unogile ugala tindiwalo kwa kipindi kitali, na mgaluko mkulu wotendigwa mbuli ya isi yetu.

3 Tweye tubokela mbuli ino kwa deng'ho na siku zose tolonga utogoligwe.

4 Silonda ng'hani kwagiza kipindi chako, lakini nokupula uwe muhole na utegeleze goya gonilonga.

5 Tona kamba munhu ino mng'hobo ng'hani, kogala ndwagi kwa Wayahudi mwiisi yose na iyo mkulu wa kibumbila cha Wanazaleti.

6 Vivija kalonda kuigela dikwe Ng'anda ya Mulungu, na tweye tumgoga. Tulonda kumtagusa kwa malagizo getu.

7 Lakini Lusia, mkulu wa wakalizi keza, kamsola kwa nguvu mmakono getu.

8 Na gweye wahamuuza munhu ino, kodaha kujuwa kulawa kumwake mbuli zose zitumtagusila.

9 Wayahudi nao watogola kiyalongile Telutulo.”

### *Paulo koigombela haulongozi wa mkulu wa isi ya Yudea Felikisi*

10 Mkulu ayo kamwinulila Paulo mkono muladi yalonge, na Paulo kalonga, “Nodeng'helela kuigombela haulongozi wako kwavija nojuwa miyaka heleketwa gweye kwa msemi wa isi ino.

11 Gweye mwenyego kujuwa kamba zibita siku longo na mbili ziiyeka toka nyhole Yelusalemu kumtambikila Mulungu.

12 Wayahudi hawambonile ngombe na munhu Mng'anda ya Mulungu hebu wambone nowading'hula wanhu, siyo mng'anda ya kumpula Mulungu hebu hanhu hohose kudibuga.

13 Nao hawadaha kukulagusila kitala kiwanigalile hano.

14 Lakini niye notogola nomgwaa ukulu Mulungu wa wahenga zetu na kuikweleleza nzila ayo iwoikema ya uvizi. Lakini vivija noitogola kila mbuli yandikigwe mna Gamalagizo ga Musa na vitabu va watula ndagu wa Mulungu.

15 Niye nomtamanila Mulungu kamba vija viwomtamanila hewo, kamba wanhu wose wanogile na wehile wozilibuka kwa wafile.

16 Avo siku zose niiyoha ng'hani sambi niwe na moyo unitagusa kamba nibananga mgameso ga Mulungu na mgameso ga wanhu.”

17 “Viibitile miyaka mingi mbwela Yelusalemu muladi kuwagwaa sente wayangu na kumulavila Mulungu nhosa.

18 Ving'halile notenda avo wanyona Mng'anda ya Mulungu, ving'homeleze kihendo cha kuisunha. Kukala kuduhu lunhu hebu ndwagi yoyose.

19 Lakini Wayahudi wayagwe walawile mwiisi ya Asiya wakala baho, awo wao walondeke kwiza hano haulongozi wako na kulava kitala chao kamba wana mbuli yoyose kumwangu.

20 Hebu leka wanhu wano weli hano walonge, mbuli gani ihile iwaiyonile
kumwangu vinimile mkitala,
21 lakini mbuli zino ziiyeka zinongile vinimile haulongozi wao kamba,
'Lelo niye ngogigwa mbuli ya kutogola kamba wanhu wafile wozilibuka.' "
22 Abaho Felikisi yakalile yaijuwile goya mbuli ya kibumbila cha wanhu
wamtogole Yesu, kawalongela wanhu wanyamale, kalonga, "Vondayeze
Lusia, mkulu wa wakalizi, nolava nhaguso ya mbuli ayo."
23 Kamulagiza mkulu wa wakalizi yamkalize Paulo, lakini sekeyamkalize
ng'hani na yawatogolele mbwiga zake wamgwee kiyolonda.

### *Paulo kahaulongozi wa mkulu wa isi ya Yudea Felikisi na Dulusila*

24 Vizibitile siku ndodo Felikisi keza hamoja na mwehe wake Dulusila,
yakalile Muyahudi. Kalagiza Paulo yagaligwe, kamtegeleza viyalongile
mbuli ya kumtogola Yesu Kilisito.
25 Lakini Paulo viyakalile kolonga mbuli ya kutenda ganogile na
kuigomesa mwenyego na mbuli ya Siku ya Mulungu kuwatagusa wanhu,
Felikisi kadumba ng'hani kalonga, "Sambi kodaha kuchola, nokukema
kabili nahapata nyafasi."
26 Mna ikipindi acho kakala yotamanila Paulo yahamgwelele sente,
lekaavo kakala yogendelela kumkema na kulonga nayo.
27 Viibitile miyaka mibili, Polikio Fesito kamuhala Felikisi nyafasi ya ukulu
wa isi. Felikisi kalonda nhogolwa kwa Wayahudi avo kamuleka Paulo
mkifungo.

## 25

### *Paulo kochola kumwande kwa Mndewa mkulu wa Lumi*

1 Siku ndatu kumwande Fesito viyavikile mwiisi ayo, kasegela Kaisalia
kachola Yelusalemu,
2 wakulu wa walava nhosa na wakulu wa Wayahudi viwagalile kitala chao
mbuli ya Paulo. Wampula Fesito,
3 yawatendele vinogile yamgale Paulo Yelusalemu, kwavija wakala kiseto
mnzila wamkome.
4 Fesito kawedika, "Paulo kamkifungo ako Kaisalia, naniye nobwela kuko
sambi baha.
5 Walekeni wakulu zenu wachole na niye Kaisalia wakamtaguse kamba
katenda gehile."
6 Fesito kakala hamoja nao siku nane hebu longo abaho kachola Kaisalia.
Imitondo yake kakala mkigoda cha nhaguso mkitala, kalagiza Paulo ya-
galigwe mgati.
7 Paulo viyavikile, Wayahudi walawile Yelusalemu wamzunguluka na
kusonga kulava vitala vikulu vikulu viwalemele kulava usindila.
8 Lakini Paulo kaigombela, "Niye sitendile chochose kihile kwa Malagizo
ga Wayahudi hebu kwa Ng'anda ya Mulungu hebu kwa Mndewa mkulu wa
Lumi."
9 Lakini Fesito kalonda nhogolwa kwa Wayahudi, avo kamuuza Paulo,
"Kotogola kuchola Yelusalemu ukatagusigwe ako mgameso gangu mbuli ya
gano?"
10 Paulo kalonga, "Niye nokwima hano mkitala cha Mndewa mkulu wa
Lumi, hano baho nilondeka kutagusigwa. Kamba viujuwile siwatendile
Wayahudi chochose kihile.
11 Nahatenda dihile dinilondeka nhaguso ya kufa silema bule. Lakini
kamba kuduhu ukweli mvitala viwagalile mbuli yangu, kuduhu munhu

yodaha kunigala kumwao nochola kumwande kwa Mndewa mkulu wa Lumi."
12 Baho Fesito viyamambukize kulonga na wanhu zake wamkitala, kamulongela Paulo, "Kuchola kumwande kwa Mndewa mkulu wa Lumi, avo kochola kwa Mndewa mkulu wa Lumi!"

### *Paulo kahaulongozi wa Agilipa na Benike*

13 Vizibitile siku nyingi mndewa Agilipa na Benike wavika Kaisalia muladi kumulamusa Fesito.
14 Viwakalile ako siku nyingi, Fesito kamsimulila mndewa mbuli za Paulo, kalonga, "Hano hana munhu yalekigwe mkifungo na Felikisi.
15 Viny'holile Yelusalemu, wakulu wa walava nhosa na wavele wa Wayahudi wagala kitala kumwangu na kumhula nimtaguse.
16 Lakini niye niwedika siyo vivo viwatendaga Walumi kumulava munhu yatagusigwe yang'hali hana iting'hana na wanhu walavile kitala kihanga kwa kihanga na kugoleligwa nyafasi yaigombele mwenyego.
17 Viwezile hano, sikawile bule, lakini imitondo yake ng'hema mting'hano mkitala na kulagiza munhu ayo yagaligwe.
18 Wanhu wamtaguse viwemile hawalavile kitala chochose kihile kamba vinigesile nene.
19 Lakini wakala woibamilila mbuli ya dini yao wenyego na mbuli ya munhu yokemigwa Yesu, yakalile yafile, lakini Paulo kagendelela kulonga kakala mgima.
20 Sijuwile dakutenda vija nahapatile mbuli zino. Avo nimpula Paulo kamba yahadahile kuchola Yelusalemu na kutagusigwa kuko.
21 Lakini Paulo kachola kumwande, kalonda Mndewa mkulu wa Lumi yalamule mbuli yake na yekigwe muukalizi. Avo nilagiza yekigwe muukalizi mbaka vondanimgale kwa Mndewa mkulu wa Lumi."
22 Agilipa kamulongela Fesito, "Maza nahanogelwe ng'hani kamba nahamuhulika munhu ayo niye mwenyego."
Fesito kamwidika, "Komuhulika mayo."
23 Imitondo yake Agilipa na Benike wengila kwa deng'ho kudigati da kuiting'hana, wakulu wa wakalizi na wakulu wa ziisi. Fesito kalagiza Paulo yagaligwe mgati.
24 Fesito kalonga, "Mndewa Agilipa na wanhu wose muli hano hamoja na tweye, mumona munhu ino Wayahudi wose ako Yelusalemu na hano wagala vitala kumwangu. Walonga munhu ino yakomigwe.
25 Lakini niye siyonile mbuli yoyose ihile iyatendile mbaka yakomigwe. Kwavija heyo mwenyego kalonda kuchola kumwande kwa Mndewa mkulu wa Lumi, nigesa nimgale kuko.
26 Lakini niye nabule mbuli ya kumwandikila Mndewa mkulu wa Lumi mbuli ya munhu ino. Avo nimgala haulongozi wenu ng'haning'hani haulongozi wako, gweye Mndewa Agilipa muladi wahamala kumulolesa, mhate dakwandika mbuli yake.
27 Kwavija vinigesa yokuwa yosekeza nahamgala mfungwa bila kwandika kilamuso kiyatagusiligwe."

## 26

### *Paulo koigombela haulongozi wa Agilipa*

1 Agilipa kamulongela Paulo, "Kodaha kuigombela." Baho Paulo kenula makono gake kalonga vino,

2 “Mndewa Agilipa! Niye noiyona nimweda, lelo kuigombela haulongozi
wako mbuli zose ziwonitagusila Wayahudi.
3 Kwavija gweye kuvijuwa goya vihendo va Wayahudi na kuihasanya
kwao. Nokupula ufunge umoyo unhegeleze.”
4 “Wayahudi wose wajuwa ving'halile toka haudodo wangu. Wajuwa
ving'halile mwiisi yangu na ako Yelusalemu.
5 Toka mwaka wanijuwa goya, na wao wahalonda wodaha kukulon-
gela kamba ng'hala mkibumbila cha Mafalisayo womgwaa ukulu Mulungu
kubanza wose.
6 Lelo nokwima hano nitagusigwe mbuli ya kutamanila lagano diwag-
weleligwe wahenga zetu na Mulungu.
7 Dino ijo lagano ditamaniligwa koneka na makabila longo na mabili,
kamba viwomsang'hanila goya Mulungu imisi na ikilo. Mbuli ya gago, go
mkulu notagusigwa na Wayahudi!
8 Mweye mose muli hano, habali mokona vidala kutogola kamba Mulungu
kowazilibula wanhu wafile?”
9 “Niye mwenyego nhenda kila mbuli kuwagoma wanhu waditogole
twaga da Yesu wa Nazaleti.
10 Lekaavo nhendile vivo ako Yelusalemu. Nigweleligwa udahi na wakulu
wa walava nhosa na kuwagodeka mkifungo wanhu wengi wamtogole Mu-
lungu, na viwatagusigwe kufa na niye niilumba nao.
11 Miyanza mingi nyhola mzing'anda za kumpula Mulungu na ni-
wananahiza wabele kutamanila kwao. Ng'hala niwehile ng'hani mbaka
nyhola mmabuga ga kutali kuwadununza.”

### *Paulo kolonga vija viyagaluke*
### *Sang'h 9:1-19; 22:6-16*

12 “Kwa mbuli ayo ving'halile nochola Damesiki kwa udahi wa wakulu wa
walava nhosa.
13 Go mkulu, kipindi ving'halile mnzila, zuwa vidikalile mdindosi, nyona
mulenge mkulu kubanza zuwa, womwemwesa kulawa kuulanga, unizun-
guluka niye na waja wayangu.
14 Tweye wose tulagala hasi na mhulika sauti yonongela kwa Kiebulania,
‘Sauli, Sauli! Habali konidununza? Koilumiza mwenyego kamba ng'ombe
yotowa mbalati ya mndewa wake.’
15 Niye nimuuza, ‘Mndewa, gweye kwa nani?’ Nayo Mndewa kanidika,
‘Niye na Yesu, yuunidununza.
16 Lakini winuke wime kwa magulu gako. Nikulawilila muladi nikusagule
uwe msang'hanaji wangu. Kowalagusila wanhu wayagwe lelo kunyona na
gaja gonda nikulagusile.
17 Nokuhonya na wanhu wa Izilaeli na vivija nokuhonya na wanhu haweli
Wayahudi ako konda nikugale.
18 Uwafumbule meso gao walawe mdiziza weze kudilenge na walawe
mmakono ga Mwenembago wambwelele Mulungu, avo kubitila kutamanila
kwao kumwangu nzambi zao zogeligwa kumgongo na wopata uhazi wao
mna iwanhu wasaguligwe na Mulungu.’ ”

### *Paulo kolonga mbuli ya sang'hano yake*

19 “Avo Mndewa Agilipa sikilemile bule kinhu acho cha kuulanga kiyanda-
gusile Mulungu.
20 Niwapetela wanhu kusongela Damesiki na Yelusalemu na abaho isi
yose ya Yudea na kwa wanhu haweli Wayahudi. Waleke nzambi zao na
wambwelele Mulungu na watende gaja golagusa waleka nzambi zao.

21 Kwa mbuli ayo lekaavo Wayahudi wangoga ving'halile mng'anda ya
kumpula Mulungu, na walonda kung'homa.
22 Lakini Mulungu kanhaza mbaka lelo, na avo nima hano kuwalongela
wanhu wose, wakulu kwa wadodo. Mbuli inonga iyo iija iwalongile watula
ndagu wa Mulungu na Musa yolawilila.
23 Mbuli ya Kilisito Mkombola kalondeka yadununzike na yawe wa ichan-
duso kuzilibuka kwa wafile, muladi yawapetele Wayahudi na wanhu haweli
Wayahudi mulenge wa kukomboligwa."
24 Paulo viyakalile koigombela avo, Fesito kakemelela, "Gweye Paulo,
kuna kibozi mbwelela! Kusoma kwako ng'hani kukwehula!"
25 Paulo kamwidika, "Go mkulu, sikwingililigwa bule, vinonga niye ukweli
wiiyeka.
26 Mndewa Agilipa! Kumwako nolonga bila kudumba kwavija mbuli
zino zose kuzijuwa goya. Vinigesa mbuli zino kuzijuwa goya kwavija
hazitendeke kinyelegezi.
27 Mndewa Agilipa, vino kowatogola watula ndagu wa Mulungu? Nojuwa
kowatogola!"
28 Agilipa kamulongela Paulo, "Viugesa kwa kipindi kino kidodo kodaha
kunhenda niwe mkilisito?"
29 Paulo kamwidika, "Kiwe kipindi kidodo hebu kitali nompula Mulungu
gweye na mweye mose munhegeleza hano lelo muwe kamba vinili niye,
lakini bila minyololo!"
30 Baho Mndewa Agilipa, na mkulu wa isi, Benike na waja wose wakalile
hamoja nao, wenuka.
31 Viwakalile wosegela wailongela, "Munhu ino hatendile mbuli ya kum-
tenda yafe hebu yagodekigwe mkifungo."
32 Nayo Agilipa kamulongela Fesito, "Maza munhu ino halondile kuchola
kumwande kwa Mndewa mkulu wa Lumi yahafunguligwe."

# 27

*Paulo kogaligwa Lumi*

1 Viwaitogolele tuchole Italia, wawagela Paulo na wafungwa wayagwe
mmakono ga Juliasi, mkulu wa kibumbila cha wakalizi wa Lumi,
kikemigwe, "Kibumbila cha Mndewa wa Lumi."
2 Tukwela meli ilawile Adilamito, ikalile yochola mhwani ya isi ya Asiya
na tusonga umwanza. Alisitaliko, mwenekae wa Makedonia kulawa Sesa-
lonike kakala na tweye.
3 Imitondo yake tuvika Sidoni. Juliasi kamonela bazi Paulo na kamtogolela
yachole kuwalola mbwiga zake, yagweleligwe kiyalondile.
4 Kulawa ako tugendelela na mwanza kwavija ubeho ukala wobuma
kwiza kumwetu, avo tubitila kisiwa cha Kupulo kukalile kuduhu ubeho.
5 Abaho tuloka bahali ya Kilikia na Pamfulia, tuvika kudibuga da Mula
mwiisi ya Lukia.
6 Baho mkulu ayo kayona meli ng'hulu yolawa Alekizandilia ikala yochola
Italia, avo katukweza.
7 Tugendelela na mwanza mholemhole, na kwa siku nyingi kwa kugaya
ng'hani tuvika mwiisi ya Nido. Ubeho ututenda seketuchole kutali ng'hani
na mwambu uja, avo tubitila mwambu wa Kilete behi na Salimone ako
ubeho haukalile mkulu bule.
8 Tubita mumgwazo mholemhole tuvika hanhu hokemigwa Bandali In-
ogile behi na buga da Lasea.

9 Aho tuhakala ng'hani, mbaka kipindi cha kufunga kuja kikala kibitile,
kwavija kipindi acho kikala hakinogile bule kugenda kwa meli. Avo Paulo
kawazuma,
10 “Wayangu, vinikona mwanza uno wokuwa na magayo mengi na kwag-
iza vinhu vingi vikwezigwe mwiimeli, vivija kwagiza ugima wetu.”
11 Lakini mkulu wa wakalizi kanogelwa na kija kiyalongile mulosaji na
mwene meli siyo gaja gayalongile Paulo.
12 Kwavija hanhu aho hakala hehile na kikala kipindi cha kihuhwe, wanhu
wengi wanogelwa kugendelela na mwanza yahadahika wavike Foiniki.
Foiniki ayo bandali ya Kilete ichola kusini kudihongela zuwa na kasikazini
kudihongela zuwa, ako wahadahile kukala kipindi cha kihuhwe.

### *Beho kulu mbahali*

13 Lubeho lunogile lwa kudihongela zuwa lusonga kubuma, na wao
wagesa kamba wapata kiwalondile, avo wafungula nzabi, wasegeza meli
yao wachola behi ya mhwani ya Kilete.
14 Lakini hakibitile kipindi kitali, ubeho mkulu ukemigwa “Ubeho wa
kaskazini,” usonga kubuma kulawa mkisiwa.
15 Ubeho uitowa ayo imeli, kwavija hatudahile kuugomesa tuileka
isoligwe na beho.
16 Kisiwa kimoja kidodo kikemigwe Kauda kitutaza kidogo na uja uubeho,
na vitubitile kusini yake tuhonyeka, hamoja tugazika ng'hani, tudaha kuki-
honya kija ikigalawa didodo cha meli ayo.
17 Wanhu wakikwega kigalawa mgati, abaho waizungulusila nzabi imeli
na kuifunga kwa nguvu. Wadumba wahananahile mumgwazo wa bahali,
mhwani ya Libiya, avo wahulumusa matanga na kuileka imeli isoligwe na
beho.
18 Beho digendelela kubuma na imitondo yake wasonga kuyasa mizigo ili
mwiimeli.
19 Siku da kadatu wasonga kwasa mgamazi vinhu viyagwe vili mwiimeli
kwa makono gao wenyego.
20 Kwa kipindi cha siku nyingi hatudahile kujona zuwa hebu nhondo, beho
digendelela ng'hani mbaka twagiza tamanilo da kuhona.
21 Viwakalile kipindi kitali bila kuja, Paulo kema haulongozi wao kawa-
longela, “Wayangu maza munhegeleze niye na kuleka kuchola Kilete, sambi
gatupate magayo gano gose na ubananzi uno.
22 Lakini sambi nowapula, gangamaleni! Kuduhu imoja wenu yonda yafe,
meli iiyeka iyo yonda ibanangike.
23 Kwavija kilo cha jana msenga wa kuulanga wa Mulungu kanizila.
Mulungu inimsang'hanila na kumgwaa ukulu.
24 Msenga ayo wa kuulanga kanilongela, ‘Paulo sekeudumbe! Kolondeka
wime haulongozi wa Mndewa mkulu wa Lumi. Kwa mbuli yako Mulungu
kouhonya ugima wa wanhu wose weli muumwanza na gweye.’
25 Avo wayangu fungeni moyo! Kwavija nomtamanila Mulungu, galaw-
ilila kamba viyanongele.
26 Lakini tokwasigwa kuna ikisiwa kiyagwe.”
27 Kilo cha longo na nne, twasigwa na ubeho kuna ibahali ya Meditelania,
kilo kikulu walosaji wasinhukila wa behi na isi inyalile.
28 Wahumulusa hasi luzabi lufungigwe kinhu kizito kuzahila utali wa
mazi, wapata utali wa mita malongo mane. Abaho watenda vivo kabili
wapata malongo madatu.
29 Wadumba kamba imeli sekeichole kuna gamabwe avo wahumulusa
nanga nne kukisogo cha imeli, wapula uche hima hima.

30 Abaho walosaji walonda kutoloka, wahumulusa ikigalawa kidodo mga-
mazi na waitenda wochola kwika nanga kuulongozi wa imeli.
31 Lakini Paulo kamulongela mkulu wa wakalizi na wakalizi, "Kamba
walosaji wano hawasigala mumuno mwiimeli, sambimutamanile kuho-
nyeka."
32 Avo wakalizi wazikanha nzabi ziigogile ngalawa ndodo na kuileka
ichole.
33 Usiku haunakucha, Paulo kawapula wanhu wose waje, "Kwa siku zose
longo na nne mukala munyawanyawa, hamudile kinhu chochose.
34 Lelo nowapula chonde muje lujo muladi mupate nguvu ya kugendelela
kuwa wagima. Kuduhu hata luvili lumoja londa lwage."
35 Paulo viyamambukize kulonga avo, kasola gate, kamgwaa nhogolwa
Mulungu mgameso gao, kadibanzula kasonga kuja.
36 Kila munhu kasamhuka, kasola gate kaja.
37 Wanhu wose kwa wose tukalile mwiimeli tukala wanhu magana mabili
na malongo saba na sita.
38 Viwegute wahunguza uzito wa meli, kwa kwasa uhule wa ngano mba-
hali.

### *Meli yobeneka*

39 Viuchile, walosaji hawaijuwile bule isi ayo, ila wona msanga wa mh-
wani, avo waitogolela kwima aho kamba yahadahika.
40 Wakanha zinanga wazileka mbahali, kipindi kikija wazifungula zinzabi
zifungigwe muusukani, abaho wadinula digolole dili kuulongozi muladi
digoge beho, wachole mhwani.
41 Lakini wavika hanhu haziiting'hanile bahali mbili, na imeli yangama.
Mwambu wa ulongozi wangama mumsenga bila kutigisika. Mwambu
wa kukisogo wa imeli usonga kubeneka vihande mbuli ya mazi geli na
ng'humbi.
42 Wakalizi walonda kuwakoma wafungwa wose kwa kudumba kamba
wahakogelele mbaka mhwani na kutoloka.
43 Mkulu wa wakalizi kalonda kumuhonya Paulo, avo kawagomesa seke-
watende avo. Ila kawalagiza wose wadahile kogelela wazumhe kulawa
mwiimeli na wogelele mbaka mhwani.
44 Wayagwe wakweleleza kwa kugoga vihande va mbao hebu vihande va
imeli ibeneke. Vivo tuhonyeke tweye wose na kuvika wagima mhwani.

# 28

### *Ako Malita*

1 Vituvikile kuna imhwani kuno twawagima, tujuwa kamba kisiwa kija
chokemigwa Malita.
2 Wenekae wa aho watunogela ng'hani. Mvula isonga kutowa na kukala
na beho, avo wabwinha moto na kutugoneka.
3 Paulo kadondola ngodi kakala yozika muumoto, mbuli ya umoto awo
mgendela hasi kalawa mzingodi kamuluma Paulo na kuizingiliza mumkono
wake.
4 Wenekae wa aho viwamone mgendela hasi mumkono wa Paulo wai-
longela, "Vitukona munhu ino kokuwa mkomaji, hamoja kahonyeka kufa
mbahali, nhaguso ya milungu haimulekile yagendelele kuwa ugima."
5 Lakini Paulo kamwasila muumoto mgendela hasi ayo na hamulumize
bule.

6 Wanhu waja wakala womulola kamba yahavimbile hebu yalagale hasi na kufa. Lakini viwabetele kwa kipindi kitali na kona haduhu kinhu kimulawilile, wagaluka na kulonga, “Heyo kakala mulungu!”

7 Behi na hanhu aho hakala na migunda ya mkulu wa ikisiwa yakemigwe Pubulio. Avo katugoneka, kwa kipindi cha siku ndatu tukala ukayake.

8 Tatake Pubulio kakala yawasile mulusazi kolumwa homa na kuhala. Paulo kachola kumulola, viyamambukize kumpula Mulungu, kamwikila makono gake, kamuhonya.

9 Viyamambukize kutenda avo, wanhu wayagwe wakalile watamu mkisiwa acho weza na wahonyigwa.

10 Wanhu watugwaa nhunza nyingi na kipindi vitusongile mwanza kabili, weka mwiimeli kila kinhu kitulondile.

*Kulawa Malita kuchola Lumi*

11 Viibitile miezi midatu tusonga kabili mwanza kwa meli ilawile Alekizandilia, ikemigwe, “Milungu Pacha.” Meli ayo ikala imile mkisiwa acho kwa kipindi chose cha kihuhwe.

12 Tuvika kudibuga da Silakusa, na tukala baho kwa siku ndatu.

13 Kulawa aho tugendelela na mwanza na tuvika mwiisi ya Legio. Imitondo yake beho disonga kubuma kulawa kusini, vizibitile siku mbili tuvika kudibuga da Potioli.

14 Ako tuwavika wayetu wamtogole Yesu, wao watupula tukale nao siku saba. Abaho tuvika Lumi.

15 Waetu wamtogole Yesu ako Lumi viwatuhulike tuvika, wayagwe weza kutubokela Kudigulilo da Apio na wayagwe hanhu hokemigwa Ng'anda Ndatu za wageni. Paulo viyawaonile kamgwaa nhogolwa Mulungu.

*Paulo kudibuga da Lumi*

16 Vituvikile kudibuga da Lumi, Paulo katogoleligwa kukala yaiyeka hamoja na mkalizi imoja wa kumkaliza.

17 Vizibitile siku ndatu, Paulo kawakema hamoja walangulizi wa Kiyahudi wa hanhu aho. Viwaiting'hane kawalongela, “Waizilaeli wayangu, hamoja sitendile mbuli yoyose ihile kwa wanhu zetu hebu kwa vihendo vetu vitubokele kwa wahenga zetu, ngodekigwa ako Yelusalemu na ngeligwa mmakono ga Walumi.

18 Viwaniuzile na kona sitendile mbuli yoyose ihile ya kung'homela, walonda kunifungulila.

19 Lakini Wayahudi viwailemile mbuli ino, niye nyhola kumwande kwa Mndewa mkulu wa Lumi, hamoja ng'hala nabule kitala chochose kwa wanhu zangu.

20 Lekaavo niwapula mwize nonge na mweye, niye nigodekigwa minyololo kamba vino, kwavija notogola Mkombola iwakalile wombeta wanhu wa Izilaeli keza.”

21 Wao wamulongela, “Tweye hatubokele baluwa yoyose kulawa Yudea mbuli yako wala kuduhu munhu yoyose yezile hano na kulonga mbuli zako hebu yalonge chochose kihile kumwako.

22 Lakini yokuwa vinoga tukuhulike mwenyego ulonge magesa gako, kwavija tweye tojuwa kamba kila hanhu wanhu wokilema kibumbila kino.”

23 Avo wapanga kuiting'hana, na wanhu wengi wavika kuyakalile. Toka imitondo mbaka ichungulo Paulo kawasimulila na kuwafambulila mbuli za Undewa wa Mulungu kageza kuwatenda wamtogole Yesu kwa kusoma Malagizo ga Musa na maandiko ga watula ndagu wa Mulungu.

24 Wanhu wayagwe wazitogola mbuli zake, ila wayagwe hawamtogole bule.
25 Viwalekile kuilumba wenyego, wasegela, Paulo viyamalile kulonga mbuli ino, “Loho Yang'alile kalonga goya kwa wahenga zenu kubitila mtula ndagu wa Mulungu Isaya!
26 Kalonga,
‘Genda ukawalongele wanhu wano,
kuhulika mohulika, lakini hondamujuwe bule,
kulola molola, lakini hondamone,
27 Kwavija mizoyo ya wanhu wano midala,
wasita magwiti gao,
wafing'hiliza meso gao.
Maza wadahile kulola kwa meso gao,
na kuhulika kwa magwiti gao,
na kujuwa kwa mizoyo yao,
wahanibwelele niye,
na niye nahawahonyile.’ ”
28 Paulo kamambukiza kulonga, “Avo mujuwe kamba usenga wa Mulungu kuwakombola wanhu, ugaligwa kwa wanhu haweli Wayahudi na wao wohulika.
29 Paulo viyamambukize kulonga avo, Wayahudi wachola mzikae zao kuno woibamilila.”
30 Kwa kipindi cha miyaka mibili Paulo kakala mng'anda iyapangile, mumo kawagoneka wanhu wose wezile kumulamusa.
31 Kawapetela wanhu mbuli za Undewa wa Mulungu na kuwafundiza mbuli za Mndewa Yesu Kilisito, kalonga kwa kugangamala na kubwihila.

# Baluwa ya Paulo kwa wanhu wa ako Lumi

## Ulongozi

Kitabu cha Walumi chogesigwa chandikigwa na mtumigwa Paulo hagati ya mwaka wa 54 na 58 toka kuvumbuka kwa Kilisito. Kipindi acho Paulo kakala hanatembelela Lumi avo kaigala baluwa ino kuwalagiza wanhu wamtogole Yesu ako Lumi, wose Wayahudi na wanhu haweli Wayahudi. Baluwa ino kayandikila kudibuga da Kolinto kuyakalile kipindi acho. Paulo kandika baluwa ino muladi wanhu wa isi zose wamtogole na kumtegeleza Yesu Kilisito (Sula ya 16:26).

Kitabu cha Walumi acho kitabu muhimu kwa wanhu wamtogole Yesu kila hanhu kila kipindi mbuli ya vija viyalongile Paulo, ukombozi ulinao kubitila Yesu Kilisito. Vivija Paulo kalumbiliza Mbuli Inogile ya Yesu Kilisito na lagano da umwaka. Wanhu wengi woifunza mbuli woibamilila kuwa mbuli ng'hulu mna ikitabu iyo ya sula ya 1:16 ilonga, “Siyonela kinyala bule Mbuli Inogile, kwavija ina udahi wa Mulungu wakumkombola munhu yoyose yotogola, tanhu kwa Wayahudi, abaho kwa wanhu haweli Wayahudi.” Mwambu wa ichanduso wa kitabu cha Lumi (Sula ya 1-12) ni mbuli za mgati ng'hani za Seoloji na mwambu uyagwe (Sula ya 13-15) una mafundizo mengi ga kusang'hana kwa ugima wa wanhu wamtogole Yesu.

**Mbuli zili mkitabu**

Miyanza mingi Paulo kosonga kwandika baluwa zake kwa kuitambula mwenyego na kolonga nani yandike (Sula ya 1:1-15).

Abaho kokwandika mbuli ya wanhu viweli na ukombozi viudahika kubitila Yesu Kilisito (Sula ya 1:16-11:36).

Abaho Paulo kolava mafundizo gayagwe mbuli vija wanhu wamtogole Yesu viwokala (Sula ya 12:1-15:13).

Komambukiza ikitabu kwa kulava ndamuso kwa wanhu wamtogole Yesu mna ikibumbila ako Lumi (Sula ya 16).

1 Niye Paulo, na mtumwa wa Yesu Kilisito na mtumigwa, nisaguligwe na ng'hemigwe na Mulungu niwapetele wanhu Mbuli yake Inogile.

2 Mbuli Inogile ilongigwe na Mulungu toka mwaka kubitila watula ndagu zake, kamba viyandikigwe mna Maandiko Gang'alile.

3 Mbuli ino Inogile yomulonga Mwana wa Mulungu, Mndewa wetu Yesu Kilisito. Heyo kawa munhu kwa kuvumbuka mulukolo lwa Daudi.

4 Kwa nzila ya Loho Yang'alile, kalagusigwa kwa udahi mkulu kuwa Mwana wa Mulungu kwa kuzilibuligwa kwa wafile nayo yuyo Yesu Kilisito Mndewa wetu.

5 Kubitila heyo na kwa mbuli ya twaga jake tubokela ng'hekewa na tuwa watumigwa, tuwalongoze wanhu wa isi zose wategeleze kwavija womtamanila.

6 Vivija mweye mwa mna iwanhu wasaguligwe kuwa wanhu wa Yesu Kilisito.

7 Avo nowandikila mweye mose mukala ako Lumi, mweye munogeligwe na Mulungu na kawasagula muwe wanhu zake wang'alile.

Ng'hekewa na tindiwalo kulawa kwa Mulungu Tataetu na Mndewa Yesu Kilisito vikale na mweye mose.

*Kumgwaa nhogolwa Mulungu*

8 Tanhu, nomgwaa nhogolwa Mulungu wangu kubitila Yesu Kilisito mbuli
ya mweye mose, kwavija kumtamanila kwenu Mulungu kuhulikigwa na
wanhu wose wa mwiisi.
9 Mulungu inimsang'hanila kwa moyo wangu wose, kwa kuwapetela
wanhu Mbuli Inogile ya Mwanage, ayo yolola kuwa nowakumbuka mweye,
10 miyanza mingi nahampula Mulungu. Nompula Mulungu yahalonda,
yatende idahike niwatembelele mweye sambi.
11 Nosulukila ng'hani niwone, muladi niwatende mumwede kiloho na
niwagangamize.
12 Niye ng'hala nifambula vino, wose mweye na niye tuigangamize,
tamanilo jangu kwa Mulungu dowagangamiza mweye na tamanilo jenu
kwa Mulungu donigangamiza niye.
13 Ndugu zangu nolonda mujuwe, miyanza mingi nilonda kuwatembelela,
lakini mhotigwa kutenda avo mbaka sambi. Nilonda kumwenu mweye
wanhu wamtogole Mulungu kamba vija viwatogole wanhu wayagwe haweli
Wayahudi.
14 Nina ng'honde ya kuwapetela wanhu wose, Wagiliki na haweli Wagiliki,
wabala na wabozi.
15 Lekaavo nosulukila ng'hani vivija niwapetele Mbuli Inogile mweye
mukala ako Lumi.

### *Udahi wa Mbuli Inogile*

16 Siyonela kinyala bule Mbuli Inogile, kwavija ina udahi wa Mulungu
wakumkombola munhu yoyose yotogola, tanhu kwa Wayahudi, abaho kwa
wanhu haweli Wayahudi.
17 Kwavija Mbuli Inogile yogubula vija Mulungu viyowatenda wanhu
wanoge mgameso gake. Mbuli ino yotendeka kwa kutamanila, kusongela
haichanduso mbaka kuuhelelo. Kamba Maandiko Gang'alile vigalonga,
“Munhu yatendigwe kanoga na Mulungu, kokuwa mgima kwa kumta-
manila.”

### *Kwiha kwa wanhu*

18 Mulungu kaigubula ng'hasiliki yake kulawa kuulanga mbuli ya gehile
gose na nzambi za wanhu, awo kwa gaja gehile gowosang'hana woukimila
ukweli sekeujuwike.
19 Avo gose gotenda Mulungu yajuwike kumwao gagubuligwa, kwavija
Mulungu mwenyego kawagubulila.
20 Toka Mulungu yaumbe isi, udahi wake wa mazuwa gose na vija viyali,
hamoja havoneka kwa meso, lakini vojuwika kwa kulola vinhu viyaumbile
Mulungu. Avo wanhu hawadaha bule kuigombela!
21 Wamjuwa Mulungu, lakini hawamgwaa ukulu, hebu kumgwaa
nhogolwa, magesa gao gamema ubozi, mizoyo yao imema ziza.
22 Wenyego woitapa wabala kumbe wabozi.
23 Woleka kumgwaa ukulu Mulungu yeli mgima siku zose, wovig-
waa ukulu vinyago, viigalile na wanhu wofa na ndege na wanyama na
wang'onyo wotambala.
24 Avo Mulungu kawaleka wasulukile gehile mmizoyo yao, na woitendela
vinhu vigela kinyala mzing'huli zao.
25 Wougalusa ukweli wa Mulungu kwa uvizi, wovitambikila na ku-
visang'hanila vija viyaumbile Mulungu na womuleka ija Yaumbile, heyo
yolondeka kutogoligwa siku zose. Ona!
26 Kwavija wotenda vino, Mulungu kawaleka wawinze mbuli zigela
kinyala mbaka watwanzi waleka kuwasa na wambigalo na woilonda wao
kwa wao.

27 Wambigalo vivija woleka kuwasa na watwanzi, woilonda wao kwa wao. Wambigalo kwa wambigalo woitendela mbuli zigela kinyala, avo waigalila wenyego nhaguso ilondeka kwa gaja gowosang'hana.

28 Kwavija wanhu awo walema kumjuwa Mulungu kwa nzewele zao, Mulungu nayo kawaleka wakweleleze nzewele zao zihile, nao wasang'hana mbuli zigomesigwe kusang'hanwa.

29 Wanhu wano wamema gose gehile, kwiha na umelo na wogevuza wayagwe. Wamema migongo na ukomaji na ndwagi na uvizi na magesa gehile. Wolonga wayao,

30 woivizila, womwihila Mulungu, wanhu weli na nyodo, wasede wanhu weli na magoda, wanhu wogesa nzila ziyagwe za kutenda gehile. Hawawategeleza tatazao na mamazao,

31 waduhu nzewele, hawatenda ziwalongile, hawawanogela wanhu na waduhu bazi kwa wanhu wayagwe.

32 Wajuwa malagizo ganogile ga Mulungu golonga wanhu wotenda mbuli azo wolondeka wafe. Hawahelele kutenda mbuli azo ziiyeka lakini vivija wowagwaa pala ukulu wanhu wotenda mbuli zizo.

# 2

*Nhaguso ya Mulungu*

1 Avo gweye mbwigangu, kamba kowatagusa wayagwe kuwa wabananga, hudaha ng'o kuigombela, hata wahawa nani. Kwavija wahawatagusa wayagwe kuno na gweye kotenda mbuli zizija ziwotenda wao, baho koitagusa mwenyego.

2 Tweye tojuwa kuwa nhaguso ya Mulungu kwa wanhu wotenda mbuli kamba azo ya kweli.

3 Lakini gweye mbwigangu uwatagusa waja wotenda mbuli kamba azo kuno gweye mwenyego kotenda vivo! Vino gweye kogesa kodaha kuhonyeka na nhaguso ya Mulungu?

4 Hebu kowehula uhole wake mkulu na viyoleka kulopola kuwatagusa wanhu na kufunga umoyo kwake. Hujuwa bule uhole wa Mulungu wokulongoza uleke nzambi na umbwelela Mulungu?

5 Lakini kuna moyo mdala na kolema kumbwelela Mulungu, avo koikila nhaguso ng'hulu mna isiku ija ya ng'hasiliki za Mulungu na nhaguso yake inogile vondaigubuligwe.

6 Kwavija Mulungu komulipa kila munhu kamba vija viyatendile.

7 Wanhu wayagwe wogendelela kutenda ganogile kuno wolonda ukulu kwa Mulungu na kutogoligwa na Mulungu na kuleka kufa. Wanhu awo Mulungu kowagwaa ugima wa mazuwa gose.

8 Wanhu wayagwe wana gahigahi na woulema ukweli, muladi wakweleleze gehile, wanhu awo Mulungu kowatagusa ng'hani kwa ng'hasiliki yake.

9 Madununzo na usungu gowapata wanhu wose wotenda gehile, tanhu kwa Wayahudi abaho kwa wanhu haweli Wayahudi.

10 Lakini Mulungu kowagwaa ukulu, kutogoligwa na tindiwalo wanhu wose wotenda ganogile, tanhu Wayahudi abaho wanhu haweli Wayahudi.

11 Kwavija Mulungu hambagula munhu yoyose.

12 Wanhu wotenda nzambi kuno waduhu Malagizo ga Musa, wopotela bila Malagizo. Wanhu wotenda nzambi kuno wagajuwa Malagizo ga Musa, wotagusigwa kwa Malagizo.

13 Kwavija siyo waja wogahulika Malagizo ga Musa, wao wanogile mgameso ga Mulungu, lakini waja wotenda vigalonda Malagizo, wao wonda watendigwe wanoge mgameso ga Mulungu.

14 Wanhu haweli Wayahudi waduhu Malagizo ga Musa, lakini wahagesa kusang'hana vigalonda Malagizo, wao wenyego wanago malagizo hata kamba waduhu Malagizo ga Musa.

15 Mbuli zao zootenda zolagusa kuwa zilagizigwe na Malagizo zandikigwa mmizoyo yao. Mizoyo yao yolagusa kuwa uno awo ukweli, kwavija magesa gao kipindi kiyagwe gowatagusa na kipindi kiyagwe gowagombela.

16 Gano golawilila mna isiku ayo Mulungu vonda yagataguse magesa ga kinyelegezi ga wanhu, kubitila Yesu Kilisito, kamba viilonga Mbuli Inogile iniwapetela.

### *Wayahudi na Malagizo ga Musa*

17 Kamba gweye koikema Muyahudi, kogatamanila Malagizo ga Musa na koigodela kuwa munhu wa Mulungu,

18 kamba gweye kujuwa viyolonda Mulungu utende kwavija Malagizo gakufunza kusagula ganogile,

19 kamba gweye kujuwa goya kuwa kwa mulongozaji wa wasuwameso, na kwa mulenge kwa wanhu weli mdiziza,

20 kamba gweye kwa mulangulizi wa wabozi na mfundiza wa wanhu hawanakangala, kamba gweye kogesa mna Gamalagizo kunayo nzewele yose na ukweli,

21 kowafundiza wayagwe, habali huifundiza mwenyego? Kowapetela wanhu sekewebe habali gweye mwenyego kokwiba?

22 Gweye kowalongela wanhu sekewatende ugoni, habali gweye kotenda ugoni? Kolonga vinyago havilondeka bule habali gweye mwenyego kokwiba vinhu vili mzing'anda za kutambikila vinyago?

23 Koigodela Malagizo ga Mulungu, vino gweye humgela kinyala Mulungu kwa kugabena Malagizo gake?

24 Maandiko Gang'alile golonga, “Mbuli ya gaja gomtenda mweye Wayahudi, wanhu wa isi ziyagwe wodiliga twaga da Mulungu.”

25 Mwahagagoga Malagizo, kwingila kumbi kwenu kofambula kinhu, lakini kamba hamugagoga Malagizo, kamba vija hamwingile kumbi bule.

26 Kamba munhu heli Muyahudi na hengile kumbi yahagagoga Malagizo, vino Mulungu hamgesa bule kamba munhu yengile kumbi?

27 Avo waja hawengile kumbi na kuno wogagoga Malagizo wowahonza mutagusigwe kuwa mubananga mweye Wayahudi mwingile kumbi na kugajuwa Malagizo, lakini mogabena.

28 Avo, siyo kila munhu yokoneka kwa kunze Muyahudi iyo Muyahudi wa kweli, na munhu hatendigwa Muyahudi wa kweli kwavija kengila kumbi mulukuli.

29 Lakini Muyahudi wa kweli ayo ija yeli Muyahudi kwa mgati, ayo ija moyo wake wingila kumbi. Ino ayo sang'hano ya Loho wa Mulungu na siyo Malagizo gandikigwe. Munhu yeli vino kobokela nhogolwa kwa Mulungu, na siyo kwa wanhu.

## 3

1 Vino Wayahudi wana choni chongezeke kuwabanza wanhu haweli Wayahudi? Hebu kwingila kumbi ni kinhu kikulu?

2 Ona, kuna vinhu vingi vikulu, Mulungu kawagwaa Wayahudi usenga wake.

3 Lakini yokuwaze kamba wanhu wayagwe hawatamaniligwa? Vino
Mulungu nayo hatamaniligwa bule?
4 Bule, Mulungu kolonga ukweli, hata kamba kila munhu koviza. Kamba
Maandiko Gang'alile vigalonga mbuli ya Mulungu,
“Wahalonga kolagusa ukweli,
wahatagusa gweye kohuma.”
5 Kamba gaja gehile gotusang'hana golagusa kamba Mulungu kotenda
goya, vino tulongeze? Tulonge Mulungu kobananga yahatutagusa? Hano
nolonga kiunhu unhu.
6 Bule, maza ikalile vivo, Mulungu yahadahile vilihi kuwatagusa wanhu
wose wa mwiisi?
7 Munhu kodaha kulonga, “Kamba uvizi wangu womsang'hanila Mulungu
na kumgwaa ukulu na wotenda ukweli wake woneke, habali notagusigwa
kamba nina nzambi?”
8 Lelo habali hatulonga, “Lekeni tutende nzambi ili ganogile geze?”
Wanhu wayagwe wandiga walonga niye nofundiza mbuli zizo! Wota-
gusigwa kamba viilondeka.

### *Kuduhu munhu yanogile mgameso ga Mulungu*

9 Sambi tulonge choni? Vino tweye Wayahudi tunoga kubanza wanhu
haweli Wayahudi? Bule, nimala kuwalongela kuwa Wayahudi na wanhu
haweli Wayahudi wose wotawaligwa na nzambi.
10 Kamba Maandiko Gang'alile vigalonga,
“Kuduhu hata munhu imoja yanogile mgameso ga Mulungu,
11 kuduhu munhu yeli na nzewele
hebu yomzahila Mulungu.
12 Wanhu wose wamuleka Mulungu,
wose wotenda gehile,
kuduhu munhu yotenda ganogile, kuduhu hata imoja.
13 Mitundu melo yao iigala na mapanga hagafukiligwe
milimi yao yolonga uvizi,
na mumilomo yao zolawa mbuli zili na sumu iigalile na sumu ya mgendela
hasi,
14 ulonzi wao umema kuduila kugela usungu.
15 Hawakawa kukoma.
16 Kokose kuwochola wohabananga na kuhananga.
17 Hawajuwile kukala kwa tindiwalo,
18 hawamdumba Mulungu.”
19 Sambi tojuwa kuwa Malagizo ga Mulungu gahalonga, golonga kwa
wanhu wose wolongozigwa na Malagizo, muladi wanhu sekewaigombele,
na wanhu wose wa mwiisi watagusigwe na Mulungu.
20 Kwavija kuduhu munhu yotendigwa kanoga mgameso ga Mulungu kwa
kutenda gaja golondigwa na Malagizo, ila Malagizo ga Mulungu gotutenda
tweye tujuwe totenda nzambi.

### *Mulungu viyowatenda wanhu wanoge mgameso gake*

21 Lakini sambi nzila ya Mulungu ya kuwatenda wanhu wanoge mgameso
gake igubuligwa. Haitendeka kwa Malagizo ga Musa, hamoja Malagizo ga
Musa na watula ndagu wa Mulungu wolonga mbuli ayo.
22 Mulungu kowatenda wanhu wanoge mgameso gake kubitila tamanilo
jao kwa Yesu Kilisito. Mulungu kotenda avo kwa wanhu wose womtogola
Kilisito, kwavija wose waigala.
23 Wanhu wose watenda nzambi na wahungukilwa na ukulu wa Mulungu.

24 Lakini kwa nhunza ya ng'hekewa ya Mulungu, wanhu wose wotendigwa wanoga na Mulungu kubitila Yesu Kilisito, yowalekesa.

25 Mulungu kamulava Yesu muladi kwa damu yake, yazigele kumgongo nzambi za wanhu kwa kumtamanila heyo. Katenda avo kulagusa viyotenda ganogile kwa wanhu, kwavija baho umwaka kafunga umoyo na hawataguse bule.

26 Katenda avo kulagusa viyanogile kwa wanhu mna ikipindi cha sambi na komtenda munhu yoyose yomtogola Yesu yanoge mgameso gake.

27 Lelo toigodela choni? Kuduhu! Choni kilamuso cha mbuli ino? Kwavija togagoga Malagizo ga Mulungu? Bule, lakini kwavija totogola.

28 Kwavija Mulungu komtenda munhu yanoge mgameso gake kwa kumtamanila kwiiyeka, na siyo kwa kutenda gaja golondigwa na Malagizo.

29 Vino Mulungu ni Mulungu wa Wayahudi waiyeka? Vino vivija heli Mulungu wa wanhu haweli Wayahudi? Ona, vivija Mulungu wa wanhu haweli Wayahudi.

30 Mulungu ni imoja, na kowatenda awo wengile kumbi wanoge mgameso gake kwa kumtamanila, vivija kowatenda awo hawengile kumbi wanoge mgameso gake kwa kumtamanila.

31 Vino ino yofambula kuwa wahamtamanila Mulungu kuduhu Malagizo? Bule, si vivo bule, togagoga Malagizo.

# 4

*Abulahamu kwa kumtamanila Mulungu katendigwa kanoga mgameso gake*

1 Vino tulonge choni mbuli ya Abulahamu, muhenga wetu, kaifunza choni?

2 Maza Abulahamu yatendigwe kanoga mgameso ga Mulungu mbuli ya zija ziyasang'hane, yahawile na kinhu cha kuigodela, lakini siyo mgameso ga Mulungu.

3 Maandiko Gang'alile golonga, "Abulahamu kamtamanila Mulungu, na mbuli ya kumtamanila kwake, Mulungu kamgesa kanoga."

4 Munhu yahasang'hana halipigwa kamba nhunza, lakini kolipigwa kamba fungu jake.

5 Lakini munhu yoleka kutamanila sang'hano zake mwenyego, ila komtamanila Mulungu yozigela kumgongo nzambi za wanhu, avo Mulungu kodigesa tamanilo da munhu ayo na komtenda yanoge mgameso gake.

6 Nayo Daudi kalonga mbuli iino, viyalongile mbuli ya kumweda kwa munhu yagesigwe na Mulungu kanoga, bila kulola gaja gayasang'hane.

7 "Wamweda wanhu waja nzambi zao zigeligwa kumgongo
na gaja gawatendile hagatongigwa!
8 Kamweda munhu ija nzambi zake Mndewa honda yazigese!"

9 Vino kumweda kuno kuyalongile Daudi ni kwa wanhu waja wengile kumbi waiyeka? Bule! Vivija kwa wanhu hawengile kumbi. Kamba vinisongile kulonga, "Abulahamu kamtamanila Mulungu, na kwa kumtamanila kwake, Mulungu kamgesa kanoga."

10 Vino Abulahamu kagesigwa kipindi gani? Yang'hali hana kwingila kumbi hebu viyengile kumbi? Yang'hali hanakwingila kumbi na siyo viyengile kumbi.

11 Abulahamu kengila kumbi kumwande, kwingila kumbi kwake kukala kilaguso kilaguse kuwa Mulungu kamgesa kanoga mbuli ya kumtamanila kwake yang'hali hanakwingila kumbi. Avo Abulahamu yuyo tata wa wanhu

wose womtamanila Mulungu hata kamba hawengile kumbi na wanhu awo wogesigwa na Mulungu wanoga.

12 Vivija Abulahamu iyo tata wa wanhu wose wengile kumbi, lakini siyo kwavija wengila kumbi kwiiyeka, ila kwavija wokweleleza nzila iija ya kumtamanila Mulungu iyaikweleleze tataetu Abulahamu yang'hali hanakwingila kumbi.

### *Kwa kumtamanila Mulungu tokipata kiyalongile*

13 Mulungu kamulongela Abulahamu na lukolo lwake kuwa isi yose yokuwa yao, siyo kwavija Abulahamu kagagoga Malagizo, lakini kwavija kamtamanila Mulungu, nayo Mulungu kamtenda kanoga mgameso gake.

14 Kwavija kamba kija kiyalongile Mulungu wogweleligwa waja wogagoga Malagizo waiyeka, baho tamanilo jao kwa Mulungu daduhu kinhu na vivija kija kiyalongile Mulungu siyo kinhu.

15 Malagizo gogala ng'hasiliki za Mulungu, lakini kamba kuduhu Malagizo, kuduhu kubena Malagizo.

16 Avo kija kiyalongile Mulungu kiza kwa kutamanila, muladi kubitila ng'hekewa ya Mulungu kwa vovose wagweleligwe nhunza wanhu wa lukolo lose lwa Abulahamu, siyo kwa waja wogagoga Malagizo waiyeka, lakini vivija kwa waja womtamanila Mulungu kamba viyatendile Abulahamu, yeli tata wa tweye wose.

17 Kamba Maandiko Gang'alile vigalonga, “Nikusagula uwe tata wa isi nyingi.” Avo mbuli azo za kweli mgameso ga Mulungu, iyamtamanile Abulahamu, Mulungu yowazilibula wanhu wafile, na kwa lagizo jake vinhu havikalile baho, vabaho.

18 Abulahamu katogola na katamanila, hamoja kukala kuduhu kinhu cha kutamanila, na avo kawa tata wa isi nyingi. Kamba Maandiko Gang'alile vigalonga, “Wanhu wa lukolo lwako wokuwa wengi.”

19 Abulahamu kakala na miyaka gana dimoja, lakini tamanilo jake kwa Mulungu hadihunguke hamoja kajuwa kakala yalalile ng'hani, na mwehe wake Sala sambo ikala imalile.

20 Abulahamu halekile kutamanila kiyalongile Mulungu, lakini tamanilo jake kwa Mulungu dimgangamiza na kamgwaa ukulu Mulungu.

21 Kajuwa goya kuwa Mulungu kodaha kutenda kija kiyamulongele.

22 Lekaavo Abulahamu kwa kumtamanila Mulungu, “Kagesigwa na Mulungu kanoga.”

23 Ulonzi wa, “kagesigwa na Mulungu kanoga” hawandikigwe kumwake yaiyeka,

24 vivija wandikigwa kumwetu kuwa togesigwa na Mulungu tunoga kwa kumtogola Mulungu yamzilibule Mndewa wetu Yesu, kwa wafile.

25 Heyo kalavigwa yafe kwa nzambi zetu, abaho kazilibuka ili Mulungu yatutende tunoge mgameso gake.

# 5

### *Tindiwalo na deng'ho*

1 Sambi kwavija tutendigwa tunoga mgameso ga Mulungu kwa kumtamanila, tuna tindiwalo na Mulungu kubitila Mndewa wetu Yesu Kilisito.

2 Kwa kumtamanila heyo, Yesu katugalila ng'hekewa ya Mulungu, itukala nayo sambi, avo tobetela kwa kudeng'helela kwingila muukulu wa Mulungu.

3 Siyo gago gaiyeka, lakini vivija toigodela gamagayo getu, kwavija tojuwa kuwa magayo gogala kufunga umoyo,

4 kufunga umoyo kogala kugangamala, na kugangamala kogala tamanilo.
5 Tamanilo dino haditugela kinyala, kwavija Mulungu keka unogelwa
wake mmizoyo yetu kubitila Loho Yang'alile, iyatugwelele tweye.
6 Vitukalile hatudaha kuihonya wenyego, kipindi kinogile vikivikile, Kil-
isito kafa mbuli ya tweye tutenda gehile.
7 Vidala ng'hani kwa munhu kufa mbuli ya munhu yanogile mgameso ga
Mulungu. Sengine munhu kodaha kugeza kufa mbuli ya munhu yanogile
ng'hani.
8 Lakini Mulungu katulagusila vija viyotunogela kwavija vitukalile
tung'hali totenda nzambi Kilisito kafa mbuli yetu tweye!
9 Kwavija sambi Mulungu katutenda tunoge mgameso gake kwa damu ya
Kilisito, kweli kotukombola na ng'hasiliki za Mulungu.
10 Vitukalile tuihila na Mulungu, tuilumba nayo kubitila ifa ya mwanage.
Sambi tuilumba na Mulungu, yokuwa vinoga ng'hani na kweli tokom-
boligwa kwa ugima wa Kilisito.
11 Lakini siyo gago gaiyeka, vivija wose todeng'helela mbuli ya gaja gaya-
tendile Mulungu kubitila Mndewa wetu Yesu Kilisito, yatutendile tuilumbe
na Mulungu.

*Adamu na Kilisito*

12 Nzambi ingila mwiisi kubitila munhu imoja, na nzambi yake igala ifa.
Avo, ifa yenela kwa wanhu wose kwavija wanhu wose watenda nzambi.
13 Malagizo ga Musa gang'hali haganagaligwa nzambi zikala mumuno
mwiisi. Lakini hanhu kuduhu Malagizo, nzambi hazigesigwe.
14 Lakini kulawa mna ikipindi cha Adamu mbaka mna ikipindi cha Musa,
ifa iwatawala wanhu wose, hata kwa waja hawatendile nzambi kamba
ziyatendile Adamu yalekile kugoga gaja gayamulagize Mulungu.
isito yawe nzewele yetu. Kubitila heyo totendigwa tunoga mgameso ga
Mulungu, na twa wanhu wa Mulungu na tokomboligwa.
31 Avo Maandiko Gang'alile golonga, "Munhu yoyose yolonda kuigoda,
yaigodele kija kiyasang'hane Mndewa."

# 2

*Usenga wa Kilisito yawambigwe mumsalaba*

1 Ndugu zangu, niye vinizile kumwenu sizile kuwapetela usenga wa
Mulungu, ufisigwe kwa ulonzi mdala hebu kwa ubala wa wanhu.
2 Kwavija vinikalile na mweye, silondile kugesa kinhu chochose lakini
Yesu Kilisito na ifa yake mumsalaba.
3 Avo vinizile kumwenu, ng'hala bule nguvu na nikala nodumba na
kugwaya.
4 Mafundizo gangu na usenga wangu havilavigwe kwa mbuli zamulile
kulawa kuna zinzewele za munhu, lakini kwa nguvu ya Loho wa Mulungu.
5 Nitenda vivo, muladi kutamanila kumwenu sekekukale mna zinzewele
za wanhu ila mna inguvu ya Mulungu.

*Nzewele ya Mulungu*

6 Avo, nowapetela usenga uli na nzewele kwa wanhu waja tamanilo jao
dikangale. Lakini siyo nzewele za mwiisi ino hebu nguvu ya wakulu wa
mwiisi ino, awo wonda wabanangigwe.
7 Nowapetela nzewele ifisigwe ya Mulungu, yaisagule mbuli ya ukulu
wetu isi ing'hali hainaumbigwa.
8 Kuduhu mndewa wa kipindi kino yaijuwile nzewele ino. Maza wai-
juwile, sambi wamuwambe mumsalaba Mndewa wa ukulu.
9 Lakini Maandiko golonga,
"Mbuli zija hazinakoneka na munhu hebu kuhulikigwa,
mbuli hazinagesigwa mmizoyo ya wanhu,
mbuli azo Mulungu kawekila wanhu womnogela."
10 Lakini Mulungu katugubulila mbuli azo kubitila Loho wake. Kwavija
Loho Yang'alile kozahila kila kinhu, hata mbuli za Mulungu ziifisile ng'hani.
11 Kuduhu munhu yojuwa viyogesa munhu iyagwe, ila loho yake munhu
ayo. Vivo ili kuduhu yajuwile mbuli za Mulungu ila Loho wa Mulungu
yaiyeka.
12 Hatubokele bule loho wa wanhu wa isi ino, lakini tubokela Loho yatu-
migwe na Mulungu, muladi tudahe kugajuwa gaja gose tugweleligwe na
Mulungu.
13 Avo hatulonga mbuli zifundizigwe na nzewele za wanhu, lakini kwa
mbuli zifundizigwe na Loho Yang'alile, vituwafambulila mbuli za loho waja
weli na Loho Yang'alile.
14 Munhu yoyose yeliduhu Loho Yang'alile hadaha kubokela vinhu kulawa
kwa Loho wa Mulungu. Wanhu wano hawazijuwa mbuli azo, kumwao
zokoneka ubozi, kwavija mbuli azo zodahika kufambuligwa kwa kutazigwa
na Loho Yang'alile yaiyeka.
15 Munhu yoyose yeli na Loho wa Mulungu, kodaha kujuwa kila kinhu
kinogile, lakini kuduhu yodaha kumtagusa.
16 Maandiko golonga,
"Nani yajuwile viyogesa Mndewa?

Nani yodaha kumgwaa magesa?”
Lakini tweye togesa viyogesa Kilisito.

# 3

*Wasang'hanaji wa Mulungu*

1 Ndugu zangu, kulonga ukweli, sidahile kulonga na mweye kamba vinilonga na wanhu weli na Loho wa Mulungu. Nilonda kulonga na mweye kamba wanhu wa mwiisi ino, kamba wana ving'hele waja tamanilo jao kwa Kilisito hadinakangala.

2 Nilondeka kuwagwaa maziwa mung'we, lakini si lujo mdala, kwavija hamudahile kukija. Hata sambi hamudaha bule kukija,

3 kwavija mweye mung'hali mokala kamba viwokala wanhu wa mwiisi ino. Avo moiyonela migongo na kugomba wenyego, vino, ino hailagusa kuwa mweye mung'hali wanhu wa mwiisi ino na mokala kamba viwokala wanhu wa isi ino?

4 Imoja wenu kolonga, “Niye nomkweleleza Paulo,” na iyagwe kolonga, “Niye nomkweleleza Apolo,” Vino, hamutenda kamba wanhu wa mwiisi viwotenda?

5 Vino, Apolo ayo nani? Na Paulo ayo nani? Tweye twa wasang'hanaji wa Mulungu, tuwatenda mweye mutogole. Kila imoja wetu kotenda sang'hano iyagweleligwe na Mndewa.

6 Niye nihanda mbeyu, Apolo kagelela mazi, lakini Mulungu heyo yaitendile ikule.

7 Kwavija yahandile na ija yaigelele mazi waduhu chochose, lakini Mulungu heyo yaitendile ikule.

8 Munhu yahandile na munhu yaigelele mazi wose wa kinhu kimoja, Mulungu komgweka kila imoja kwa sang'hano yake yaitendile.

9 Kwavija wose tosang'hana hamoja na Mulungu, mweye muwa kamba mgunda wa Mulungu.

Vivija mwa ng'anda ya Mulungu.

10 Kwa ng'hekewa iyangwelele Mulungu, nhenda sang'hano ya mzengaji yanogile, nika chandusilo chake na munhu iyagwe kozenga uchanha yake. Lakini kila munhu yozenga kolondeka yatiganye viyozenga.

11 Kuduhu munhu iyagwe iyodaha kwika chandusilo, kwavija Mulungu kamwika Yesu Kilisito yaiyeka yawe chandusilo.

12 Uchanha mwa chandusilo acho wanhu wozenga kwa zahabu hebu shaba hebu mabwe ganogile ng'hani, na wayagwe wozenga kwa mibiki, majani hebu usoti.

13 Ukunoga kwa sang'hano ya munhu hokoneka mna isiku ija Kilisito vondayaifisule. Kwavija mna isiku ayo moto wogubula sang'hano ya kila munhu, moto wozigeza sang'hano zao kulagusa kamba zinoga.

14 Kamba kija kizengigwe uchanha mwa ichandusilo chokala bila kulukula moto, mzengaji kobokela nhunza.

15 Lakini kamba sang'hano ya munhu yolukula, mzengaji koyagiza, lakini heyo mwenyego kokomboligwa, kamba munhu yahonyeke kulawa kuna umoto.

16 Mweye mujuwa kuwa mwa ng'anda ya Mulungu na Loho wa Mulungu kokala mgati mmwenu!

17 Avo, munhu yoyose yoibananga ng'anda ya Mulungu, Mulungu nayo kombananga munhu ayo. Kwavija ng'anda ya Mulungu ing'ala, na mweye wenyego mwa ng'anda ya Mulungu.

18 Sekemwiivizile! Munhu yoyose kumwenu yogesa kana nzewele za mwiisi ino, muleke yawe mbozi, muladi yawe na nzewele.

19 Kwavija nzewele za wanhu wa mwiisi ino ni ubozi mgameso ga Mulungu. Kamba Maandiko Gang'alile vigolonga, “Mulungu kowanamata weli na nzewele muubala wao,”

20 na vivija Maandiko golonga, “Mndewa kojuwa viwogesa wanhu weli na nzewele siyo chochose.”

21 Avo, sekemuigodele wanhu, kwavija vinhu vose venu.

22 Paulo na Apolo na Kefa na isi ino na ugima na ifa na mbuli za sambi na za kumwande, gose gano genu.

23 Na mweye mwa wanhu wa Kilisito, nayo Kilisito wa Mulungu.

# 4

### *Watumigwa wa Kilisito*

1 Mtugese tweye kamba wasang'hanaji wa Kilisito, tugweleligwe udahi wa kuwafambulila wanhu mbuli zifisigwe za Mulungu.

2 Kinhu kilondeka kwa wanhu wose wagweleligwe sang'hano ni kutenda kamba viyolonda mkulu wao.

3 Niye sitonga bule nahatagusigwa na mweye, hebu munhu yoyose mwiisi, na wala sidaha kuitagusa mwenyego.

4 Muumoyo wangu kuduhu kinhu kinitagusa niye, lakini mbuli ino hailagusa kuwa sibanange. Mndewa ayo wa kunitagusa niye.

5 Avo sekemumtaguse munhu yoyose king'hali kipindi hakinavika. Lekeni mbaka Mndewa vondayeze, nayo kokwiza kugamwemwesela gaja gafisigwe mdiziza na kugafisula gaja gose geli mmizoyo ya wanhu. Aho kila munhu kobokela nhogolwa yake kulawa kwa Mulungu.

6 Ndugu zangu, mbuli ya mweye, niye nimtenda Apolo na niye tuwe kinhu cha mweye kuifunza, avo mudahe kujuwa fambulo da ulonzi uno, “Mukweleleze vija vandikigwe.” Muladi muleke kuigodela imoja na kumwehula iyagwe.

7 Sekeugese gweye kunoga kubanza wayagwe? Vino siyo Mulungu yakugwelele kila kinhu kiulinacho? Avo lelo koigodela choni, kamba vija vinhu viulinavo hugweleligwe bule?

8 Vino, mupata vose vimulonda? Mweye mwa matajili tiyali? Mweye mwa wandewa bila tweye? Ona, kamba mweye kweli mwahakuwile wandewa, avo na tweye twahadahile kuwa wandewa hamoja na mweye.

9 Kwavija vinikona niye, Mulungu katutenda tweye watumigwa tuwe wanhu wa kimambukizo, kamba wanhu watagusigwe kukomigwa mgameso ga wanhu, tuwe kilozo mwiisi yose haulongozi ha wasenga wa kuulanga na wanhu.

10 Tweye twawabozi mbuli ya Kilisito, lakini mweye mwawabala kwa kuilumba na Kilisito! Tweye tunyolila, lakini mweye mugangamala! Mweye motegelezigwa lakini tweye tokwehuligwa!

11 Mbaka sambi tweye tuna nzala na ng'hilu, tovala vikumbi, totowigwa, twaduhu hanhu ha kuwasa,

12 vivija todununzika na kusang'hana kwa makono getu wenyego. Twahaduiligwa, towapulila kwa Mulungu vinhu vinogile, na twahadununzigwa tofunga umoyo,

13 twahaligigwa, tokwidika vinogile. Tokoneka kamba wanhu wafitile mwiisi, mbaka sambi tweye twa dikwe da mwiisi!

14 Sandika mbuli zino niwagele kinyala, lakini kuwazuma mweye kamba wanangu niwanogela.

15 Avo hata kamba mwahawa na walangulizi elufu kumi muugima wenu kwa Kilisito, mweye mduhu tata wengi, kwavija kwa kuilumba na Yesu Kilisito, niye na tataenu kwa kuwagalila Mbuli Inogile.

16 Avo, nowapula, loleni vinhendile munikweleleze.

17 Lekaavo nimtuma Timoseo kumwenu, mwanangu nimnogela yosang'hana kwa kumtamanila Mndewa. Nayo kowakumbusa nzila inikweleleza niye kwa kuilumba na Yesu Kilisito, nzila ija inifundiza kila hanhu mna ivibumbila va wanhu wamtogole Yesu.

18 Wanhu wayagwe vimwili wasonga kuigoda, kwavija wogesa niye siza kumwenu kabili.

19 Lakini Mndewa yahalonda, nolopola kwiza kumwenu, aho nolola mwenyego kija kiwolonga awo woigoda na nguvu iwelinayo.

20 Kwavija Undewa wa Mulungu hauli muulonzi lakini kuna inguvu.

21 Mweye munogelwa na choni? Nize kumwenu na mbalati, hebu kwa unogelwa na uhole?

# 5

*Ugoni mna ivibumbila va wanhu wamtogole Yesu*

1 Avo lelo, kuna mbuli zilongigwa kamba kumwenu mweye kuna wanhu wotenda ugoni, na vivija uchafu hauna koneka hata kwa wamhazi. Nilongeligwa munhu kowasa na mamake wa kuvikila!

2 Modahaze kuigoda? Maza mulondeka munyunyuwale, na munhu yatendile kilozo acho kolondeka yawingigwe kumwenu.

3 Hata kamba na kutali na mweye, lakini muumoyo wangu na hamoja na mweye, nimtagusa mwaka munhu yatendile kinhu acho kamba vija nabaho na mweye.

4 Mwahaiting'hana hamoja kwa twaga da Mndewa Yesu na niye na hamoja na mweye muumoyo wangu, na nguvu ya Mndewa wetu Yesu ya hamoja na mweye,

5 mgweleleni Mwenembago munhu ayo, muladi lukuli lwake lubanangigwe, avo loho yake idahe kukomboligwa mna isiku ya Mndewa.

6 Kuigoda kumwenu hakunogile bule! Vino hamujuwile kuwa, mela kidogo youtenda usage wose ugongomoke?

7 Avo isunheni, mulave mela da umwaka da nzambi muladi muwe bonge da sambi dililuhu mela, kamba vimulondeka kuwa. Kwavija Yesu Kilisito ayo mwana ng'hondolo wa Pasaka yetu, kalavigwa nhosa.

8 Lelo tudeng'helele Pasaka yetu, siyo kwa gate dili na mela da umwaka dili na nzambi na ubananzi, lakini kwa gate hadigeligwe mela, gate dinogile na ukweli.

9 Nimwandikileni mna ibaluwa yangu iyagwe, mwiinege na wanhu weli wagoni.

10 Silonga mwiinege na wanhu hawamtogola Mulungu weli wagoni hebu wagila hebu wabavi hebu waja wotambikila vinyago. Kwavija mwahalonda kuinega nao wose, molondeka kulawanya mwiisi ino.

11 Fambulo da mbuli zinyandike ijo dino, mwiinege na munhu yoyose yoikema Mkilisito kuno kotenda ugoni hebu mgila hebu kovitambikila vinyago hebu muligaji hebu kokoligwa hebu mbavi. Hata kuja sekemuje nayo munhu ayo.

12 Lekaavo, silondeka kuwatagusa wanhu weli kunze ya vibumbila va wanhu wamtogole Yesu. Vino mweye hamulondeka kuwatagusa wanhu weli mna ivibumbila venu?
13 Mulungu kowatagusa wanhu weli kunze ya vibumbila va wanhu wamtogole Yesu. Mweye muwingeni munhu yehile mkibumbila chenu.

# 6

### *Kitala cha Wakilisito*

1 Vino, kamba imoja wenu kana kitala na Mkilisito miyage, yokuwaze komgala mkitala cha wanhu hawamtogole Yesu, koleka kumgala kwa wanhu wa Mulungu?
2 Vino, hamujuwile bule wanhu wa Mulungu wokwiza kuwatagusa wanhu wa mwiisi? Kamba wanhu wa mwiisi wotagusigwa na mweye, vino molemelwa kutagusa mbuli ndoo ndodo?
3 Vino, mweye hamujuwile tokwiza kuwatagusa wasenga wa kuulanga? Todaha ng'hani kutagusa vinhu va ugima uno!
4 Kamba mwahagomba, vino mowakema wanhu hawategelezigwa mkibumbila chenu cha wanhu wamtogole Yesu wawe wasemi?
5 Mogela kinyala! Vino kuduhu hata munhu imoja kumwenu yeli na nzewele yodaha kuwazuma Wakilisito wagombile?
6 Lakini Mkilisito komgala Mkilisito miyage mkitala, kwa wasemi hawamtogole Yesu!
7 Kulonga ukweli, kuigala kwenu mkitala mweye kwa mweye kolagusa kuwa muhumigwa. Vinoga mweye koneligwa. Vinoga mweye kuviziligwa na kubokigwa vinhu venu.
8 Lakini mweye wao muwonela na kuwaboka ndugu zenu vinhu vao kwa uvizi!
9 Vino, hamujuwile kuwa wanhu wotenda gehile honda waupate Undewa wa Mulungu? Sekemwiivizile, wanhu wokala kwa ugima wa ugoni ubanzile hebu wovitambikila vinyago hebu wotenda ugoni hebu wambigalo wohindusa wayao,
10 hebu wabavi hebu wagila hebu wokoligwa hebu kuwaliga wayao hebu wabokaji, wao wose kuduhu yonda yaupate Undewa wa Mulungu.
11 Wanhu wayagwe kumwenu mukala vivo. Lakini sambi nzambi zenu zisegezigwa, mulavigwa kwa Mulungu, mutendigwa munoga mgameso ga Mulungu kwa twaga da Mndewa Yesu Kilisito na Loho wa Mulungu wetu.

### *Sang'hanileni ng'huli zenu kwa ukulu wa Mulungu*

12 Munhu kodaha kulonga, “Vinhu vose nodaha kutenda.” Lakini siyo vinhu vose vinoga kumwangu. Notogola nodaha kutenda kinhu chochose, lakini sitogola kinhu chochose kinhende niwe mtumwa wake.
13 Munhu iyagwe kolonga, “Lujo kwa mbuli ya inda, na inda kwa mbuli ya lujo.” Ona, lakini Mulungu kovibananga vose vibili. Lukuli lwa munhu siyo kwa mbuli ya ugoni, lakini kwa mbuli ya kumsang'hanila Mndewa, nayo mndewa ayo yowika goya lukuli.
14 Mulungu kamzilibula Mndewa Yesu kwa wanhu wafile, na tweye vivija kotuzilibula kwa nguvu zake.
15 Vino, hamujuwile kuwa ng'huli zenu ni maungo ga lukuli lwa Kilisito? Hebu mogesa nodaha kusola maungo ga lukuli lwa Kilisito na kugatenda gawe maungo ga ulukuli lwa munhu yosulukila ugoni? Aka!
16 Hebu hamujuwile bule munhu yonda yailumbe na munhu yosulukila ugoni kokuwa lukuli lumoja na munhu ayo? Kwavija yandikigwa mna Gamaandiko Gang'alile, “Weli wabili wokuwa lukuli lumoja.”

17 Lakini munhu ija yoilumba na Mndewa kahamoja nayo kiloho.
18 Avo muinege ng'hani na ugoni. Kwavija nzambi ziyagwe zitendigwa
na munhu haziubananga lukuli, lakini munhu yotenda ugoni kolutendela
nzambi lukuli lwake mwenyego.
19 Vino, hamujuwile bule ng'huli zenu ayo ng'anda ya Loho Yang'alile, yeli
mgati mmwenu imugweleligwe na Mulungu? Avo lelo, mweye siyo kinhu
chenu wenyego, lakini cha Mulungu,
20 kwavija muguligwa kwa bei ng'hulu. Avo zisang'hanileni ng'huli zenu
kwa ukulu wa Mulungu.

# 7

*Mbuli ya kusola na kusoligwa*

1 Lelo, kwa mbuli zija zimnyandikile,
"Mbigalo kotenda goya yahaleka kusola mtwanzi."
2 Lakini kwavija kuna ugoni, kila mbigalo yawe na mwehe wake
mwenyego, na kila mtwanzi yawe na mkasano wake mwenyego.
3 Mbigalo yatende vija viyolondeka kwa mwehe wake na vivija mtwanzi
yatende vija viyolondeka kwa mkasano wake.
4 Mwehe kaduhu udahi na lukuli lwake, lakini mkasano wake kanao. Vivo
ili kwa mkasano kaduhu udahi na lukuli lwake, lakini mwehe wake kanao.
5 Sekemuleke kuwasa hamoja lakini vonda muitogolele wenyego kutenda
vivo muladi mupate kipindi kinogile cha kumpula Mulungu. Abaho ib-
weleleni kabili, muladi Mwenembago sekeyawageze kwavija hamudaha
kuitawala wenyego.
6 Siwalongela vino kwa kuwalagiza, lakini vinigesa niye.
7 Maza vinonda niye wanhu wose wakale kamba vinili niye, lakini kila
munhu kana nhunza yake kulawa kwa Mulungu. Imoja kana nhunza ino,
na iyagwe kana nhunza ija.
8 Lelo, kwa waja hawanasola na weli wagane, vinoga kumwenu kukala
usaka kamba vinili niye.
9 Lakini mwahalemelwa kukala usaka, soleni, kwavija vinoga kusola
kubanza kusulukila watwanzi.
10 Kwa waja wasolile na kusoligwa nowagwaa lagizo, sijangu lakini da
Mndewa, mwehe sekeyaileke na mkasano wake,
11 lakini kamba yahatenda vivo, yakale usaka hebu wailumbe kabili na
mkasano wake. Nayo mkasano sekeyamwase mwehe wake.
12 Kwa wanhu wayagwe nolonga niye, lakini siyo Mndewa, kamba mbi-
galo Mkilisito kana mwehe yolema kumtogola Yesu na imwehe kotogola
kukala nayo, sekeyamwase.
13 Na kamba mtwanzi Mkilisito kasoligwa na mbigalo hamtogola Yesu na
kotogola kukala nayo, sekeyamuleme.
14 Kwavija mkasano hamtogola Yesu kotogoligwa na Mulungu kwa
kuilumba na mwehe wake, na mwehe hamtogola Yesu kotogoligwa na
Mulungu kwa kuilumba na mkasano wake. Maza haili vivo, wana wao
sambi watogoligwe na Mulungu, lakini Mulungu kawatogola.
15 Lakini kamba ija hamtogola Yesu kolonda kumuleka miyage yeli Mk-
ilisito na yamuleke. Kwa kilamuso acho, ayo imkilisito, mbigalo hebu
mtwanzi, hagomigwa kutenda vivo. Kwavija Mulungu kawakema mukale
moyo uholile.
16 Gweye mwehe Mkilisito, kojuwa vilihi kuwa hudaha kumkombola
mkasano wako? Hebu gweye mkasano Mkilisito, kojuwa vilihi kuwa hu-
daha kumkombola mwehe wako?

### *Ukale kamba Mulungu viyakukemile*

17 Avo kila munhu na yakale kamba vija Mndewa viyamtendile yawe, na vivija ukale kamba viukalile Mulungu viyakukemile. Dino dijo lagizo jangu kwa vibumbila vose va wanhu wamtogole Yesu.

18 Kamba munhu yengile kumbi kakemigwa na Mulungu, sekeyaivizile kuwa hanakwingila kumbi. Na kamba viyakemigwe kakala hanakwingila kumbi, sekeyengile kumbi.

19 Kwavija kwingila kumbi hebu kuleka kwingila kumbi siyo kinhu, kilondeka ni kugagoga malagizo ga Mulungu.

20 Avo kila munhu yakale kamba viyakalile kipindi viyakemigwe na Mulungu.

21 Vino, gweye viukemigwe na Mulungu kukala mtumwa? Sekeugelegeze, lakini wahapata kipindi cha kulekesigwa, kisang'hanile.

22 Kwavija mtumwa yakemigwe na Mndewa kokuwa munhu yalekesigwe kwa Mndewa. Vivo ili kwa munhu yalekesigwe yakemigwe na Mndewa kokuwa mtumwa wa Kilisito.

23 Mulungu kawagula kwa bei ng'hulu, avo sekemuwe watumwa wa wanhu.

24 Ndugu zangu, kila munhu na yakale kwa kuilumba na Mulungu kamba vija viyakalile kipindi Mulungu viyamkemile.

### *Mbuli ya wanhu wasaka na wagane*

25 Kwa gaja gamtwandikile mbuli ya wanhu wasaka, nabule lagizo kulawa kwa Mndewa, lakini nolonga vinigesa kamba munhu nitamaniligwa mbuli ya koneligwa bazi na Mndewa.

26 Lakini mbuli ya kugaya kuli sambi, vinikona niye yokuwa vinoga kwa munhu kukala kamba viyali.

27 Vino gweye kuna mwehe? Avo sekeumwase. Vino gweye hunasola? Avo sekeulonde kusola.

28 Lakini wahasola, hutendile nzambi. Na mndele yahasoligwa hatendile nzambi. Lakini wao waisolile wogazika ng'hani mwiisi ino, na niye silonda mweye muwe kamba wao.

29 Ndugu zangu, nolonga vino, kipindi kisigale kidodo. Avo kulawa sambi wanhu weli na wehe wakale kamba wasaka,

30 na waja wolila wakale kamba hawalila na waja wodeng'helela wakale kamba hawadeng'helela na wagulaji wakale kamba hawagulile kinhu,

31 na waja wosang'hanila vinhu va mwiisi ino wakale kamba waduhu sang'hano navo. Kwavija isi ino kamba viili sambi, hondaikale ng'hani.

32 Nolonda mweye sekemunyawenyawe. Munhu msaka kohunganikila mbuli za Mndewa, kwavija kolonda kumnogeza Mndewa.

33 Lakini mbigalo mwene mwehe kohunganikila mbuli za mwiisi, kwavija kolonda kumnogeza mwehe wake,

34 nayo kokwegigwa mhande mbili. Mtwanzi yeliduhu mkasano hebu mhambe kohunganikila sang'hano za Mndewa, kwavija kolonda kung'ala kwa lukuli na loho, lakini mtwanzi yeli na mkasano kohunganikila mbuli za mwiisi, kwavija kolonda kumnogeza mkasano wake.

35 Nolonga vino kwavija nolonda kuwataza mweye. Siwagoma bule, lakini nolonda mweye mutende gaja ganogile muladi mupate kumsang'hanila Mndewa kwa moyo umoja.

36 Kamba munhu yoyose kogesa hamtendela vinogile mhambe yoolonda kufunga nayo zengele. Na kamba mhambe ayo kokuwa na miyaka mingi kwa kusoligwa na komsulukila ng'hani na yatende kamba viyolonda. Yafunge nayo zengele, aho hatenda nzambi.

37 Lakini kamba mbigalo kolonda mwenyego muumoyo wake kuleka kusola, na kodaha kuleka kusulukila na kutenda viyolonda, aho kotenda goya ng'hani yahaleka kumsola mhambe ayo.

38 Avo munhu yosola mtwanzi kotenda vinogile, lakini munhu yoleka kusola kotenda vinogile ng'hani.

39 Mtwanzi yasoligwe kokuwa kafungigwa na mkasano wake kipindi chose cha ugima wake, lakini mkasano wake yahafa, kodaha kusoligwa na mbigalo yoyose yoomulonda lakini kolondeka yawe Mkilisito.

40 Lakini vinikona niye, mtwanzi ayo komweda ng'hani yahakala usaka. Avo vinigesa niye, vivija ninayo Loho wa Mulungu.

# 8

### *Mbuli ya Lujo lulavigwe nhosa kwa vinyago*

1 Sambi, kwa mbuli ya lujo lulavigwe nhosa kwa vinyago.

Tojuwa, wose tuna ubala, na ubala awo womtenda munhu yaigode, lakini unogelwa wozenga.

2 Waja wogesa wojuwa kinhu, hawajuwa kamba viwolondeka kujuwa.

3 Lakini munhu yomnogela Mulungu, kojuwigwa na Mulungu.

4 Avo mbuli ya kuja lujo lulavigwe nhosa kwa vinyago, tojuwa vinyago siyo kinhu chochose mwiisi, tojuwa Mulungu imoja yaiyeka.

5 Hata yahawa kuna vinhu vikemigwa, “walungu”, mwiisi hebu kuulanga. Ona, hata kamba wanhu wolonga kuna vinhu vikemigwa, “walungu” na “wandewa,”

6 lakini kumwetu tweye tuna Mulungu imoja yaiyeka, Tata ija yaumbile vinhu vose na kubitila heyo tokuwa wagima. Na kuna Mndewa imoja yaiyeka, nayo ayo Yesu Kilisito, kubitila heyo vinhu vose viumbigwa, na tweye twawagima kubitila heyo.

7 Lakini siyo kila munhu kana ubala uno. Wanhu wayagwe wakala wazowele kuvitambikila vinyago, mbaka sambi wahakala kuna ukuja wogesa woja lujo lulavigwe nhosa kwa vinyago, kwavija mizoyo yao yonyolila, na yogeligwa dikwe.

8 Lakini lujo haludaha bule kutugala behi na Mulungu. Avo twahaleka kuja hatuhungukiligwa kinhu, na twahaja hatukongezeligwa kinhu.

9 Lakini muiteganye, kulekesigwa kwenu sekekuwatende waja weli na mizoyo inyolile watende nzambi.

10 Kamba munhu moyo wake unyolila, yahakona gweye uli na kija kiukema ubala, koja mna ing'anda ya kulavila nhosa kwa vinyago, vino hageligwa moyo kuja lujo lulavigwe nhosa kwa vinyago?

11 Avo mkilisito miyago yeli na moyo unyolile, ija Kilisito yafile mbuli yake, kopotela mbuli ya kija kiukema ubala wako!

12 Kwavija mowatendela nzambi wakilisito waenu na kuilumiza mizoyo yao inyolile, momtendela nzambi Kilisito.

13 Avo kamba lujo lomuhonza mkilisito miyangu yatende nzambi, sija nyama ng'o, muladi sekenimuhonze mkilisito miyangu yatende nzambi.

# 9

### *Sang'hano za watumigwa*

1 Vino, niye silekesigwe bule? Vino, niye sili mtumigwa bule? Vino, niye simonile bule Mndewa wetu Yesu? Vino mweye siyo ulawililo wa sang'hano yangu kwa Mndewa?

2 Hata kamba wanhu wayagwe hawatogola kuwa niye na mtumigwa, lakini kumwenu mweye na mtumigwa! Mweye awo kilaguso cha utumigwa wangu, kwavija muilumba na Mndewa.

3 Munhu yoyose yononga vihile, vino vivo vonda niigombele.

4 Vino, silondeka kuja na kung'wa kwa sang'hano yangu?

5 Vino, silondeka kukweleleza viwotenda watumigwa wayagwe na Kefa na ndugu zake Mndewa, kwa kumsola mwehe Mkilisito mna imiyanza yetu?

6 Hebu niye niiyeka na Balinaba wao tulondeka kusang'hana muladi tupate gaja gatulondeka?

7 Vino, mkalizi gani yoilipa mwenyego kwa sang'hano yake? Vino, mulimaji gani yoleka kuja matunda ga mgunda? Vino, msusilaji gani yoleka kung'wa maziwa ga fugo yake?

8 Silonga ulonzi uno kwa udahi wa kiunhu, kwavija Malagizo ga Musa golonga vivo.

9 Yandikigwa mna Gamalagizo ga Musa, “Sekeumfunge ng'ombe mulomo wahamsang'hanila kuhulula uhemba.” Vino lelo, tulonge Mulungu kosang'hanila ng'ombe?

10 Vino, hakalile kotugesa tweye viyalongile avo? Ona, gano gandikigwa mbuli ya tweye, kwavija mulimaji na msengaji wose wotamanila kuigolela kija kisengigwe.

11 Tweye tuhanda mbeyu ya Loho mgati mwenu. Vino mbuli ng'hulu twahapata vinhu vitulondeka?

12 Kamba wayagwe wolondeka kupata vinhu avo kwa kutamanila kulawa kumwenu, vino tweye hatulondeka kupata ng'hani kubanza wao?

Tweye hatukisang'hanila kitulondeka kupata. Lakini, tofunga umoyo kwa kila kinhu muladi seketuikimile Mbuli Inogile ya Kilisito.

13 Vino hamujuwile kuwa waja wosang'hana Mng'anda ya Mulungu, wopata lujo lwao kulawa mumo, na waja wolava nhosa muupango wopata fungu kulawa mwiinhosa ayo?

14 Vivo ili kwa Mndewa, kalagiza waja wopeta Mbuli Inogile wapate lujo lwao kulawa mumo.

15 Lakini niye sisang'hanile hata dimoja dinilondeka kupata, na wala sikwandika muladi mhate zinondeke kupata. Kumwangu niye nokona vinoga kufa, kubanza munhu yoyose yanyone noigoda kwa mulomo wiiyeka!

16 Lakini nopeta Mbuli Inogile, siyo mbuli ya kuigoda kwa mulomo. Ino ayo sang'hano inigweleligwe. Nojona nahaleka kuwapetela wanhu Mbuli Inogile!

17 Maza niisagule sang'hano ino kwa kulonda mwenyego, nahatamanile fungu, lakini noisang'hana siyo kwa kulonda niye kwavija Mulungu ayo yanisagule nimsang'hanile.

18 Vino, nopata fungu gani? Fungu jangu ni kuwapetela Mbuli Inogile bila kupula sente, bila kupula kinondeka kupata kwa kuwapetela wanhu Mbuli Inogile.

19 Niye sili mtumwa wa munhu yoyose bule, lakini niitenda mwenyego mtumwa wa kila munhu, muladi mhate wanhu bwando wamtogole Kilisito.

20 Vinikalile nosang'hana na Wayahudi ng'hala kamba Muyahudi muladi niwapate Wayahudi, hamoja niye silongozigwa na Malagizo ga Musa, lakini ng'hala kamba viwakalile wao muladi niwapate waja wolongozigwa na Malagizo ga Musa.

21 Vivo ili, vinisang'hane kwa waja weliduhu Malagizo ga Musa, ng'hala kamba viwokala wao, muladi niwapate waja weliduhu Malagizo ga Musa.

Ino hainhenda sekenilongozigwe na Malagizo ga Mulungu, lakini nolon-
gozigwa na Malagizo ga Kilisito.
22 Kwa waja wanyolile, naniye ninyolila muladi niwapate wao. Avo
niitenda kila kinhu kwa wanhu wose muladi nidahe kuwatenda wayagwe
wakomboligwe kwa nzila yoyose idahika.
23 Notenda gano gose kwa mbuli ya Mbuli Inogile muladi mhate fungu
mna ivinhu vake vinogile.
24 Vino, hamujuwile bule kuna ulubuga lwa kukimbilila wanhu bwando
wokimbila, lakini ija yonda yahume kobokela fungu? Avo kolondeka ukim-
bile muladi ubokele fungu.
25 Kila mkimbilaji kowamba kuitanda goya muladi yapate taji
dibanangika, lakini tweye totenda avo tupate taji dileka kubanangika.
26 Lekaavo, nowamba kukimbila nidahe kuvika kuuhelelo, niye niigala na
munhu yoitowa, yoleka kwagiza ng'honde zake.
27 Lekaavo, nolugangamiza lukuli lwangu muladi nilutawale ludahe ku-
sang'hana muladi sekenyoneke sifaya nahakomeleza kuwapetela wayagwe.

# 10

*Wanhu wozumigwa mbuli ya vinyago*

1 Ndugu zangu, nolonda mujuwe kilawilile kwa wahenga zetu wamk-
weleleze Musa. Wose wakala wokalizigwa hasi ya wingu, na wose wabita
goya kuna Ibahali Ndung'hu.
2 Wose wabatizigwa mdiwingu na mna ibahali kamba wanahina wa Musa.
3 Wose waja gate didija da kiloho.
4 Vivija wang'wa kinhu kikija cha kiloho. Wang'wa kulawa mdibwe dija
da kiloho diwacholile najo, dibwe dijo dikala Yesu Kilisito mwenyego.
5 Lakini wanhu bwando hawamnogeze Mulungu, na mitufi yao ipwililika
kuluwala.
6 Lelo, mbuli zose zino ziwe kinhu cha kuifunzila, kutuzuma tweye
seketusulukile gehile, kamba viwatendile wao.
7 Vivija seketuvitambikile vinyago, kamba viwatendile wayagwe. Kamba
Maandiko vigolonga, “Wanhu waja na kung'wa, wafeng'hula kwa ugoni.”
8 Seketutende ugoni kamba viwatendile wayagwe, siku dimoja wafa
wanhu elufu ishilini na ndatu.
9 Seketumgeze Kilisito, kamba viwatendile wayagwe, na wakomigwa na
mizoka.
10 Seketuiyalale kamba viwatendile wayagwe, na wakomigwa na msenga
wa ifa wa kuulanga.
11 Mbuli zose azo ziwalawilila wao, iwe kilaguso kwa wayagwe na
zandikigwa kutuzuma tweye. Kwavija tokala mna ikipindi cha mmabehi na
uhelelo wa isi.
12 Avo munhu yoigesa kema goya yaitiganye sekeyagwe.
13 Kugezigwa kwenu siyo kilozo kwa wanhu. Lakini Mulungu kotenda
kiyalongile, na honda yatogole mugezigwe kubanza nguvu zenu. Hamoja
mogezigwa, lakini kowagwaa nguvu ya kugangamala na kowagwaa nzila ya
kulawila.
14 Avo, mbwiga zangu niwanogela, kaleni kutali na nhambiko za vinyago.
15 Nolonga na mweye wanhu muli na nzewele, gelegezeni wenyego gano
gonilonga.

16 Twahamgwaa nhogolwa Mulungu na kung'wa divai mkikasi, toilumba na damu ya Kilisito. Twahabanzula gate na kudija toilumba na lukuli lwa Kilisito.
17 Hamoja tweye twa wanhu bwando twa lukuli lumoja, kwavija kuna gate dimoja, wose toigolela gate dijo.
18 Waloleni wanhu wa Izilaeli, awo wajaga lujo lwa nhosa lulavigwe muupango, woilumba na nhosa ilavigwe kwa Mulungu.
19 Avo lelo, nonge choni? Vino, vinyago hebu lujo lulavigwe nhosa kwa vinyago vofaya choni?
20 Aka! Kinilonga niye ni kija kilavigwe nhosa muupango wa wamhazi, siyo kwa Mulungu. Na niye silonda mweye muilumbe na vinyamkela.
21 Hamudaha kung'wela kikasi cha Mndewa na vivija kung'wela kikasi cha vinyamkela, hamudaha kuja lujo lwa Mndewa na kuja lujo lwa vinyamkela.
22 Hebu tolonda kumgeza Mndewa yaone migongo? Vino tweye tuna nguvu kubanza heyo?
23 Mweye molonga, "Vinhu vose todaha kutenda," lakini niye nolonga siyo vinhu vose vinoga. Mweye molonga, "Vinhu vose todaha kutenda," lakini niye nolonga siyo vinhu vose vozenga.
24 Munhu yoyose kumwenu sekeyaigese mwenyego yaiyeka, lakini yawagese wanhu wayagwe.
25 Diyeni chochose kiuzigwa kudigulilo, bila kuuza uza na kuitenda mizoyo nyunguwaa.
26 Kwavija Maandiko Gang'alile golonga, "Isi na vose vilimumo ni vinhu va Mndewa."
27 Kamba munhu hamtogola Yesu kowagoneka muulujo na mweye motogola kuchola, diyeni chochose chonda yawatandileni, sekemuuze uze mmizoyo yenu.
28 Lakini kamba munhu kowalongela, "Lujo luno lulavigwa nhosa kwa vinyago," kwa mbuli ya ayo yawalongele na kwa mbuli ya mizoyo, sekemuje.
29 Nolonga vino, siyo mbuli ya mizoyo yenu, lakini mbuli ya moyo wa ayo yawalongele.
Munhu kodaha kulonga, "Habali kulekesigwa kwangu kutamanile moyo wa munhu iyagwe?
30 Kamba noja kuno nomgwaa nhogolwa Mulungu mbuli ya lujo lwangu, habali munhu yanonge vihile mbuli ya lujo lunimgwelele nhogolwa Mulungu?"
31 Avo chochose kimutenda, iwe kuja hebu kung'wa, gose tendeni mbuli ya ukulu wa Mulungu.
32 Sekemuwe ng'hwalo kwa Wayahudi hebu kwa wanhu haweli Wayahudi hebu kwa wanhu wose wa Mulungu.
33 Muwe kamba niye, nogeza kuwanogeza wose kwa kila nzila, sitenda gaja gonyona kumwangu ganoga, lakini notenda gaja gokona wayagwe wose ganoga, avo wadahe kukomboligwa.

# 11

1 Loleni vinhendile munikweleleze, kamba vija niye vinilolile viyatendile Kilisito na kumkweleleza.

### *Kugubika pala kipindi cha kumtambikila Mulungu*

2 Nowagwaa nhogolwa kwa kung'humbuka niye kwa kila kinhu na kugagoga mafundizo ganiwagwee.

3 Lakini nolonda mujuwe kuwa Kilisito ayo pala kwa kila munhu, na mkasano ayo pala kwa mwehe wake, na Mulungu ayo pala kwa Kilisito.

4 Avo kila mbigalo yompula Mulungu, hebu yolonga usenga wa Mulungu kuno kagubika pala jake, ayo kombeza Kilisito.

5 Mtwanzi yoyose yompula Mulungu hebu kulonga usenga wa Mulungu bila kugubika pala jake, ayo komgela kinyala mkasano wake. Mtwanzi yotenda avo kaigala na mtwanzi yabeiye pala jake.

6 Mtwanzi yoleka kugubika pala jake, vivija yabee mvili zake. Kwavija yogela kinyala kwa mtwanzi kusenya mvili zake hebu kubea, kolondeka yagubike pala jake.

7 Mbigalo halondeka kugubika pala jake, kwavija heyo ayo sisila na ukulu wa Mulungu. Lakini mtwanzi ayo ukulu wa mbigalo.

8 Kwavija mbigalo haumbigwe kulawa kwa mtwanzi, lakini mtwanzi kaumbigwa kulawa kwa mbigalo.

9 Vivija mbigalo haumbigwe mbuli ya mtwanzi, lakini mtwanzi kaumbigwa mbuli ya mbigalo.

10 Kwa mbuli ayo na mbuli ya wasenga wa kuulanga, lekaavo mtwanzi kogubika pala jake iwe kilaguso cha kulongozigwa na mbigalo wake.

11 Lakini kwa kuilumba na Mndewa mtwanzi siyo kinhu bila mbigalo, na mbigalo siyo kinhu bila ya mtwanzi.

12 Kamba vija mtwanzi viyalawile kwa mbigalo, vivo ili mbigalo kovumbuka kulawa kwa mtwanzi, lakini vinhu vose volawa kwa Mulungu.

13 Gelegezeni wenyego, kamba vinoga kwa mtwanzi kumpula Mulungu bila kugubika pala jake.

14 Hata Mulungu viyaumbile kolagusa kuwa mbigalo yahawa na mvili nhali koigela kinyala mwenyego.

15 Lakini kwa mtwanzi kuwa na mvili nhali yolagusa unovu wake, kwavija kagweleligwa mvili nhali zimgubike.

16 Kamba munhu yoyose kolonda kuibamila kwa mbuli ayo, tweye twaduhu mila iyagwe, vivija kwa vibumbila va wanhu wamtogole Mulungu.

### *Lujo lwa kukumbuka ifa ya Mndewa*
### *Mat 26:26-29; Mlk 14:22-25; Luk 22:14-20*

17 Mna gamalagizo gano, siwagwaa bule nhogolwa, kwavija miting'hano yenu ya kumtambikila Mulungu yogala gehile kubanza ganogile.

18 Aho haichanduso, mhulika kuwa mwahaiting'hana hamoja moigola mna ivibumbila, na niye notogola kidogo.

19 Ona molondeka muigole, muladi waja wemile mna uukweli woneke goya.

20 Avo mwahaiting'hana mogesa moja lujo lwa Mndewa kumbe haili vivo bule.

21 Kwavija muulujo, kila imoja kolongola kusola lujo lwake mwenyego, kuno wayagwe wana nzala na wayagwe wakoligwa.

22 Vino, mweye mduhu kae za kudila na kung'wela? Hebu mowazeha kibumbila cha wanhu wamtogole Mulungu na kuwagela kinyala wanhu weliduhu kinhu? Vino niwalongele choni? Niwagwee nhogolwa? Siwagwaa nhogolwa kwa mbuli ayo!

23 Kwavija nibokela mafundizo kulawa kwa Mndewa niwagwee mweye. Kilo kija Mndewa Yesu viyahindukigwe, kasola gate,

24 kamgwaa nhogolwa Mulungu, kadibanzula na kalonga, “Uno awo lukuli lwangu, umugweleligwe, mutende vivo kwa kung'humbuka niye.”

25 Vivija, viyamambukize kuja kasola kikasi cha divai, kalonga, “Kikasi kino ni lagano da sambi da Mulungu, mwiidamu yangu, kokose konda mung'we, ing'weni kwa kung'humbuka niye.”

26 Kwavija mwahaja gate dino na kung'wela kikasi kino cha divai, mowapetela wanhu ifa ya Mndewa mbaka vondayeze kabili.

27 Avo munhu yoyose yoja gate da Mndewa hebu kung'wela vihile kikasi acho cha divai, munhu ayo kotagusigwa kwa kulutendela vihile lukuli na damu ya Mndewa.

28 Avo kila munhu tanhu yailolese mwenyego, yang'hali hanakuja gate na kung'wela kikasi acho.

29 Kwavija munhu yoyose yoja na kung'wa bila kujuwa fambulo da lukuli lwa Mndewa, munhu ayo koja na kung'wa nhaguso yake mwenyego.

30 Lekaavo, wanhu bwando kumwenu wanyolila na watamu, na wanhu bwando wafa.

31 Maza tusongile kuilolesa goya wenyego, sambi tutagusigwe na Mulungu.

32 Lakini totagusigwa na kufunzigwa na Mndewa, muladi seketoneke tubananga hamoja na wanhu wa mwiisi.

33 Avo ndugu zangu, mwahaiting'hana hamoja kuja lujo lwa Mndewa, kila munhu yambete miyage.

34 Na kamba hana munhu yoyose kana nzala na yaje ukayake, muladi kuiting'hana kwenu sekekuwatende mutagusigwe na Mulungu. Lakini kwa mbuli zija ziyagwe, nowapetela vondanize.

# 12

*Nhunza zilawa kwa Loho Yang'alile*

1 Sambi ndugu zangu, kwa mbuli ya nhunza zitugweleligwe na Loho Yang'alile.

Nolonda mujuwe vinogile mbuli azo.

2 Mojuwa kuwa vimukalile mung'hali hamunamjuwa Mulungu, mulongozigwa na kutawaligwa na mbuli za kuvitambikila vinyago viliduhu ugima.

3 Nolonda mujuwe kuwa, kuduhu munhu yoyose yolongozigwa na Loho wa Mulungu yodaha kulonga, “Yesu yaduiligwe,” na kuduhu munhu yodaha kulonga, “Yesu ayo Mndewa,” bila kulongozigwa na Loho Yang'alile.

4 Kuna nhunza nyingi, lakini Loho yolava nhunza zizo imoja.

5 Kuna nzila nyingi za kusang'hana, lakini Mndewa yosang'haniligwa imoja.

6 Kuna nzila nyingi za kusang'hana, lakini Mulungu ayo yowagwaa wanhu wose udahi wa kusang'hana.

7 Loho Yang'alile koilagusa kwa kila munhu kwa nzila nyingi muladi wanhu wose wamwede.

8 Loho komgwaa munhu usenga uli na nzewele, na kwa munhu iyagwe Loho iija komgwaa udahi wa kujuwa mbuli.

9 Loho iija komgwaa munhu imoja tamanilo, na komgwaa iyagwe udahi wa kuhonya wanhu.

10 Loho Yang'alile komgwaa munhu udahi wa kutenda unzonza, iyagwe komgwaa nhunza ya kulonga usenga wa Mulungu, na iyagwe komgwaa nhunza ya kujuwa nhunza zilawa kwa Loho hebu hazilawa kwa Loho. Vivija Loho komgwaa munhu nhunza ya kulonga ulonzi wa sambi, na iyagwe nhunza ya kuzifambula.

11 Gano gose gotendigwa na Loho ayo imoja, komgwaa kila munhu nhunza
yake kamba viyolonda Loho.

### *Lukuli lumoja, maungo mengi*

12 Kamba vija lukuli lumoja viuli na maungo mengi, hata kamba maungo
gago mengi, lakini gotenda lukuli lumoja, vivija vivo ili kwa Kilisito.
13 Vivo ili kumwetu tweye wose, tuwe Wayahudi hebu haweli Wayahudi,
watumwa hebu wanhu walekesigwe, wose tubatizigwa kwa Loho imoja
mna ulukuli lumoja na wose tugweleligwa Loho imoja tumng'we.
14 Kwavija lukuli hauumbigwe kwa kiungo kimoja kiiyeka, lakini kwa
maungo mengi.
15 Maza mgulu wahalongile, "Kwavija niye sili mkono bule, sili kiungo cha
lukuli," vino sambi uwe kiungo cha lukuli? Aka!
16 Na gwiti dahalongile, "Kwavija niye sili siso bule, niye sili lukuli bule,"
vino, sambi diwe kiungo cha lukuli? Aka!
17 Maza lukuli lose lwahawile siso, munhu yahadahile vilihi kuhulika?
Na maza lukuli lose lwahakalile gwiti diiyeka, munhu yahadahile vilihi
kunusa?
18 Avo Mulungu kakika kila kiungo mulukuli kamba viyalondile.
19 Maza lukuli lose lwahawile kiungo kimoja, sambi kuwe na lukuli!
20 Vivo ili, maungo mengi, lakini lukuli lumoja.
21 Avo, siso hadidaha kuulongela mkono, "Sikulonda gweye!" hebu pala
hadidaha kugalongela magulu, "Siwalonda mweye!"
22 Lakini viikoneka, hatudaha kutenda kinhu bila maungo ga lukuli
gokoneka ganyolila.
23 Na maungo gotugesa hagafaya ng'hani, gago maungo gololesigwa goya,
kuno maungo gogela kinyala gogubikigwa goya.
24 Lakini maungo gotugesa todaha kugalagusa hatugatonga. Avo Mulungu
ayo yawikile lukuli hamoja, kakigwaa kutegelezigwa ng'hani kiungo kija
kihungukiligwe kutegelezigwa.
25 Avo, kuduhu kuigola mulukuli, lakini maungo gose goitaza.
26 Kamba kiungo kimoja chahalumila, maungo gose gayagwe golumila
hamoja nacho na kamba kiungo kimoja chahatogoligwa, maungo gose
gayagwe godeng'helela hamoja nacho.
27 Avo, mweye mose mwa lukuli lwa Kilisito, kila munhu kiungo cha lukuli
lulo.
28 Mvibumbila va wanhu wamtogole Yesu Mulungu kaweka, mosi watu-
migwa, pili watula ndagu na kadatu wafundiza, abaho kaweka waja weli na
nhunza ya kutenda unzonza, abaho waja weli na nhunza ya kuhonya hebu
kuwataza wayagwe hebu udahi wa kuwalongoza wanhu hebu kulonga
ulonzi wa sambi.
29 Wanhu wose siyo watumigwa hebu watula ndagu hebu wafundiza. Siyo
kila munhu kana udahi wa kutenda unzonza,
30 hebu kuhonya watamu hebu kulonga ulonzi wa sambi hebu kufambula
ulonzi.
31 Avo, sulukileni nhunza zili ng'hulu ng'hani.

Na niye nowalagusila nzila inogile ng'hani.

## 13

### *Unogelwa*

1 Hata nahadaha kulonga ulonzi wa wanhu na hata wa wasenga wa
kuulanga, lakini kamba naduhu unogelwa, ulonzi wangu nyangi ziiyeka
kamba munhu yotowa mpatu kuna dizengele hebu mbugi.
2 Vivija nodaha kuwa na nhunza ya kupeta usenga wa Mulungu, nozijuwa
mbuli zose zifisigwe, na nodaha kuwa na tamanilo da kuhamiza vigongo,
lakini nahaswela unogelwa niye siyo kinhu.
3 Nodaha kulava vinhu vangu vose kuwagwaa wakiwa, hata kuulava
lukuli lwangu lulukuzigwe, lakini nahaswela unogelwa hainifaya chochose.
4 Yeli na unogelwa kobetela kwa kufunga umoyo, muhole, kaduhu
migongo hebu kuitapa hebu kuigoda.
5 Yeli na unogelwa kotegeleza, haigesa mwenyego bule, hebu kugevuzika
himahima, kaduhu mfundo.
6 Yeli na unogelwa hadeng'helela gehile, lakini kodeng'helela ukweli.
7 Yeli na unogelwa habwela kukisogo, kotamaniligwa na kotamanila gose
na kogangamala.
8 Unogelwa haulemelwa. Kamba kuna nhunza za kupeta usenga wa
Mulungu, zose zobita siku dimoja, yahawa nhunza ya kulonga ulonzi wa
sambi, yohuhwa, wahawa ubala nao wobita.
9 Kwavija ubala wetu na nhunza yetu ya kupeta mbuli ya Mulungu
hawenele,
10 lakini kipindi chahavika Mulungu kotenda chenela kija kihunguke na
hachenele cholawanya.
11 Ving'halile mwana, nilonga na nigelegeza na nigesa kamba mwana,
lakini sambi na mkulu, mbuli zose za uwana nizileka.
12 Kituona sambi kamba lumvuye mvuye mna ikiyoo, lakini aho
kumwande tokona meso kwa meso. Sambi nojuwa hadodo, aho kumwande
nojuwa goya, kamba vija Mulungu viyanjuwile niye.
13 Vinhu vino vidatu vosigala, kutogola, kutamanila na unogelwa, lakini
dilikulu kubanza gose awo unogelwa.

# 14

*Nhunza ziyagwe zilawa kwa Loho Yang'alile*

1 Uzahileni unogelwa. Vivija zahileni nhunza ziyagwe zilawa kwa Loho
Yang'alile, ng'hani ng'hani nhunza ya kuwapetela wanhu usenga wa Mu-
lungu.
2 Munhu yolonga kwa ulonzi ukanganya, halonga na wanhu lakini ko-
longa na Mulungu, kwavija kuduhu munhu yojuwa. Kolonga mbuli ziifisile
kwa udahi wa Loho.
3 Lakini waja wowapetela wanhu usenga wa Mulungu, wolonga na wanhu
mbuli ya kuwagela moyo, kuwagangamiza na kuwahoza mizoyo.
4 Waja wolonga ulonzi ukanganya woigangamiza wenyego, lakini waja
wowapetela wanhu usenga wa Mulungu, wao wokigangamiza kibumbila
chose cha wanhu wamtogole Yesu.
5 Vinilonda niye mweye mose mulonge ulonzi ukanganya, lakini nolonda
ng'hani muwe na nhunza ya kuwapetela wanhu usenga wa Mulungu.
Kwavija munhu yeli na nhunza ya kuwapetela wanhu usenga wa Mulungu
kofaya ng'hani kubanza ija yolonga ulonzi wa kukanganya, mbaka hawe na
munhu wa kufambula mbuli zilongigwa, avo wanhu wose wamtogole Yesu
wadahe kugangamizwa.
6 Ndugu zangu, vino yowafaya choni naheza kumwenu kulonga na mweye
ulonzi ukanganya? Hakiwafaya chochose, mbaka niwalongeleni ugubulo

wa Mulungu hebu ubala fulani, hebu usenga wa Mulungu hebu mafundizo fulani.
7 Vivo ili kwa vinhu viliduhu ugima vilava sauti, kamba vija kifengwa, hebu bango. Vino munhu kodahaze kujuwa lwila lutoigwa kamba kifengwa acho hebu bango vahatoigwa havilava sauti vinogile?
8 Kamba mhalati hailila goya, nani yonda yaitande kwa kuitowa?
9 Vivo ili kumwenu mweye, kamba lulimi lwenu halulonga kinhu kijuwika, nani yonda yadahe kugajuwa gomulonga? Kwavija kamba molonga na ubeho.
10 Kuna ulonzi mwingi mwiisi, lakini kuduhu ulonzi uliduhu fambulo jake.
11 Lakini nahaleka kujuwa fambulo da ulonzi wa munhu, niye nokuwa munhu baki kumwake nayo kokuwa munhu baki kumwangu.
12 Kwavija mweye mosulukila kupata nhunza ya Loho, molondeka muwambe kuzisang'hanila nhunza azo kwa kuwagangamiza wanhu wamtogole Yesu.
13 Avo munhu yolonga ulonzi ukanganya, kolondeka yampule Mulungu yapate udahi wa kufambula.
14 Kwavija nahampula Mulungu kwa ulonzi ukanganya, loho yangu ayo ipula, lakini nzewele zangu zokala bule.
15 Avo nhende choni? Nompula Mulungu kwa loho yangu, vivija nompula Mulungu kwa nzewele zangu na nokwimba kwa loho yangu, vivija nokwimba kwa nzewele zangu.
16 Wahamgwaa nhogolwa Mulungu kwa loho yako iiyeka, yodahika vilihi kwa wanhu waiting'hane kwidika nhogolwa zako kwa Mulungu kwa kulonga, “Ona,” kamba hawakijuwa kiulonga?
17 Hata kamba nhogolwa zako kwa Mulungu zahanoga vilihi, wanhu wayagwe haziwagangamiza bule.
18 Nomgwaa nhogolwa Mulungu kwavija niye nolonga ulonzi ukanganya kubanza mweye mose.
19 Lakini nahaiting'hana na kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu, nonogelwa kulonga mbuli tano zijuwika goya muladi niwafundize wayagwe, kubanza kulonga mbuli magana kwa magana kwa ulonzi ukanganya.
20 Ndugu zangu, sekemugese kamba wana wadodo. Kwa mbuli ya gehile mukale kamba wana ving'hele weliduhu vitala, lakini mugese kamba viwogesa wanhu wabala goya.
21 Yandikigwa mna Gamalagizo kamba,
“Mndewa kolonga vino,
‘Kubitila wanhu wolonga ulonzi ukanganya,
na kwa milomo ya wanhu baki,
nowalongela wanhu zangu,
lakini hawanitegeleza bule.’ ”
22 Avo nhunza ya kulonga ulonzi ukanganya ni kilaguso kwa wanhu hawamtogola Yesu, siyo kwa wanhu wamtogole Yesu, lakini nhunza ya kuwalongela wanhu usenga wa Mulungu ni kilaguso kwa wanhu wamtogole Yesu, siyo kwa wanhu hawamtogole Yesu.
23 Avo, wanhu wose wamtogole Yesu wahaiting'hana hamoja, na wose wolonga kwa ulonzi ukanganya, baho waheza wanhu hawajuwa hebu wanhu hawamtogole Yesu, vino honda walonge kuwa mweye mose mna kibozi mbwelela?
24 Lakini wose wahalonga usenga wa Mulungu, yaheza munhu hajuwile kinhu hebu munhu hamtogola Yesu gose gonda yahulike gomulagusila nzambi zake na vivija gomtagusa.

25 Gaja gafisigwe mmizoyo yao gogubuligwa, nao wofugama na kumtam-
bikila Mulungu, kwa kulonga, “Kweli Mulungu kabaha hamoja na mweye!”

*Viilondeka kutenda mvibumbila va wanhu wa Mulungu*

26 Ndugu zangu, nofambula vino, mwahaiting'hana hamoja kumtambik-
ila Mulungu, imoja kana nyila, iyagwe kofundiza, iyagwe kana ugubulo ku-
lawa kwa Mulungu, iyagwe kana nhunza ya kulonga kwa ulonzi ukanganya,
na iyagwe kofambula kija kilongigwe. Kila kinhu kiwe kwa kuwagangamiza
wanhu waiting'hane.
27 Kamba munhu kolonga ulonzi ukanganya, wanhu wabili hebu wadatu,
walonge imoja imoja, munhu iyagwe kolondeka yafambule kija kilongigwa.
28 Lakini kamba kuduhu munhu yodaha kufambula mbuli ilongigwa, avo
ija yolonga kwa ulonzi ukanganya yanyamale, yalonge mwenyego na kwa
Mulungu.
29 Wanhu wabili hebu wadatu wagweleligwe usenga wa Mulungu, wa-
longe na kuno wayagwe walolese goya gaja gowolonga.
30 Na kamba munhu yakalile aho kobokela usenga kwa Mulungu, ija
yolonga yanyamale.
31 Mose modaha kulonga usenga wa Mulungu, imoja imoja, avo kila
munhu koifunza na kugangamizwa.
32 Nhunza ya kulonga usenga wa Mulungu yolondeka iwe mmakono ga
mulongaji.
33 Kwavija Mulungu siyo Mulungu wa kuding'huka, lakini Mulungu wa
tindiwalo.
Kamba viili mna ivibumbila vose va wanhu wa Mulungu,
34 watwanzi wolondeka wanyamale mna ivibumbila va wanhu wamto-
gole Yesu. Hawatogoleligwa kulonga, lakini wategeleze, kamba Malagizo ga
Wayahudi vigalonga.
35 Kamba hana kinhu wolonda kukijuwa, wahabwela ukae wodaha
kuwauza wambigalo zao. Yogela kinyala kwa mtwanzi kulonga mvibumbila
va wanhu wamtogole Yesu.
36 Vino, usenga wa Mulungu usonga kumwenu? Hebu uwavikila mweye
mwiiyeka?
37 Kamba mweye moigesa wenyego molonga usenga wa Mulungu hebu
wanhu wa Loho, avo muvijuwe kamba nokwandika gaja gaiyeka gayalagize
Mndewa.
38 Kamba munhu hatonga kija kinyandika, sekemumtonge munhu ayo.
39 Ndugu zangu, sulukileni kuwapetela wanhu usenga wa Mulungu na
sekemumgomese munhu yoyose kulonga ulonzi ukanganya.
40 Lakini tendeni goya kila kinhu, kamba viilondeka.

# 15

*Kuzilibuka kwa Kilisito*

1 Ndugu zangu, lelo nolonda kuwakumbusa Mbuli Inogile iniwapetele,
na mweye muibokela, Mbuli ayo Inogile acho chandusilo cha kumtamanila
kwenu Mulungu.
2 Usenga uniwapeteleni, ayo Mbuli Inogile. Mwahaigoga ng'hani mokom-
boligwa. Kamba mwahaleka kuigoga mugaya bule kutogola.
3 Niwagwaa kinhu kikulu ng'hani kimbokele, Kilisito kafa kwa nzambi
zetu, kamba Maandiko Gang'alile vigolonga,
4 kamba kazikigwa, abaho siku da kadatu kazilibuka, kamba Maandiko
Gang'alile vigolonga,

5 kamulawilila Kefa, abaho kawalawilila watumigwa wose longo na wa-
bili.
6 Abaho kawalawilila kwa mwanza umoja wanahina zake bwando,
kubanza magana matano, wanhu bwando mna iwao wang'hali wagima
lakini wayagwe wafa.
7 Kumwande kamulawilila Yakobo, abaho kawalawilila watumigwa wose.
8 Kukimambukizo kandawilila naniye vivija, hata kamba niigala na
munhu yavumbuke kipindi kihile.
9 Kwavija mna iwatumigwa wose niye na munhu mdodo ng'hani, niye
sifaya hata kukemigwa mtumigwa, kwavija niwadununza wanhu wamto-
gole Yesu.
10 Lakini kwa ng'hekewa ya Mulungu niwa kamba vinili, na ng'hekewa
iyanigwelele hayagile bule. Nisang'hana ng'hani kubanza wayagwe wose,
hata avo siyo niye nisang'hane, lakini ng'hekewa ya Mulungu ya hamoja na
niye.
11 Lakini siyo kinhu, kamba niye niwapetela wanhu Mbuli Inogile hebu
wao wawapetela wanhu. Mweye mose mutogola usenga awo.

*Kuzilibuka kwa wafile*

12 Lelo, kamba towapetela wanhu kuwa Mulungu kamzilibula Kilisito kwa
wanhu wafile, wanhu wayagwe kumwenu wodaha vilihi kulonga kuwa
wanhu wafile honda wazilibuke bule?
13 Kamba kweli wanhu wafile honda wazilibuke bule, yofambula kuwa
Kilisito hazilibuke bule.
14 Kamba Kilisito hazilibuke kwa wanhu wafile, togaya bule kuwapetela
wanhu na kutamanila kwetu kuduhu kinhu.
15 Avo tokoneka wavizi mgameso ga Mulungu, kwavija tulonga Mulungu
kamzilibula Kilisito kwa wanhu wafile. Kamba kweli, Mulungu hamzilibule
Kilisito, avo wanhu wafile honda wazilibuke.
16 Kwavija kamba wanhu wafile hawazilibuka bule, avo Kilisito
hazilibuke bule.
17 Kamba Kilisito hazilibuke kwa wanhu wafile, kumtamanila kwenu
kuduhu kinhu, na mung'hali mopotela mzinzambi zenu.
18 Vivija ino yofambula kuwa waja wamtogole Kilisito abaho wafa,
wapotela.
19 Kamba tomtamanila Kilisito vinogile kwa ugima uno wiiyeka, tofaya
koneligwa bazi ng'hani na wanhu kubanza munhu yoyose iyagwe mwiisi.
20 Lakini kweli Kilisito ayo waichanduso kuzilibuka kwa wanhu wafile,
ino yolagusa kuwa waja wafile wozilibuka vivija.
21 Kwavija kamba ifa viigaligwe mwiisi na munhu, vivo ili kuzilibuka kwa
wanhu wafile kogaligwa na munhu.
22 Kwavija kamba wanhu wose viwofa mbuli ya kuilumba kwao na
Adamu, vivo ili wanhu wose wozilibuligwa kwa wanhu wafile mbuli ya
kuilumba kwao na Kilisito.
23 Lakini kila munhu kozilibuligwa mna ikipindi chake, tanhu Kilisito,
abaho waja weli wanhu zake mna ikipindi chonda yeze Kilisito.
24 Abaho wahavika uhelelo, Kilisito kobananga utawala wose na udahi
wose na mamulaka gose, na komgwaa Undewa Mulungu Tata.
25 Kwavija Kilisito kolondeka yatawale mbaka Mulungu vonda yawahume
wose wamwihile na kuweka hasi ya magulu gake.
26 Mdumuka wa kimambukizo kubanangigwa kokuwa ifa.

27 Kwavija Maandiko Gang'alile golonga, “Mulungu kokwika vinhu vose hasi ya magulu gake.” Avo yahalonga, “Vinhu vose.” Mulungu mwenyego kahaduhu, heyo ayo yokwika vinhu vose hasi ya Kilisito.

28 Lakini vinhu vose vahekigwa hasi ya utawala wa Kilisito, nayo Imwana, koika mwenyego hasi ya Mulungu, yekile vinhu vose hasi yake, na Mulungu kovitawala vose kila hanhu.

29 Kamba wanhu wafile hawazilibuka bule, vino wotenda choni wanhu waja wobatizigwa mbuli ya wao? Habali wobatizigwa mbuli ya wanhu awo wafile?

30 Na tweye, habali twamdizumozumo kila saa?

31 Ndugu zangu, kila siku na mmabehi na ifa! Magoda ganilinago kumwenu kwa kuilumba na Yesu Kilisito Mndewa wetu gonhenda nonge vino.

32 Vino mogesa nipata choni kwa kuitowa na wanhu waigalile na ming'onyo ako Efeso? Kamba wanhu wafile hawazilibuka, “Tuje na tung'we, kwavija mayo tofa.”

33 Sekemuwe wabozi, “Mbwiga wehile woibananga tabiya inogile.”

34 Muwe na nzewele na muleke kutenda nzambi, kwavija wanhu wayagwe kumwenu hawamjuwile Mulungu, na nolonga vino kuwagela kinyala.

### *Kuzilibuka kwa lukuli*

35 Wanhu wayagwe wodaha kuuza, “Vino, wanhu wafile wodaha vilihi kuzilibuka? Na lukuli lwao lokuwaze?”

36 Uuzaji awo wakibozi! Mwahahanda mbeyu, haikota mbaka tanhu ife.

37 Na kiuhanda ni mbeyu iiyeka, yodaha kuwa mbeyu ya ngano hebu mbeyu ziyagwe, lakini wonda wote aho kumwande wokuwa mnoga.

38 Mulungu koitenda mbeyu ayo yote na koigwaa mnoga uyolonda mwenyego, kila mbeyu koigwaa mnoga wake.

39 Vinhu vose viumbigwe haviigalile. Wanhu, wanyama, ndege na somba wana ng'huli, lakini ng'huli zao haziigalile bule.

40 Kuna ng'huli za kuulanga na ng'huli za mwiisi. Unovu wa ng'huli za kuulanga hauigalile na unovu wa ng'huli za mwiisi.

41 Zuwa dina unovu wake, mwezi vivija una unovu wake na nhondo vivija zina unovu wake. Hata nhondo vivija haziigalile kwa unovu.

42 Vivo vonda iwe, kwa waja wafile vonda wazilibuke. Lukuli lwahazikigwa lokola, lwahazilibuka halukola bule.

43 Lwahazikigwa lwiha, lwahazilibuka lunoga, lwahazikigwa lonyolila lwahazilibuka luna nguvu.

44 Lwahazikigwa lokuwa lukuli, lwahazilibuka lokuwa lukuli lwa loho. Kamba tuna lukuli lwa kiunhu, vivija tokuwa na lukuli lwa kiloho.

45 Kwavija Maandiko Gang'alile golonga, “Munhu wa ichanduso, Adamu kaumbigwa yawe ugima,” lakini Adamu wa ikimambukizo ayo Loho yowagwaa wanhu ugima.

46 Siyo lukuli lwa kiloho ulo lulongole, lakini lukuli lwa kiunhu ulo lulongole.

47 Adamu wa ichanduso, kaumbigwa kwa udongo, Adamu wa kabili kalawa kuulanga.

48 Awo weli mwiisi waigala na munhu yaumbigwe kwa udongo, na awo wa kuulanga waigala na heyo yalawile kuulanga.

49 Kamba vija vituigalile na heyo yaumbigwe kwa udongo, vivo vonda tuigale na heyo yalawile kuulanga.

50 Ndugu zangu, nolonda mujuwe kamba, kija kili na lukuli na damu haki-
daha kuwa na fungu Muundewa wa Mulungu, na kija kinangika chaduhu
fungu da kija kileka kunangika.
51 Tegelezeni, nowalongeleni mbuli ifisigwe. Wose hatufa bule, lakini
wose togaluka.
52 Yolawilila kwa kusinhukiza, himahima kubanza siso vidibwenza. Mha-
lati ya ikimambukizo yahalila, wanhu wafile wozilibuka, wose togaluka, avo
hatufa kabili.
53 Ng'huli zetu zifa na kunangika, zogaluka kuwa ng'huli zileka kufa hebu
kunangika.
54 Avo yahalawilila vino, lukuli lunangika logaluka sekelunangike na kija
kifa honda kife, aho golawilila Maandiko Gang'alile galongile, "Ifa ihumigwa
na kuhuma kuvika!"
55 "Ifa, kuhuma kwako kwa kwahi?
Ifa, udahi wako wa kulumiza wa kwahi?"
56 Ifa yopata udahi wa kulumiza kulawa kwa nzambi, na nzambi zopata
udahi kulawa kwa Malagizo.
57 Lakini tumgwee nhogolwa Mulungu yotugwaa kuhuma kubitila Mndewa
wetu Yesu Kilisito!
58 Avo, ndugu zangu woniwanogela, gangamaleni. Siku zose muhun-
ganike kumsang'hanila Mndewa, kwavija kuduhu kinhu chonda mutende
mwiisang'hano ya Mndewa chonda chage bule.

# 16

*Kusanga sente kuwataza wakilisito*

1 Mwahasanga sente mbuli ya wanhu wa Mulungu, nowalonda mutende
kamba vija vinivilongele vibumbila va wanhu wamtogole Yesu ako Galatia.
2 Kila jumapili kila munhu kumwenu yabagule sente, ziigale na vija
vimupatile, zikeni goya, muladi vondanize sekemulonde kusanga sente.
3 Vondanize, nowagwaa baluwa na nhunza zenu waja muwasagule na
nowatuma wachole Yelusalemu.
4 Kamba yofaya naniye nichole, aho wodaha kuchola na niye.

*Mbuli zoyogesa Paulo kusang'hana*

5 Nahabitila mwiisi ya Makedonia, nokwiza kuwalola, kwavija nogesa
kubitila Makedonia.
6 Sengine nokala na mweye kipindi kidodo, hebu sengine nodaha kukala
na mweye kipindi chose cha kihuhwe, avo modaha kunitaza nigendelele na
mwanza wangu kokose konda nichole.
7 Mndewa yahalonda, nokwiza kumwenu kukala ng'hani, kubanza kwima
aho kwa kipindi kidodo.
8 Nokala hano kudibuga da Efeso mbaka siku ya Pentekosite.
9 Kwavija nivuguliligwa lwivi mkulu mbuli ya sang'hano yangu, hamoja
hana wanhu bwando wondema.
10 Timoseo yaheza, mbokeleni goya, kwavija kotenda sang'hano ya Mn-
dewa, kamba niye.
11 Munhu yoyose sekeyamwehule, lakini mumtaze yagendelele goya na
mwanza wake, muladi yabwele kumwangu, kwavija niye nombeta hamoja
na ndugu zangu.
12 Avo, kwa mbuli ya ndugu yetu Apolo, baho kwa baho nimnanahiza yeze
kumwenu hamoja na wanhu wayagwe wamtogole Yesu, lakini halonda bule
kwiza sambi bule, avo yahadahika kokwiza.

*Mbuli za kimambukizo*

13 Kaleni meso, gangamaleni mditamanilo, muwe magalu na weli na nguvu.

14 Sang'hano zenu zose muzitende kwa unogelwa.

15 Ndugu zangu, mojuwa kuwa Sitefana na wanhu wa lubuga lwake wakala wa ichanduso kumtogola Yesu mwiisi ya Akaya. Watenda vi-wadahile kuwasang'hanila wanhu wa Mulungu. Ndugu zangu, nowapula,

16 wategelezeni wanhu kamba wano, na munhu yoyose iyagwe yosang'hana hamoja na wao.

17 Nodeng'helela ng'hani kwavija Sitefana, Folitunata na Akaiko wavika hano. Kukala kwao hano, ni kamba wasola hanhu ha kukala na mweye.

18 Wautenda moyo wangu usamhuke ng'hani, kamba viwawatendile mw-eye musamhuke. Wategelezeni wanhu kamba wao.

19 Vibumbila va wanhu wamtogole Yesu mwiisi ya Asiya kwa kuilumba na
Kilisito vowalamuseni ng'hani. Akula na Pilisila na wanhu wa Mulungu weli
mzing'anda zao, womulamuseni kwa twaga da Mndewa.

20 Wanhu wose hano wamtogole Yesu womulamuseni.
Muilamuse kwa nzila ilagusa moinogela.

21 Niye Paulo nowalamusa, nokwandika kwa makono gangu mwenyego.

22 Munhu yoyose hamnogela Mndewa, yaduiligwe na Mulungu!
Mndewa wetu izo!

23 Ng'hekewa ya Mndewa Yesu ikale hamoja na mweye.

24 Nowanogela mose kwa kuilumba na Yesu Kilisito.

# Baluwa ya Kabili ya Paulo kwa wanhu wa ako Kolinto

## Ulongozi

2 Wakolinto chandikigwa na mtumigwa Paulo muumwaka 55 na 56 toka kuvumbuka kwa Kilisito (Sula ya 1:1). Ino ayo baluwa ya kabili mna izibaluwa zitulinazo ziyandike Paulo kwa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu ako Kolinto. Wanhu woifunza mbuli woitogolela kuwa ichanduso Paulo kandika baluwa ng'hali kwa wanhu wa ako Kolinto. Twaduhu baluwa ino ilongigwe mzisula za 2:3-4:2. Baluwa ino kwa Wakolinto yogesigwa yandikigwa kipindi Paulo kakala ako Makedonia (Sula ya 2:13).

2 Wakolinto cha vingine, cholonga mbuli zake mwenyego na cholonga mbuli za moyo. Paulo kosimulila deng'ho mbuli ya usenga unogile uyapatile kulawa kwa Tito mbuli ya wanhu wamtogole Yesu ako Kolinto. Mna ibaluwa ino, tona mafundizo mengi mbuli ya kulava kulawa mna idilagano da sambi, hanhu Paulo hayalavile malagizo mbuli ya kusanga sente na kuzigala kuwataza wanhu wamtogole Yesu ako Yelusalemu (Sula ya 8-9). Yokoneka wanhu wayagwe watumigwa wa uvizi kulawa kunze ya kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu wobitila wanhu wayagwe mna ikibumbila kumulonga vihile Paulo na kuitogola wenyego. Wawatenda wanhu wanyawe nyawe mbuli ya mamulaka ga Paulo, mbuli ayo yogesigwa kamba ayo imtendile Paulo yalaguse mamulaka kamba mtumigwa wa Yesu Kilisito kukimambukizo cha Wakolinto wa kabili.

**Mbuli zili mkitabu**

Paulo kosonga baluwa yake kwa kuwalamusa wanhu wa kibumbila wamtogole Yesu (Sula ya 1:1-7).

Abaho Paulo kolonga viyagimbule mwanza wake uyagesile na usenga uyabokele mbuli yao na viwaibokele baluwa yake ya ichanduso (Sula ya 1:8-7:16).

Abaho Paulo kolava mafundizo mbuli ya sente zisangigwe kwa kuwataza wanhu wamtogole Yesu ako Yelusalemu (Sula ya 8:1-9:15).

Kukimambukizo Paulo koigombela mbuli ya utumigwa wake na kolonga mbuli ya mwanza wake wa kutembelela (Sula ya 10:1-13:10).

1 Niye Paulo, namtumigwa wa Yesu Kilisito kwa kulonda Mulungu, na ndugu yetu Timoseo towatumileni baluwa mweye kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu ako Kolinto, hamoja na wanhu wose wa Mulungu mwiisi yose ya Akaya,

2 Mulungu Tataetu na Mndewa Yesu Kilisito wawagwee ng'hekewa na tindiwalo.

*Paulo komgwaa nhogolwa Mulungu*

3 Tumgwee nhogolwa Mulungu, Tata wa Mndewa wetu Yesu Kilisito, Tata Mulungu yowonela wanhu bazi na kuwahoza mizoyo yao!

4 Mulungu kotuhoza mizoyo mna gamagayo getu, muladi na tweye tuwahoze mizoyo awo weli mna gamagayo, kwa kuhozigwa kukuja kutuhozigwe tweye na Mulungu.

5 Kamba vija madununzo ga Kilisito vigokongezeka kumwetu, vivija kubitila Kilisito kuhozigwa kwetu mizoyo kokongezeka.

6 Twahagaya, togaya mbuli ya kuhozigwa kwenu mizoyo na kukomboligwa kwenu. Kamba twahahozigwa mizoyo na mweye vivija mohozigwa

mizoyo muladi kuwagangamiza mufunge umoyo mna gamagayo kamba
vitugaya tweye.
7 Vivija, tamanilo jetu kumwenu digangamala, kwavija tojuwa kuwa
kamba vija vitugaya hamoja, vivija mohozigwa mizoyo hamoja na tweye.

8 Ndugu zetu, hatulonda kuwafisa vitugaiye mwiisi ya Asiya. Tugaya
ng'hani mbaka tugesa tolemelwa kufunga umoyo na tofa.
9 Tugesa tukala kamba wanhu watagusigwe ifa. Mbuli ino ilawilila mu-
ladi seketuitamanile wenyego, lakini tumtamanile Mulungu, yowazilibula
wanhu wafile.
10 Mulungu katuhonya mdizumozumo da ifa, na kogendelela kutuhonya.
Tweye totamanila kuwa Mulungu kotuhonya kabili,
11 mweye mwahatutaza kutupulila kwa Mulungu. Vinhu bwando vinogile
vitupatile kwa wanhu bwando kutupulila, votenda wanhu bwando wamg-
wee nhogolwa Mulungu yetu.

### *Paulo kogimbula viyalondile kutenda*

12 Tweye toigodela kinhu kimoja, mizoyo yetu yotulongela vitukala mwiisi
ino, ng'hani ng'hani vituilumba na mweye, kwa kung'ala na ukweli kulawa
kwa Mulungu. Tutenda vivo siyo kwa kulongozigwa na nzewele za wanhu
wa mwiisi, lakini kwa ng'hekewa ya Mulungu.
13 Towandikila mweye gaja gamudahile kugasoma na kugajuwa. Niye
notamanila motujuwa goya,
14 kwavija mbaka sambi mutujuwa kidogo. Tojuwa kuwa mna isiku ija
ya kwiza Mndewa Yesu modaha kuigodela tweye kamba tweye vituigodela
mweye.

15 Kwavija ng'hala nijuwile goya, tanhu nilonda kwiza kumwenu muladi
mumwede kunyona miyanza mibili.
16 Muumwanza wangu wa kuchola isi ya Makedonia, nilonda kubitila
kumwenu, na umbwelo kulawa Makedonia vivija mbitile kumwenu, muladi
mungale mwanza wangu wa kuchola Yudea.
17 Vino mweye vimgesa vinifungile mwanza wangu, ng'hala
nonyawanyawa? Hebu mogesa notenda mbuli zangu kamba viwotenda
wanhu, nahalonga, "Dimema, ona," nahalonga, "Da hindi, ona"?
18 Kamba Mulungu viyolonga ukweli, usenga wetu kumwenu siyo ku-
longa, "Ona" na "Bule."
19 Kwavija Yesu Kilisito, Mwana wa Mulungu, itumpetile kumwenu, niye
na Sila na Timoseo, hakalile munhu wa kulonga, "Ona" na "Bule". Lakini
kumwake heyo siku zose, "Ona."
20 Kwavija haitongigwa Mulungu kalonga miyanza mingahi, vija viya-
longile kubitila Kilisito vokuwa, "Ona." Lekaavo "Ona" yetu itulonga ku-
bitila Kilisito, toilonga kwa kumgwaa ukulu Mulungu.
21 Mulungu mwenyego ayo yotutenda tweye na mweye tugangamale kwa
kuilumba na Kilisito. Mulungu ayo yatusagule tweye,
22 katwikila kinhu kilagusa tweye twa wanhu zake, na kamwika Loho
wake mmizoyo yetu kamba fungu dodo da gaja gose gayatwikile.

23 Mulungu ayo msindila wangu, kaujuwa moyo wangu! Niye sibwelile
ako Kolinto kwavija niwonela bazi.
24 Hatulonda kuwananahiza choni cha kutamanila, tojuwa kamba mu-
gangamala mditamanilo jenu, lakini tweye tosang'hana na mweye mbuli ya
deng'ho jenu.

# 2

1 Avo nigelegeza, sekeniwatembelele kabili na kuwanyunyuwaza.

2 Kwavija nahawanyunyuwaza mweye, nani yonda yanihoze umoyo? Siyo wawaja waniwanyunyuwaze?

3 Lekaavo niwandikila baluwa, silondile kwiza kumwenu na kunyunyuwazwa na mweye mulondeke kunhenda niye ndeng'helele. Vinikona niye nahadeng'helela na mweye vivija modeng'helela.

4 Mna ibaluwa ija niwandikila kwa kunyunyuwala na usungu muumoyo na mahozi mengi, sandike kwa kuwagela usungu, lakini kuwalagusila viniwanogela ng'hani.

### *Kugela kumgongo nzambi za munhu*

5 Kamba munhu yahamgela usungu miyage, hangelile usungu ng'hani niye, ila kawagela usungu mweye mose, silonda kuwa msabalu ng'hani bule.

6 Nhaguso iyatagusigwe munhu ayo na wanhu bwando kumwenu yomfaya.

7 Kisigale sambi, mugele kumgongo na kumuhoza umoyo, muladi sekeyanyunyuwale ng'hani na kubwela kukisogo.

8 Nowapula ng'hani, mulagusileni kabili munhu ayo kuwa mumnogela.

9 Kilamuso cha kuwandikila baluwa ija, nilonda kuwageza nijuwe kamba modaha kugoga kila kinhu.

10 Mwahagela kumgongo nzambi za munhu, na niye vivija nogela kumgongo. Kwavija nahagela kumgongo, kamba kweli ya cha baho kinhu cha kugela kumgongo, aho nogela kumgongo mgameso ga Kilisito mbuli ya mweye,

11 muladi Mwenembago sekeyawe mbala kumwetu, kwavija tojuwa viyogesa.

### *Paulo konyawanyawa kudibuga da Toloa*

12 Vimvikile kudibuga da Tuloasi kuwapetela wanhu Mbuli Inogile ya Kilisito, nivika Mndewa kanivugulila nzila nimsang'hanile.

13 Lakini nikala moyo yungwa yungwa, kwavija simvikile ndugu yangu Tito. Avo niwalaga nichola Makedonia.

### *Kuhuma kubitila Kilisito*

14 Lakini, Mulungu yagweleligwe nhogolwa, yotulongoza mna ikibumbila cha kudeng'helela kuhuma kubitila Kilisito na kubitila tweye topwililisa kila hanhu usenga wa Kilisito kamba mnung'ho.

15 Kwavija tweye tuigala na mnung'ho unogile wa ubani ulavigwe na Kilisito kwa Mulungu, ukwenela kwa wanhu wose wokomboligwa na waja wopotela.

16 Kwa waja wopotela, mnung'ho awo wogala ifa, lakini kwa waja wokomboligwa, mnung'ho awo wogala ugima. Vino nani yofaya kwa sang'hano ayo?

17 Tweye hatuigalile na wanhu wayagwe, wopata sente kwa kuchuuza usenga wa Mulungu, tweye kwa kuilumba na Kilisito tolonga fulu ipile mgameso ga Mulungu, kamba wanhu tutumigwe na Mulungu.

# 3

### *Wasang'hanaji wa Lagano da Sambi*

1 Vino, tosonga kabili kuitogola wenyego? Hebu tolonda baluwa ya yandikigwe na mweye kututogola tweye hebu tuwandikila baluwa kuitogola wenyego kamba viwotenda wanhu wayagwe?

2 Mweye wenyego mwa baluwa yetu, yandikigwe mmizoyo yetu, baluwa ijuwike na kusomigwa na kila munhu.

3 Yolagusa kamba mweye mwa baluwa ya Kilisito yaigalile kwa makono getu. Baluwa ayo hayandikigwe kwa wino lakini yandikigwa kwa Loho wa Mulungu yeli mgima, hayandikigwe mdibwe ila mmizoyo ya wanhu.

4 Tweye hatunyawanyawa kulonga vino mgameso ga Mulungu, kwavija tomtamanila Kilisito.

5 Hatudaha kulonga tusang'hana chochose kwa udahi wetu wenyego, ila udahi wose tuli nao wolawa kwa Mulungu,

6 yatugwelele udahi wa kuwa wasang'hanaji wa lagano da sambi, siyo kwa malagizo gandikigwe, ila kwa Loho wa Mulungu. Kwavija malagizo gandikigwe gogala ifa, lakini Loho Yang'alile kogala ugima.

7 Malagizo gekigwa mgamabwe, na ukulu wa Mulungu woneka mbaka wanhu wa Izilaeli walemelwa kulola kihanga cha Musa hata mng'alo wa kihanga viukalile wovulala. Kamba malagizo gogala ifa gasang'hana na kugala ukulu kamba awo,

8 vino, sang'hano ya Loho Yang'alile haigala ukulu ubanzile ng'hani?

9 Kamba kukala na ukulu mna isang'hano igala kutagusigwa, avo sang'hano itutenda tunoge mgameso ga Mulungu yogala ukulu ubanzile ng'hani!

10 Kwa mbuli ayo, kija kikalile na ukulu aho haichanduso, sambi chaduhu ukulu mbuli ya kija kili na ukulu ubanzile ng'hani.

11 Kwavija kamba kija kikalile kwa kipindi kidodo kikala na ukulu, avo kija kikala siku zose chokuwa na ukulu ubanzile ng'hani!

12 Kwavija tweye totamanila avo, hatudumba kulonga.

13 Tweye hatuigalile na Musa yagubike kihanga chake kwa kikumbi muladi wanhu wa Izilaeli sekewone mng'alo viukalile wovulala.

14 Lakini nzewele zao zifungigwa, mbaka sambi wahasoma vitabu va lagano da umwaka nzewele zao zigubikigwa na kikumbi acho. Kikumbi acho hakisegezigwa mbaka munhu yailumbe na Kilisito.

15 Ona, mbaka sambi, wahasoma Malagizo ga Musa, nzewele zao zigubikigwa na kikumbi acho.

16 Lakini munhu yahambwelela Mndewa, kikumbi acho chosegezigwa.

17 Avo, "Mndewa," ayo Loho, na aho kuyali Loho wa Mndewa baho kuli na kulekesigwa.

18 Avo tweye wose, vihanga vetu havigubikigwe tuigala na kiyoo kulagusa ukulu wa Mndewa. Togalusigwa tuigale ng'hani na tuvike muukulu ng'hani. Ino ayo sang'hano ya Loho wa Mndewa.

# 4

*Ngama mzinongo*

1 Avo, Mulungu kwa bazi jake, katugwaa sang'hano ino, na tweye hatubwela kuchugu.

2 Tuzileka mbuli zose zigela kinyala na za kinyelegezi, hatulonga mbuli za uvizi hebu kuilonga vihile mbuli ya Mulungu. Lakini kwa kulonga ukweli mgameso ga Mulungu, muladi wayagwe watugese mmizoyo yao kamba totamaniligwa.

3 Avo kamba Mbuli Inogile ituwapetela wanhu ifisigwa, ifisigwa kwa hewo wopotela.

4 Hawatogola kwavija Mwenembago, mulungu wa isi ino kazigela nzewele zao mdiziza, muladi sekewawone mulenge wa Mbuli Inogile ya ukulu wa Kilisito, yaigalile na Mulungu kwa kila kinhu.

5 Kwavija hatuipetela wenyego, ila tompeta Kilisito yeli Mndewa na tweye twa wasang'hanaji zenu kwa Yesu.

6 Mulungu yalongile, “Mulenge umwemwese kulawa mdiziza!” Ayo yatendile mulenge wake umwemwese mmizoyo yetu, katugwelela mulenge wa nzewele za ukulu wa Mulungu mkihanga cha Yesu Kilisito.

7 Lakini tweye tuli na ngama ino tuigala na nongo, muladi kulagusa kamba nguvu ng'hulu yolawa kwa Mulungu, siyo kumwetu.

8 Siku zose togaya, lakini hatuhondigwa, tokona shaka, lakini hatubwela kukisogo,

9 todununzigwa, lakini hatulekigwa kutazigwa, tolagazigwa hasi, lakini hatubanangigwe bule.

10 Kipindi chose toisola ifa ya Yesu mzing'huli zetu, muladi ugima wa Yesu vivija woneke mzing'huli zetu.

11 Siku zose za ugima wetu twa mdizumozumo da ifa mbuli ya Yesu, muladi ugima wake woneke mzing'huli zetu zifa.

12 Avo, ifa yosang'hana mgati mmwetu, lakini ugima wosang'hana mgati mmwenu.

13 Maandiko Gang'alile golonga, “Nitogola lekaavo nonga.” Kwa kutamanila kukuja, na tweye vivija totogola lekaavo tolonga,

14 kwavija tojuwa kamba Mulungu yamzilibule Mndewa Yesu kwa wafile, vivija kotuzilibula tweye hamoja na Yesu, na kotwika tweye na mweye kuulongozi wake.

15 Kwavija gano gose kwa sama ya mweye, muladi ng'hekewa ya Mulungu iwavikile wanhu bwando, itende wamtogole Mulungu na wamgwelele ukulu.

### *Kukala kwa kumtamanila Mulungu*

16 Lekaavo hatubwela kuchugu. Hata kamba ng'huli zetu zofa, lakini siku zose loho zetu zotendigwa za sambi.

17 Magayo gotupata gabuha na gokala kwa kipindi kidodo, lakini gotugalila ukulu wa mazuwa gose kubanza gago gamagayo.

18 Avo sambi tugese vinhu vikoneka, ila tugese vija havikoneka. Kwavija vinhu vikoneka vokala kwa kipindi kidodo, lakini vija havikoneka vaduhu uhelelo.

## 5

1 Kwavija tojuwa kamba kiheha kitukala mwiisi ino, awo lukuli lwetu, chahabanangika Mulungu kotuvaza kae iyagwe ako kuulanga, kae ilibule uhelelo haizengigwe kwa makono ga wanhu.

2 Lakini sambi togutilila, kipindi vitubeta kwa kusulukila tugweleligwe lukuli lwa kuulanga,

3 kwavija twahavazigwa lukuli lwa sambi, hatukoneka twa mwazi.

4 Vitukala mkiheha kino cha mwiisi, togutilila kwa lusikisiki, kwavija hatulonda kululeka lukuli luno lwa mwiisi, lakini tolonda kuvazigwa kae yetu ya kuulanga, muladi kija kifa kigalusigwe na ugima wa mazuwa gose.

5 Mulungu mwenyego ayo yatutandile gano gose. Katugwaa Loho wake kamba fungu dodo da gaja gayatwikile.

6 Avo siku zose togangamala. Tojuwa kamba vitukala mzing'huli zino, twa kutali na kae yetu hamoja na Mndewa.

7 Kwavija tokala kwa kumtamanila Mulungu, siyo kwa gaja gotulola.
8 Lakini togangamala na tolonda kululeka ukazi uno wa lukuli na kukala hamoja na Mndewa.
9 Mbuli ng'hulu, towamba ng'hani kumnogeza Mndewa, iwe tokala mwiisi ino hebu kuulanga.
10 Kwavija kila munhu kokwima kuulongozi wa Kilisito yatagusigwe. Kila munhu kobokela kija kiyolondeka, kamba vija viyasang'hane mwiisi, kamba ganoga hebu geha.

### *Umbwiga na Mulungu kubitila Kilisito*

11 Tweye tojuwa choni kumdumba Mndewa, avo towamba kuwatewenza wanhu wayagwe. Mulungu kotujuwa goya, na niye nogesa kamba mweye vivija munjuwa mmizoyo yenu.
12 Tweye hatugeza kuitogola kabili kumwenu. Lakini towagwaa kila-muso kinogile mweye muigodele tweye, muladi mudahe kuwedika waja woigodela vija vikoneka na woleka vija vili mmizoyo.
13 Kamba tokoneka twaduhu nzewele, mbuli ya Mulungu na kamba tuna nzewele, mbuli ya mweye.
14 Tolongozigwa na unogelwa wa Kilisito, sambi tojuwa munhu imoja kafa mbuli ya wanhu wose, avo wose wafa nayo.
15 Kafa mbuli ya wanhu wose, muladi wanhu wokala sekewakale wenyego, lakini wakale mbuli ya heyo yafile na kazilibuligwa mbuli ya hewo.
16 Avo kulawa sambi, hatumgesa munhu kwa kumulola. Hamoja hana kipindi tumgesa Kilisito kwa kumulola, sambi hatutenda vivo kabili.
17 Munhu yoyose yahailumba na Kilisito kotendigwa wa sambi, ga umwaka gabita, ga sambi geza.
18 Gano gose golawa kwa Mulungu, yatutendile tuilumbe nayo kubitila Kil-isito na katugwelela sang'hano ya kuwatenda wanhu wayagwe wailumbe nayo.
19 Avo, kubitila Kilisito Mulungu kailumba na wanhu wa mwiisi, hagesile nzambi zao, katugwaa usenga wa kuwapetela wanhu wailumbe nayo.
20 Avo, tweye tolonga mbuli ya Kilisito, kubitila tweye Mulungu kowapula mweye. Towapula kwa twaga da Kilisito, muilumbe na Mulungu.
21 Mulungu kamtenda ija yeliduhu nzambi yasole nzambi zetu, muladi kubitila heyo Mulungu yatutende tunoge mgameso gake.

# 6

1 Kwavija tosang'hana hamoja na Mulungu, towapula mweye mubokele ng'hekewa ya Mulungu, sekemutogole yage bule.
2 Mulungu kolonga,
“Kipindi kinogile vikivikile cha kukonela bazi,
nikutegeleza,
kipindi cha kukukombola vikivikile,
nikutaza.”
Tegelezeni! Sambi acho kipindi kinogile, lelo dijo siku da kukomboligwa!
3 Hatulonda kumwikila munhu yoyose ng'hwalo, muladi sang'hano yetu sekeilongigwe vihile.
4 Avo toilagusa kamba kweli twa wasang'hanaji wa Mulungu kwa kila kinhu, kwa kufunga umoyo na kwa kugaya na kwa kipindi kidala na kwa madununzo,

5 kwa kutoigwa na kwa kugodekigwa mkifungo na kwa kuding'huligwa
na kwa kusang'hana ng'hani na kwa kuwasa meso na kwa nzala.
6 Tuilagusa twa wasang'hanaji zake kwa kung'ala kwetu na kwa nzewele
na kwa kubetela na kwa moyo unogile na kwa Loho Yang'alile na unogelwa
wa ukweli,
7 na kwa kulonga ukweli na kwa nguvu ya Mulungu. Totenda goyolonda
Mulungu kamba mgoha wetu wa kuitowela na kuigombela wenyego.
8 Totenda kwa kutegelezigwa na kugeligwa kinyala, tolongigwa vinogile
na tolongigwa vihile, tolongigwa twa wavizi, lakini tolonga ukweli.
9 Tojuwika, lakini totendigwa kamba hatujuwika, tokoneka tofa, lakini
tung'hali wagima, tutoigwa lakini hatukomigwe bule.
10 Tunyunyuwala lakini siku zose todeng'helela, twa wakiwa lakini towa-
tenda wanhu bwando wawe wagoli, tokoneka tuduhu kinhu lakini kila
kinhu chetu.
11 Ndugu zetu Wakolinto! Tulonga na mweye vinogile, mizoyo yetu
yaduhu lusikisiki.
12 Tweye tuduhu lusikisiki na mweye, lakini mweye muna lusikisiki na
tweye.
13 Sambi nolonga na mweye kamba wanangu, sekemuwe na lusikisiki
mmizoyo yenu kamba tweye vitutendile.

### *Paulo kowazuma sekewailumbe na wanhu hawamtogole Yesu*

14 Sekemuilumbe na wanhu hawamtogola Yesu. Vino ganogile na gehile
gana umbwiga gani? Hebu yodahikaze mulenge na ziza kukala hamoja?
15 Vino Kilisito na Mwenembago woilumbaze? Vino munhu yomtogola
Kilisito koilumbaze na ija hamtogola Kilisito?
16 Vino Ng'anda ya Mulungu yoilumbaze na vinyago? Avo tweye twa
Ng'anda ya Mulungu yeli mgima! Kamba viyalongile Mulungu mwenyego,
“Nokala nao
na kutembela hamoja nao.
Niye nokuwa Mulungu wao,
na wao wokuwa wanhu zangu.”
17 Avo Mndewa kolonga,
“Segeleni kumwao
na mwiinege nao.
Sekemukwase kinhu kili na dikwe,
na niye nowabokela mweye.
18 Nokuwa Tataenu,
na mweye mokuwa wanangu wa kimbigalo na wa kitwanzi,
kolonga Mndewa yeli na Udahi wose.”

## 7

1 Mbwiga zangu niwanogela, gaja gose gayalongile Mulungu ni mbuli
ya tweye. Avo tusunhe dikwe da ng'huli zetu hebu mizoyo yetu, tung'ale
ng'hani na tumtegeleza Mulungu.

### *Deng'ho da Paulo*

2 Twikeni mmizoyo yenu. Hatumtendele gehile munhu yoyose, hatumu-
lumize hebu kumnyonya munhu yoyose.
3 Silonga mbuli zino kwa kumtagusa munhu, kamba vinongile, mweye
mwa mmizoyo yetu, tufe hamoja hebu tuwe wagima hamoja.
4 Nojuwa mugangamala, noigodela mweye! Nihozigwa moyo ng'hani
kipindi chose cha magayo getu, nodeng'helela ng'hani.

5 Hata vituvikile Makedonia, hatubwihile bule. Kila mwambu tukala na magayo, kunze migomvi na mizoyo yetu imema bwembwe.

6 Lakini Mulungu yowahoza mizoyo wanhu wokala moyo nyunguwaa, katuhoza mizoyo viyezile Tito kumwetu.

7 Siyo kwiza kwake kwiiyeka, lakini vivija mbuli ya mweye vimumuhozile umoyo. Nayo katulongela vimusulukila kunyona na vimunyunyuwale kwa gaja galawilile, na vija vimulonda kunigombela, avo nodeng'helela ng'hani.

8 Hata kamba kwa baluwa yangu ija niwatenda munyunyuwale, sigelegeza habali nhendile vivo. Nogesa baluwa ija iwatenda munyunyuwale, lakini kwa kipindi kidodo.

9 Sambi nodeng'helela, siyo kwavija munyunyuwala, lakini kwavija kunyunyuwala kwenu kuwatenda muleke nzambi na mumbwelela Mulungu, na Mulungu kakusang'hanila kunyunyuwala kuko, avo hatuwalumize bule.

10 Kwavija kunyunyuwala kulawaga kwa Mulungu kotenda wanhu waleke nzambi muladi wakomboligwe, avo hailondeka kona usungu kwa mbuli ayo. Lakini kunyunyuwala kwa mwiisi kogala ifa.

11 Loleni, viyatendile Mulungu kubitila kunyunyuwala kwenu, sambi mowamba ng'hani, modaha kulagusa kamba munoga. Mokona usungu mwahagona gehile gosang'hanwa, mosinhuka na kudumba, mosulukila ganogile, muilava kwa kusang'hana, molonda kona ganogile gotendeka. Kwa kila mbuli muilagusa mduhu gehile.

12 Avo, hamoja nyandika baluwa ija, sandike mbuli ya munhu yatendile gehile hebu mbuli ya munhu yatendeligwe gehile. Lakini nyandika muladi yoneke mgameso ga Mulungu, vija mweye vimuwambile kutusang'hanila.

13 Lekaavo tweye tuhozigwa mizoyo.

Siyo kuhozigwa umoyo kwiiyeka, lakini vivija tudeng'helela vitumone Tito kana deng'ho, mbuli ya kumuhoza moyo kwenu.

14 Mbuli ya mweye niye niigoda ng'hani kumwake, na hamungelile kinyala bule. Siku zose tuwalongela ukweli, na vivija kuigoda kwetu kwa Tito mbuli ya mweye kulagusa ukweli wiiyeka.

15 Avo unogelwa wake kumwenu wokongezeka ng'hani, yahakumbuka vimugagogile mafundizo gake, na vija vimumbokele kwa bwembwe na kugwaya.

16 Sambi nodeng'helela ng'hani kwavija nodaha kuwatamanila ng'hani!

# 8

*Kulava kwa moyo unogile*

1 Ndugu zetu, tolonda mujuwe, Mulungu viyavigwelele ng'hekewa vibumbila va wanhu wamtogole Kilisito ako Makedonia.

2 Wanhu awo wagaya ng'hani, lakini deng'ho jao dikala kulu, na wakala na moyo wa kulava vinhu vao hamoja wakiwa ng'hani.

3 Nowalongela ukweli, walava ng'hani, na walava kubanza viwadahile. Kwa kulonda wenyego,

4 watupula ng'hani vivija na wao wengile mwiisang'hano ino inogile ya kuwataza wanhu wa Mulungu.

5 Wasang'hana kubanza vitugesile! Tanhu wailava wenyego kwa Mndewa, abaho wailava kumwetu, kamba viyalondile Mulungu.

6 Avo tumpula Tito yaisongile sang'hano ino ya kulava kwa moyo unogile, vivija yawataze kuimambukiza kumwenu.

7 Mweye mna vinhu bwando, kumtamanila Mulungu, ulonzi unogile, nzewele, kuwamba ng'hani kutenda ganogile na unogelwa wenu kumwetu.

Avo vivija towalonda mweye muwe na moyo unogile ng'hani mwi-
isang'hano ino ya kulava.
8 Niye siwagwaa lagizo bule, lakini nolonda kuwalagusila mweye
wayagwe viwowamba kuwataza wanhu, muladi nijuwe unogelwa wenu
viwili wa ukweli.
9 Kwavija muijuwa ng'hekewa ya Mndewa wetu Yesu Kilisito, hamoja
kakala na kila kinhu, lakini kaitenda mkiwa mbuli yenu mweye, muladi
kubitila ukiwa wake mweye muwe na kila kinhu.
10 Kwa mbuli ino, niye vinigesa vinoga mweye mwahamambukiza gaja
gamusongile mwaka ubitile. Mweye mukala wanhu wa ichanduso siyo
kulava kwiiyeka, lakini vivija kwa moyo wa kulonda kulava.
11 Avo mambukizeni sang'hano ayo ya kulava kwa moyo unogile, kamba
vija vimusulukile ng'hani kuisang'hana, avo isang'haneni sambi kwa kija
kimulinacho.
12 Kamba munhu kana moyo wa kulava, Mulungu kobokela kija kiyalina-
cho, halola kija kiyeduhu.
13 Niye silonda kuwadikwa mweye mizigo abaho wayagwe wabwihile,
lakini mweye mose muwe sawa.
14 Vinhu vingi vimulinavo sambi viwataze waenu waliduhu, muladi na
wao vonda wawe na vinhu vingi viwataze mweye kipindi mduhu kinhu.
Baho mose mokuwa sawa.
15 Kamba Maandiko Gang'alile vigolonga, “Ija yakubile kingi hapatile
kingi ng'hani, na ija yasolile kidogo hahungukilwe kinhu.”

### *Tito na wayage*

16 Nomgwaa nhogolwa Mulungu kwa kumgwaa Tito moyo wa kuwataza
mweye kamba moyo unilinao niye!
17 Siyo kwavija tweye tumulongela, lakini vivija kakala kosulukila ng'hani
kuwataza, kwa kulonda mwenyego keza kumwenu.
18 Tomtuma ndugu imoja hamoja nayo, yotegelezigwa ng'hani mna
ivibumbila vose va wanhu wamtogole Yesu, kwa sang'hano yake ya
kuwapetela wanhu Mbuli Inogile.
19 Vivija, ndugu ayo kasaguligwa na vibumbila va wanhu wamtogole Yesu
yange na tweye kipindi vitugala sente zino, sente zigala ukulu kwa Mndewa
na zilagusa moyo wetu wa kuwataza wanhu.
20 Toitiganya wanhu sekewatuyalalile vitwika hamoja na kugola sente
zino zilavigwe kwa moyo unogile.
21 Tweye tolonda kusang'hana ganogile siyo mgameso ga Mndewa
yaiyeka, lakini vivija mgameso ga wanhu.
22 Vivija tomtuma hamoja nao ndugu yetu, miyanza mingi tumgeza na
tumona kana moyo wa kuwataza wanhu. Sambi kana moyo wa kuwataza
ng'hani wanhu kwavija kowatamanila mweye ng'hani.
23 Tito ayo miyangu, tosang'hana hamoja mbuli ya mweye. Ndugu zetu
wayagwe wokwiza hamoja nayo, wao wasenga wa vibumbila va wanhu
wamtogole Yesu na wogala ukulu kwa Kilisito.
24 Avo walagusileni unogelwa wenu, muladi vibumbila va wanhu wamto-
gole Yesu wajuwe totenda goya vituigodela mweye.

## 9

### *Kuwataza wakilisito waetu*

1 Silondeka kuwandikila mbuli ya sang'hano ya kuwataza wanhu wa
Mulungu.

2 Nowajuwa vimuwamba kuwataza wanhu, niye niigodela mbuli ayo kwa wanhu wa Makedonia. Niwalongela toka mwaka ubitile mweye wanhu wa Akaya muitanda kulava, moyo wenu wa kulava uwatenda wanhu bwando watende vivo.
3 Avo nowatuma ndugu wano, muladi kuigoda kwetu mbuli ya mweye sekekuwe mulomo wiiyeka. Lakini muitande kuwataza, kamba viniwalongele wao motenda.
4 Kwavija kamba naheza na munhu wa Makedonia na twahawavika hamuitandile, baho tweye togwa kinyala kwavija tuigodela ng'hani mweye. Na mweye vivija mogwa kinyala kwavija tuwatamanila ng'hani!
5 Avo nigesa vinoga kuwapula ndugu wano wanongolele kwiza kumwenu, waitande nhunza yenu ng'hulu yumulongile moilava. Baho yolagusa kuwa nhunza ayo yolavigwa kwa kulonda mweye wenyego, siyo kwa kunanahizigwa.
6 Kumbukeni, munhu yohanda kidogo kosenga kidogo. Munhu yohanda vingi kosenga vingi.
7 Kila munhu kamba viyagesile muumoyo wake yalave kija kiyalinacho, siyo kwa moyo hamgwazo hebu kunanahizigwa, kwavija Mulungu komnogela munhu yolava kinhu kuno moyo kwatu!
8 Avo Mulungu kodaha kuwagwaa vingi ng'hani kubanza vija vimulonda, siku zose mpate kila kinhu kimulonda, avo muvisang'hanile kwa kila sang'hano inogile.
9 Kamba vigalonga Maandiko Gang'alile,
“Kowagwaa kwa moyo unogile wanhu wakiwa
na moyo wake unogile waduhu uhelelo.”
10 Nayo Mulungu yomgwaa mbeyu mulimaji na lujo, vivija kowagwaa mweye mbeyu zimulonda, na kozitenda zote, zikule na zilele ng'hani mbuli ya kulava kwenu kwa mizoyo yenu inogile.
11 Kowatenda muwe wagoli siku zose kwa kila kinhu, mudahe kuwa na moyo unogile kipindi chose, muladi wanhu wamgwee nhogolwa Mulungu mbuli ya nhunza zenu ziwabokele kubitila tweye.
12 Kwavija sang'hano ino yumutenda siyo tu yowataza wanhu wa Mulungu, lakini vivija yowatenda wanhu bwando wamgwee nhogolwa ng'hani Mulungu.
13 Kwa mbuli zinogile zilagusigwa kwa sang'hano yenu ino, wanhu bwando womgwaa nhogolwa Mulungu mbuli ya kuigoga kwenu Mbuli Inogile ya Kilisito yumuitogola, na mizoyo yenu inogile ya kulava vinhu venu kumwao na kwa wanhu wose wayagwe.
14 Avo mizoyo yao yowanogela na wowapulila mweye mbuli ya ng'hekewa ng'hulu iyawagwelele Mulungu.
15 Tumgwee nhogolwa Mulungu mbuli ya nhunza yake iswelile ulonzi wa kuisimulila!

# 10

*Paulo koigombela sang'hano yake*

1 Niye Paulo mwenyego, wanhu wayagwe wolonga namuhole kipindi nahawa na mweye, lakini nahawa kutali na mweye namsabalu. Nowapula kwa bazi na moyo unogile wa Kilisito,
2 vondanize sekemunhende niwe msabalu, kwavija nojuwa nodaha kuwa msabalu kwa waja wolonga tokala kamba viwokala wanhu wa mwiisi ino.
3 Ona, tokala mwiisi, lakini hatuitowa kamba viwoitowa wanhu wa mwiisi.

4 Silaha zituitowela tweye siyo silaha za mwiisi ino, lakini nguvu ya Mulungu, itulaga ng'hambi zose. Tobananga mbuli zose za uvizi,
5 togabananga magoda gose gotenda viyagwe na nzewele ya kumjuwa Mulungu. Togaboka magesa gose na kugatenda gamtegeleze Kilisito.
6 Mwahagoga kila kinhu, tweye tuitanda kumtagusa munhu yoyose yoleka kugoga.
7 Mweye molola mbuli za kunze. Kamba munhu yoyose kogesa heyo munhu wa Kilisito, kolondeka yagese kabili kuwa tweye twa wanhu wa Kilisito kamba viyali heyo.
8 Niye sikona kinyala hata kamba nibanza kuigoda mbuli ya udahi uyatugwelele Mndewa, katugwaa udahi wa kuwazenga mweye siyo wa kuwabomola.
9 Silonda mweye mugese nolonda kuwagela bwembwe kwa baluwa zangu.
10 Kwavija wolonga, “Baluwa za Paulo zizama na zimema mbuli ng'hulu, lakini yahawa hamoja na tweye konyolila, na ulonzi wake siyo kinhu chochose!”
11 Wanhu kamba awo wolondeka wajuwe kuwa vose vibili sawa, gaja gatwandika kipindi twahawa kutali na gaja gonda tusang'hane twahawa hamoja na mweye.
12 Tweye hatudaha kuika hamoja hebu kuigala na wanhu waja woitogola wenyego. Wanhu woitenda wenyego kinhu cha kupimila na wanhu woilinga wao kwa wao, wanhu awo waduhu nzewele!
13 Lakini tweye hatuigoda ng'hani, kuigoda kwetu kokuwa mna isang'hano iyatugwelele Mulungu, vivija sang'hano ayo, iyo itusang'hana kumwenu.
14 Tweye hatunabanza kuigoda, kamba vija hatunakwiza kumwenu, kwavija tweye twiza kumwenu na tuwagalila Mbuli Inogile ya Kilisito.
15 Avo tweye hatubanza kuigoda mbuli ya sang'hano itendigwe na wanhu wayagwe. Lakini tololela kuwa kumtamanila kwenu Mulungu kogendelela na sang'hano yetu kumwenu yokuwa ng'hulu kwa kukweleleza viyolonda Mulungu.
16 Abaho todaha kuipeta Mbuli Inogile mziisi ziyagwe, zili kutali na mweye. Kwavija hatulonda kuigodela sang'hano imalile kusang'hanigwa na munhu iyagwe hanhu aho.
17 Lakini, kamba vigolonga Maandiko Gang'alile, “Munhu yolonda kuigoda, yaigodele kija kiyasang'hane Mndewa.”
18 Kwavija munhu yotogoligwa siyo ija yoitogola mwenyego, lakini ija yotogoligwa na Mndewa.

# 11

*Paulo na watumigwa wavizi*

1 Nogesa mofunga umoyo mbuli ya niye, hata kamba nokoneka nambozi, sekemutonge ng'hani!
2 Nowonela migongo, kamba Mulungu viyowonela migongo, mweye muigala na mhambe inimtandile yafungiligwe zengele na mbigalo imoja, nayo ayo Kilisito.
3 Lakini nodumba kamba dija dizoka kwa ubala wake wa uvizi viyamvizile Hawa, nzewele zenu zodaha kugalusigwa na moleka kung'ala kwenu na kuilava kwenu kweli kwa Kilisito.
4 Kwavija munhu yoyose yokwiza kumwenu na kuwapetela usenga wa Yesu hauigalile na uja utuwapetele mweye mombokela, na moitogola loho

iyagwe haiigalile na Loho Yang'alile yumumbokele na moutogola usenga uyagwe hauigalile na Mbuli Inogile yumubokele kumwetu.

5 Niye sigesa kuwa na mdodo kubanza awo woikema, “Watumigwa wakulu.”

6 Sengine nokoneka sili mulongaji goya, lakini nzewele ninazo, mbuli ino tuilagusa goya siku zose na kipindi chose.

7 Vino niye nhenda vihile, viniitendile mwenyego sifaya na kuwatenda mweye mufaye, kwa kuwapetela Mbuli Inogile ya Mulungu na silondile fungu jojose?

8 Vinikalile nowasang'hanila mweye, fungu jangu dilawa mna ivibumbila viyagwe va wanhu wamtogole Yesu. Avo kamba vija niwaboka vinhu vao muladi niwasang'hanile mweye.

9 Ving'halile na mweye simgazile munhu yoyose yangwee chochose kinonda, kwavija ndugu walawile Makedonia wangalila kila kinhu kinondile. Kamba vija vindekile kuwagaza kwa kinhu chochose, avo nogendelela kutenda vivo!

10 Kamba vija ukweli wa Kilisito viuli mgati mmwangu, kuduhu munhu yoyose mwiisi ya Akaya yodaha kunhenda sekeniigodele mbuli ayo.

11 Vino niye nolonga vino kwavija siwanogela bule? Mulungu kojuwa kuwa nowanogela!

12 Nogendelela kusang'hana kamba vinisang'hana sambi, muladi niwagwise waja “watumigwa wakulu” wolonga kwa kuigoda kuwa wosang'hana kamba vitusang'hana tweye.

13 Kwavija wanhu awo siyo watumigwa wa ukweli, wasang'hanaji wavizi, woitenda kuwa watumigwa wa Kilisito.

14 Ona, mbuli ino siyo kilozo! Kwavija hata Mwenembago mwenyego koitenda msenga wa mulenge kulawa kuulanga!

15 Avo hatukanganya bule kamba wasang'hanaji wa Mwenembago nao woitenda wasang'hanaji wa gaja ganogile. Kukimambukizo wobokela fungu jao dilondeka kwa sang'hano zao.

### *Kugaya kwa Paulo kamba mtumigwa*

16 Nolonga kabili, munhu sekeyanhende niye nambozi. Lakini yahanhenda mbozi, yanibokele kamba mbozi muladi naniye niigode kidogo.

17 Mbuli ino inonga sambi silagilizigwe na Mndewa nonge, mbuli ino ya kuigoda, nolonga kamba munhu mbozi.

18 Kwavija wanhu bwando woigodela mbuli za kiunhu, naniye vivija notenda vivo.

19 Kwavija mweye mna nzewele, lekaavo mokala kwa kufunga umoyo na wanhu wabozi.

20 Mweye mokala kwa kufunga umoyo hata munhu yowatenda watumwa, hebu yowanyonya hebu yopata vinhu kwa migongo yenu hebu yowehula hebu yowazaba mkihanga.

21 Nokona kinyala kulonga tweye tunyolila kusang'hana mbuli azo!

Nolonga kamba munhu mbozi, kamba munhu yoyose kogeza kuigodela kinhu, naniye vivija sidumba kuigodela.

22 Kamba wao Waebulania? Naniye vivija na Muebulania. Kamba wao Waizilaeli? Naniye vivija na Muizilaeli. Kamba wao wolawa mulukolo lwa Abulahamu? Naniye vivija nolawa mulukolo lwa Abulahamu.

23 Kamba wao wasang'hanaji wa Kilisito? Nolonga kamba munhu yeli na kibozi mbwelela, niye na msang'hanaji wa Kilisito kubanza awo! Niye nisang'hana sang'hano ndala ng'hani, ngodekigwa mkifungo miyanza

bwando, nhoigwa miyanza bwando, ng'hala mdizumozumo da ifa miyanza
bwando.
24 Miyanza mitano Wayahudi wanhowa mbalati malongo madatu na tisa.
25 Miyanza midatu Walumi wanhowa mbalati, mwanza umoja wanhowa
mabwe. Miyanza midatu mbenekeligwa na ngalawa ng'hulu mbahali na
mwanza umoja nisinda mgamazi imisi na ikilo.
26 Mna imiyanza yangu ng'hala mdizumozumo da kusoligwa na mazi
ga lwanda, ng'hala mdizumozumo da wabokaji, ng'hala mdizumozumo da
wayahudi wayangu, ng'hala mdizumozumo da wanhu haweli Wayahudi,
ng'hala mdizumozumo kudibuga, ng'hala mdizumozumo da kumuhulo,
ng'hala mdizumozumo mbahali na ng'hala mdizumozumo da ndugu wa
uvizi.
27 Nisang'hana na kugaya, ng'hala meso miyanza mingi, ng'hala na nzala
na ng'hilu na miyanza mingi nisinda na nzala, ng'hala nokona beho na
ng'hala nabule viwalo.
28 Kubanza avo vose, siku zose nina ng'honde ya kuvisang'hanila vibum-
bila va wanhu wamtogole Yesu.
29 Kamba munhu konyolila, naniye vivija nonyolila. Kamba munhu
katenda nzambi, naniye nokona usungu.
30 Kamba nahaigoda, noigodela kunyolila kwangu.
31 Mulungu, Tata wa Mndewa Yesu, yotogoligwa siku zose, kojuwa niye
siviza bule.
32 Ving'halile ako Damesiki, mkulu wa isi, yakalile yolongozigwa na
mndewa Aleta, keka wakalizi kudibuga da Damesiki muladi wangoge.
33 Lakini nihumulusiligwa mdigelo, kubitila zonzo dikalile muuluwa, vino
vivo vinihonyeke mmakono gake.

# 12

### *Vinhu viyalagusiligwe Paulo na kugubuliligwa na Mndewa*

1 Nolonda kuigoda, hamoja haifaya chochose. Lakini sambi nolonga mbuli
ya vinhu viyanilagusile Mndewa na kunigubulila.
2 Nomjuwa munhu imoja Mkilisito, miyaka longo na nne ibitile kagaligwa
mbaka kuulanga. Sijuwile bule kamba kakala ako na lukuli hebu na loho,
Mulungu heyo yajuwile.
3 Nolonga kabili, nojuwa munhu ayo kagaligwa kuulanga, lakini sijuwa
bule kamba kakala mulukuli hebu siyo mulukuli, Mulungu kojuwa.
4 Kuko kuulanga kahulika mbuli hazidahika kusimulila, mbuli azo munhu
halondeka kuzilonga.
5 Avo noigodela munhu kamba ayo, lakini siigodela mwenyego, ila mbuli
za kunyolila kwangu.
6 Maza nondile kuigoda, sambi niwe mbozi, kwavija nahalongile ukweli.
Lakini siigoda kwavija silonda munhu yangese ng'hani kubanza vija viyony-
ona na kuhulika vinilonga.
7 Lakini kunhenda niye sekeniigode ng'hani mbuli ya vinhu vingi viyan-
gubulile Mndewa, nigweleligwa usungu mulukuli kamba mwiba, msenga
wa Mwenembago kanhowa, muladi sekeniigode ng'hani.
8 Nimpula Mndewa miyanza midatu yanisegezele mbuli ayo.
9 Lakini Mndewa kanongela, “Ng'hekewa yangu kumwako gweye yotosha,
kwavija udahi wangu wokuwa mkulu ng'hani gweye wahanyolila.” Avo
nodeng'helela ng'hani kuigodela kunyolila kwangu, muladi udahi wa Kil-
isito ukale kumwangu.

10 Avo niye nodeng'helela kunyolila, kuligigwa, kuzehigwa, kugaya na
madununzo mbuli ya Kilisito. Kwavija nahanyolila, baho nogangamala.

*Paulo viyowagesa Wakolinto*

11 Niye niitenda nambozi, lakini mweye wao munhendile niwe vivo.
Mweye wao mulondeke kungwaa nhogolwa. Kwavija hata kamba niye
sifaya, sili mdodo bule kubanza awo woikema, "watumigwa wakulu."
12 Unzonza na vifukuzi vitendeke kumwenu kwa kufunga umoyo vilagusa
goya kuwa niye na mtumigwa.
13 Vino mweye muswela choni kubanza vibumbila viyagwe va wanhu
wamtogole Yesu, lakini niye siwagazile mweye munitaze? Chonde, geleni
kumgongo kwa kuwatendela vihile!
14 Sambi niitanda kwiza kumwenu kwa mwanza wa kadatu, na silonda
kuwagaza bule, kwavija niye nowalonda mweye siyo vinhu vimulinavo.
Siku zose tata na mama wowekila ngama iwana na siyo iwana wowekila
ngama tata zao na mama zao.
15 Niye nodeng'helela kulava vinhu vose vinilinavo na vivija kuilava
mwenyego mbuli ya kuwataza mweye. Vino mweye hamuninogela ng'hani
kwavija niye nowanogela ng'hani?
16 Motogola kuwa siwagazile bule. Lakini munhu iyagwe kodaha kuwa-
longela kwavija niye na mbala ng'hani niwavizila.
17 Vino niye niwanyonya mweye kubitila msenga yoyose inimtumile
kumwenu?
18 Niye nimpula Tito yeze kumwenu, na nimtuma ndugu yetu weze
hamoja. Vino Tito kawanyonya? Vino mweye hamujuwile bule kuwa tweye
tolongozigwa na moyo umoja na tosang'hana hamoja?
19 Modaha kulonga kuwa tweye toigombela wenyego kumwenu! Lakini
tweye tolonga mbuli zino mgameso ga Mulungu, kuno tuilumba na Kilisito.
Mbwiga zangu, kila kinhu kitusang'hana, tosang'hana kuwagangamiza mw-
eye.
20 Nodumba naheza kumwenu, honda niwavike kamba vinonda niye, na
mweye honda mumbone kamba vimulonda niye niwe. Nodumba nodaha
kuvika wanhu wogomba hebu kuyonela migongo hebu kuigevuza hebu
kuwa na gahigahi hebu kuideta hebu kuiliga hebu kuigoda na kuiding'hula.
21 Nodumba naheza kumwenu kabili, Mulungu wangu konhenda niwe
muhole mgameso genu, nowalilila wanhu bwando watendile nzambi aho
haichanduso, lakini hawalekile uchafu wao, kusulukila kwihile na ugoni.

# 13

*Paulo komambukiza kwa kuwazuma na kuwalamusa*

1 Uno wokuwa mwanza wangu wa kadatu kwiza kumwenu. Kamba
Maandiko Gang'alile vigalonga, "Kitala chochose cholondeka choneke na
wanhu wabili hebu wadatu."
2 Ving'halile na mweye muumwanza wangu wa kabili niwazuma, na
sambi nowazuma kabili ning'hali kutali, kipindi naheza honda niwonele
bazi waja watendile nzambi aho umwaka hebu munhu yoyose iyagwe.
3 Mweye wenyego molola kamba Kilisito kolonga mgati mmwangu.
Kumwenu mweye Kilisito hanyekile, lakini kolagusa nguvu zake kumwenu.
4 Kwavija hata kamba kawambigwa mumsalaba kwa kunyolila, lakini
sambi mgima kwa nguvu ya Mulungu. Na tweye vivija tonyolila kwa
kuilumba nayo, lakini kwa nguvu ya Mulungu twa wagima hamoja nayo
muladi tuwasang'hanile mweye.

5 Muilolese wenyego mujuwe kamba momtamanila Mulungu. Muigeze
wenyego. Vino mweye hamujuwile kuwa Yesu Kilisito kokala mgati
mmwenu? Kamba haili avo, mweye mulemelwa.
6 Lakini notogola mweye mojuwa kuwa tweye hatulemelwe bule.
7 Avo tompula Mulungu sekemutende mbuli yoyose ihile. Siyo kamba
tolonda wanhu watugese tweye tuhuma, lakini mweye mutende ganogile
hata kamba tweye tokoneka tulemelwa.
8 Kwavija tweye hatudaha kuulema ukweli, lakini tougendeleza ukweli.
9 Todeng'helela kuwa tweye tunyolila, lakini mweye mugangamala, na
tompula Mulungu mutelele ng'hani.
10 Lekaavo, nowandikila mbuli zino ning'hali kutali, muladi naheza
kumwenu sekeniwe msede kwa kuusang'hanila udahi uyanigwelele Mn-
dewa, udahi wa kuwagangamiza siyo wa kuwabomola.
11 Avo ndugu zangu, nowalaga! Wambeni kukala mutelele, gogeni mbuli
zangu, muilumbe, kaleni moyo hole. Nayo Mulungu wa unogelwa na
tindiwalo kokuwa hamoja na mweye.
12 Muilamuse kwa nzila ilagusa moinogela.
13 Wanhu wose wa Mulungu wowalamusa.
14 Ng'hekewa ya Mndewa Yesu Kilisito na unogelwa wa Mulungu kwa
kuilumba na Loho Yang'alile, vikale na mweye mose.

# Baluwa ya Paulo kwa wanhu wa ako Galatia

## Ulongozi

Kitabu cha Wagalatia chandikigwa na Mtumigwa Paulo (Sula ya 1:1). Baluwa ino Paulo kawandikila vibumbila va wanhu wamtogole Yesu ako Galatia hagati ya mwaka wa 48-57 toka kuvumbuka kwa Kilisito. Wagalatia wogesigwa awo wanhu wakalile ako Lumi mwiisi ya Galatia. Wanhu woifunza mbuli hawajuwile bule kamba Paulo kakala kwahi viyandike baluwa ino, lakini yogesigwa sengine kayandikila Efeso hebu Kolinto.

Paulo kawandikila wanhu wamtogole Yesu, wose Wayahudi kwa wanhu haweli Wayahudi mna ivibumbila va wanhu wamtogole Yesu ako Galatia. Kandika baluwa ino kuwalemela wafundiza wavizi walongile wanhu wamtogole Yesu wolondeka kukweleleza malagizo ga Wayahudi kulawa mna idilagano da umwaka, ng'hani ng'hani kwingila kumbi. Kukala na kibumbila cha wanhu mna iwanhu wamtogole Yesu kikemigwe Wayuda walondile wanhu haweli Wayahudi wamtogole Yesu wengile kumbi. Vivija walonga Paulo hakalile Mtumigwa bule, Paulo kaigombela mbuli ya utumigwa wake kwa kulonga mbuli zake za umwaka (Sula ya 1:11-2:14) na kaigombela Mbuli Inogile kwa kusimulila wanhu wokomboligwa kwa kumtamanila Yesu Kilisito (Sula ya 2:16). Ino yolawilila kwa bazi da Mulungu na siyo kija kiwosang'hana wanhu.

**Mbuli zili mkitabu**

Paulo kosonga baluwa yake kwa kuwalamusa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu ako Galatia (Sula ya 1:1-5).

Abaho Paulo kosimulila mbuli zake ziyagwe za kukisogo muladi kuigombela viilondeka kumwake kuwafundiza wanhu na kolonga viyagezile kukala kwa kukweleleza malagizo lakini mbuli ayo haitendile chochose (Sula ya 1:6-2:21).

Abaho kosimulila sang'hano ya malagizo na ng'hekewa mna uukombozi (Sula ya 3-4).

Abaho kolonga mbuli ya malagizo gayagwe mbuli ya viilondeka kukala kwa wanhu wamtogole Yesu (Sula ya 5:1-6:10).

Paulo komambukiza baluwa yake kwa kuwalamusa na kowapula wakumbuke Mulungu kiyagaluse mgati ya munhu kinoga ng'hani kubanza malagizo ga lukuli, kamba vija kwingila kumbi (Sula ya 6:11-18).

1 Niye Paulo, namtumigwa, sikemigwe hebu kutumigwa na wanhu, lakini nhumigwa na Yesu Kilisito na Mulungu Tata, yamzilibule Yesu kwa wafile.

2 Ndugu wose weli hamoja na niye tovilamusa vibumbila va wanhu wamtogole Yesu ako Galatia.

3 Mulungu Tataetu na Mndewa Yesu Kilisito wawagwee ng'hekewa na tindiwalo.

4 Kwa kutegeleza viyolonda Tataetu Mulungu, Kilisito kailava mwenyego kwa nzambi zetu, muladi yatukombole na nzambi za wanhu wa lukolo luno lwa sambi.

5 Mulungu yagweleligwe ukulu siku zose! Ona.

*Mbuli imoja Inogile*

6 Mweye mong'hanganya, sambi sambi baha, momuleka Mulungu yawakemile kwa ng'hekewa ya Kilisito, na mokweleleza usenga uyagwe ukoneka kamba mbuli inogile.

7 Kulonga ukweli kuduhu mbuli iyagwe inogile. Nolonga vino, kwavija
kuna wanhu wayagwe wowading'hula na wolonda kuigalusa Mbuli Inogile
ya Kilisito.
8 Lakini hata kamba imoja wetu hebu msenga wa kuulanga, kowapete-
leni usenga uyagwe hauigalile na Mbuli Inogile ituwapetele tweye, ayo
yaduiligwe na Mulungu!
9 Tweye tulonga, na sambi nolonga kabili, munhu yoyose yowapetela
usenga uyagwe hauigalile na Mbuli Inogile imupeteligwe, munhu ayo
yaduiligwe na Mulungu!
10 Vino vinongile vino nolonda kutogoligwa na wanhu? Haili vivo bule!
Niye nolonda kutogoligwa na Mulungu! Vino, niye nolonda kuwanogeza
wanhu? Maza nhendile vivo, sambi niwe msang'hanaji wa Kilisito.

### *Paulo viyapatile utumigwa*

11 Ndugu zangu, nolonda mujuwe kuwa Mbuli Inogile iniwapetele
hailawa kwa wanhu.
12 Niye siipatile kulawa kwa munhu yoyose, hebu kufundizigwa na
munhu. Yesu Kilisito mwenyego yuyo yanigubulile.
13 Mweye muhulika vinikalile noigoga goya dini ya Kiyahudi, muhulika
vinividununze ng'hani vibumbila va wanhu wamtogole Yesu bila kuvonela
bazi na nilonda kudibananga tamanilo jao.
14 Niye niwahuma Wayahudi wayangu wengi wanileleke nao kwa kuk-
weleleza dini ya Kiyahudi, niwamba ng'hani kuvigoga vihendo vitug-
weleligwe na wahenga zetu.
15 Lakini Mulungu kwa ng'hekewa yake kanisagula ning'hali sinavum-
buka, kanikema nimsang'hanile.
16 Viyone vinoga kunigubulila Mwanage, muladi niwapetele Mbuli yake
Inogile wanhu haweli Wayahudi, sikimbilile kwa munhu kumuuza mbuli
yoyose,
17 hebu kuchola kudibuga da Yelusalemu kuwauza waja wanongolele
kuwa watumigwa, lakini tanhu nichola mwiisi ya Alabiya abaho nibwele-
ganya kudibuga da Damesiki.
18 Viibitile miyaka midatu, nichola Yelusalemu kumulola Kefa,* na nikala
nayo kwa siku longo na tano.
19 Lakini siiting'hane na watumigwa wowose wayagwe ila Yakobo, ndugu
yake Mndewa Yesu.
20 Kino kinyandika cha ukweli, Mulungu kojuwa siviza!
21 Abaho nichola mziisi za Siliya na Kilikia.
22 Kipindi acho vibumbila va wanhu wamtogole Yesu ako Yudea vikala
havinanyona.
23 Wao wakala wakijuwile kija kiiyeka kiwahulike kwa wanhu, “Munhu
ija yakalile yotudununza, sambi kowapetela wanhu Mbuli Inogile iija ya
kumtamanila Kilisito iyakalile yolonda kuibananga!”
24 Avo mbuli ya niye wamgwaa ukulu Mulungu.

## 2

### *Paulo na watumigwa wayage*

1 Viibitile miyaka longo na nne, nibweleganya Yelusalemu hamoja na
Balinaba, vivija nimsola Tito.

* **1:18** Kefa kwa ulonzi wa Kigiliki Petulo.

2 Nichola kuko kwavija Mulungu kanigubulila nichole, vituiting'hane
twiiyeka na walangulizi niwasimulila usenga wa Mbuli Inogile iniwapetela
wanhu haweli Wayahudi. Nhenda vivo muladi sang'hano yangu in-
isang'hane na ino inisang'hana sekeyage bule.
3 Miyangu Tito hamoja kakala Mgiliki, hawamnanahize yengile kumbi,
4 vivija kukala na wanhu waitendile wamtogola Yesu walonda yengile
kumbi. Wanhu awo wengila kinyelegezi mna ikibumbila chetu kutusepa,
muladi wajuwe vitubwihila kwa kuilumba na Yesu Kilisito. Walonda tukale
kamba watumwa.
5 Lakini hatuwatogolele bule, muladi ukweli wa Mbuli Inogile usigale na
mweye.
6 Lakini wanhu wano wolongigwa kuwa walangulizi, kamba kweli wakala
vivo hebu si vivo, niye sitonga bule. Kwavija Mulungu hamtagusa munhu
kwa kumulola kwa kunze, wanhu awo hawakalile na magesa ga kuny-
ongezela.
7 Lakini wajuwa kuwa Mulungu kanhuma niwapetele Mbuli Inogile
wanhu haweli Wayahudi, kamba vija Petulo viyatumigwe yawapetele Mbuli
Inogile Wayahudi.
8 Kwavija Mulungu yamtendile Petulo mtumigwa kwa Wayahudi, yuyo
yanhendile niye kuwa mtumigwa kwa wanhu haweli Wayahudi.
9 Yakobo, Kefa na Yohana wokoneka kuwa walangulizi wakulu, wai-
juwa ng'hekewa inigweleligwe na Mulungu, avo watugoga makono niye
na Balinaba, kulagusa tweye na wao twa kinhu kimoja. Tuitogolela kuwa
niye na Balinaba tukasang'hane kwa wanhu haweli Wayahudi na wao
wakasang'hane kwa Wayahudi.
10 Lakini watupula kino kiiyeka, tuwagese wakiwa weli mkibumbila chao,
na niye ng'hala niwamba kuisang'hana mbuli ayo.

*Paulo komzuma Kefa*

11 Lakini Kefa viyezile kudibuga da Antiokia, nimulemela mgameso ga
wanhu kwavija kakala yabanange.
12 Kwavija wang'hali hawanavika wanhu wayagwe watumigwe na
Yakobo, Kefa kakala yoja na wanhu haweli Wayahudi. Lakini wanhu awo
viwavikile kasonga kuinega na wanhu haweli Wayahudi, kwa kuwadumba
wanhu wa kibumbila wakalile wonanahiza kwingila kumbi.
13 Wayahudi wayagwe wailumba na Kefa mna imbuli ayo ya unafiki, hata
Balinaba nayo kakala mumo.
14 Vinyonile mbuli zao zootenda haziigalile na viilonda Mbuli In-
ogile, nimulongela Kefa mgameso ga wanhu wose, "Hamoja gweye
kwa Muyahudi, kokala kamba wanhu haweli Wayahudi na siyo kamba
Muyahudi. Habali kowananahiza wanhu haweli Wayahudi wakweleleze
vihendo va Wayahudi?"

*Wayahudi na wanhu haweli Wayahudi wokomboligwa kwa kumtamanila Mulungu*

15 Tweye twa Wayahudi kwa kuvumbuka, na siyo wanhu haweli
Wayahudi wene nzambi!
16 Tweye tojuwa kuwa munhu hatendigwa kanoga mgameso ga Mulungu
kwa kugagoga Malagizo ga Musa, ila kwa kumtamanila Yesu Kilisito. Na
tweye tumtamanila Yesu Kilisito muladi tutendigwe tunoge mgameso ga
Mulungu, kubitila kumtamanila kwetu Kilisito, na siyo kwa kugagoga Mala-
gizo ga Musa. Kwavija kuduhu munhu yoyose yotendigwa kanoga mgameso
ga Mulungu kwa kugagoga Malagizo ga Musa.

17 Lakini kamba tweye tolonda kutendigwa tunoge mgameso ga Mulungu kwa kuilumba na Kilisito, tokoneka kamba totenda nzambi, vino gano gofambula kamba Kilisito kowataza wanhu watende nzambi? Haili vivo bule!
18 Niinanga nzila ya kugatamanila Malagizo. Kamba sambi noizenga kabili, aho nolagusa niye nogabena Malagizo.
19 Mbuli ya Malagizo niye nifa, Malagizo genyego gang'homa muladi niwe mgima kwa mbuli ya Mulungu. Niye niwambigwa mumsalaba hamoja na Kilisito.
20 Sambi namgima, lakini sili niye kabili ila Kilisito yokala mgati mmwangu. Sambi nokala kwa kumtamanila Mwana wa Mulungu, yaninogele niye, na kaulava ugima wake mbuli ya niye.
21 Siilema ng'hekewa ya Mulungu. Kwavija kamba munhu kotendigwa kanoga mgameso ga Mulungu kwa kugagoga Malagizo, avo Kilisito kafa bule!

# 3

*Malagizo na kumtamanila Mulungu*

1 Mweye Wagalatia mwa wabozi! Vino nani yawalogile? Mbuli ya kuwambigwa kwa Yesu Kilisito mumsalaba ilongigwa goya mgameso genu.
2 Nolonda kujuwa kinhu kimoja kumwenu, vino mumbokela Loho wa Mulungu mbuli ya kusang'hana vigalonda Malagizo hebu kwa kuhulika Mbuli Inogile na kuitogola?
3 Vino mweye mwa wabozi? Mweye musonga kusang'hana mbuli zose kwa kutazigwa na Loho wa Mulungu, vino sambi molonda kumambukiza kwa udahi wenu wenyego?
4 Vino mbuli zose ziwapatile mugaya bule? Aka, havidahika!
5 Vino Mulungu kowagwaa Loho wake na kutenda unzonza kumwenu kwavija motenda vigalonda Malagizo ga Musa hebu kwavija moihulika Mbuli Inogile na kuitogola?
6 Kamba Maandiko Gang'alile vigolonga mbuli ya Abulahamu, “Kamtamanila Mulungu, nayo Mulungu kamgesa kanoga.”
7 Avo mujuwe kuwa, wanhu wose womtogola Mulungu, awo wao wana too wa Abulahamu.
8 Maandiko Gang'alile galagula toka mwaka kuwa Mulungu kowatenda wanhu wa isi zose wanoge mgameso gake kubitila kumtamanila kwao. Avo Maandiko Gang'alile gampetela Abulahamu Mbuli Inogile, “Kubitila gweye Mulungu kowatenda wanhu wa ng'holo zose za mwiisi wamwede.”
9 Avo wanhu wose womtamanila Mulungu womweda hamoja na Abulahamu, yamtamanile Mulungu.
10 Lakini wanhu wose wotamanila kugatenda golondigwa na Malagizo, wanhu awo waduiligwa na Mulungu. Kwavija Maandiko Gang'alile golonga, “Munhu yoyose yoleka kugoga kila kinhu chandikigwe mna ikitabu cha Malagizo, munhu ayo kaduiligwa na Mulungu!”
11 Sambi yojuwika goya Malagizo hagadaha kumtenda munhu yanoge mgameso ga Mulungu, kwavija Maandiko Gang'alile golonga, “Munhu yotendigwa kanoga mgameso ga Mulungu kokala kwa kumtamanila Mulungu.”
12 Lakini Malagizo siyo mbuli ya kumtamanila Mulungu, lakini Maandiko Gang'alile golonga, “Munhu yoyose yotenda mbuli zilondeka na Malagizo kokala kwa mbuli zizo.”

13 Kilisito katukombola mna ukuduiligwa na Malagizo, kwa kuduiligwa
mbuli ya tweye, kwavija Maandiko Gang'alile golonga, “Munhu yoyose
lukuli lwake lunanikigwe mumbiki kaduiligwa.”
14 Mbuli ino itendeka muladi vinhu vinogile, vija Mulungu viyailagane
na Abulahamu wagweleligwe wanhu haweli Wayahudi kubitila Yesu Kil-
isito, avo kwa kumtamanila Mulungu tobokela Loho Yang'alile iyalongile
Mulungu.

*Lagizo na Kija kiyalongile Mulungu*

15 Ndugu zangu, nolonda nilonge vinhu viigalile na vinhu vootenda
wanhu siku zose. Wanhu wabili wahaitogolela mbuli na kwika kilaguso cha
kuilagana, kuduhu munhu yodaha kusegeza hebu kwengeza kinhu.
16 Avo kija kiyalongile Mulungu kagweleligwa Abulahamu na munhu
yaleleke mulukolo lwa mwanage Abulahamu. Maandiko Gang'alile ha-
galonga, “Wanhu waleleke,” fambulo jake wanhu wengi, lakini golonga,
“Munhu yaleleke,” fambulo jake munhu imoja, nayo ayo Kilisito.
17 Niye nolonga vino, Mulungu kailagana na Abulahamu na kalonga
kotenda kiyailagane nayo. Malagizo ga Musa gagaligwe miyaka magana
mane na malongo madatu kumwande hagadaha kudisegeza lagano. Avo
hagadaha kusegeza kija kiyalongile Mulungu.
18 Kwavija kamba nhuza ya Mulungu yotamanila Malagizo, baho haidaha
kutamanila kija kiyalongile Mulungu. Lakini, mbuli ya kija kiyalongile,
Mulungu kamgwaa nhunza Abulahamu.
19 Vino kilamuso cha Malagizo choni? Gongezigwa muladi kulagusa zilihi
azo nzambi, Malagizo gokala mbaka kwiza kwa munhu yaleleke mulukolo
lwa mwanage Abulahamu, ayuja yalongigwe mna idilagano. Malagizo
gagaligwa na wasenga wa kuulanga kubitila ija yogala kuilumba.
20 Munhu yowatenda wanhu wailumbe halondeka kamba mbuli yenyego
ya munhu imoja, lakini Mulungu imoja.

*Kilamuso cha Malagizo*

21 Vino ino yofambula kuwa Malagizo ga Musa hagailumba na kija
kiyalongile Mulungu? Aka, haili vivo! Kwavija kamba wanhu wabokela
Malagizo godaha kugala ugima, baho munhu yoyose kodaha kutendigwa
yanoge mgameso ga Mulungu kwa kugagoga Malagizo.
22 Lakini Maandiko Gang'alile golonga kuwa wanhu wose wa mwiisi
wotawaligwa na nzambi, na nhunza iyalongile Mulungu kwa kumtamanila
Yesu Kilisito, wogoleligwa wanhu waja womtogola.
23 Lakini kipindi cha kumtamanila Mulungu vikikalile hakinavika, Malag-
izo gakala gatufungile mbaka kipindi cha kumtamanila Mulungu vikigubu-
ligwe.
24 Avo Malagizo gatulongoza mbaka viyezile Kilisito, muladi kwa kumta-
manila kwetu Mulungu yatutende tunoge mgameso gake.
25 Lakini kipindi cha kumtamanila Mulungu kivika, avo Malagizo hagatu-
longoza kabili.
26 Kwa kumtamanila Yesu Kilisito mweye mose mwa wana wa Mulungu.
27 Mweye mose mubatizigwe kwa kuilumba na Kilisito, na sambi mum-
vala Kilisito mwenyego.
28 Avo kwa kuilumba na Yesu Kilisito wanhu wose kuduhu kuibagula.
Kuduhu Wayahudi na Wagiliki, kuduhu watumwa na wanhu wakom-
boligwe, kuduhu wambigalo na watwanzi, wose kinhu kimoja.
29 Kamba mweye mwa wanhu wa Kilisito, baho mwa wanhu wa lukolo
lwa Abulahamu, na mubokela kija kiyalongile Mulungu.

# 4

1 Avo, nolonga vino, muhazi yahawa yang'hali mwana, kaigala na mtumwa, hamoja vinhu vose vake.

2 Kipindi acho chose kolongozigwa na wanhu womulela na wanhu wovilola goya vinhu vake, mbaka chahavika kipindi kikigwe na tatake.

3 Vivo ili kumwetu tweye, vitukalile tung'hali wana, tukala watumwa wa loho zitawala mwiisi.

4 Lakini vikivikile kipindi kinogile, Mulungu kamtuma mwanage mwenyego, yaleligwe na mtwanzi, na kalongozigwa na Malagizo,

5 muladi yawakombole wanhu waja wose watawaligwe na Malagizo, ili tuwe wana wa Mulungu.

6 Kwavija mweye mwa wanage, Mulungu kamtuma Loho wa Mwanage mmizoyo yenu, Loho ayo yokemelela, “Aba, fambulo jake Tata.”

7 Avo gweye huli mtumwa kabili, lakini kwa mwana. Na kwavija kwa mwana, Mulungu kokugwaa vinhu vose viyawekile wanage.

*Paulo na Wagalatia*

8 Kuko umwaka mukala hamumjuwile Mulungu, na avo mukala watumwa wa loho zilibule udahi wa kutawala.

9 Lakini sambi mumjuwa Mulungu, hebu nonge mujuwigwa na Mulungu, habali mozibwelela loho za ukiwa zilibule nguvu na molonda kuwa watumwa wao kabili?

10 Mung'hali mozigoga siku na miezi na vipindi na miyaka.

11 Nodumba sengine sang'hano yangu inisang'hane mbuli yenu yaga bule.

12 Ndugu zangu, nowapula muwe kamba niye. Kwavija hata niye niwa kamba mweye. Mweye hamunhendele mbuli yoyose ihile.

13 Mojuwa kuwa utamu awo unhendile kuwapetela Mbuli Inogile kwa mwanza wa ichanduso.

14 Hata ivo, kipindi kija hamnibezile hebu kundema mbuli ya utamu wangu, hamoja mugaya ng'hani mbuli ya utamu awo, lakini munibokela kamba vonda mumbokele msenga wa kuulanga, na munibokela kamba vonda mumbokele Yesu Kilisito mwenyego.

15 Mweye mukala na deng'ho! Vino kulawililila choni? Niye nodaha kulonga, kipindi kija, maza mudahile mwahang'olile meso genu wenyego na kungwaa niye.

16 Vino sambi monihila mbuli ya kuwalongela ukweli?

17 Wanhu wayagwe wowagaiya mweye, lakini hawagesa ganogile kumwenu. Wolonda mweye na niye tuigole, muladi mweye muwagaiye wao.

18 Kweli siku zose vinoga kugaiya mbuli zinogile, hata kamba niye nahaduhu.

19 Wanangu! Kamba vija mtwanzi viyogaya kipindi cha kulela mwana, na niye nowagaiya mbaka Kilisito vonda yalumbigwe mgati mmwenu.

20 Nosulukila, maza nahakalile na mweye sambi, nahalongile ulonzi unogile! Niye nokala moyo yungwa yungwa mbuli yenu!

*Hajili na Sala*

21 Nongeleni mweye mulonda kutawaligwa na Malagizo ga Musa, vino hamuhulika bule vigalonga Malagizo?

22 Kwavija yandikigwa kuwa Abulahamu kakala na wana wabili, mwana imoja kaleleka na mtwanzi yakalile mtumwa, na mwana iyagwe kaleleka na mtwanzi yakomboligwe.

23 Mwanage yaleleke na mtwanzi yakalile mtumwa kaleleka kamba vi-
waleleke wana wayagwe, lakini mwanage yaleleke na mtwanzi yakom-
boligwe kaleleka kubitila kija kiyalongile Mulungu.
24 Kinhu kilawilile kwa wana wabili wa Abulahamu kiigala na kinhu
cha ukweli, watwanzi wao wabili wolagusa malagano mabili. Lagano
dimoja dija ditendigwe hana Ulugongo lwa Sinai, dolonga mbuli ya Hajili,
na wanage woleleka muutumwa.
25 Hajili kolagusa Ulugongo lwa Sinai luli ako Alabiya, na yolagusa buga
da Yelusalemu dili sambi mwiisi, dili muutumwa hamoja na wanage wose.
26 Lakini Yelusalemu ili kuulanga ni buga dikomboligwe, najo dijo ma-
maetu.
27 Kwavija Maandiko Gang'alile golonga,

“Deng'helela gweye mtwanzi uli mgumba,
Toa lukenze gweye hupatile usungu wa kulela mwana!
Kwavija wana wa mtwanzi yalekigwe wokuwa wengi
kubanza wana wa mtwanzi yokala na mkasano.”

28 Avo ndugu zangu, mweye mwa wana kwavija vivo viyalongile Mulungu
kilawilile, kamba viikalile kwa Isaka.
29 Lakini kamba kipindi kija kiyaleleke mwana ija kamba viwoleleka
wana wayagwe, kamdununza ija yaleleke kwa udahi wa Loho wa Mulungu,
sambi vivo ili.
30 Lakini Maandiko Gang'alile golonga, “Muwinge mtwanzi yeli mtumwa
na mwanage, kwavija mwana wa mtwanzi yeli mtumwa, honda yahazi
hamoja na mwana wa mtwanzi yakomboligwe.”
31 Avo ndugu zangu, tweye hatuli wana wa mtwanzi yeli mtumwa, ila twa
wana wa mtwanzi yakomboligwe.

# 5

### *Tweye tulekesigwa kwa Kilisito*

1 Tulekesigwa kwavija Kilisito katutenda tulekesigwe! Gangamaleni na
sekemutogole kuwa watumwa kabili.
2 Tegelezeni! Niye Paulo nolonga na mweye, mwahatogola kwingila
kumbi, Kilisito honda yawafaye chochose.
3 Nolonga kabili, munhu yoyose yotogola kwingila kumbi kolondeka
yagagoge Malagizo gose ga Musa.
4 Kamba molonda kutendigwa munoge mgameso ga Mulungu kwa ku-
gagoga Malagizo, baho mwiinega na Kilisito, na muileka ng'hekewa ya
Mulungu.
5 Lakini tweye, totamanila kutendigwa tunoge mgameso ga Mulungu
kwa kumtamanila. Kino acho tukibetela ng'hani kwa udahi wa Loho wa
Mulungu.
6 Kwavija twahailumba na Yesu Kilisito, kwingila kumbi hebu kuleka
kwingila kumbi siyo kinhu, kilondeka ni kumtamanila Mulungu kubitila
unogelwa.
7 Mweye mukala musang'hana goya! Nani yawagomese kuutogola uk-
weli?
8 Mbuli ayo haitendigwe na Mulungu, yawakemile mweye.
9 “Mela kidogo doutenda usage wose ugongomoke!”
10 Kwavija muilumba na Mndewa, nogesa kuwa mogesa kamba vinigesa
niye. Munhu yoyose yowading'hula hata kamba yahawa nani, munhu ayo
kotagusigwa na Mulungu.

11 Ndugu zangu, kamba nogendelela kuwapetela wanhu kwingila kumbi,
habali ning'hali nodununzigwa? Maza ikalile avo kuwapetela kwangu
wanhu mbuli ya msalaba wa Kilisito sambi kuwading'hule wanhu.
12 Maza nolonda wanhu awo wowading'hula mweye, wahabenigwe vim-
bigalo wao wenyego.
13 Mweye ndugu zangu, mukemigwa muladi mulekesigwe. Lakini kuleke-
sigwa kuko sekekuwe kilamuso cha kutenda chochose kimulonda mweye
wenyego, ila molondeka muisang'hanile kwa kuinogela.
14 Kwavija Malagizo gose ga Musa gotendigwa kwa kugoga lagizo dino
dimoja, "Mnogele miyago kamba viuinogela mwenyego."
15 Lakini mwahailuma na kuidafuna wenyego kamba ming'onyo, aho
muitiganye sambi muibanange mweye kwa mweye.

### *Gaja goyolonda Loho na gaja gotulonda tweye*

16 Avo, nolonga vino, mbuli zenu zimsang'hana zilongozigwe na Loho wa
Mulungu, na aho honda mukweleleze usulukilo wihile uli mgati mmwenu.
17 Kwavija viulonda usulukilo wihile uli mgati mmwenu hakuitogolela
na vija viyolonda Loho wa Mulungu, na vija viyolonda Loho wa Mulungu
hakuitogolela na vija viulonda usulukilo wihile uli mgati mmwenu. Vinhu
vino vibili haviilumba bule, avo hamudaha kutenda kinhu chochose kimu-
londa wenyego.
18 Kamba mwahalongozigwa na Loho wa Mulungu, aho hamutawaligwa
na Malagizo ga Musa.
19 Sang'hano za wanhu wokweleleza usulukilo wihile uli mgati mmwao
zijuwika goya, ugoni na uchafu na ugoni ubanzile ng'hani,
20 na kuvitambikila vinyago na uhawi na kuihila na ndwagi na kuyonela
migongo na ng'hasiliki na ugila na kuiding'hula na kuigola mna ivibumbila,
21 migongo ibanzile na kukoligwa na nyimwili nyimwili ya kukoligwa na
mbuli ziyagwe kamba azo. Sambi nowazuma kamba viniwazumile aho
haichanduso, wanhu wose wotenda mbuli azo honda wengile Muundewa
wa Mulungu.
22 Lakini muugima wa munhu yolongozigwa na Loho wa Mulungu vinhu
vino vokoneka mgati mmwake, unogelwa na deng'ho na tindiwalo na
kufunga umoyo na bazi na moyo unogile na kutenda kija kiyalongile,
23 uhole, kuitawala mwenyego. Kuduhu Malagizo goleka kuitogolela na
gano.
24 Wanhu wose wailumbile na Yesu Kilisito wauwamba unhu wao wa
nzambi uli na usulukilo wihile na magesa gehile.
25 Twahakala kwa kulongozigwa na Loho wa Mulungu, tukweleleze viy-
olonda Loho.
26 Avo, seketuigode, seketuigobole hebu kuyonela migongo.

# 6

### *Tuitaze wenyego*

1 Ndugu zangu, mwahamona munhu yoyose katenda nzambi, mweye
mulongozigwa na Loho wa Mulungu mzumeni munhu ayo, muladi yaleke
nzambi zake. Lakini mzumeni kwa uhole, kuno moiteganya muladi seke-
mugezigwe.
2 Muitaze mna gamagayo, kwa kutenda avo mogagoga malagizo ga Kil-
isito.
3 Munhu yahayona kinhu, na kuno heli kinhu chochose, koivizila
mwenyego.

4 Lakini kila munhu yalole goya mbuli zake mwenyego zoyosang'hana. Kamba kotenda mbuli zinogile aho kodaha kuigodela mbuli zako, bila kulola choni kiyatendile munhu iyagwe.

5 Kwavija kila munhu kana mzigo wa kupapa mwenyego.

6 Munhu yofundizigwa mbuli ya Kilisito kolondeka waigwelele vinhu vake vose vinogile na mfundiza wake.

7 Sekemuivizile, Mulungu hagewezigwa, kwavija kija kiyahandile munhu acho chonda yasenge.

8 Munhu yohanda kuzinogeza nzambi zili mgati mmwake, mumo kosenga ifa, lakini yahahanda kuinogeza loho wa Mulungu, mumo kosenga ugima wa kweli wa mazuwa gose.

9 Avo seketudonhe kusang'hana ganogile, kwavija kamba hatubwela kukisogo, chahavika kipindi cha kusenga tosenga.

10 Avo twahawa tung'hali tuna kipindi, tuwatendele ganogile wanhu wose, ng'hani ng'hani waetu wamtogole Mndewa.

### *Kulamusigwa na kuzumigwa kwa uhelelo*

11 Loleni vinyandike kwa helufi ng'hulu kwa makono gangu mwenyego!

12 Wanhu wolonda koneka wanoga kwa vinhu va kunze, awo wolonda kuwananahiza mweye mwingile kumbi, wotenda avo kwavija wodumba kudununzigwa mbuli ya msalaba wa Kilisito.

13 Hata waja wengile kumbi hawagagoga Malagizo ga Musa, wao wolonda mweye mwingile kumbi muladi waigodele kija kitendeke mzing'huli zenu.

14 Lakini niye noigodela msalaba wa Mndewa wetu Yesu Kilisito wiiyeka, kwavija kubitila msalaba wake vija viwokala wanhu wa mwiisi kumwangu kamba kufa na niye kamba nifa kumwao.

15 Kwingila kumbi hebu kuleka kwingila kumbi siyo kinhu, kilondeka kuumbigwa kabili.

16 Wanhu wose wokala kwa kukweleleza nzila ino, Mulungu yawagwee tindiwalo na bazi, vivija kwa waja Waizilaeli weli wa Mulungu.

17 Avo, munhu yoyose sekeyanigaze kabili, kwavija ng'hovu zili mulukuli lwangu mbuli ya Yesu.

18 Ndugu zangu, ng'hekewa ya Mndewa wetu Yesu Kilisito ikale na loho zenu mweye mose. Ona.

# Baluwa ya Paulo kwa wanhu wa ako Efeso

## Ulongozi

Baluwa kwa Waefeso yandikigwa kipindi kimoja na baluwa kwa Wakolosai behi na mwaka wa 60 toka kuvumbuka kwa Kilisito. Mwandikaji koitambula mwenyego kamba Mtumigwa Paulo (Sula ya 1:1) Wanhu woifunza mbuli woitogolela kuwa Paulo ayo yandike baluwa kwa Waefeso hamoja hawalamuse wanhu kamba viyatendile kwa Wakolosai. Kwa kilamuso acho yogesigwa baluwa ino ilondigwa kuwavikila wanhu wamtogole Yesu mna ivibumbila vili mwiisi ayo. Vivija Paulo kolonga kakala mkifungo viyandike baluwa ino (Sula ya 3:1, 4:1, na 6:20). Paulo kaigala baluwa ino kwa makono ga Tukiko muumwanza wake wa kuwatembelela wanhu wamtogole Yesu mna ikibumbila kili ako Efeso (Sula ya 6:21-22).

Efeso dikala buga kulu kwa wakulu wa isi ya Lumi na mwiisi yose ya Asiya Ndodo. Buga da Efeso dijuwika ng'hani kwa ng'anda ilavigwe kwa mulungu wa kitwanzi wa Kigiliki Atemi (Sang'h 19:23-31). Wanhu wamtogole Yesu mkibumbila cha Efeso wakala wasongile goya mna ukutamanila lakini kumwande wona wavika kuuhelelo (Ugub 2:1-7).

Mdifungu da ichanduso da baluwa ino Paulo kosimulila Mulungu viyawasagule wanhu zake na kawakombola na nzambi zao kubitila Yesu Kilisito. Kawalinganya wanhu wamtogole Yesu na lukuli na Kilisito ayo pala na vivija kawalinganya kamba ng'anda izengigwe kwa mabwe na Kilisito ayo dibwe kulu da chandusilo. Fungu da kabili da ibaluwa Paulo kofundiza mbuli ya wanhu wamtogole Yesu viwolondeka kukala.

**Mbuli zili mkitabu**

Mna isula ya 1:1-2 Paulo koitambula mwenyego na kowalamusa wanhu wa ako Efeso.

Abaho kosimulila vija wanhu wamtogole Yesu viwoilumba na Kilisito (Sula ya 1:3-3:21).

Abaho Paulo kokwandika mbuli ya wanhu wamtogole Yesu viwolondeka kukala (Sula ya 4:1-6:20).

Kukimambukizo Paulo kolonga mbuli za kimambukizo (Sula ya 6:21-24).

1 Niye Paulo, namtumigwa wa Yesu Kilisito kwa kulonda Mulungu, nowandikila mweye wanhu wa Mulungu muli ako Efeso, mweye muganga-male kumtamanila Mulungu kwa kuilumba na Yesu Kilisito.

2 Mulungu Tataetu na Mndewa wetu Yesu Kilisito wawagwee ng'hekewa na tindiwalo.

*Kumweda kiloho kwa kuilumba na Kilisito*

3 Tumgwee nhogolwa Mulungu yeli Tata wa Mndewa wetu Yesu Kilisito! Kwavija kwa kuilumba na Kilisito katutenda tumwede kwa kutugwaa kila kinhu kinogile cha kiloho cha ako kuulanga.

4 Avo isi ing'hali hainaumbigwa, Mulungu katusagula tweye kwa kuilumba na Kilisito, muladi tung'ale na seketuwe na nzambi mgameso gake.

Mbuli ya unogelwa wake,

5 toka mwaka kalonda kututenda wanage kubitila Yesu Kilisito, vivo viyanogelwe na viyalondile.

6 Tumtogole Mulungu mbuli ya ng'hekewa yake inogile iyatugwelele, kubitila Mwanage iyamnogele!

7 Kwavija kwa damu ya Kilisito tweye tolekesigwa, nzambi zetu zogeligwa kumgongo kwa ukulu wa ng'hekewa ya Mulungu,

8 iyatugwee kwa kumema kwa nzewele na ubala wake wose.

9 Na katulagusila vinhu vake vifisigwe, viyalondile kutenda. Kanogelwa kutenda vivo kubitila Kilisito.

10 Vikivikile kipindi chake, katenda kija kiyalondile, kuvika hamoja vinhu vose viumbigwe kuulanga na mwiisi, kavigela mmakono ga Kilisito.

11 Kwa kuilumba na Kilisito, tweye tusaguligwa tuwe wanhu zake kamba viyalondile Mulungu toka mwaka. Mulungu kotenda kila kinhu kamba viyolonda mwenyego.

12 Mulungu katenda avo muladi tweye tusongile kumtamanila Kilisito, tumtogole Mulungu kwa ukulu wake!

13 Na mweye vivija muhulike usenga wa kweli wa Mbuli Inogile iwagalile ukombozi, na mumtogola Kilisito. Na vivija Mulungu kawekila kinhu cha kulagusa kwa kuwagwaa Loho Yang'alile iyalongile kulagusa mwa wanhu zake, kwa kuilumba na Kilisito.

14 Loho Yang'alile ayo yotutenda tubokele kija kiyalongile Mulungu kwa wanhu zake, na mbuli ino yotulagusila kuwa Mulungu kowagombola wanhu zake. Avo tumtogole Mulungu kwa ukulu wake!

### *Paulo kowapulila Waefeso kwa Mulungu*

15 Kwa mbuli ayo, toka vinihulike mbuli ya kumtamanila kwenu Mndewa Yesu, na unogelwa wenu kwa wanhu wose wa Mulungu,

16 silekile bule kumgwaa nhogolwa Mulungu mbuli ya mweye. Nahampula Mulungu siwasemwa mweye bule.

17 Nogendelela kumpula Tata yeli mkulu, Mulungu wa Mndewa wetu Yesu Kilisito, yawagwee Loho wake, yonda yawagwee nzewele na kuwagubulila Mulungu kumwenu muladi mumjuwe goya.

18 Nompula Mulungu yawataze mudahe kujuwa goya tamanilo diyawakemele na vinhu vingi vinogile viyawekile wanhu zake,

19 na mudahe kujuwa udahi wake viwili mkulu ng'hani mbuli ya tweye tumtogola. Udahi awo usang'hana mgati mmwetu uigala na nguvu ibanzile ng'hani,

20 iyamzilibule nayo Kilisito kwa wanhu wafile, na kamwika yakale muukulu mwambu wa mkono wake wa kudila ako kuulanga.

21 Ako Kilisito kotawala kila ukulu na udahi na nguvu na undewa na kotawala kila twaga da loho yoyose itambuligwa mwiisi ino na isi yonda ize.

22 Mulungu kavika vinhu vose mmakono ga Kilisito na kamtenda Yesu yawe mkulu wa wanhu wose wamtogole.

23 Wanhu wose wamtogole Kilisito wao lukuli lwa Kilisito, na wao utimilifu wa Kilisito nayo ayo yotimiliza kila kinhu, kila hanhu.

# 2

### *Kulawa mkufa kwingila muugima*

1 Aho umwaka mweye mukala kamba mufa mbuli ya ubananzi na nzambi zenu.

2 Kipindi kija mukala kwa ubananzi na kukweleleza gehile ga wanhu wa mwiisi ino, mukala momtegeleza mtawala wa gehile wa undewa wa ulanga, loho ija yowatawala wanhu iwoleka kumtegeleza Mulungu.

3 Na tweye wose tukala kamba wao, na tukala kwa kukweleleza usulukilo
wihile uli mgati mmwetu, na tusang'hana mbuli zija zinogeligwe na ng'huli
zetu na nzewele zetu. Kamba vitukalile, kamba viweli wanhu wayagwe,
tumgevuza Mulungu na tulondeka kutagusigwa.
4 Lakini Mulungu kana bazi ng'hani. Na katunogela kwa unogelwa mkulu,
5 hata vitukalile tofa kwa nzambi, katutenda wagima hamoja na Kilisito.
Kwa ng'hekewa ya Mulungu mweye mukomboligwa.
6 Kwa kuilumba na Yesu Kilisito, Mulungu katuzilibula hamoja nayo,
tukale nayo kuulanga.
7 Vivo viyalondile kulagusa kwa kipindi chose chonda kize ukulu wa
ng'hekewa yake iyatugwee kwa unogelwa kwa kuilumba kwetu na Yesu
Kilisito.
8 Kubitila ng'hekewa ya Mulungu mukomboligwa kwa kumtamanila.
Mbuli ino hailawilile kwa udahi wenu, lakini ilawilila kwa nhunza ya
Mulungu,
9 hailawilile kwa sang'hano zenu, avo munhu yoyose sambi yaitape.
10 Tweye twa sang'hano ya makono ga Mulungu, na kwa kuilumba na Yesu
Kilisito, Mulungu katuumba muladi tukale kwa kusang'hana mbuli zinogile
ziyatutandile tuzisang'hane.

### *Kuilumba na Kilisito*

11 Avo, mweye wanhu hamwili Wayahudi kwa kuvumbuka, mukemigwa,
“Wanhu hawengile kumbi,” na Wayahudi woikema, “Wanhu wengile
kumbi,” wao wengila kumbi mzing'huli zao, kulagusa kuwa wanhu wa
Mulungu, kumbukeni vimukalile aho umwaka.
12 Vivija, kipindi kija mweye mukala hamuilumbile na Kilisito. Mukala
wanhu baki na hamukalile mna iwanhu wasaguligwe na Mulungu, mukala
mduhu fungu jojose mna gamalagano ga Mulungu gayawalongele wanhu
zake, mukala mduhu cha kutamanila na mukala mduhu Mulungu.
13 Aho umwaka mukala kutali na Mulungu, lakini sambi, kwa kuilumba
na Yesu Kilisito, mugaligwa behi kwa damu ya Kilisito.
14 Kwavija Kilisito mwenyego katugalila tindiwalo kwa kuwatenda
Wayahudi na wanhu haweli Wayahudi kinhu kimoja. Kwa kulava lukuli
lwake mwenyego kamba nhosa kasegeza kuihila kwao, kuigalile na luwa
lukalile lowagola.
15 Kagasegeza Malagizo ga Wayahudi na vihendo vake, muladi kulawa
mzing'holo azo mbili yatende lukolo lumoja lwa sambi kwa kuilumba nayo
mwenyego na avo kugala tindiwalo.
16 Kwa kulava nhosa lukuli lwake mumsalaba Kilisito kasegeza kuihila
kwao, kazitenda ng'holo azo ziilumbe ziwe kinhu kimoja kamba lukuli na
kuzitenda zimbwelele Mulungu.
17 Avo Kilisito keza kuwapetela Mbuli Inogile igala tindiwalo kumwenu,
mweye wanhu hamwili Wayahudi, mukalile kutali na Mulungu na vivija
kwa Wayahudi wakalile behi na Mulungu.
18 Avo kubitila Kilisito tweye wose, Wayahudi na wanhu haweli Wayahudi,
todaha kumcholela Tata kwa Loho imoja Yang'alile.
19 Avo mweye wanhu hamwili Wayahudi sambi hamwili wanhu baki
hebu wanhu wa kutali, mweye sambi mwa wenekae hamoja na wanhu wa
Mulungu na mwa wanhu wa lukolo lwa Mulungu.
20 Na mweye vivija muzengigwa mna ichandusilo kikigwe na watumigwa
na watula ndagu wa Mulungu. Nayo Yesu Kilisito mwenyego ayo dibwe kulu
da chandusilo.

21 Avo Kilisito mwenyego ayo yogogeleza ng'anda yose na kuitenda ikule
iwe ng'anda ing'alile ya Mulungu ilavigwe kwa Mndewa.
22 Kwa kuilumba na Kilisito, na mweye vivija mozengigwa hamoja na
wayagwe wose, Mulungu yakale kumwenu kubitila Loho wake Yang'alile.

# 3

*Sang'hano ya Paulo kwa wanhu haweli Wayahudi*

1 Avo, niye Paulo, namfungwa kwavija nomsang'hanila Yesu Kilisito mbuli
ya mweye wanhu hamwili Wayahudi, nompula Mulungu.
2 Nojuwa kweli muhulika, Mulungu viyanigwelele ng'hekewa ya ku-
sang'hana sang'hano ino mbuli ya mweye.
3 Mulungu kangubulila vinhu vake vifisigwe, mna ibaluwa ino niwapetela
kidogo mbuli ayo,
4 na mwahakisoma kija kinyandike, modaha kujuwa vinhu vinjuwile niye,
vifisigwe kwa mbuli ya Kilisito.
5 Baho umwaka wanhu wakala hawavijuwile vinhu vino vifisigwe, lakini
sambi Mulungu kawagubulila vinhu avo watula ndagu na watumigwa zake
wang'alile kubitila Loho Yang'alile.
6 Kinhu chenyego kifisigwe acho kino, kubitila Mbuli Inogile wanhu
haweli Wayahudi wopata fungu mna ivinhu vinogile va Mulungu hamoja
na Wayahudi, wao wokuwa maungo ga lukuli luluja, na wobokela kikija
kiyalongile Mulungu kubitila Yesu Kilisito.
7 Niye nitendigwa msang'hanaji wa Mbuli Inogile kwa ng'hekewa iyanig-
welele Mulungu kwa udahi wake mkulu.
8 Niye na munhu mdodo kubanza wanhu wose wa Mulungu, lakini Mu-
lungu kanigwaa ng'hekewa, muladi niwapetele wanhu haweli Wayahudi
Mbuli Inogile, ya vinhu vinogile va Kilisito vilibule uhelelo,
9 na niwatende wanhu wose wazijuwe mbuli za Mulungu zifisigwe na
vizisang'hana. Mulungu yaumbile vinhu vose, kavifisa vinhu vake avo toka
mwaka,
10 muladi sambi, kubitila wanhu wamtogole Yesu, watawala na weli na
ukulu wa kuulanga waijuwe nzewele ya Mulungu viili na nzila nyingi.
11 Mulungu kaitenda mbuli ayo, kamba viyagesile toka mwaka, na ka-
tenda kubitila Mndewa wetu Yesu Kilisito.
12 Kwa kuilumba na Kilisito na kumtamanila, todaha kumgendela Mu-
lungu bila kudumba na kuno totamanila kuwa kotubokela.
13 Avo nowapulila kwa Mulungu, sekemubwele kukisogo, kwavija niye
nogaya mbuli ya mweye, gago gose mbuli ya kuwatenda mumwede.

*Unogelwa wa Kilisito*

14 Kwa kilamuso kino, nomfugamila Tata,
15 yeli chanduso cha ng'holo zose kuulanga na mwiisi.
16 Nompula Mulungu yeli na ukulu wa vinhu vingi, yawagangamize
mmizoyo yenu kubitila Loho wake,
17 nayo Kilisito yakale mmizoyo yenu kwa kumtamanila kwenu. Nopula
muwe na mizizi na chandusilo mna ukuinogela,
18 muladi mweye hamoja na wanhu wa Mulungu mujuwe goya unogelwa
wa Kilisito viwenela kwa ugazi na utali, kwa kwingila hasi na kuchola
uchanha.
19 Ona, muujuwe unogelwa wa Kilisito ubanzile nzewele zose, na
mumemezigwe utimilifu wose wa Mulungu.

20 Kumwake Mulungu kubitila nguvu yake isang'hana mgati mmwetu, kodaha kusang'hana mbuli ng'hulu ng'hani kubanza gaja gotupula hebu kugesa.
21 Mulungu yatogoligwe kwa ukulu wake ukoneka kwa wanhu wose wamtogole Yesu, na kwa Yesu Kilisito, kipindi chose, kiliduhu uhelelo! Ona.

# 4

*Kuilumba na Kilisito*

1 Avo, niye nili mfungwa kwavija nomsang'hanila Mndewa, nowapula mukale kamba Mulungu viyawakemile.
2 Siku zose muwe wahole na moyo unogile, muinogele kwa kufunga umoyo.
3 Wambeni ng'hani sekemwagize kuilumba kwenu, kuyawagwee Loho Yang'alile kubitila tindiwalo dili kumwenu.
4 Kuna lukuli lumoja na Loho imoja, kamba vija vikuli na tamanilo dimoja dimukemeligwe na Mulungu.
5 Hana Mndewa imoja na tamanilo dimoja na ubatizo umoja,
6 hana Mulungu imoja nayo ayo Tata wa wanhu wose, nayo ayo Mndewa wa wanhu wose, kosang'hana kubitila gose, na kabaho mna igose.
7 Kila imoja wetu kagweleligwa ng'hekewa kamba viyalondile Kilisito kumgwaa.
8 Kamba Maandiko Gang'alile vigolonga,
“Viyacholile uchanha ng'hani kuulanga,
kawasola wanhu bwando wakalile wafungigwe,
kawagwaa wanhu nhunza.”
9 Vino yahalonga, “kachola uchanha” kofambula choni? Kofambula kuwa tanhu kahumuluka mbaka hasi ng'hani ya isi.
10 Avo munhu iija yahumuluke ayo iija yacholile uchanha kuulanga na kubanza kuulanga, muladi yaimemeze isi yose kila hanhu.
11 Heyo ayo, “yawagwelele wanhu nhunza.” Na kawasagula wanhu wayagwe wawe watumigwa na wayagwe wawe watula ndagu wa Mulungu, na wayagwe wawapetele wanhu Mbuli Inogile na wayagwe wawe wasusilaji na wafundiza.
12 Katenda vivo, yawatande wanhu wose wa Mulungu mbuli ya kumsang'hanila Kilisito, muladi kulugangamiza lukuli lwa Kilisito.
13 Avo na tweye wose tuwe kinhu kimoja kwa kumtamanila na kumjuwa Mwana wa Mulungu, tuwe wanhu wakangale na kuuvikila utimilifu wake Kilisito mwenyego.
14 Avo hondatuwe wana kabili, twahasigwa na kuhembelusigwa kuno na kuno na beho da wanhu wofundiza uvizi muladi wawagize wanhu wayagwe kwa ubala.
15 Lakini twahalonga ukweli kwa moyo wa unogelwa, tokula mzimbuli zose kwa Kilisito, yeli mkulu.
16 Kwa kulongozigwa na Kilisito maungo gose ga lukuli goilumba, na lukuli lose logogelezwa kwa kutazigwa na maungo gake. Avo kila maungo gahasang'hana viilondeka, lukuli lose lokula na kuizenga mna ukuinogela.

*Ugima kubitila Kilisito*

17 Avo, nowazuma kwa twaga da Mndewa, sekemukale kabili kamba wanhu hawamjuwile Mulungu, weli na magesa gamemile ubozi wiiyeka.
18 Wanhu awo nzewele zao za mdiziza, wakutali na ugima ulavigwa na Mulungu mbuli ya ubozi wao na udala wao wa mizoyo.

19 Wanhu awo waduhu kinyala, wasede na wotenda mbuli zose zigela
kinyala na wogendelela kulonda kutenda vivo.
20 Lakini mweye hamuifunzile avo mbuli ya Kilisito.
21 Mweye muhulika goya mbuli zake, na mufundizigwa ukweli uli kwa
Yesu.
22 Uvuleni unhu wenu wa umwaka, uja ukalile wonangigwa kwa kusuluk-
ila vinhu va uvizi.
23 Mizoyo yenu na nzewele zenu vitendigwe va sambi.
24 Uvaleni unhu wa sambi, uumbigwe kwa kuigala na Mulungu, uja
uigubula wenyego muugima wa ukweli wa kutenda golondigwa na Mu-
lungu na kung'ala.
25 Avo lekeni uvizi! Kila munhu kolondeka kumulongela miyage ukweli,
kwavija kila imoja wetu ni maungo ga lukuli lwa Kilisito.
26 Mwahagevuzika, sekemutogole kugevuzika kwenu kuwatende mu-
tende nzambi, na sekemukale na ng'hasiliki kutwa ngima.
27 Sekemumgwelele mwenembago nyafasi.
28 Wanhu wose wakalile wokwiba waleke na wasonge kusang'hana kwa
makono gao, muladi wakale kwa kutamaniligwa na wadahe kuwataza
wakiwa.
29 Sekemulosoke, lakini mulonge mbuli zinogile, za kuwataza wanhu,
muladi mbuli zimulonga ziwataze kamba viilondeka kwa awo wozihulika.
30 Sekemumtende Loho Yang'alile wa Mulungu, yanyunyuwale kwavija
Loho ayo kilaguso cha Mulungu kuwa mweye mwa wanhu zake. Nayo Loho
kolagusa kuwa siku yovika Mulungu kowatenda mulekesigwe.
31 Sekeukone usungu, sekemuding'huke na kugevuzika. Sekemuibamilile
hebu kuiliga, sekemuihile kwa mbuli yoyose.
32 Lakini muyonele bazi na kuinogela, na kila munhu yagele kumgongo
gehile ga miyage, kamba Mulungu viyazigelile kumgongo nzambi zenu,
kubitila Kilisito.

# 5

*Kukala mna umulenge*

1 Avo muigale na Mulungu, kwavija mweye mwa wanage yowanogela.
2 Ugima wenu ulongozigwe na unogelwa, kamba Kilisito viyatunogele
na mbuli yetu kailava mwenyego kamba nhunza inung'hila goya na nhosa
imnogela Mulungu.
3 Kwavija mweye mwa wanhu wa Mulungu, mbuli ya ugoni, uchafu
wowose hebu ugila, sekevilongigwe kumwenu.
4 Sekemulonge mbuli zigela kinyala hebu mbuli za ubozi hebu utalazi
wa maligo, gose gago haganogile kumwenu. Lakini mbuli za kumgwaa
nhogolwa Mulungu azo zinogile.
5 Mujuwe goya, munhu yotenda ugoni, hebu mchafu hebu msede, ugila
uigala na kuvitambikila vinyago. Wanhu wotenda mbuli azo honda wawe
na fungu Muundewa wa Kilisito na wa Mulungu.
6 Sekemutogole munhu yawavizile kwa mbuli za ubozi, kwavija
kwa mbuli azo ng'hasiliki ya Mulungu yowezila wanhu wose woleka
kumtegeleza.
7 Avo sekemutende nao mbuli yoyose.
8 Aho umwaka mweye mukala mdiziza, lakini sambi mokala kumulenge
kwa kuilumba na Mndewa. Avo mukale kamba wanhu wa mulenge,
9 kwavija mulenge wogala kutenda mbuli zinogile, kutenda goyolonda
Mulungu na ukweli.

10 Mugeze kugajuwa gaja gomnogela Mulungu.
11 Sekemutende sang'hano zihile za mdiziza, lakini zilaveni kunze kuna umulenge.
12 Mbuli zitendigwa kwa kinyelegezi, zogela kinyala kuzilonga.
13 Lakini mbuli zose zitendigwa mna umulenge, ukweli wake wogubuligwa goya,
14 kwavija kila kinhu kigubuligwe goya chokuwa mulenge. Lekaavo yolongigwa,

"Lamuka gweye uwasile,
zilibuka kwa wafile,
nayo Kilisito kokumwemwesela."

15 Avo, muitiganye vija vimukala. Sekemukale kamba wanhu wabozi, lakini kaleni kamba wanhu weli na nzewele.
16 Kisang'hanileni goya kipindi kino kimuli nacho, kwavija siku zino ziha.
17 Avo sekemuwe wabozi, lakini zahileni gaja goyolonda Mndewa mweye musang'hane.
18 Sekemukoligwe, kwavija ayo yowabananga, lakini mumemezigwe Loho Yang'alile.
19 Longeni kwa mbuli za zabuli na nyila na tenzi za kiloho, mwimbileni Mndewa nyila na zabuli kwa kumgwaa nhogolwa mmizoyo yenu.
20 Siku zose mgweleleni nhogolwa Mulungu Tata, kwa twaga da Mndewa wetu Yesu Kilisito kwa kila kinhu.

### *Watwanzi na Wakasano*

21 Kila munhu tanhu yamgese miyage mbuli ya kumtegeleza Kilisito.
22 Watwanzi wategelezeni wakasano zenu kamba kumtegeleza Mndewa.
23 Kwavija mbigalo kana udahi kwa mwehe wake, kamba vija Kilisito viyali na udahi kwa wanhu wamtogole. Nayo Kilisito mwenyego ayo yowakombola wanhu wamtogole, wanhu wamtogole awo lukuli lwake.
24 Kamba vija wanhu wamtogole Kilisito viwomtegeleza, vivija watwanzi wategelezeni wakasano zenu mna zimbuli zose.
25 Na mweye wakasano, wanogeleni wehe zenu kamba vija Kilisito viyowanogele wanhu wamtogole, na kailava mwenyego mbuli yao.
26 Katenda avo muladi yawalave kwa Mulungu, yahamambukiza kuwasunha kwa mazi kubitila mbuli yake,
27 muladi wawe wanhu wang'alile na wanogile ng'hani, wanhu weliduhu dowa, kwiha hebu chochose kili kamba acho.
28 Avo, wakasano wolondeka wawanogele wehe zao kamba viwozinogela ng'huli zao wenyego. Munhu yomnogela mwehe wake koinogela mwenyego.
29 Kuduhu munhu yoyose yolwihila lukuli lwake, lakini kolugwaa lujo na kululolesa. Nayo Kilisito vivija vivo viyowalolesa goya wanhu wamtogole,
30 kwavija tweye twa maungo ga lukuli lwake.
31 Kamba Maandiko Gang'alile vigolonga, "Kwa mbuli ino mbigalo komuleka tatake na mamake, nayo koilumba na mwehe wake, na wanhu wao wabili wokuwa kinhu kimoja."
32 Kuna ukweli ufisigwe ugubuligwe mna zimbuli zino, naniye nokona kuwa zomulonga Kilisito na kanisa jake.
33 Lakini vivija zowalonga mweye, kila mbigalo kolondeka yamnogele mwehe wake, kamba viyoinogela mwenyego, nayo mtwanzi kolondeka yamtegeleze mkasano wake.

# 6

### *Wana na tata zao na mama zao*

1 Mweye wana, wategelezeni tata zenu na mama zenu kamba viilondeka kwa wanhu wa Kilisito, kwavija mbuli ayo inoga.
2 “Wategeleze tatako na mamako,” dino dijo lagizo da ichanduso dili na nhunza,
3 “Muladi ukale goya na ukale siku nyingi mwiisi.”
4 Na mweye kina tata sekemuwagevuze wanenu ila waleleni goya na wafundizeni mafundizo ga Kilisito.

### *Watumwa na wakulu zao*

5 Watumwa wategelezeni wakulu zenu kwa kudumba na kugwaya, tendeni avo kwa moyo unogile kamba vija momsang'hanila Kilisito.
6 Tendeni vivo siyo mna ikipindi wao wowalola muladi wawatogole, lakini sang'haneni kwa moyo umoja kamba viyolonda Mulungu kwavija mweye mwa wasang'hanaji wa Kilisito.
7 Mutogole kusang'hana kwa kuwamba mbuli ya Mndewa na siyo mbuli ya wanhu.
8 Kumbukeni kuwa, Mndewa komgwaa nhunza munhu yoyose, yawe mtumwa hebu kakomboligwa mbuli ya sang'hano yake inogile.
9 Na mweye iwakulu, vivija watendeleni ganogile watumwa zenu, sekemulonge kwa kukomhoka. Kumbukeni kuwa mweye vivija kamba wao, mnayo Mndewa iija kuulanga, nayo habagula munhu.

### *Ng'hondo ya Kiloho*

10 Kisigale, nowapula mugangamale kwa kuilumba na Mndewa na kwa kutazigwa na udahi wake.
11 Soleni silaha zose zilondeka kwa kuitowela ziyowagwaa Mulungu mudahe kuuhuma ubala wihile wa Mwenembago.
12 Kwavija tweye hatuitowa na wanhu ila toitowa na nguvu za loho zihile zili kuulanga, toitowa na watawala na wakulu weli na nguvu, wotawala isi imemile.
13 Kwa mbuli ayo soleni silaha zose zilondeka kwa kuitowela ziyowagwaa Mulungu muladi yahavika siku ija ya gehile mudahe kuzihuma nguvu za ija yamwihileni, mwahaitowa mbaka kuuhelelo mokuwa mung'hali na nguvu.
14 Avo muitande goya na ukweli uwe kamba mkwiji mvigudi venu, na kutenda goyolonda Mulungu kamba kiwalo cha zuma cha kukimila mmhambaga zenu,
15 musulukile kuwapetela wanhu Mbuli Inogile kamba vilatu mmagulu genu.
16 Kipindi chose acho, mumtamanile Mulungu kamba ngao, muladi mudahe kuizima misale ikwaka ipigisigwe na ija Imdumuka.
17 Ubokeleni ukombozi kamba kofiya da kuvala mdipala, na Mbuli ya Mulungu iwe kamba panga dimugweleligwe na Loho Yang'alile.
18 Siku zose mpuleni Mulungu yawataze. Mpuleni Mulungu kipindi chose, kwa kulongozigwa na Loho. Kwa mbuli ino muitiganye sekemubwele kukisogo, siku zose wapulileni wanhu wose wa Mulungu.
19 Vivija nipulileni na niye, Mulungu yanigwee mbuli ya kulonga, muladi nidahe kuwalongela wanhu kinhu kifisigwe cha mna Imbuli Inogile bila kudumba.
20 Niye na msenga wa Mbuli ino Inogile, hamoja sambi na mkifungo. Mnipulile nidahe kulonga Mbuli Inogile inilondeka bila kudumba.

*Kimambukizo cha kuilamusa*

21 Ndugu yangu Tukiko inimnogela na msang'hanaji yomtamanila Mulungu mwiisang'hano ya Mndewa, kowalongela mbuli zangu zose, muladi mujuwe kija kinhenda.

22 Lekaavo nomtuma kumwenu yawalongele mbuli zetu, na yawagangamize.

23 Mulungu Tata na Mndewa Yesu Kilisito wawagwee wanhu wose wamtogole Yesu tindiwalo na unogelwa kwa kutamanila.

24 Ng'hekewa ya Mulungu ikale na wanhu wose womnogela Mndewa wetu Yesu Kilisito kwa unogelwa wa mazuwa gose.

# Baluwa ya Paulo kwa wanhu wa ako Filipi

## Ulongozi

Paulo kandika baluwa ino kwa wanhu wamtogole Yesu ako Filipi behi na mwaka wa 61 toka kuvumbuka kwa Kilisito viyakalile mkifungo (Sula ya 1:13) yogesigwa kayandikila ako Lumi. Baluwa ino wandikiligwa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu kudibuga da Filipi. Todaha kujuwa mbuli kidogo za buga da Filipi kulawa mna ikitabu cha Sang'hano za Iwatumigwa. Filipi dijo buga kulu mwiisi ya Makedonia. Vivija acho kibumbila cha ichanduso cha wanhu wamtogole Yesu mwiisi ya Makedonia. Paulo na Sila wao wakisongile kibumbila acho cha wanhu wamtogole Yesu na wakala wekigwe mkifungo kwa siku dimoja viwakalile kuko (Sang'hano 16).

Paulo kakala na vilamuso vingi va kwandika baluwa ino. Katumia nyafasi ayo kuwagwaa asente kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu kuko mbuli ya nhunza ziwamtumile viwahulike kakala mkifungo (Sula ya 4:10-19). Vivija kalonda wajuwe mbuli vizigendelela ako mkifungo na kalonda wamjuwe Timoseo na Epafuladito mkibumbila cha wanhu wamtogole Yesu (Sula ya 2:19-30) muladi wawabokele na wawategeleze viwowalongoza.

**Mbuli zili mkitabu**

Paulo kosonga baluwa yake kwa kuwalamusa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu ako Filipi (Sula ya 1:1-2).

Abaho kalonda wajuwe mbuli vizigendelela kumwake na mbuli ziyolonda kusang'hana (Sula ya 1:3-2:30).

Abaho kowagwaa malagizo golondigwa kwa wanhu wamtogole Yesu (Sula ya 3:1-4:9).

Paulo komambukiza kwa kuwagwaa asente kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu ako Filipi mbuli ya nhunza zao na kowalamusa (Sula ya 4:10-23).

1 Niye Paulo na Timoseo, twa wasang'hanaji wa Yesu Kilisito, towandikila mweye wanhu wa Mulungu muli ako Filipi, mweye muilumbile na Yesu Kilisito, hamoja na walangulizi na watazaji wa wanhu wamtogole Yesu.

2 Mulungu Tataetu na Mndewa Yesu Kilisito wawagwee ng'hekewa na tindiwalo.

*Paulo kowapulila wanhu wamtogole Yesu*

3 Kila nahawagesa mweye nomtogola Mulungu,

4 nahawapulila mweye mose kwa Mulungu, nowapulileni kwa deng'ho,

5 kwavija mweye muilumba na niye muisang'hano ya kubwililisa Mbuli Inogile kulawa haichanduso mbaka sambi.

6 Nabule shaka kwa Mulungu yaisongile sang'hano ino inogile mmizoyo yenu, koigendeleza mbaka vondaimale mna isiku ya kubwela Yesu Kilisito.

7 Kwavija mwa muumoyo wangu, vinoga kumwangu kuwagesa, hata kamba namkifungo hebu ndekesigwa, mweye mose muilumba na niye mna ing'hekewa iyanigwelele Mulungu ya kuigombela Mbuli Inogile na kulagusa ukweli wake kwa wanhu.

8 Mulungu ayo yajuwile nolonga fulu ipile vija viniwasulukila kuwona kwa unogelwa ulawa kwa Yesu Kilisito.

9 Nompula Mulungu unogelwa wenu wengezeke ng'hani, na muwe wabala ng'hani na nzewele zose,

10 muladi mudahe kusagula kinhu kinogile. Baho mong'ala na mokuwa
mduhu kitala chochose mbaka mna isiku ya kubwela Kilisito.
11 Baho mutende mbuli zinogile mgameso ga Mulungu, mbuli azo zolawa
kwa Yesu Kilisito yaiyeka, muladi wanhu wose wamgwee Mulungu ukulu
na nhogolwa.

### *Paulo kodeng'helela kupetigwa kwa Kilisito*

12 Ndugu zangu nolonda mujuwe kuwa, kindawilile niye acho kitendile
Mbuli Inogile ipetigwe.
13 Kwa mbuli ayo wakalizi wose wa ng'anda ya kindewa na wanhu wose
wayagwe wojuwa niye na mkifungo mbuli ya Kilisito.
14 Kufungigwa kwangu, kuwatenda ndugu bwando wamtamanile ng'hani
Mndewa, na wageligwa moyo wawe magalu kulonga mbuli ya Mulungu bila
kudumba.
15 Kulonga ukweli wanhu wayagwe woipeta Mbuli ya Kilisito kwa
migongo na ndwagi, lakini wayagwe woipeta vinogile.
16 Awo woipeta vinogile wotenda avo kwa unogelwa, kwavija wojuwa
Mulungu kanigwaa sang'hano ya kuigombela Mbuli Inogile.
17 Lakini awo wayagwe woupeta usenga wa Kilisito kwa kuitapa, waduhu
ukweli, wogesa kuwa wodaha kunyongezela madununzo gangu mkifungo.
18 Niye sitonga bule, niye nodeng'helela kwavija kwa nzila yoyose wanhu
wopeta usenga wa Kilisito, iwe woupeta kwa kilamuso kinogile hebu kwa
kilamuso kihile. Niye sileka kudeng'helela bule,
19 kwavija nojuwa kwa kumpula kwenu Mulungu na kutazigwa na Loho
wa Yesu Kilisito, nolekesigwa.
20 Vinikona niye notamanila kuwa honda nigwe kinyala lakini noganga-
mala ng'hani, avo sambi kamba viili siku zose iwe muugima hebu mwiifa
nimgwee ukulu Kilisito.
21 Kwavija kumwangu niye kuwa mgima ni kumsang'hanila Kilisito na
kufa konyongezela kinhu.
22 Kamba nahagendelela kuwa mgima mulukuli luno, sang'hano yangu
yokongezeka ng'hani. Mmhane nisagule choni!
23 Miyenu na mnzila mhanda. Kuno nolonda kusegela na kukala na
Kilisito, mbuli ayo ibanga kunoga,
24 lakini vinoga ng'hani kumwenu kamba nahagendelela kuwa mgima.
25 Nojuwa ukweli wa mbuli ino, nojuwa nokuwa mgima na nogendelela
kukala hamoja na mweye mose muladi tamanilo jenu na deng'ho jenu
vongezeke,
26 muladi nahawa na mweye kabili, mbuli ya niye mokuwa na kinhu cha
kuigodela mna ukuilumba kwenu na Yesu Kilisito.
27 Avo kinhu kilondeka hano mbuli zenu ziigale kamba viilonda mbuli
inogile ya Kilisito, kamba nahadaha kwiza kuwalola hebu nahawahulika,
nojuwa kuwa mose mogangamala hamoja kwa loho imoja na kudigombela
hamoja tamanilo dilawa kwa Mbuli Inogile.
28 Avo sekemuwadumbe wanhu wowehila, siku zose muwe magalu na ino
yolagusa kumwao awo wopotela na mweye mokomboligwa, kwavija mbuli
ayo yolawa kwa Mulungu.
29 Kwavija mweye mugweleligwa kwa mbuli ya kumsang'hanila Kilisito,
siyo kumtamanila kwiiyeka lakini vivija kugaya mbuli yake.
30 Sambi mweye muilumba na niye mna ing'ondo ya kuigombela Mbuli
Inogile. Ng'ondo ayo iyo ija yumunyonile nayo aho haichanduso na mbaka
sambi ning'hali mwiing'ondo ayo.

# 2

*Ukulu na uhole wa Kilisito*

1 Kamba mwahailumba na Kilisito na kugangamala, kamba unogelwa wake wowasamhusa, kamba moilumba na Loho Yang'alile na kamba mwahawa na mizoyo inogile na kuyonela bazi mweye kwa mweye,

2 avo itendeni ndeng'helelo yangu yenele kwa kugesa kinhu kimoja na unogelwa umoja na moyo umoja na muwe na nzewele imoja.

3 Sekemuwe na gahigahi hebu magoda gelibule kinhu, lakini kwa uhole muwagese wayagwe kuwa wanoga kubanza mweye.

4 Kila munhu sekeyalole kiyolonda mwenyego kiiyeka, lakini vivija yalole kiwolonda wanhu wayagwe.

5 Mugese kamba viyagesile Yesu Kilisito.

6 Kilisito viyali kakala kweli Mulungu,
lakini hagesile bule kamba kuigala na Mulungu kinhu cha kunanahila,
7 lakini kwa kulonda mwenyego,
kaleka vinhu avo vose kaitenda kamba viyali mtumwa,
kaleligwa kamba viwoleligwa wanhu,
kaoneka kwa kihanga cha wanhu.
8 Kaitenda mwenyego mdodo, munhu yotegeleza mbaka ifa yake,
ona ifa yake mumsalaba.
9 Lekaavo Mulungu kamwinula mbaka uchanha ng'hani,
kamgwaa twaga kulu kubanza matwaga gose.
10 Avo kwa ukulu wa twaga da Yesu,
vinhu vose viumbigwe, vili kuulanga na vili mwiisi na kuwochola wanhu wafile,
vose vimfugamile,
11 na kila lulimi lulonge kuwa Yesu Kilisito ayo Mndewa,
kwa ukulu wa Mulungu Tata.

*Mumwemwese kamba mulenge*

12 Mbwiga zangu siku zose vinikalile na mweye munitegeleza, na hata sambi nakutali na mweye wambeni kunitegeleza. Kwa bwembwe na kugwaya sang'haneni muladi ukombozi wenu utelele,

13 kwavija Mulungu ayo yosang'hana siku zose mgati mmwenu, kuwatenda musulukile kusang'hana kamba viyolonda mwenyego.

14 Tendeni kila kinhu bila kuiyalala hebu kuibamilila,

18 Mwanangu Timoseo nokugwaa lagizo dino, kulawa mna zimbuli zilongigwe na wanhu wa Mulungu baho umwaka mbuli yako. Sang'hanila mbuli zizo kamba mgoha wa kuitowela goya Mbuli Inogile,
19 na goga kutamanila kwako na moyo wako uleka kukutagusa kamba kubananga. Wanhu wayagwe wagaleka higo na wabananga kutamanila kwao.
20 Mna iwanhu awo wamumo Humenayo na Alekizanda waniwataguse kwa kuwagela mmakono ga Mwenembago, muladi wafunzigwe sambi wamulige Mulungu.

# 2

*Mafundizo ga kumtambikila Mulungu*

1 Tanhu, mulongeleni Mulungu gaja gomulonda, mumpule Mulungu na muwapulile wanhu wayagwe na mumgwee nhogolwa kwa sama ya wanhu wose,
2 mpuleni Mulungu kwa sama ya wandewa na wanhu wose wayagwe weli na ukulu mziisi, muladi tukale na tindiwalo na tukale moyo hole na kumdumba Mulungu na kutenda ganogile.
3 Mbuli ayo inoga na yomnogela Mulungu Mkombola wetu,
4 yolonda wanhu wose wakomboligwe na waujuwe ukweli.
5 Kwavija hana Mulungu imoja na hana imoja yotenda Mulungu na wanhu wailumbe, munhu ayo Yesu Kilisito,
6 yailavile mwenyego kutenda wanhu wose wakomboligwe, mbuli ino ayo iyalaguse Mulungu mna ikipindi kinogile.

[7] Lekaavo nhumigwa kamba mtumigwa na mfundiza kwa wanhu haweli Wayahudi, kuwapetela usenga wa kutamanila na ukweli. Niye siviza bule, nolonga ukweli!

[8] Avo mwahaiting'hana kumtambikila Mulungu, nolonda wanhu wailavile kwa Mulungu na wodaha kwinula makono gao na kumpula Mulungu bila kugevuzika hebu bamila.

[9] Vivija nolonda watwanzi wavale goya viwalo vao na wawe na nzewele, siyo kwa kugesa kuluka mvili kwa zahabu na lulu hebu viwalo va bei ng'hulu,

[10] lakini kwa sang'hano zinogile, kamba viilondeka kwa watwanzi womtambikila Mulungu.

[11] Watwanzi wolondeka wanyamale kipindi munhu iyagwe kolonga na waifunze kwa uhole.

[12] Niye siwatogolela bule watwanzi wafundize hebu wawe na ukulu kwa wambigalo, wolondeka wanyamale kipindi munhu iyagwe kolonga.

[13] Kwavija Adamu heyo yasongile kuumbigwa, abaho Hawa.

[14] Vivija siyo Adamu ayo yaviziligwe ila mtwanzi ayo yaviziligwe na kabena lagizo da Mulungu.

[15] Lakini mtwanzi kokalizigwa kipindi viyolela wana, kamba yahagendelela kukala kwa kutamanila na kung'ala na unogelwa na kwa kutenda gago gose kwa kugesa vinogile.

# 3

### *Walangulizi wa wanhu wamtogole Yesu*

[1] Ulonzi uno wa ukweli, munhu yosulukila kuwa mulangulizi wa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu, kosulukila sang'hano inogile.

[2] Mulangulizi wa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu kolondeka sekeyalongigwe vihile na wanhu, kolondeka yawe na mwehe imoja, yailongoze mwenyego na yawe na nzewele, yawe kotegelezigwa na yawagoneke wanhu baki mng'anda mmwake na yadahe kufundiza wanhu.

[3] Sekeyakoligwe hebu ndwagi, lakini yawe muhole na kukala moyo hole na wanhu, kolondeka sekeyazinogele sente.

[4] Kolondeka yawe munhu yodaha kuwalongoza goya wanhu wa mng'anda mmwake na kuwatenda wanage wamtegeleze kwa kila kinhu.

[5] Kamba munhu hadaha kuwalongoza goya wanhu wa mng'anda mmwake, kodahaze kuwalola goya wanhu wa Mulungu?

[6] Kolondeka sekeyawe munhu yamtogole Yesu sambi sambi, kwavija kodaha kuitapa na kutagusigwa kamba viyatagusigwe Mwenembago.

[7] Kolondeka yawe munhu yotegelezigwa na wanhu weli kunze ya mting'hano wa wanhu wamtogole Yesu, muladi sekeyehuligwe na kwingila mumtego wa Mwenembago.

### *Watazaji wa vibumbila va wanhu wamtogole Yesu*

[8] Watazaji wa wanhu wamtogole Yesu wolondeka wawe na tabiya inogile na watamaniligwe, sekewang'we ng'hani hebu umelo wa sente.

[9] Wolondeka wagoge ukweli wa kutamanila ugubuligwe kwa mizoyo ileka kutagusa kuwa wabananga.

[10] Tanhu wolondeka wagezigwe, wahakoneka wofaya wasang'hane kamba watazaji wa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu.

[11] Vivija wehe zao wolondeka wawe na tabiya inogile sekewawalonge wanhu vihile, wailongoze wenyego na wotenda gaja gawalongile mzimbuli zose.

12 Mtazaji wa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu yawe na mwehe
imoja na yadahe kuwalongoza goya wanage na wanhu wose wokala
mng'anda yake.
13 Watazaji wosang'hana goya sang'hano yao, wodaha kwima goya na
wodaha kulonga kwa kugangamala mbuli ya kutamanila kwao kwa Yesu
Kilisito.

### *Ukweli ugubuligwe*

14 Vinikwandika baluwa ino, nogesa kwiza kumwako sambi baha.
15 Lakini nahakawa, baluwa ino yowalongela vija viilondeka tweye tu-
sang'hane mna ing'anda ya Mulungu nayo ayo wanhu wamtogole Mulungu
yeli mgima, yeli mhanda na chandusilo cha ukweli wose.
16 Kuduhu shaka mbuli ya vinhu vifisigwe va kutamanila kwetu.
Koneka mulukuli lwa kiunhu,
kalagusigwa na Loho Yang'alile kuwa kotenda ganogile,
koneka na wasenga wa kuulanga.
Mbuli zake zipetigwa mziisi zose,
katogoligwa mwiisi yose,
kagaligwa kuulanga.

## 4

### *Wafundiza wa uvizi*

1 Loho Yang'alile kolonga fulu ipile kuwa baho kumwande wanhu
wayagwe woleka kutamanila, na wozitegeleza loho za uvizi na kugoga
mafundizo ga vinyamkela.
2 Mafundizo kamba gago gogaligwa na wanhu wanafiki na wavizi, mizoyo
yao ileka kuwatagusa kuwa wabananga isomigwa na zuma da moto.
3 Wanhu awo wofundiza kuwa havinogile kusola na kuja lujo fulani.
Lakini Mulungu kaumba vinhu vose vidigwe na vibokeligwe kwa kumgwaa
nhogolwa na awo wamtogole Yesu na kujuwa ukweli.
4 Kila kinhu kiyaumbile Mulungu kinoga, kuduhu kilondeka kulemigwa,
lakini kila kinhu chobokeligwa kwa kumgwaa nhogolwa Mulungu,
5 kwavija imbuli ya Mulungu na kumpula votenda kinhu acho kitogoligwe
na Mulungu.

### *Msang'hanaji yanogile wa Yesu Kilisito*

6 Kamba uhawagwaa mafundizo gano wanhu wamtogole Yesu, kokuwa
msang'hanaji yanogile wa Yesu Kilisito na uhagendelela kukula kiloho kwa
mbuli za kutamanila na mafundizo ga ukweli gaukweleleze.
7 Iteganyeni na simo hazili mna ukutamanila na zaduhu kinhu. Izoweze
kukala muugima wa kumgwaa ukulu Mulungu.
8 Mazoezi galukuli ganoga, lakini kukala kwa kumnogeza Mulungu
kunoga ng'hani, kwavija kotwikila ugima wa sambi na wa kuko kumwande.
9 Ulonzi awo wa ukweli na wolondeka kutogoligwa.
10 Tweye toiyoha kusang'hana ng'hani, kwavija tomulolela Mulungu yeli
mgima, Mkombola wa wose na ng'hani ng'hani kwa hewo wamtogole Yesu.
11 Uwalagize na uwafunze mbuli azo.
12 Sekeutogole munhu yakubeze kwavija gweye kwa mbwanga, lakini
uwe kilaguso kwa wanhu wamtogole Yesu, kwa ulonzi wako na sang'hano
zako na unogelwa wako na kutamanila kwako na ugima unogile.
13 Mbaka vondanize, sang'hanila kipindi chako kwa kusoma Maandiko
Gang'alile mgameso ga wanhu na kuwapetela wanhu na kuwafundiza.

14 Sambiuileme nhunza ya Loho Yang'alile ili mgati mmwako, yuug-
weleligwe kubitila mbuli za wavele za ulaguzi viwakwikile makono gao.
15 Gesa goya kwa sama ya mbuli azo na uzisang'hane muladi kugendelela
kwako koneke na wanhu wose.
16 Uiteganye mwenyego na mafundizo gako. Gendelela kusang'hana
mbuli zino, kwavija uhasang'hana koikombola mwenyego na waja
wokutegeleza.

# 5

*Viilondeka kukala na wayago wamtogole Kilisito*

1 Sekeumkomhokele munhu mvele, lakini umzume kamba tatako. Waten-
dele wabwanga wayago kamba ndugu zako.
2 Watendele watwanzi wavele kamba mama zako na watendele wandele
kamba lumbu zako, bila kuwasulukila.
3 Walolese goya wagane waliduhu kinhu chochose.
4 Lakini kamba mgane kana wana hebu wazukulu, awo wolondeka
kuwalola goya wanhu wa mng'anda mmwao kamba viyolonda Mulungu.
Kwa kutenda vivo kamba wowalipa tata zao na mama zao na wavele wao,
kwa gaja gawawatendele, kwavija mbuli ayo yomnogela Mulungu.
5 Mgane yeli yaiyeka, yaliduhu munhu wa kumulolesa, ayo komulolela
Mulungu na kogendelela kumpula Mulungu yamtaze imisi na ikilo.
6 Lakini mgane yokala kwa ugima wa kumnogela mwenyego kafa kamala,
hamoja yang'hali mgima.
7 Walagize wanhu awo wasang'hane mbuli azo, avo munhu yoyose
sekeyawalonge vihile.
8 Kamba munhu yoyose hawatonga wanhu wa lukolo lwake, ng'hani
ng'hani awo weli mng'anda mmwake, munhu ayo kakubeza kutamanila na
keha ng'hani kubanza imunhu hamtogola Yesu.
9 Sambiujandike twaga da mgane mna ikitabu cha matwaga ga wagane
mbaka yavikize miyaka malongo sita. Vivija yawe mwehe wa mbigalo
imoja.
10 Yawe na tabia inogile, yawe mtwanzi yawalelile goya wanage, yawe
mbokela wageni, yawe muhole na kowasang'hanila wanhu wayagwe
wamtogole Yesu, yawe munhu yowataza wayagwe mna gamagayo, na
yailave mwenyego kutenda ganogile.
11 Sekemuwengize mkibumbila wagane wandele, kwavija wahasulukila
kusoligwa, womuleka Kilisito,
12 avo woitagusa wenyego kwa kubena lagizo diwalongile.
13 Vivija wagane kamba awo wosonga kuwa wanyeke na wokwanga
mzikae za wanhu kipindi chose na kulonga mbuli hawalondigwa kwa
kuwalonga vihile wanhu na kuigela mzimbuli za wanhu wayagwe.
14 Avo niye ninogeligwa ng'hani wagane wandele wasoligwe na walele
wana, na wakalize goya ng'anda zao, avo seketuwagwee wanhu watwihile
kilamuso cha kulonga vihile.
15 Kwavija wagane wayagwe wahinduka na kumkweleleza Mwenembago.
16 Kamba mtwanzi yoyose yamtogole Yesu kana wagane mulukolo lwake,
kolondeka yawalolese na sekeyawagwee mzigo kibumbila cha wanhu
wamtogole Yesu, avo wanhu wamtogole Yesu wadahe kuwalolesa wagane
waliduhu wanhu wa kuwataza.
17 Wavele wowalongoza wanhu wamtogole Yesu wosang'hana vinogile,
wolondeka wapate fungu kulu, ng'hani ng'hani waja wosang'hana ng'hani
kuwapetela wanhu na kuwafundiza.

18 Kwavija Maandiko Gang'alile golonga, “Sekeumfunge ng'ombe mulomo
wahamsang'hanila kuhulula uhemba.” Vivija golonga, “Msang'hanaji yag-
weleligwe fungu jake.”
19 Sekeutegeleze vitala vilavigwa kwa mvele yowalongoza kibumbila cha
wanhu wamtogole Yesu mbaka vigaligwe na wanhu wabili hebu wadatu
wavonile.
20 Wanhu wose wotenda nzambi, wazume mgameso ga wanhu, muladi
wanhu wayagwe wadumbe.
21 Nokulagiza mgameso ga Mulungu na mgameso ga Yesu Kilisito na
mgameso ga wasenga wang'alile wa kuulanga, gagoge gano ganikulongele,
bila kutagusa kwa kulola kihanga cha munhu yoyose hebu kulagusa uno-
gelwa ng'hani kwa munhu yoyose.
22 Sekeulopole kumwikila makono munhu yoyose yailavile
kumsang'hanila Mndewa. Sekeuilumbe na munhu yoyose mzinzambi.
Ukale kwa kumnogela Mulungu.
23 Sambiung'we mazi gaiyeka, lakini ung'we divai mbuli ya inda yako,
kwavija kolumwa lumwa.
24 Nzambi za wanhu wayagwe zokoneka kunze kunze, wang'hali
hawanatagusigwa. Lakini nzambi za wanhu wayagwe zokoneka
kumwande.
25 Vivo ili, kwa ganogile gokoneka kunze kunze na hata kamba ha-
gakoneka hagadaha kufisigwa.

# 6

1 Waja weli watumwa wolondeka wawategeleze wakulu zao kwa kila
mbuli, muladi wanhu sekewadilige twaga da Mulungu na mafundizo getu.
2 Watumwa weli na wakulu wamtogole Yesu sekewawabeze, kwavija
sambi wose wotogola Kilisito. Wolondeka wawasang'hanile vinogile, kwav-
ija waja womweda kwa sang'hano yao ni wanhu wamtogole Yesu awo
wowanogela. Uwafundize na uwapetele wanhu mbuli zino.

### *Mafundizo ga uvizi*

3 Munhu yoyose yofundiza viyagwe na hazitogola mbuli za ukweli za
Mndewa wetu Yesu Kilisito na vivija hagatogola mafundizo ga Mulungu
wetu,
4 munhu ayo kamema magoda na hajuwa kinhu chochose. Ayo mtatali wa
kuibamilila na ndwagi mbuli ya mbuli, mbuli azo zogala migongo, kugomba,
maligo na magesa gehile,
5 na kuibamilila siku zose kwa wanhu wabanangike nzewele na waduhu
ukweli na wogesa kuwa kumsang'hanila Mulungu ayo nzila ya kupata ugoli.
6 Ona, kumsang'hanila Mulungu komtenda munhu yawe mgoli kamba
yahenela na vinhu viyalinavo.
7 Hatugalile kinhu chochose mwiisi wala honda tusegele na kinhu cho-
chose.
8 Avo twahawa na lujo na viwalo, tolondeka twenele navo.
9 Lakini waja wolonda kuwa wagoli wokwingila mna ukugezigwa na
wonamata mumtego wa kusulukila vinhu kwa ubozi, navo vowakwega
mbaka kuna ukunangika na kufa.
10 Kwavija kuzinogela sente ng'hani acho chanduso cha nzambi zose.
Wanhu wayagwe wasulukila ng'hani kupata sente mbaka wapotela kutali
na tamanilo na mizoyo yao imema kunyunyuwala ng'hani.

### *Paulo komulongela Timoseo viyolondeka kutenda*

11 Lakini gweye munhu wa Mulungu, vigwale vinhu vose avo. Goga
kutenda goyolonda Mulungu, kumgwaa ukulu Mulungu, kutamanila, uno-
gelwa, kubetela kwa kufunga umoyo na uhole.
12 Wamba ng'hani kugahuma magayo goupata mbuli ya kutamanila
kwako, muladi upate ugima wa mazuwa gose. Kwavija ugima uno awo
uyakukemele Mulungu viutogole kumtamanila Kilisito mgameso ga wanhu
wengi wakalile aho.
13 Nokulagiza mgameso ga Mulungu, yovigwaa ugima vinhu vose, na
nokulagiza mgameso ga Yesu Kilisito, yalongile kwa mulomo wake mbuli ya
tamanilo jake mgameso ga Pontio Pilato,
14 nokulagiza ugagoge malagizo na kugategeleza goya mbaka siku dija
vonda yabwele Mndewa wetu Yesu Kilisito.
15 Yesu kolawilila mna ikipindi kinogile kikigwe na Mulungu, yofaya
kutogoligwa na yeli yaiyeka Mtawala, Mndewa wa iwandewa na Mkulu wa
iwakulu.
16 Heyo yaiyeka yeli mgima siku zose, yakalaga kuna umulenge uleka
kuvikigwa na munhu. Kuduhu munhu yamonile, kuduhu yodaha kumona.
Kumwake uwe ukulu na kutegelezigwa siku zose! Ona.
17 Walagize wanhu weli wagoli wa vinhu va mwiisi ino sekewaitape,
na kulolela vinhu avo, lakini wamulolele Mulungu yeli na moyo unogile
yotugwaa kila kinhu tudeng'helele.
18 Walagize watende ganogile, wawe wagoli kwa kutenda ganogile, wawe
na moyo unogile na watogole kuwagwaa wayagwe vinhu vao.
19 Kwa kutenda vivo woikila ngama inogile kuko kumwande, avo wadahe
kupata ugima, uli ugima wa ukweli.
20 Gweye Timoseo, vilole goya vose viugweleligwe uvilolese. Iteganye
na ulonzi wa chaka chaka na kuibamilila kwa mbuli za kibozi, mbuli azo
wayagwe wozikema kwa uvizi “Ubala.”
21 Kwavija wanhu wayagwe waitenda kuwa na ubala awo na kukimam-
bukizo wagiza kutamanila.
Ng'hekewa ya Mulungu ikale na mweye mose.

# Baluwa ya Kabili ya Paulo kwa Timoseo

## Ulongozi

Kitabu cha kabili kwa Timoseo ni baluwa ya kabili ya mtumigwa Paulo kwa mwanahina wake Timoseo. Baluwa ya kabili kwa Timoseo yandikigwa mna ikipindi behi na uhelelo wa ugima wa Paulo. Kipindi acho Paulo kakala mkifungo ako Lumi (Sula ya 1:16). Paulo kakala yailumbile ng'hani na Timoseo na kamkema mwanage (Fil 2:22, 1 Tim 1:2, 1:18).

Ino ayo baluwa iyagwe mna izibaluwa nne za Paulo ziyandike kwa munhu imoja imoja badala ya kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu. Baluwa ndatu ziyagwe azo 1 Timoseo na Tito na Filimoni. Kipindi baluwa ya kabili kwa Timoseo yokwandikigwa wanhu wamtogole Yesu wakala wodununzigwa mwiisi ya Lumi. Sengine kino acho kilamuso cha Paulo kukala mkifungo na kamulagiza Timoseo yafunge umoyo mbuli ya kugaya kwake. Kamba viikalile kwa baluwa ya ichanduso kwa Timoseo, Paulo komzuma ng'hani Timoseo mbuli ya wafundiza wa uvizi (1 Tim 1:16-18). Vivija komulongela Timoseo kuwa kokuwa na kipindi kidala ako kumwande (Sula ya 3:1).

**Mbuli zili mkitabu**

Paulo kosonga kwa kumulamusa Timoseo na kumgela moyo (Sula ya 1:1-18).

Abaho komulongela yafunge umoyo (Sula ya 2:1-13).

Abaho komulagiza malagizo gayagwe mbuli ya kumtamanila Kilisito (Sula ya 2:14-26).

Abaho komzuma mbuli ya mbuli za ako kumwande na viilondeka kutenda (Sula ya 3:1-4:8).

Paulo komambukiza kwa kumulagiza Timoseo heyo mwenyego (Sula ya 4:9-24).

1 Niye Paulo, namtumigwa wa Yesu Kilisito kwa kulonda Mulungu, nhumigwa niwalongele wanhu ugima uja ulongigwe na Mulungu kotugwaa kwa kuilumba na Yesu Kilisito.
2 Nokwandikila gweye Timoseo mwanangu inikunogela ng'hani.
Mulungu Tataetu na Mndewa wetu Yesu Kilisito wakugwee ng'hekewa na bazi na tindiwalo.

*Paulo komgela moyo Timoseo*

3 Nomtogola Mulungu, inimsang'hanila kwa moyo uleka kunitagusa kuwa nibananga kamba viwatendile wahenga zangu. Nomtogola vinikukumbuka gweye siku zose mna ukumpula kwangu imisi na ikilo.
4 Nogakumbuka mahozi gako na nolonda kukona, muladi nimeme deng'ho.
5 Nokumbuka kutamanila kwako kwa ukweli, kutamanila kuwakalile nako bibi yako Loisi na mamako Enike, nojuwa kuwa na gweye vivija kunako.
6 Kwa mbuli ino nokukumbusa uikong'heze nhuza iyakugwee Mulungu vinikwikile makono gangu.
7 Kwavija Loho Yang'alile iyatugwee Mulungu hatugela bwembwe, lakini kotugwaa nguvu na unogelwa na kuilongoza wenyego.
8 Avo sekeukone kinyala kuwalongela wanhu mbuli ya Mndewa, na sekeukone kinyala kuilumba na niye mfungwa wake, lakini ilumbe na niye

mna ukugaya mbuli ya Mbuli Inogile, kamba Mulungu viyokugwaa nguvu
ya kutenda vivo.
9 Mulungu katukombola na katukema tuwe wanhu zake, siyo mbuli ya
gaja gatusang'hane, lakini mbuli ya magesa gake mwenyego na ng'hekewa
yake. Isi ing'hali hainaumbigwa katugwaa ng'hekewa kubitila Yesu Kilisito.
10 Lakini sambi ng'hekewa yake igubuligwa kumwetu kubitila kwiza kwa
Mkombola wetu Yesu Kilisito. Kauhuma udahi wa ifa, na kubitila Mbuli
Inogile kaugubula ugima uliduhu ifa.
11 Mulungu kanisagula niwe mtumigwa na mfundiza, niwapetele wanhu
Mbuli Inogile.
12 Kwa mbuli ayo, nodununzika kamba vino, lakini sikona kinyala, kwav-
ija nimjuwa inimtamanila, na nomjuwa goya kodaha kukika goya kija
kiyanigwee mbaka siku dija da kubwela kwake.
13 Zigoge mbuli za ukweli zinikufundize kamba kinhu kinogile cha kuk-
weleleza, na usigale mna ukutamanila na unogelwa uli mna ukuilumba na
Yesu Kilisito.
14 Kinhu kija kiugweleligwe, ukilolese kwa udahi wa Loho Yang'alile,
yokala mgati mmwetu.
15 Gweye kojuwa kamba wanhu wose wamtogole Yesu wokala Asiya
hamoja na Figelo na Helimogene wandeka.
16 Nompula Mulungu yawonele bazi wanhu wa mng'anda ya Onesifoli,
kwavija kanisamhusa miyanza mingi na hanyonele kinyala kwavija ng'hala
mkifungo.
17 Lakini bahaja viyavikile kudibuga da Lumi, kanizahila mbaka kanyona.
18 Nompula Mndewa yamonele bazi mna disiku da nhaguso. Na gweye
kojuwa goya vija viyanisang'hanile ako Efeso.

# 2

*Mkalizi yanogile wa Yesu Kilisito*

1 Avo gweye mwanangu Timoseo, gangamala mna ing'hekewa itulinayo
mna ukuilumba na Yesu Kilisito.
2 Mafundizo gaja gauhulike nowapetela wanhu mgameso ga wanhu
wengi, uwafunze gago wanhu wotamaniligwa, wodaha kuwafunza
wayagwe vivija.
3 Funga umoyo mna gamagayo hamoja na tweye kamba mkalizi yanogile
wa Yesu Kilisito.
4 Mkalizi mna ing'hondo koleka sang'hano za ugima wa siku zose muladi
yamnogeze mkulu wa wakalizi.
5 Vivija munhu yokimbila kwa kuihuma hagweleligwa fungu mbaka
yamambukize kwa kukweleleza malagizo ga kuihuma.
6 Mlimaji yosang'hana ng'hani kolondeka yawe wa ichanduso kupata vija
visengigwe.
7 Gesa gano gonilonga, kwavija Mndewa kokutenda udahe kugajuwa gose.
8 Mkumbuke Yesu Kilisito, yazilibuke kwa wafile, yakalile mulukolo lwa
Daudi, kamba viilonga Mbuli Inogile inipeta.
9 Kwavija nowapetela wanhu Mbuli Inogile nodununzika na ngodekigwa
kamba vija munhu yatendile gehile, lakini Mbuli ya Mulungu haigodekigwa
bule.
10 Avo nofunga umoyo kila kinhu mbuli ya wanhu wasaguligwe na Mu-
lungu, muladi wapate ukombozi ulawa kwa Yesu Kilisito na kugala ukulu
wa mazuwa gose.

11 Ulonzi uno waukweli,
“Kamba tufa hamoja na Kilisito,
vivija tokuwa wagima hamoja nayo.
12 Kamba twahagendelela kufunga umoyo,
vivija totawala hamoja nayo.
Kamba twahambela,
na heyo vivija kotubela.
13 Kamba tweye hatutamaniligwa,
heyo kotamaniligwa,
kwavija hadaha kuviza.”

### *Msang'hanaji yatogoligwe na Mulungu*

14 Uwakumbuse vinhu avo, na uwazume mgameso ga Mulungu, sekewag-
ombe kwa sama ya mbuli. Kuibamililila kuko kwiha na kowananga waja
wotegeleza.
15 Wamba ng'hani kusang'hana ganogile mgameso ga Mulungu na uwe
msang'hanaji yeliduhu kinyala kwa sang'hano yake, yofundiza goya usenga
wa ukweli wa Mulungu.
16 Winege na kuibamililila kwa mbuli za kibozi, kwavija zowagala wanhu
kutali na Mulungu.
17 Mbuli kamba azo ziigala na londa dijaga lukuli lwa munhu. Mna
iwanhu awo wamumo wano wabili, Humenayo na Fileto.
18 Waileka nzila ya ukweli na wawatenda wanhu wayagwe wamtogole
Yesu waleke kutamanila kwa kuwalongela kamba tuzilibuka tumala.
19 Lakini ukweli wa Mulungu wima goya kamba chandusilo cha mabwe
na uchanha zandikigwa mbuli zino, “Mndewa kawajuwa wanhu wake,” na
“Kila munhu yolonga heyo wa Mndewa yaleke gehile.”
20 Mng'anda ng'hulu kuna viya va kila aina, viya viyagwe va zahabu na
shaba, avo vosang'hanilwa kwa sang'hano ng'hulu ng'hulu na viyagwe va
mibiki na ulongo, avo vosang'hanilwa sang'hano ndoo ndodo.
21 Avo, kamba munhu yoyose yahaing'aza kwa kuinega na gago gose
gehile, kokuwa kiya cha sang'hano zitogoligwa ng'hani, kwavija katendigwa
wa Mndewa na komfaya, na kaitanda kwa kila sang'hano inogile.
22 Winege na usulukilo wihile wa ubwanga, kweleleza mbuli zilondeka,
kutamanila na unogelwa na tindiwalo na mtambikile Mndewa hamoja na
wose weli na mizoyo inogile.
23 Winege na kuibamililila kwa mbuli za kibozi na wehu, kwavija kukimam-
bukizo ago gogala ndwagi.
24 Kamba msang'hanaji wa Mndewa, sekeuwe na ndwagi, uwe na moyo
unogile kwa wanhu wose, uwe mfundiza yanogile na ufunge umoyo.
25 Uwe muhole wahawalanguliza wanhu wokulema gweye, sengine Mu-
lungu kowatenda wambwelele na kuujuwa ukweli.
26 Abaho nzewele zao zowabwelela na wolawa mumtego wa Mwenem-
bago, yawagogile na kuwatenda wagagoge goyolonda.

# 3

### *Siku za kimambukizo*

1 Kumbuka kuwa mna zisiku za kimambukizo kokuwa na magayo
makulu.
2 Wanhu wokuwa na gahigahi, wokuwa na magoda, woitapa, wozinogela
sente, womuliga Mulungu, honda wawategeleze tata zao na mama zao,
waduhu asente, hawamgesa Mulungu.

3 Wanhu hawanogela wayagwe, wanhu hawalonda kuilumba, wanhu wowalonga wayagwe vihile, wanhu watatali, wanhu wakali, wanhu hawalonda ganogile.

4 Wanhu woihinduka, wanhu wotenda mbuli bila kugesa, wanhu womema bezi, wanhu wounogela ugima uno kubanza kumnogela Mulungu.

5 Kwa kunze wokoneka kamba womtambikila Mulungu, lakini woulema udahi wake. Muinege na wanhu kamba awo.

6 Wanhu awo wayagwe wochola mzing'anda za wanhu na kuwananahiza wawategeleze watwanzi wonyolila na wapapile mizigo mikulu ya nzambi, watwanzi awo wolongozigwa na kusulukila kwihile.

7 Watwanzi awo wogeza kuifunza siku zose, lakini hawadaha ng'o kuujuwa ukweli.

8 Wanhu awo woulema ukweli kamba vija Yane na Yambule viwamulemile Musa. Wanhu awo wougula utamu wa nzewele, na waduhu kutamanila kwa ukweli.

9 Lakini honda wagendelele kumwande kwavija ubozi wao wokoneka na wanhu wose. Vivo viikalile kwa Yane na Yambule.

### *Mafundizo ga kimambukizo*

10 Lakini gweye Timoseo, kugagoga mafundizo gangu na kukweleleza vija vinhendile, na vija vinondile muugima wangu, kukona kutamanila kwangu, kufunga umoyo kwangu unogelwa wangu na kubetela kwangu,

11 madununzo gangu na magayo gangu. Kugajuwa gose gandawilile ako Antiokia na Ikonia na Lusitila, magayo makulu ganifungile umoyo. Lakini Mndewa kamhonya nago.

12 Munhu yoyose yolonda kukala na ugima umnogeza Mulungu kwa kuilumba na Yesu Kilisito kodununzigwa.

13 Wanhu wotenda gehile na wavizi wobanza kutenda gehile ng'hani, kuwavizila wayagwe na wao wenyego woviziligwa.

14 Lakini gweye gendelela mna uukweli uufundizigwe na gendelela kutogola ng'hani. Kuwajuwa waja iwakalile wafundiza wako.

15 Na gweye kojuwa kuwa toka haudodo kugajuwa Maandiko Gang'alile, godaha kukugwaa nzewele zigala ukombozi kubitila kumtamanila Yesu Kilisito.

16 Maandiko Gang'alile gose gana mhumuzi ya Mulungu, na gofaya kwa kufundizila ukweli, gofaya kuwazuma wanhu, gofaya kugagolosa ago ganyolodoke, na gofaya kuwalanguliza wanhu wawe na ugima unogile mgameso ga Mulungu,

17 avo munhu yomsang'hanila Mulungu yadahe kutenda goya, na yadahe kusang'hana kila sang'hano inogile.

## 4

1 Nokulagiza mgameso ga Mulungu na mgameso ga Yesu Kilisito, yonda yawataguse wanhu wagima na wafile, kwavija kokwiza kuwatawala kamba Mndewa,

2 nokulagiza uwapetele wanhu usenga, uitande kwa kipindi kinogile na kihile, uwalangulize wanhu na uwazume na uwagangamize kwa uhole.

3 Siku zokwiza aho wanhu honda wategeleze mafundizo ga ukweli, lakini wokweleleza gaja goyolonda wenyego na wosola wafundiza wengi wonda wafundize gaja gowolonda wao kuhulika.

4 Wolema kutegeleza ukweli, na wohindukila simo za uvizi.

5 Lakini gweye uiteganye na ufunge umoyo mna gamagayo, usang'hane
kuwapetela wanhu Mbuli Inogile na uimambukize sang'hano yako.
6 Kwavija kipindi changu cha kufa cha mmabehi na damu yangu yo-
gidigwa kamba vija walava nhosa viwogida divai.
7 Niye niwamba mna ing'hondo, niumambukiza mwanza wangu na ni-
gogeleza goya kutamanila.
8 Sambi nobetela kugweleligwa nhunza ya kuhuma, ya kutendigwa noge
mgameso ga Mulungu. Mndewa yotagusa wanhu goya, konigwaa nhunza
siku dijo. Si niye niiyeka, lakini na waja wose wombeta kwa kusulukila
yalawilile.

*Mbuli za Paulo kwa Timoseo*

9 Sekeukawe kwiza kundola.
10 Dema kavinogela ng'hani vinhu va mwiisi ino mbaka kandeka kachola
ako Sesalonike. Kilesike kachola Galatia na Tito kachola Dalimatia.
11 Luka yaiyeka ayo yeli hamoja na niye. Msole Maluko wize nayo, kwavija
kodaha kunhaza mwiisang'hano.
12 Nimtuma Tukiko yachole Efeso.
13 Waheza ngalile koti jangu, dindekile kwa Kalipo ako Tuloasi, vivija
ngalile vija ivitabu, ng'hani ng'hani vija va ng'hwembe.
14 Ija mfuwa zuma Alekizanda, kanhendela gehile, lakini Mndewa ko-
mulipa mbuli ya gaja gayasang'hane.
15 Gwegwe vivija winege nayo, kwavija kaulema ng'hani usenga wetu.
16 Viniigombele mwanza wa ichanduso kuduhu munhu yailumbile na
niye, wanhu wose wandeka. Mulungu sekeyailole mbuli yao ihile!
17 Lakini Mndewa kanhaza na kanigwaa nguvu, niwapetela wanhu
usenga wake, muladi wanhu haweli Wayahudi wauhulike. Mndewa kani-
honya na ifa kamba mudilomo da simba.
18 Mndewa komhonya na gehile gose, na konigala muundewa wake wa
kuulanga. Ukulu uwe kwa Mulungu siku zose. Ona.

*Mbuli za kimambukizo za ibaluwa*

19 Walamuse Pilisila na Akula, hamoja na wanhu wa mng'anda ya Onesi-
foli.
20 Elasito kasigala Kolinto na Tulofimo nimuleka Mileto, kwavija kakala
mtamu.
21 Ulopole kwiza kihuhwe hakinavika.
Ebulo na Pudensi na Lino na Kilaudia wokulamusa, vivija wakilisito
wayagwe wokulamusa.
22 Mndewa yakale na gweye, ng'hekewa ya Mulungu ikale na mweye
mose.

# Baluwa ya Paulo kwa Tito

## Ulongozi

Kitabu cha Tito acho kitabu mna ivitabu vine va Paulo viyandike kwa munhu imoja imoja badala ya kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu. Baluwa ndatu ziyagwe azo 1 Timoseo na 2 Timoseo na Filimoni. Paulo kamwandikila Tito, lakini vivija kandika kamba vija ibaluwa yolondigwa isomigwe kwa sauti mgameso ga wanhu. Mbuli ino toijuwa kwavija kasimulila heyo viyali kamba Mtumigwa, mbuli ayo ijuwika mwaka na Tito. Yogesigwa Paulo kandika baluwa ino hagati ya mwaka wa 63-65 toka kuvumbuka kwa Kilisito.

Paulo kamulagiza Tito yawalongoze wanhu wamtogole Yesu mna ivibumbila ako mna ikisiwa cha Kilete. Paulo kandika baluwa ino muladi yamulagize Tito yawasagule na kuwafunza walangulizi wa wanhu wamtogole Yesu. Vivija vivo viyalagize mna ibaluwa yake iyamwandikile Timoseo. Baluwa yake yosimulila vija walangulizi wa wanhu wamtogole Yesu viwolondeka kuika goya muladi wategelezigwe ng'hani. Wanhu wamtogole Yesu na walangulizi wa wanhu wamtogole Yesu wa kipindi kino wolondeka waifunze mbuli zilondeka mna ukuwalongoza wanhu.

**Mbuli zili mkitabu**

Paulo komulagiza Tito yasagule walangulizi womdumba Mulungu (Sula ya 1:1-16).

Vivija komulagiza yawafunze wanhu wakale kwa kumdumba Mulungu (Sula ya 2:1-3:11).

Paulo komambukiza kwa kwandika mbuli za uhelelo (Sula ya 3:12-15).

1 Niye Paulo, namsang'hanaji wa Mulungu na mtumigwa wa Yesu Kilisito. Nisaguligwa na nhumigwa kugangamiza kutamanila kwa wanhu wa Mulungu waujuwe ukweli na wakale kamba Mulungu viyolonda wakale.
2 Ukweli uno wa mditamanilo da ugima wa mazuwa gose. Mulungu yoleka kuviza, katulongela kotugwaa ugima uno, isi ing'hali hainaumbigwa,
3 na mna ikipindi kinogile kaugubula usenga wake. Naniye nigweleligwa usenga awo, niupeta kwa kulagizigwa na Mulungu Mkombola wetu.
4 Nokwandikila gweye Tito, mwanangu wa ukweli mditamanilo dimoja dituilumbile. Mulungu Tataetu na Yesu Kilisito Mkombola wetu wakugwee ng'hekewa na tindiwalo.

*Sang'hano ya Tito ako Kilete*

5 Nikuleka ako Kilete muladi wike goya kila kinhu na kuwasagula wavele wa vibumbila va wanhu wamtogole Yesu mna kila buga, kamba vinikulagize.
6 Mvele wa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu sekeyalongigwe vihile na wanhu na yawe na mwehe imoja na wanage wolondeka wamtogole Yesu na wanhu sekewawalonge kwa gehile ng'hani.
7 Kwavija mulangulizi wa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu koilola goya sang'hano ya Mulungu kolondeka yawe munhu halongigwa vihile na wanhu, sekeyaitape, sekeyagevuzike hima hima, sekeyakoligwe, sekeyakomhoke na sekeyasulukile kupata vinhu kwa nzila ihile.
8 Kolondeka yawe munhu yowagoneka wanhu mng'anda yake na yagoge ganogile. Kolondeka yawe mbala, yatende ganogile, yawe munhu yang'alile na yoilongoza mwenyego.

9 Kolondeka yagoge goya usenga wa mafundizo ga ukweli kamba viyafunzigwe muladi yawagangamize wayagwe na kugubula gehile ga waja wogalema mafundizo gago.

10 Kwavija kuna wanhu wengi hawalonda kutegeleza, na wolonga mbuli za ubozi na wowagiza wanhu, ng'hani ng'hani wanhu walawile mkibumbila cha Wayahudi na sambi wamtogola Yesu.

11 Wolondeka wanyamale kulonga, kwavija wowading'hula wanhu mzing'anda kwa kuwafundiza mbuli hazilondeke kufundizigwa, wotenda vivo muladi wapate sente.

12 Vivija imoja wa mtula ndagu wao kalonga, “Wanhu wa Kilete siku zose wolonga uvizi, wotenda gehile kamba ming'onyo, wadoda na wamelo.”

13 Usindila uno wa ukweli, avo kolondeka uwakomhokele ng'hani muladi wawe na tamanilo dinogile,

14 na waleke kugendelela kutegeleza simo za Kiyahudi na malagizo golawa kwa wanhu waulemile ukweli.

15 Kila kinhu king'ala kwa wanhu weli na mizoyo ing'alile, lakini kuduhu chochose king'alile kwa waja weli na dikwe na wolema kutogola, kwavija nzewele zao na mizoyo yao ina dikwe.

16 Wanhu awo wolonga kamba womjuwa Mulungu lakini sang'hano zao zolagusa kamba womulema. Wanhu wogevula mizoyo na hawategeleza, hawafaya kwa mbuli yoyose inogile.

# 2

### *Mafundizo ga ukweli*

1 Lakini gweye kolondeka ufundize mafundizo gailumbile na mafundizo ga ukweli.

2 Walongele wambigalo wavele wailongoze wenyego, wakale kwa kutegelezigwa, wawe na nzewele zinogile, wawe na tamanilo digangamale, unogelwa na kufunga umoyo.

3 Vivija walongele watwanzi wavele wakale ugima wa kung'ala, sekewawalonge vihile wanhu hebu kuwa watumwa wa ugimbi. Wolondeka kufundiza mbuli zinogile,

4 muladi wawafundize wandele kuwanogela wakasano zao na wanao,

5 wailongoze vinogile, wang'ale, walolese kae zao, wawategeleze wakasano zao, muladi usenga wa Mulungu sekeulongigwe vihile.

6 Vivija wagangamize wabwanga wailongoze wenyego mna ikila kinhu.

7 Mzimbuli zose gweye kolondeka uwe kilaguso cha kutenda ganogile, mna gamafundizo gako ulaguse ukweli na sambi utende mwangalo.

8 Ulonzi wako sekeutagusigwe, muladi wose wokulema gweye wagwe kinyala kwa kuswela kulonga gehile kumwetu.

9 Vivija walongele watumwa wawategeleze wakulu zao na wawanogeze mna izimbuli zose. Sekewaibamilile nao,

10 hebu kuwebila vinhu vao, lakini walaguse wanoga na kutamaniligwa kwa sang'hano zao zose, muladi mafundizo ga Mulungu Mkombola wetu gagweleligwe nhogolwa na wanhu.

11 Kwavija ng'hekewa ya Mulungu igubuligwa kwa kuwakombola wanhu wose.

12 Ng'hekewa ino yotufunza tuleme mbuli hazimnogelaga Mulungu na kusulukila vinhu va mwiisi ino, lakini tuilongoze wenyego, tukale ugima wa kumnogela Mulungu mwiisi ino ya sambi,

13 kuno tobeta siku dijo da deng'ho ditutamanila, kipindi ukulu wa Mu-
lungu wetu mkulu na Mkombola wetu Yesu Kilisito vonda ulawilile.
14 Yesu kailava mwenyego mbuli yetu muladi yatulekese kulawa mna
izinzambi na kututenda wanhu wanogile weli wake mwenyego, wanhu
wosulukila kutenda ganogile.
15 Avo ufundize vinhu vino, sang'hanila udahi wako wose kwa kuwa-
gangamiza na kuwazuma. Munhu yoyose sekeyakubeze.

# 3

*Ugima kwa Kilisito*

1 Wakumbuse wanhu wawategeleze wakulu na watawala, na waitande
kusang'hana kila sang'hano inogile.
2 Walongele waleke kumuliga munhu yoyose, lakini wakale goya na
waitegeleze na walaguse uhole kwa kila munhu.
3 Aho umwaka tweye tukala wabozi, tuleka kutegeleza, tuviziligwa na
tukala watumwa wa kusulukila vinhu vitulondile, tukala kwa gehile na
migongo, wanhu watwihila na tweye tuwehila.
4 Lakini kipindi cha bazi na unogelwa wa Mulungu Mkombola wetu
vikivikile,
5 katukombola, siyo kwavija tusang'hana mbuli zinogile lakini kwa mbuli
ya bazi jake. Na kubitila Loho Yang'alile, yotutenda tuvumbuke sambi na
ugima wa sambi kwa kutusunha kwa mazi.
6 Mulungu katugwaa Loho Yang'halile ng'hani kubitila Yesu Kilisito
Mkombola wetu,
7 muladi kwa ng'hekewa ya Mulungu yatutende tunoge mgameso gake na
tubokela ugima wa mazuwa gose utubeta.
8 Mbuli ino inilonga ukweli wiiyeka.
Nolonda uilonge mbuli ino kwa kugangamala, muladi waja wamtogole
Mulungu wasulukile ng'hani kipindi chose kusang'hana ganogile. Mbuli
zino zinoga na zomfaya kila munhu.
9 Lakini inege na mbuli za ubozi, ndwagi na kuibamilila mbuli ya msafa
wa ng'holo za wahenga na mbuli ya Malagizo ga Musa. Mbuli zizo hazi-
wafaya bule na zaduhu kinhu.
10 Munhu yotenda wanhu waigole mzume kwa miyanza mibili abaho
muleke.
11 Kojuwa kuwa munhu kamba ayo koulema ukweli, na nzambi zake
zomulagusa kabananga.

*Mbuli za kimambukizo*

12 Vonda nimtume Alitemi hebu Tukiko kumwako, tenda viudaha wize
ako Nikopoli kundola, kwavija nigesa kukala ako kipindi cha kihuhwe.
13 Wamba ng'hani kumtaza Zena ija yagajuwile goya malagizo na Apolo
muladi wadahe kusonga mwanza wao, na sekewahungukilwe kinhu.
14 Wanhu zetu waifunze kipindi chose kutenda ganogile muladi wawataze
mna ivinhu vilondeka muugima, na ugima wao uwafaye.
15 Wanhu wose weli hamoja na niye wowalamusa. Walamuseni mbwiga
zetu mna ukumtamanila Mulungu.
Ng'hekewa ya Mulungu ikale na mweye mose.

# Baluwa ya Paulo kwa Filimoni

## Ulongozi

Baluwa ino nguhi kwa Filimoni yandikigwa na mtumigwa Paulo (Sula ya 1:1). Paulo kakala mkifungo viyandike baluwa ino, nayo yogesigwa kipindi acho Paulo kakala ako Lumi. Avo kamba kakala Lumi baluwa ayo yogesigwa yandikigwa behi na mwaka wa 61 toka kuvumbuka kwa Kilisito, avo mna ikipindi acho vivija kandika baluwa kwa wanhu wa ako Kolosai.

Baluwa ino kamwandikila munhu imoja yokemigwa Filimoni. Filimoni kakala imoja mna ikibumbila cha wanhu wamtogole Yesu na vivija kakala na watumwa. Paulo kamwandikila Filimoni kumpula sekeyamkoboze Onesimo yakalile yatoloke kwa Filimoni. Kwa malagizo ga Kilumi Filimoni yahadahile kumkoma Onesimo. Paulo kalonga kwa ulonzi wa kutewenza muladi Filimoni yamtogole Onesimo kamba ndugu kwa kuilumba na Kilisito na vivija kalonda yamtogolele Onesimo yakasang'hane hamoja na Paulo (Sula ya 1:13-14).

**Mbuli zili mkitabu**

Paulo komulamusa Filimoni (Sula ya 1:1-3).

Abaho Paulo kompula Filimoni mbuli ya Onesimo yamtogole kamba ndugu kwa kuilumba na Kilisito (Sula ya 1:4-21).

Paulo komambukiza kwa kulonga wanhu womulamusa na heyo viyolonda kumtembelela (Sula ya 1:22-25).

1 Niye Paulo, namfungwa mbuli ya kumsang'hanila Yesu Kilisito. Niye na ndugu yetu Timoseo, tokwandikila gweye Filimoni mbwigaetu na msang'hanaji miyetu,

2 na wanhu wamtogole Yesu iwoiting'hana ukayako na gweye lumbu jetu Afia na mkalizi miyetu Alikipo.

3 Mulungu Tataetu na Mndewa Yesu Kilisito wawagwee ng'hekewa na tindiwalo.

*Filimoni viyomnogela Mulungu na kumtamanila*

4 Ndugu Filimoni, kipindi chose nahampula Mulungu, nokutambula gweye na kumgwaa Mulungu nhogolwa,

5 kwavija nohulika unogelwa wako kwa wanhu wose wa Mulungu na tamanilo diulinajo kwa Mndewa Yesu.

6 Nompula Mulungu yakugangamize ulonge kwa wanhu wayagwe kutamanila kwako, muladi udahe kujuwa kila kinhu kinogile kitulinacho kwa kuilumba na Kilisito.

7 Ndugu yangu, unogelwa wako ungalila ndeng'helelo ng'hulu na kunigela moyo, vivija kuwagela moyo wanhu wa Mulungu.

*Paulo kompula Filimoni yambokele Onesimo*

8 Kwa kilamuso kino, niye kamba ndugu yako kwa kuilumba na Kilisito nahadahile kukulagiza bila kudumba utende kiulondeka kusang'hana,

9 lakini kwavija nikunogela, tanhu nokupula. Notenda vino hata kamba niye Paulo namvele, na vivija sambi na mkifungo mbuli ya kumsang'hanila Yesu Kilisito.

10 Avo nokupula umtaze Onesimo, yeli mwanangu kwa kuilumba na Kilisito, kwavija niwa kamba tatake hano mkifungo.

11 Baho umwaka kakala hakufaya bule, lakini sambi konifaya niye na
gweye vivija.
12 Sambi nombweza kumwako nayo konhenda niwe na usungu.
13 Maza niye nilonda ng'hale nayo kipindi na mkifungo mbuli ya
kuwapetela wanhu Mbuli Inogile muladi yanitaze badili yako.
14 Lakini silonda kukunanahiza unhaze, niye nolonda unhaze kwa ku-
londa mwenyego. Avo sitenda kinhu chochose mbaka utogole mwenyego.
15 Yodahika kuwa Onesimo kakala yasegele kumwako kwa kipindi kidodo,
muladi uwe nayo kabili kwa kipindi chose.
16 Na sambi heli kamba mtumwa, lakini kabanza ng'hani ya kuwa
mtumwa. Kumwangu niye ndugu kwa kuilumba na Mndewa, lakini
kumwako gweye kabanza ng'hani, kawa kamba ndugu kwa kuilumba na
Mndewa na vivija mtumwa wako!
17 Avo kamba konigesa niye kamba ndugu yako kwa kuilumba na Mn-
dewa, mbokele kabili kamba wahambokele niye.
18 Kamba kakutendela jojose dihile hebu kodaigwa, undai niye.
19 Nokwandika gano kwa mkono wangu mwenyego, niye Paulo nokulipa,
silonda kukulongela kamba kumwangu kodaigwa ugima wako.
20 Avo ndugu yangu, nhendela mbuli ino inogile mbuli ya Mndewa,
nisamhuse moyo wangu kamba ndugu kwa kuilumba na Kilisito!
21 Nokwandika kuno notamanila kuwa konhogolela kupula kwangu na
nojuwa kotenda kubanza aho.
22 Vivija nitandileni gati da kuwasa, kwavija notamanila kamba Mulungu
kokwidika kupula kwenu na kunibweza kumwenu.

*Ndamuso za kimambukizo*

23 Epafulasi, mfungwa miyangu mbuli ya kumsang'hanila Yesu Kilisito,
kokulamusa,
24 na vivija wasang'hanaji wayangu Maluko na Alisitaliko na Dema na
Luka wokulamusa.
25 Ng'hekewa ya Mndewa Yesu Kilisito ikale na mweye mose.

# Baluwa kwa Waebulania

## Ulongozi

Kitabu cha Waebulania ni baluwa ya kuwagangamiza wanhu na yolagusa Yesu viyatimilize mbuli za ulaguzi mna idilagano da umwaka. Ikitabu chandikigwa kamba vija munhu yowapetela wanhu. Mkitabu kino cha Waebulania kuna vilaguso kubanza 60 va lagano da umwaka, avo vose volagusa goya Yesu viyatimilize ulaguzi na sang'hano ya Mulava nhosa Mkulu wa Wayahudi. Kwa kilamuso acho ikitabu chandikigwa kuwagangamiza Wayahudi wamtogole Yesu. Kitabu cha Waebulania cholagusa Yesu viyagamambukize malagizo ga Musa, avo walava nhosa hawalondeka kulava nhosa kabili. Yesu kakala nhosa kwa nzambi zose, mwanza umoja na kwa kipindi chose. Vivija wanhu wamtogole Yesu mna ikipindi chetu wogangamizigwa mna ibaluwa ino ya Waebulania muladi wagendelele kumkweleleza Yesu Kilisito ayo yotenda idahike kumwetu tumtamanile Mulungu, na vivija tugendelele kumtamanila heyo (Sula ya 12:2).

Kuduhu munhu yajuwile yandike baluwa ino ya Waebulania, lakini wanhu woifunza mbuli wogesa sengine munhu yandike kodaha kuwa mtumigwa Paulo hebu Luka hebu Balinaba. Vivija mwaka uyandikigwe baluwa ino haujuwike bule, lakini wanhu wengi wogesa yandikigwa kuchugu ya mwaka wa 70 toka kuvumbuka kwa Kilisito. Buga da Yelusalemu dinangigwa mwaka wa 70 toka kuvumbuka kwa Kilisito, lakini mwandikaji wa baluwa ino kolonga mbuli ya Yelusalemu kamba vidikalile ding'hali kunangigwa. Baluwa ino ya Waebulania yandikiligwa kudibuga da Lumi (Sula ya 13:24) na yogesigwa ipwililisigwa kwa wanhu wamtogole Yesu mna ivibumbila.

**Mbuli zili mkitabu**

Mwandikaji kolagusa kuwa Yesu ayo mkulu kubanza watula ndagu wa Mulungu na wasenga wa kuulanga (Sula ya 1:1-4:13).

Abaho kagendelela kulagusa kuwa Yesu ayo mkulu kubanza walava nhosa wakalile wosang'hana mna Ing'anda ya Mulungu ako Yelusalemu (Sula ya 4:14-7:28).

Vivija sang'hano ya Yesu ayo ng'hulu mna idilagano da umwaka diyatendile Mulungu na wanhu zake kubitila malagizo gayamgwelele Musa (Sula ya 8:1-10:31).

Viyamambukize kulonga ukulu wa Yesu mna izinzila zose mwandikaji kolava mafundizo gayagwe (Sula ya 10:32-13:17).

Kukimambukizo mwandikaji komambukiza kwandika kwa kulonga mbuli za kugangamiza na kuwalamusa wanhu (Sula ya 13:18-25).

*Mulungu kalonga kubitila Mwanage*

1 Baho umwaka, Mulungu kalonga na wahenga zetu miyanza mingi na kwa nzila nyingi kubitila watula ndagu wake,

2 lakini siku zino za kuuhelelo, kalonga na tweye kubitila Mwanage, heyo iyo ija kwa nzila yake Mulungu kaumba ulanga na isi na vinhu vose vili mumo. Mulungu kamsagula ayo na kamgwaa vinhu vose viwe vake.

3 Heyo ayo mng'alo wa ukulu wa Mulungu na koigala na Mulungu too! Kila kinhu cholawilila kwa lagizo jake dili na nguvu. Viyamambukize kuzisunha nzambi za wanhu, kakala kuna uukulu kuko kuulanga mwambu wa mkono wa kudila wa Mulungu mkulu.

### *Ukulu wa Mwana wa Mulungu*

4 Mwana kagweleligwa ukulu kubanza wasenga wa kuulanga, kwavija twaga diyagweleligwe na Mulungu dolagusa heyo mkulu kubanza wose.
5 Kwavija Mulungu hamulongele bule msenga wa kuulanga yoyose,
“Gweye kwa Mwanangu na lelo nolonga wose wajuwe,
niye na Tatako.”
Wala Mulungu halongile bule mbuli ya msenga yoyose wa kuulanga,
“Niye nokuwa Tatake,
na heyo kokuwa Mwanangu.”
6 Lakini Mulungu viyomtuma Mwanage chaudele mwiisi, kolonga,
“Wasenga wa kuulanga wose wa Mulungu wamtambikile.”
7 Lakini mbuli ya wasenga wa kuulanga, Mulungu kalonga,
“Mulungu kawatenda wasenga zake wa kuulanga wawe beho,
na wasang'hanaji zake wawe milambi ya moto.”
8 Lakini kwa Mwanage, Mulungu kalonga,
“Go Mulungu undewa wako waduhu uhelelo!
Kowalongoza goya wanhu zako.
9 Gweye kuganogela ganogile na kugehila gehile.
Lekaavo Mulungu, yeli Mulungu wako kakugwaa ukulu,
kubanza wayago,
avo kudeng'helela.”
10 Na vivija kalonga,
“Mndewa, gweye kusimika mhanda za isi baho haichanduso,
na kutenda ulanga kwa makono gako mwenyego.
11 Avo vosegela, lakini gweye kosigala siku zose,
vose volala kamba viwalo.
12 Kowakunzakunza kamba kitanga,
nao wogaluka kamba mgolole ulalile.
Lakini gweye kwavivija siku zose,
na ugima wako waduhu uhelelo.”
13 Mulungu hamulongele ng'o msenga wa kuulanga yoyose,
“Kala hano muukulu mwambu wangu wa mkono wa kudila,
mbaka niwahume wanhu wakwihile na niweke
hasi mmagulu gako.”
14 Vino wasenga wa kuulanga ndio choni? Wao loho iwomsang'hanila Mulungu yawatumile kuwataza wanhu waja wonda waubokele ukombozi.

# 2

### *Ukombozi mkulu*

1 Lekaavo tolondeka kugagoga goya gatuhulike, muladi seketusonge mhole mhole kuleka kutamanila.
2 Baho umwaka usenga ulongigwe kubitila wasenga wa kuulanga ulagusa wa ukweli, na munhu yoyose yalekile kuukweleleza hebu kuugoga katagusigwa kamba viilondeke.
3 Vino tohonyeka vilihi kamba hatuutonga ukombozi mkulu kamba uno? Tanhu Mndewa mwenyego iyo yanduse kulonga mbuli ino ya ukombozi, na waja wamuhulike watulagusila kuwa ya ukweli.
4 Vivija Mulungu mwenyego kalagusa kumwao kwa kutenda unzonza mwingi na vifukuzi na kuwagolela wanhu nhunza za Loho Yang'alile kamba viyalondile.

### *Yesu iyo yowakombola wanhu*

5 Mulungu hawekile wasenga wa kuulanga wawe watawala wa isi ayo, isi ayo ya sambi itulonga mbuli zake.

6 Lakini hana hanhu mna Gamaandiko Gang'alile holonga,
“Go Mulungu, vino munhu ayo nani, mbaka umgese,
vino munhu ayo nani mbaka umulole goya?
7 Kwa kipindi kidodo kumtenda yawe munhu mdodo kubanza wasenga wa kuulanga,
kumgwaa taji ya ukulu na kutegelezigwa,
8 na kumtenda mtawala wa vinhu vose.”
Yolongigwa kuwa Mulungu kamtenda munhu, “Mtawala wa vinhu vose,” bila kuleka hata kinhu kimoja. Hata sambi tung'hali hatunamona munhu kotawala vinhu vose.
9 Lakini tomona Yesu yatendigwe munhu mdodo kubanza wasenga wa kuulanga kwa kipindi kidodo, muladi mbuli ya ng'hekewa ya Mulungu kumwetu Yesu kafa mbuli ya wanhu wose. Sambi tomona kavazigwa taji ya ukulu na kutegelezigwa mbuli ya kugaya kwake mbaka kufa.
10 Ikala vinoga kwa Mulungu, yaumbile na kuvika goya vinhu vose, na kamtenda Yesu yawe viyali kubitila madununzo, muladi yawagale wana wengi muukulu wake. Kwavija Yesu ayo yowakombola wanhu.

11 Yesu kowasunha wanhu nzambi zao, heyo hamoja na iwaja wasunhigwe, wose Tatao imoja. Lekaavo Yesu hakona kinyala kuwakema ndugu zake.

12 Kalonga kwa Mulungu,
“Nowalongela ndugu zangu kiutendile,
muumting'hano wao nokwimbila nyila za kukutogola.”
13 Vivija kalonga, “Nomtamanila Mulungu.” Na kagendelela kulonga, “Niye na hano hamoja na wanhu nigweleligwe na Mulungu, wawe wanangu.”

14 Avo kwavija wana awo ni wanhu weli na lukuli na damu, vivija Yesu nayo keza kawa kamba wao na kuilumba muunhu wao. Katenda vivo, muladi kubitila ifa yake yamuhume Mwenembago, yakalile na udahi wa ifa.

15 Lakini vivija Yesu kafa kuwalekesa waja kwa bwembwe da ifa wakala watumwa muugima wao wose.

16 Kwavija yojuwika kuwa Yesu hezile kuwataza wasenga wa kuulanga, ila kowataza lukolo lwa Abulahamu.

17 Lekaavo kalondeka yaigale na ndugu zake kwa kila nzila, muladi yawe Mulava nhosa Mkulu yotamaniligwa na yeli na bazi mwiisang'hano yake kwa Mulungu, muladi nzambi za wanhu zigeligwe kumgongo.

18 Kwavija heyo mwenyego viyagezigwe na kudununzigwa kafunga umoyo, kodaha kuwataza iwaja wogezigwa.

# 3

### *Yesu iyo mkulu kubanza Musa*

1 Avo, ndugu zangu wanhu wa Mulungu na vivija mukemigwe na Mulungu! Gelegezeni mbuli ya Yesu yatumigwe na Mulungu yawe Mulava nhosa Mkulu wa tamanilo ditutogola.

2 Nayo kakala yotamaniligwa na Mulungu, yamsagule kutenda sang'hano yake, kamba vija Musa, viyatamaniligwe kuwasang'hanila wanhu wa Izilaeli wakemigwe ng'anda ya Mulungu.

3 Avo Yesu kolondeka yagweleligwe ukulu ng'hani kubanza Musa, kamba vija munhu yozenga ng'anda viyogweleligwa ukulu ng'hani kubanza ing'anda yenyego.

4 Ona, kila ng'anda izengigwa na munhu, na Mulungu ayo mzengaji wa vinhu vose.
5 Heyo Musa kakala msang'hanaji yotamaniligwa mwiisang'hano yake yose ayo. Sang'hano yake ayo ikala ilagusa mbuli zonda yalonge Mulungu baho kumwande.
6 Lakini heyo Kilisito kotamaniligwa kamba Mwana yeli na udahi kwa wanhu weli ng'anda ya Mulungu. Tweye wao ng'anda yake kamba twahagendelela kuwa magalu na kugangamala mna iditamanilo dituigodela.

### *Kubwihila kwa wanhu wa Mulungu*

7 Kamba Loho Yang'alile viyalongile mna Gamaandiko Gang'alile,
“Mwahahulika sauti ya Mulungu lelo,
8 sekemutende mizoyo yenu midala, kamba viwakalile wahenga zenu viwalemile kumtegeleza Mulungu,
kipindi acho viwamgezile ako kuluwala.
9 Ako wahenga zenu wanigeza na kunilolesalolesa,
hamoja wazona sang'hano zangu kwa miyaka malongo mane.
10 Avo niwagevuzikila wanhu awo na kulonga,
‘Siku zose wokweleleza nzila zao,
na hawazijuwile ng'o nzila zangu.’
11 Nigevuzika na kuiduila,
‘Honda wengile ng'o hanhu hangu ha kubwihila!’ ”
12 Avo ndugu zangu, iteganyeni sekeyalawilile munhu yoyose kumwenu yeli na moyo wihile wa kuleka kutogola kwa kuinega na Mulungu yeli mgima.
13 Lakini mwahagendelela kuhulika mbuli ino “Lelo” yosomigwa mna Gamaandiko, muigangamize kila siku, muladi munhu yoyose sekeyavi-ziligwe kutenda nzambi na kuleka kutegeleza.
14 Kwavija tweye wose hamoja twa mgati ya Kilisito Mkombola kamba twahagogeleza goya mbaka kuuhelelo kija kitutamanile aho haichanduso.
15 Kumbukeni Maandiko Gang'alile vigolonga,
“Mwahahulika sauti ya Mulungu lelo,
sekemutende mizoyo yenu midala, kamba viwakalile wahenga zenu,
viwalemile kumtegeleza Mulungu.”
16 Wanhu gani iwahulike sauti ya Mulungu wamulema? Wao waja wose walongozigwe na Musa kulawa Misili.
17 Vino kwa miyaka malongo mane Mulungu kawagevuzikila kina nani? Kawagevuzikila wanhu waja watendile nzambi, wafa kuko kuluwala.
18 Mulungu viyaiduile, “Honda wengile ng'o hanhu hangu ha kubwihila” kakala kowalonga kina nani? Kakala kowalonga wanhu awo wamulemile.
19 Avo tokona, hawadahile kwingila kuko kwavija walema kutogola.

# 4

8 Lakini kuduhu munhu yodaha kulufuga lulimi lwake. Lulimi lwiha na
halulongozigwa na lumema sumu igalaga ifa.
9 Kwa lulimi tomgwaa nhogolwa Mndewa Tataetu na vivija kwa lulimi
towaduwila wanhu, waumbigwe kwa kuigala na Mulungu.
10 Mumulomo umoja munhu kolonga mbuli za kutambikila na mbuli za
kudumiliza. Ndugu zangu sambi iwe vivo.
11 Vino, mazi gamulila na mazi ga usungu godaha kulawa mwiinzasa
imoja?
12 Ndugu zangu, vino mbiki wa mtini wodaha kulela zeituni? Hebu
mzabibu wodaha kulela tini? Vivija nzasa ya mazi gausungu haidaha kulava
mazi gamulile.

*Nzewele ilawa kwa Mulungu*

13 Vino nani yeli na nzewele na ubala kumwenu? Yalaguse mbuli ayo
kwa kusang'hana ganogile, ganogile gotendeka kwa moyo wa uhole uli kwa
munhu yeli na nzewele.
14 Lakini kamba mizoyo yenu imema migongo na usungu na gahigahi,
sambi muugubike ukweli kwa kuitapa mbuli ya nzewele yenu.
15 Nzewele kamba ayo hailawa kuulanga, ila yolawa mwiisi na ya wanhu
na vinyamkela.
16 Kwavija wahawa na migongo na gahigahi, vivija kokuwa na bamila na
kila kinhu kihile.

17 Lakini nzewele ilawa kuulanga tanhu isunhigwa, na vivija ina tindiwalo
na unogelwa na uhole, yowatonga wayagwe na imema bazi na yotenda
ganogile, haibagula wanhu na yaduhu unafiki.
18 Wanhu wonogelwa kuwatenda wanhu wakale goya wohanda mbeyu ya
tindiwalo na wosenga ganogile.

# 4

### *Kuilava kwa Mulungu*

1 Migomvi na kuitowa kwenu kolawa kwahi? Volawa mumo mna ukusu-
lukila kwenu, avo vogomba siku zose mmizoyo yenu.
2 Mosulukila ng'hani vinhu na kwavija hamuvipata mokoma, movonela
migongo vinhu va wayagwe lakini hamuvipata, avo mogomba na kuitowa.
Mweye mduhu vinhu vimulonda kwavija hamumpula Mulungu.
3 Na mwahampula, hawagwelela bule, kwavija mopula kwa mizoyo ihile,
muladi muvisang'hanile kamba vimulonda mna ukusulukila kwenu.
4 Mweye wanhu hamutamaniligwa! Vino hamujuwile bule kamba kuino-
gela isi ino kuko kuihila na Mulungu? Munhu yoyose yoinogela isi ino
koihila na Mulungu.
5 Sekemugese kamba Maandiko Gang'alile galonga bule, vigalongile,
“Loho yekigwe na Mulungu mgati mmwetu kotusulukila mbaka kokona
migongo.”
6 Lakini ng'hekewa iyotugwaa Mulungu ina nguvu ng'hani. Kamba
Maandiko vigalonga, “Mulungu kowalema wanhu woitapa, lakini kowag-
waa ng'hekewa wanhu wahole.”
7 Avo, ilaveni kwa Mulungu, mulemeni Mwenembago nayo kowakimbila.
8 Mkweseleni behi Mulungu nayo kowakwesela behi. Sunheni makono
genu mweye wene nzambi. Sunheni mizoyo yenu, mweye wanafiki!
9 Nyunyuwaleni na lileni na kuiyalala. Daba jenu digaluke ndilo, na
deng'ho jenu diwe kunyunyuwala!
10 Igweni kuulongozi wa Mndewa na mumtamanile nayo kowenula
uchanha.

### *Mbuli ya kumtagusa miyago yamtogole Yesu*

11 Ndugu zangu, sekemuilonge vihile mweye kwa mweye. Munhu yoyose
yomulonga vihile ndugu yake hebu kumtagusa kogalonga vihile malagizo
na kugatagusa. Wahagatagusa malagizo hugagoga malagizo, lakini kogata-
gusa.
12 Mulungu yaiyeka yolava malagizo na kutagusa, nayo kodaha kukom-
bola na kunanga. Avo gweye kwa nani mbaka komtagusa miyago?

### *Kuzumigwa mbuli ya kuitapa*

13 Avo, tegelezeni mweye mulongaga, “Lelo hebu mayo tochola kudibuga
dino hebu dija tokala mwaka mgima na tochuuza vinhu na kupata sente.”
14 Mweye hamujuwile ugima wenu mayo vondauwe! Ugima wako una
choni? Mweye muigala na kungugu dolawilila kwa kipindi kidodo na
kulawanya.
15 Molondeka mulonge, “Kamba Mndewa yahalonda, tokala wagima na
kutenda kino hebu kija.”
16 Lakini sambi moitapa na kuigoda, kuitapa kamba kuko hakunogile
bule.
17 Avo munhu yoyose yogajuwa ganogile ga kusang'hana, lakini ha-
gasang'hana, munhu ayo kotenda nzambi.

# 5

*Kuwazuma wanhu wagoli*

[1] Sambi tegelezeni mweye wanhu wagoli, lileni na kuiyalala mbuli ya magayo gonda gawezile.
[2] Vinhu venu vokola, na viwalo venu vidigwa na wang'onyo.
[3] Zahabu zenu na sente zigwa lungwi, na lungwi alo lolonga kimutendile na loja ng'huli zenu kamba moto. Mweye muikila ugoli mzisiku za uhelelo.
[4] Kwavija hamuwalipile fungu wanhu wasang'hane mmigunda yenu, tegelezeni kuiyalala kwao! Ndilo ya wanhu wasengile mmigunda yenu Mulungu yeli na Udahi wose kaihulika.
[5] Mukala mwiisi kwa ugima wa kutenda vimulonda wenyego na uhondo. Muneneha mbuli ya siku da kuchinjigwa.
[6] Muwatagusa na kuwakoma wanhu wanogile na hewo hawawalemele kwa chochose!

*Kufunga umoyo na kumpula Mulungu*

[7] Ndugu zangu, fungeni moyo, mbaka vonda yeze Mndewa. Loleni, mlimaji viyobetela minoga yake ilave ndiya zinogile. Heyo kofunga umoyo na kubetela mvula za vuli na mashika.
[8] Mweye vivija mufunge umoyo na kugangamala, kwavija Mndewa kammabehi kwiza!
[9] Ndugu zangu, sekemuinung'unikile, bule Mulungu kowatagusa. Kwavija msemi ka haulwivi.
[10] Ndugu zangu, kwa mbuli ya kufunga umoyo mna gamagayo, waloleni watula ndagu wa Mulungu walongile usenga ulawile kwa Mndewa.
[11] Towakema wao wamweda kwavija wafunga umoyo. Muhulika Ayubu viyafungile umoyo na mojuwa Mndewa viyamtendele mbaka kuuhelelo. Kwavija Mndewa kana bazi ng'hani na muhole.
[12] Ndugu zangu! Kubanza gose, sekemuiduile. Sekemuiduile kwa ulanga hebu kwa isi hebu kwa kinhu chochose kiyagwe. Mwahalonga, “Ona” Iwe ona, na “Bule” iwe bule, kamba siyo avo Mulungu kowatagusa.
[13] Kamba munhu yoyose kumwenu kogaya, yampule Mulungu. Munhu yeli na deng'ho, yamwimbile Mulungu nyila za kumtogola.
[14] Kamba munhu yoyose kumwenu mtamu, yawakeme wavele wa kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu, nao wampulile kwa twaga da Mndewa na wambake mavuta.
[15] Avo wahapula kwa kutamanila mtamu ayo kohonyigwa, na Mndewa komtenda yakone goya, na kamba katenda nzambi, zogeligwa kumgongo.
[16] Avo kila munhu yamulongele miyage nzambi zake, muipulile muladi muhonyigwe. Kupula kwa munhu yanogile mgameso ga Mulungu kuna nguvu ng'hani ya kutenda mengi.
[17] Eliya kakala munhu kamba tweye. Kawamba kumpula Mulungu mvula sekeitowe, mvula nayo haitowile mwiisi kwa miyaka midatu na miezi sita.
[18] Abaho kampula kabili, na mvula itowa na vihandigwe mwiisi vilela.
[19] Ndugu zangu, kamba imoja wenu yahaga kuujuwa ukweli, na iyagwe yahambweza,
[20] mujuwe kamba, munhu yoyose yombweza mnzila inogile munhu mwene nzambi, komkombola na ifa na nzambi zake nyingi zogeligwa kumgongo.

# Baluwa ya Ichanduso yandikigwe na Petulo

## Ulongozi

Baluwa ya ichanduso ya Petulo yandikigwa na mtumigwa Petulo. Petulo kosonga baluwa yake kwa kulonga heyo ayo nani na kamwandikila nani. Kawandikila wanhu wose wamtogole Yesu wapwililike mziisi zose yawakemile wanhu baki miyanza mingi mna ibaluwa ino (Sula ya 1:1, 1:17, 2:11). Kwavija baluwa ino iigala na baluwa ya Paulo kwa wanhu wa ako Efeso, wanhu wengi wogesa baluwa ya ichanduso ya Petulo yandikigwa kumwande ya baluwa ya kwa Waefeso behi na mwaka wa 65 toka kuvumbuka kwa Kilisito. Petulo kandika baluwa ino ako kudibuga da Lumi kuyakukemile Babuloni (Sula ya 5:13).

Petulo kalonga kandika baluwa ino mbuli ya kuwagela moyo na kuwalagusila kamba ino ayo ng'hekewa ya kweli ya Mulungu (Sula ya 5:12). Kuna mbuli nyingi ziigalile hagati ya sula ya 2:11-3:7 na Waefeso 5:18-6:9 na Wakolosai 3:18-4:6. Kila hanhu mna ivifungu avo vidatu holagiza mbuli ya kuinogela kwa wanhu wa ng'anda imoja na kuwategeleza wanhu weli na ukulu. Vivija kowagela moyo wanhu wamtogole Yesu wafunge umoyo kipindi cha kudununzigwa kwavija Kilisito kammabehi kubwela (Sula ya 4:1).

**Mbuli zili mkitabu**

Petulo koitambula mwenyego na kowalamusa wasomaji zake (Sula ya 1:1-2).

Abaho komgwaa nhogolwa Mulungu mbuli ya ukombozi iwoilumba hamoja na viugogeleza ugima wao (Sula ya 1:3-2:10).

Abaho kowalagiza wanhu wamtogole Yesu viwolondeka kukala goya mwiisi na kotambula mbuli nyingi kamba vija mkasano na mwehe wake na mtumwa na mkulu wake (Sula ya 2:11-4:11).

Abaho Petulo kowagela moyo wafunge umoyo kipindi cha kudununzigwa (Sula ya 4:12-5:11).

Abaho komambukiza baluwa yake (Sula ya 5:12-14).

1 Niye Petulo namtumigwa wa Yesu Kilisito, nowandikila mweye wanhu musaguligwe na Mulungu, mupwililike na mokala kamba wanhu baki mziisi za Ponto na Galatia na Kapadokia na Asiya na Bisiniya.

2 Toka mwaka Mulungu Tata kajuwa na kawasagula mweye, na kawatenda mung'ale kwa Loho wake, kubitila kumtegeleza kwenu Yesu Kilisito na kawasunha kwa damu yake.

Mulungu yawagwee ng'hani ng'hekewa na tindiwalo.

*Tumtogole Mulungu kwa tamanilo digala ugima*

3 Tumgwee nhogolwa Mulungu, yeli Tata wa Mndewa wetu Yesu Kilisito! Kwavija kwa bazi jake, katutenda tuwe na ugima wa sambi, kwa kumzilibula Yesu Kilisito kwa wafile. Sambi tugweleligwa tamanilo da ugima,

4 avo tobeta kupata vinhu vinogile vija Mulungu viyawekile wanhu zake. Kawekila mweye kuulanga vinhu havikola hebu kunangika hebu kuhuhwa.

5 Mweye vivija mokalizigwa kwa udahi wa Mulungu, kubitila kutamanila kwenu muladi mupate ukombozi wenu wikigwe kwa kugubuligwa kipindi cha uhelelo.

6 Deng'heleleni kwa mbuli ayo, hamoja sambi kwa kipindi kidodo
monyunyuwala kwa kugezigwa vino na vija,
7 muladi tamanilo jenu, difaya ng'hani kubanza zahabu joneke goya.
Zahabu yobanangika lakini yogezigwa muumoto. Vivo ili kwa tamanilo
jenu dogezigwa muladi joneke goya na dilave ukulu na kutogoligwa na
kutegelezigwa mna isiku yonda yagubuligwe Yesu Kilisito.
8 Hamoja hamnamona lakini momnogela na vivija momtogola hamoja
sambi hammona na modeng'helela kwa deng'ho kulu hadidahika ku-
longeka,
9 kwavija mobokela fungu da tamanilo jenu, fungu dijo awo ukombozi wa
mizoyo yenu.
10 Watula ndagu wa Mulungu, walongile mbuli ya ng'hekewa iwezile
mweye, walolesa na kuzahila ng'hani mbuli ya ukombozi wenu.
11 Walonda kujuwa kipindi gani mbuli ino vonda ilawilile. Kwavija Loho
wa Kilisito yakalile mgati mmwao kawalagusila avo walagula magayo ga
Kilisito na ukulu wonda wize.
12 Mulungu kawagubulila watula ndagu awo, kamba hawaisang'hanila
wenyego lakini wowasang'hanila mweye. Wao wakala wolonga mbuli ya
kija kimulongeligwe sambi na waja wawapetele Mbuli Inogile kwa nguvu ya
Loho Yang'alile yatumigwe kulawa kuulanga. Hata wasenga wa kuulanga
wosulukila ng'hani kuzijuwa goya.

### *Mbuli ya kukala kwa kung'ala*

13 Avo mugese goya na muitande kusang'hana, muilongoze goya wenyego.
Ikeni tamanilo jenu mna ing'hekewa yonda mugweleligwe vonda yabwele
Yesu Kilisito.
14 Muwe wana mumtegeleza Mulungu, sekemukale kwa kusulukila vihile
kumukalile nako baho umwaka vimukalile hamujuwile ukweli mbuli ya
Mulungu.
15 Kamba vija Mulungu yawakemile voyong'ala avo na mweye mung'ale
mzimbuli zose zimusang'hana,
16 kwavija Maandiko Gang'alile golonga, “Kaleni kwa kung'ala kwavija
niye vining'ala.”
17 Kwavija mwahampula momkema Tata, yuyo yonda yamtaguse kila
munhu bila kubagula kamba viyasang'hane, mukale hano mwiisi kamba
wanhu baki kuno momtegeleza kwa kugwaya.
18 Kwavija mweye mojuwa hamulekesigwe kulawa mna igago gehile
gamubokele kwa wahenga wenu, kwa vinhu vinangika kamba vija shaba
hebu zahabu,
19 lakini mulekesigwa kwa damu inogile ya Kilisito, yakalile kamba
mwana ng'hondolo yeliduhu kitala hebu kilema chochose.
20 Kakala yasaguligwe na Mulungu isi ing'hali hainaumbigwa, na kagubu-
ligwa mbuli yenu mna ikipindi kino cha uhelelo.
21 Kubitila heyo momtogola Mulungu yamzilibule kwa wafile na kamgwaa
ukulu, avo momtogola na momtamanila Mulungu.
22 Na sambi mweye kwa kuugoga ukweli musunhigwa, na muwanogela
kwa ukweli ndugu zenu, avo muinogele kwa mizoyo yenu yose.
23 Mweye muvumbuka mwanza wa kabili kubitila mbuli ya ugima ya
Mulungu ikalaga siku zose, siyo kwa mbeyu inangika lakini kwa mbeyu
hainangika.
24 Kamba Maandiko Gang'alile vigalonga,
“Wanhu wose waigala na mijani,
na ukulu wao uigala na maluwa.

Mijani yonyala na maluwa gohuluka,
25 lakini mbuli ya Mndewa yosigala siku zose."
Na mbuli ino ayo mbuli inogile ipetigwa kumwenu.

# 2

*Yesu yuyo dibwe dikalaga siku zose*

1 Avo lekeni gose gehile na uvizi na unafiki na migongo na kuwalonga wayagwe vihile.

2 Muwe kamba wana ving'hele, viwogasulukila matombo, avo na mweye sulukileni matombo ganogile nago zizo mbuli zinogile za Mulungu, muladi mudahe kukula muukombozi wenu.

3 Kamba vigalonga Maandiko Gang'alile, "Mweye mulanza kamba Mndewa kanoga."

4 Avo mwize kumwake, heyo yeli dibwe dili gima dilemigwe na wanhu, lakini Mulungu kadisagula na domfaya.

5 Vivija na mweye kamba mabwe magima, mozengigwa mng'anda ya kiloho, mosang'hana kamba walava nhosa wang'alile, molava nhosa za kiloho zimnogela Mulungu kubitila Yesu Kilisito.

6 Kwavija Maandiko Gang'alile golonga,
"Lola nodika dibwe ako Sayuni,
dibwe kulu dinisagule na da kutamaniligwa,
munhu yoyose yomtamanila honda yagwe kinyala."
7 Avo mweye muditogola difaya ng'hani, lakini kwa waja hawaditogola,
"Dibwe dilemigwe na wazengaji kamba hadifaya,
diwa dibwe kulu kubanza gose."
8 Na vivija,
"Dibwe diwatenda wanhu waikwale,
na dibwe kulu dowatenda wagwe."
Woikwala kwavija hawautogole usenga, na vivo viyalondile Mulungu kumwao.

9 Lakini mweye mwa wanhu musaguligwe, walava nhosa wa kindewa na wanhu wa isi ing'alile, wanhu wa Mulungu, muladi mupete mbuli za unzonza ziyatendile, kawakema mulawe mdiziza mwize mmulenge wa kukanganya.

10 Baho umwaka hamukalile wanhu wa Mulungu, lakini sambi mwa wanhu zake, umwaka hawonele bazi, lakini sambi kawonela bazi.

*Wasang'hanaji wa Mulungu*

11 Mbwiga zangu nowapula kamba wabita nzila na wanhu baki hano mwiisi, lekeni kusulukila vihile kwa lukuli ako kugomba siku zose na loho zenu.

12 Mkale goya na wanhu hawamtegeleza Mulungu, hamoja wowalonga vihile kamba motenda gehile, wagone gaja ganogile gomsang'hana na wamgwelele ukulu Mulungu mwiisiku ya kwiza kwake.

13 Wategelezeni wanhu weli na ukulu hano mwiisi mbuli ya Mndewa, mtegelezeni yeli mtawala mkulu,

14 na wakulu wa isi, yawasagule wawakoboze wose wotenda gehile na wawatogole waja wotenda ganogile.

15 Kwavija Mulungu vivo yolonda mweye muwafunge milomo wanhu wabozi kwa kusang'hana ganogile.

16 Kaleni kamba wanhu walekesigwe lakini kulekesigwa kwenu sekekuwe kinhu cha kufisila nzambi zenu. Kaleni kamba wasang'hanaji wa Mulungu.

17 Mtegelezeni kila munhu na wanogeleni waenu wamtogole Yesu na
mdumbeni Mulungu na mtegelezeni mkulu wa isi.

### *Kugaya kamba Kilisito*

18 Mweye wasang'hanaji ilaveni kwa wakulu zenu na muwategeleze,
siyo waja wotenda ganogile na kuwatonga waiyeka, lakini vivija kwa waja
wowakomhokela.
19 Kwavija Mulungu kowatendela ganogile wanhu wofunga umoyo kwa
magayo gowogaya bila kitala chochose kwavija wotenda goyolonda heyo.
20 Mopata choni, mwahafunga umoyo mwahatoigwa kwa gehile gamu-
tendile? Lakini kamba mofunga umoyo mna gamagayo mbuli ya kutenda
ganogile, Mulungu kowagwaa ganogile.
21 Mbuli ino ayo imukemeligwe, kwavija Kilisito kagaya mbuli yenu na
kawalagusila va kutenda, avo kwelelezeni viyatendile.
22 Heyo hatendile nzambi na halongile mbuli yoyose ya uvizi.
23 Viyaligigwe heyo hedike kwa kuliga, viyagaiye halongile mbuli za
kuwatenda wadumbe, lakini kamtamanila Mulungu, yeli msemi yanogile.
24 Heyo mwenyego kazipapa nzambi zetu muulukuli lwake mumsalaba,
muladi tufe kwa nzambi na tuwe wagima kwa ganogile. Kwa kulumizigwa
kwake mweye muhonyigwa.
25 Kwavija mweye mukala kamba ng'hondolo wapotele, lakini sambi
mumbwelela Msusilaji na Mkalizi wa ugima wenu.

## 3

### *Watwanzi na wakasano*

1 Vivija na mweye watwanzi wategelezeni wakasano zenu, muladi kamba
wakasano zenu hawatogola mbuli ya Mulungu, watogole kwa sang'hano
zenu bila kulongeligwa,
2 wahakona vimtenda zinogile na motegeleza.
3 Unovu sekewoneke kwa kuihamba kwa kunze, kamba vija kuluka mvili
hebu kuvala zahabu na viwalo vinogile.
4 Lakini unovu wenu wolondeka uwe muumoyo unogile, unovu uleka ku-
vulala na moyo wa uhole, unovu uno wofaya ng'hani mgameso ga Mulungu.
5 Kwavija uno awo unovu uwakalile nao watwanzi wamtamanile Mu-
lungu baho umwaka, viwawategeleze wakasano zao.
6 Kamba vija Sala viyamtegeleze Abulahamu na kamkema mndewa wake.
Mweye mwa wandele zake kamba mwahatenda ganogile bila kudumba
kinhu chochose.
7 Vivija na mweye iwakasano molondeka mukale goya na wehe zenu na
mujuwe kamba watwanzi waduhu nguvu kamba wambigalo avo muwa-
tendele kwa kuwategeleza, kwavija vivija nao wobokela hamoja na mweye
nhunza ya ugima. Tendeni vivo muladi kupula kwenu sekekukimilwe.

### *Kugaya mbuli ya kutenda ganogile*

8 Kukimambukizo, mweye mose muwe na moyo umoja na mugese dimoja,
molondeka muinogele kamba ndugu, muyonele bazi na muitonge wenyego.
9 Sekemuwalipe wanhu gehile kwa gehile, hebu ligo kwa ligo, lakini
walipeni ganogile kwavija mbuli ino ayo imukemeligwe muladi mubokele
ganogile.
10 Kamba Maandiko Gang'alile vigalonga,
“Munhu yoyose younogela ugima
na kolonda siku zinogile,

yailole sekeyalonge gehile
na sekeyalonge uvizi.
11 Yaleke gehile na yasang'hane ganogile
yazahile tindiwalo na yadiwinze kwa moyo wake.
12 Kwavija Mndewa kowalola wanhu wanogile mgameso gake
na kohulika kumpula kwao,
lakini Mndewa kowalema wanhu wotenda gehile."

13 Nani yonda yawalumize kamba mowamba kutenda ganogile?
14 Lakini hata kamba mwahagaya kwa kutenda ganogile mmweda! Seke-
mudumbe kija kiwodumba hewo na sekemunyawenyawe.
15 Lakini mumgwee ukulu Kilisito kamba Mndewa mmizoyo yenu. Siku
zose muitande kumwidika munhu yoyose yowauza kilamuso cha tamanilo
jenu dimulinajo.
16 Lakini tendeni vivo kwa uhole na kutegeleza. Tendeni kwa mizoyo ileka
kuwatagusa kamba mubananga, muladi wose wolonga gehile kwa tabiya
yenu inogile kwa Kilisito, wagwe kinyala kwa kija kiwolonga.
17 Kwavija vinoga ng'hani kamba vivo viyolonda Mulungu, kugaya kwa
kutenda ganogile kubanza kwa kutenda gehile.
18 Kwavija Kilisito kafa mwanza umoja kwa nzambi za wanhu wose,
munhu yotenda ganogile kwa wanhu wotenda gehile muladi yawagale
mweye kwa Mulungu. Kafa kilukuli lakini katendigwa mgima kwa udahi
wa Loho Yang'alile,
19 na vivija kachola kuzipetela loho zikalile zigodekigwe,
20 za wao walemile kumtegeleza Mulungu baho umwaka viyawabetele
kwa kufunga umoyo mna kipindi cha Nuhu viyakalile kozenga safina.
Wanhu wadodo wahonyeka na mazi, wakala wanhu wanane waiyeka.
21 Na mazi gago sambi golagusa ubatizo, awo uwakombola. Siyo kwa
kusunha dikwe da lukuli lakini lagano kwa Mulungu ditendigwa kwa moyo
unogile kumwake. Ubatizo wowakombola kwa kuzilibuka kwa Yesu Kilisito,
22 yacholile kuulanga na kakala muukulu mwambu wa mkono wa kudila
wa Mulungu, ako kowatawala wasenga wa kuulanga na wakulu na weli na
udahi na nguvu.

# 4

*Kukala mbuli ya Mulungu*

1 Kwavija Kilisito kagaya mulukuli lwake, na mweye vivija muitande kwa
mbuli ayo, kwavija munhu yagaiye mulukuli lwake kamduhu mzinzambi.
2 Kusongela sambi ugima wenu usigale hano mwiisi sekemukale kwa kuk-
weleleza kusulukila kwa lukuli, lakini mukale kamba viyolonda Mulungu.
3 Kwavija baho umwaka kwa kipindi kitali mukala motenda mbuli zi-
wotenda wanhu hawamjuwile Mulungu. Mukala kwa ugoni, kusulukila,
kukoligwa, nyimwili nyimwili za kung'wa ng'hani na kuvitambikila vinyago
vigevuza.
4 Sambi wanhu awo wokanganya kwavija hamuilumba nao mna ukukala
vihile kubanzile ng'hani, avo wowaliga.
5 Lakini wolondeka kumwidika Mulungu mbuli zao ziwatendile, heyo
yaitandile kuwatagusa wagima na wafile.
6 Lekaavo Mbuli Inogile vivija ipetigwa kwa waja wafile muladi hata
kamba watagusigwa wafe muugima wao wa lukuli kamba viwotagusigwa
wanhu wose, lakini wakale kiloho kamba Mulungu viyokala.

*Kuzisang'hanila goya nhuza za Mulungu*

7 Ukumala kwa kila kinhu kwa mmabehi. Avo molondeka mugese goya na muilongoze wenyego muladi mudahe kumpula Mulungu.
8 Kubanza mbuli zose, muinogele kwa mizoyo yenu yose, kwavija kuinogela kogubika nzambi nyingi.
9 Muigoneke mweye kwa mweye mzikae zenu bila kuinung'unikila.
10 Kila munhu yaisang'hanile nhunza iyagweleligwe na Mulungu kwa kuwatenda wayagwe wamwede. Mutamaniligwe kwa kuzisang'hanila vinogile nhunza mbasakanyo ziyawagwelele Mulungu.
11 Munhu yoyose yowapetela wanhu yawapetele mbuli za Mulungu. Munhu yoyose yosang'hanila yasang'hane kwa nguvu zose ziyagweleligwe na Mulungu, muladi mna izimbuli zose Mulungu yatogoligwe kubitila Yesu Kilisito. Kumwake uwe ukulu na udahi siku zose. Ona.

### *Magayo mbuli ya kumtogola Kilisito*

12 Ndugu zangu, sekemukanganye mbuli ya kugezigwa kwa usungu kumugaya, kamba vija kiwapata mweye kilozo.
13 Lakini deng'heleleni kwavija moilumba mna gamagayo ga Kilisito, muladi mudeng'helele ng'hani kipindi vonda yabwele muukulu wake.
14 Kamba moligigwa kwavija momtogola Kilisito, mumweda, kwavija Loho wa ukulu, yeli Loho wa Mulungu kokala na mweye.
15 Kamba munhu kogaya sekeiwe mbuli ya kukoma hebu ubavi hebu ubananzi wowose hebu kwa kuigela mzimbuli za wanhu.
16 Lakini kamba kogaya kwavija komtogola Kilisito sekeukone kinyala, lakini mgwelele nhogolwa Mulungu kuwa kwa munhu wa Kilisito.
17 Kipindi cha nhaguso kivika, na nhaguso yosonga kwa wanhu wa Mulungu, avo kamba nhaguso yosongela kumwetu, yokuwa vilihi kwa wanhu wolema kutogola Mbuli Inogile ya Mulungu?
18 Kamba vigalonga Maandiko Gang'alile,
“Vidala ng'hani kwa wanhu wanogile kukomboligwa,
yokuwaze kwa wanhu wolema kutegeleza na wanhu wene nzambi?”
19 Avo, wanhu waja wogaya kamba viyolonda Mulungu, wagendelele kutenda ganogile na wailave wenyego kwa Ija yawaumbile, ayo yotamaniligwa.

## 5

### *Bumbila da Mulungu*

1 Niye mvele wakibumbila cha wanhu womtogola Kilisito, niye nigonile mwenyego magayo ga Kilisito, na nokuwa na fungu muukulu wonda ugubuligwe. Nowapula, mweye wavele walangulizi wayangu,
2 mdisusile bumbila da Mulungu dili mmakono genu, mdilolese goya, siyo kwa kunanahizigwa lakini kwa kulonda wenyego, kamba Mulungu viyolonda. Sekemusulukile sente, lakini muwambe kusang'hana.
3 Sekemuwatawale kwa nguvu wanhu awo weli mmakono genu, lakini muwe kinhu cha kuifunzila kwa wanhu wamdibumbila.
4 Avo kipindi vonda yabwele Msusilaji Mkulu, mobokela taji ya ukulu, hauvulala.
5 Vivija na mweye wabwanga wategelezeni wavele. Mweye mose molondeka sekemuitonge wenyego na muisang'hanile, kamba vigalonga Maandiko, “Mulungu kowalema wanhu woitapa, lakini kowagwaa ng'hekewa wanhu wahole.”
6 Avo, ikeni hasi wenyego mumkono wa Mulungu uli na nguvu, muladi yawenule mna ikipindi chake kinogile.

7 Mgweleleni magayo genu gose kwavija heyo kowalolesa mweye.
8 Mugese goya na mukale meso. Ija yawehile, mwenembago kokwanga
kamba simba yong'ula komzahila munhu wa kumuja.
9 Mulemeni, na mugangamale mditamanilo, kwavija mojuwa waenu
wamtogole Yesu mwiisi yose wogaya kamba mweye vimugaya.
10 Mwahamambukiza kugaya kwa kipindi kidodo, Mulungu yeli na
ng'hekewa yawakemile mweye muwe na fungu kwa kuilumba na Yesu
Kilisito muukulu wake wa mazuwa gose, kowatenda mutelele na kowa-
gangamiza na kowagwaa nguvu na kowatenda muwe kamba chandusilo.
11 Nguvu zikale kumwake heyo siku zose. Ona.

*Ndamuso za kimambukizo*

12 Niwandikila baluwa ino nguhi kwa kutazigwa na Sila, inimgesa kamba
ndugu yotamaniligwa. Nolonda niwagele moyo na kuwalagusila kamba ino
iyo ng'hekewa ya kweli ya Mulungu. Wambeni kuigoga.
13 Kibumbila cha wanhu wamtogole Yesu ako Babeli, kisaguligwe na
Mulungu hamoja na mweye, chowalamusa na vivija mwanangu Maluko
kowalamusa.
14 Muilamuse kwa nzila ilagusa moinogela.
Tindiwalo dikale na mweye mose mumtogole Kilisito.

# Baluwa ya Kabili yandikigwe na Petulo

## Ulongozi

Baluwa ya kabili ya Petulo yokoneka yandikigwa na mtumigwa Petulo, lakini wanhu woifunza mbuli mna izisiku zino wolonga siyo kweli. Yodahika kamba munhu iyagwe kandika kwa mbuli ya Petulo. Mwandikaji kolonga kamba kawona kwa meso gake ugima wa Yesu viyakalile hano mwiisi na kalonga mbuli ya Yesu kugaluka kihanga (Sula ya 1:17-18). Kamba Petulo iyo yandike baluwa ino avo kayandikila ako Lumi behibehi ya mwaka wa 65 mbaka 67 toka kuvumbuka kwa Kilisito, yang'hali hanakufa. Vivija Petulo kolonga ino baluwa yake ya kabili toka viyandike baluwa ya ichanduso ya Petulo (Sula ya 3:1). Baluwa ino kawandikila wanhu wose wamtogole Yesu.

Petulo kandika baluwa ino muladi kuwagela moyo wanhu wamtogole Yesu wakale ugima unogile na kuwazuma mbuli ya wafundiza wa uvizi (Sula ya 2). Kowagela moyo sekewawatonge wanhu wolonga Yesu kokawa kubwela. Lakini kolonga Mulungu hakawa bule ila kolonda kila munhu yakomboligwe (Sula ya 3:8-9). Kino acho kilamuso cha tweye kukala ugima unogile (Sula ya 3:14).

## Mbuli zili mkitabu

Petulo koitambula mwenyego na kowatambula wasomaji zake (Sula ya 1:1-2).

Abaho kowakumbusa wakale ugima unogile kwavija Mulungu katutenda tudahe (Sula ya 1:3-21).

Abaho kowazuma mbuli ya wafundiza wa uvizi na choni chonda kilawilile ako kuuhelelo kwa wafundiza awo wavizi (Sula ya 2:1-22).

Abaho Petulo komambukiza kwa kuwagela moyo wanhu wamtogole Yesu wakale ugima unogile na waitande mbuli ya kubwela kabili kwa Yesu (Sula ya 3:1-17).

1 Niye Simoni Petulo, namsang'hanaji na mtumigwa wa Yesu Kilisito, nowandikila mweye mugweleligwe tamanilo dinogile ng'hani kamba ditugweleligwe tweye kubitila kunoga kwa Mulungu wetu na Mkombola wetu Yesu Kilisito.
2 Ng'hekewa na tindiwalo vimeme ng'hani kumwenu, kwa nzewele ya Mulungu na Yesu Mndewa wetu.

*Mukemigwa na Mulungu na musaguligwa*

3 Kwa udahi wa Mulungu katugwaa kila kinhu kitulonda muugima wetu wa kutenda goyolonda, kubitila kumjuwa kwetu heyo yatukemile tuwe na fungu muukulu wake na ganogile gake.
4 Avo katugwaa nhunza zinogile ng'hani ziyatulongele kotugwaa, muladi kwa nhunza zizo muwe na moyo kamba wake, na sekemukale kwa kusulukila gehile geli mwiisi.
5 Avo kwa kilamuso acho, wambeni kongeza kutenda ganogile mditamanilo jenu, na mna ukutenda ganogile yongezeni kujuwa ganogile,
6 na mna ukujuwa ganogile yongezeni kuilongoza wenyego na mna ukuilongoza wenyego yongezeni kufunga umoyo na mna ukufunga umoyo yongezeni kutenda ga Mulungu,
7 na mna ukutenda ga Mulungu yongezeni moyo unogile kwa waenu wamtogole Yesu na mna umoyo unogile kwa waenu wamtogole Yesu yongezenu unogelwa.

8 Kamba mokuwa mumema vinhu vose avo, honda muwe wanyeke ila
modaha kutenda ganogile mna ukumjuwa Mndewa wetu Yesu Kilisito.
9 Lakini kamba munhu yoyose kaduhu vinhu avo, kamba msuwameso
na hadaha kulola kutali, na kaisemwa kamba kasunhigwa nzambi zake za
umwaka.
10 Avo ndugu zangu, wambeni ng'hani kutenda lukemo mukemigwe na
Mulungu na kusaguligwa kwenu kamba kinhu cha ukweli. Kwavija kamba
mwahatenda mbuli azo hamugwa ng'oo.
11 Abaho motogoleligwa ng'hani kwingila muundewa wa mazuwa gose wa
Mndewa wetu na Mkombola wetu Yesu Kilisito.
12 Avo nogendelela kuwakumbusa mbuli zino siku zose, hata kamba
mumala kuzijuwa na mogangamala muikweli imuibokele.
13 Nokona vinoga ng'hani, niwakumbuseni mbuli zino, ning'hali na lukuli
luno,
14 kwavija nojuwa nammabehi kufa na kululeka lukuli luno, kamba
Mndewa wetu Yesu Kilisito viyanilongele kunze kunze.
15 Avo, nowamba ng'hani muladi nahafa mudahe kukumbuka mbuli zino
siku zose.

### *Tweye tuwone ukulu wa Kilisito*

16 Vituwafundizeni mbuli ya ukulu wa kwiza kwa Mndewa wetu Yesu
Kilisito, hatutamanile simo zitungigwe na wanhu, tweye tuwona ukulu
wake kwa meso getu wenyego.
17 Tweye tukala baho kipindi viyabokele kutegelezigwa na ukulu kulawa
kwa Mulungu Tata, sauti viimwizile kulawa kwa Mulungu yeli na Ukulu
Ng'hani, ilonga, “Ino iyo mwanangu inimnogela, ninogelwa nayo.”
18 Tweye wenyego tuihulika sauti ayo ilawile kuulanga vitukalile hamoja
nayo kuna ulugongo lung'ala.
19 Avo mbuli za watula ndagu wa Mulungu zilagusigwa goya kumwetu, na
motenda goya mwahazigoga, kwavija ziigala na taa ikwaka mdiziza mbaka
imitootondo na mulenge wa nhondo za imitondo womwemwesa mmizoyo
yenu.
20 Kubanza gose, mujuwe kamba kuduhu mtula ndagu wa Maandiko
Gang'alile yalongile mbuli za ulaguzi kwa kulonda mwenyego.
21 Kwavija kuduhu usenga wa ulaguzi ulawa kwa munhu, lakini munhu
kolonga gaja galawile kwa Mulungu kwa kulongozigwa na Loho Yang'alile.

# 2

### *Wafundiza wa uvizi*

1 Kukala na watula ndagu wa uvizi kwa wanhu, na vivija wolawilila
wafundiza wa uvizi kumwenu. Wanhu awo wowafundiza kwa kinyelegezi
malagizo ga uvizi gogala ubananzi, na ga kumulema Mndewa yawakom-
bole, avo wao woigalila wenyego kubanangigwa kwa kusinhukiza.
2 Wanhu wengi wokweleleza mbuli zao zigela kinyala, na kwa sama ya
hewo wayagwe woibeza Nzila ya Ukweli.
3 Kwa kusulukila kwao kwihile wopata vinhu kwa kuwafundiza mbuli za
uvizi. Nhaguso yao yabaho toka mwaka na hewo yowabananga kameso.
4 Kwavija Mulungu hawonele bazi wasenga wa kuulanga watendile
nzambi, lakini kawapigisila hanhu ha kugaya ako wagodekigwa minyololo
mdiziza wobeta siku ya Nhaguso.

[5] Mulungu hayonele bazi isi ya umwaka, kagala galika ya mazi mwiisi ya wanhu hawamtonga, lakini kamuhonya Nuhu yawapetele wanhu watende gamnogele Mulungu, na vivija kawahonya wanhu saba wayagwe.

[6] Mulungu kawatagusa wanhu wa mabuga mabili ga Sodoma na Gomola, na kawasakaza wanhu wose kwa moto, na kawatenda wawe kilaguso kwa kija chonda kilawilile kwa wanhu hawamtonga Mulungu.

[7] Kamuhonya Lutu munhu yanogile, yanyunyuwale kwa gehile gasang'hanigwe na wanhu awo wehile,

[8] munhu ayo yanogile kakala konyunyuwala ng'hani kila siku viyone na kuhulika gehile gasang'hanigwe na wanhu awo wehile.

[9] Kamba vino vivo ili, avo Mndewa kojuwa vonda yawahonye mna ukugezigwa kwao wanhu womtegeleza, na kojuwa vonda yaweke wanhu wotenda gehile mna ukubanangigwa mbaka siku ya nhaguso.

[10] Ng'hani ng'hani wanhu waja wokweleleza vizisulukila ng'huli zao na woubeza udahi wa Mulungu.

Wanhu awo wavizi na woitapa, hawadumba kuviliga vinhu ving'ala viumbigwe vili ako kuulanga.

[11] Lakini hata wasenga wa kuulanga, hamoja wana udahi na nguvu kubanza awo iwafundiza wa uvizi, hawalava vitala na kuwaliga mgameso ga Mndewa.

[12] Lakini wanhu awo woliga kila kinhu hawakijuwile. Wanhu awo waigala na wanyama wotenda bila kugesa woleligwa abaho wogogigwa na kuchinjigwa, avo nao wobanangigwa kamba wanyama.

[13] Wolipigwa magayo kwa magayo gawatendile. Wonogelwa kutenda chochose kihile mgameso ga wanhu. Wanhu awo wogela kinyala vonda wakale mna zinyimwili nyimwili zenu kuno wodeng'helela nzila zao zihile.

[14] Meso gao gamema ugoni, na hawaleka kutenda nzambi. Wowalongoza wanhu wanyolile mbaka kuna imitego ya gehile, magalu wa kusulukila vinhu, wagakalila makungu ga Mulungu.

[15] Waileka nzila igoloke, wapotela na kukweleleza nzila yaikweleleze Balaamu, mwana wa Beoli ija yanogelwe kupata fungu kwa kutenda gehile,

[16] na kazumigwa kwa nzambi zake. Mhunda halongaga, kalonga kamba munhu na kaukimila ubozi wa mtula ndagu ayo.

[17] Awo wafundiza wa uvizi waigala na nzasa zinyalile, na kamba kungugu dihembelusigwa na beho. Ziza baho hanhu hao hakukala hawekiligwe na Mulungu.

[18] Wolonga mbuli za kuitapa na za kibozi, kwa kusulukila kwihile kwa ng'huli, wowahonza wanhu waja wasongile kuinega na waja wokala kwa kutenda gehile.

[19] Wowalongela wanhu wolekesigwa, akuno wao wenyego watumwa wa gehile, kwavija munhu kokuwa mtumwa kwa kinhu chochose kimtawala.

[20] Kamba wanhu awo wakala wahonyeke na gehile geli mwiisi gagalaga ubananzi kwa kumjuwa Mndewa wetu na Mkombola Yesu Kilisito, abaho watogola kugogigwa kabili na kutawaligwa na gago gehile, kukimambukizo wanhu awo wokwiha ng'hani kubanza aho haichanduso.

[21] Vihanogile ng'hani kumwao wanhu awo sambi wajuwe nzila inogile kubanza kuijuwa abaho wogaleka malagizo gang'alile gawagweleligwe.

[22] Kumwao wao ulonzi uno ulawilila, “Umbwa kabwelela kija kiyadekile mwenyego,” na ulonzi uyagwe “Nguluwe yakoshigwe kabwelela kuibulu-giza mnhope.”

# 3

*Siku ya kubwela Mndewa*

1 Ndugu zangu, baluwa ino ya kabili kuwandikila. Mna zibaluwa zose
mbili nigeza kuwatenda mugese goya kwa kuwakumbusa mbuli zino.
2 Nolonda mukumbuke mbuli zilongigwe baho umwaka na watula ndagu
wang'alile, na lagizo da Mndewa na Mkombola dimugweleligwe na watu-
migwa zenu.
3 Tanhu molondeka mujuwe siku za uhelelo, wolawilila wanhu
wotawaligwa kwa kusulukila gehile gao. Wowazeha mweye,
4 kwa kuwauza, “Kakwahi ija yawalongele kokwiza? Toka kufa kwa
wahenga zetu, kila kinhu cha vivija kamba viikalile baho kunaichanduso
cha kuumbigwa kwa isi.”
5 Lakini wanhu awo woisemwa giladi baho umwaka kwa kulonga Mu-
lungu kaumba ulanga na isi. Isi iumbigwa kulawa mgamazi na kwa mazi.
6 Vivija kwa mazi gago, isi ya umwaka ikumbigwa na kunangigwa.
7 Lakini ulanga na isi ya sambi vikigwa goya kwa mbuli iija ya Mu-
lungu muladi vibanangigwe kwa moto. Vikigwa kwa siku ija wanhu
hawamtegeleze Mulungu vonda watagusigwe na kunangigwa.
8 Ndugu zangu, sekemuisemwe kinhu kino, mgameso ga Mndewa siku
dimoja sawa na miyaka magana longo, na miyaka magana longo sawa na
siku dimoja.
9 Mndewa hakawa bule kutenda gaja gayawalongele kamba wanhu
wayagwe viwogesa kokawa. Heyo kofunga umoyo mbuli yenu, kwavija
halonda munhu yoyose yabanangigwe, lakini kolonda kila munhu yaleke
nzambi zake.
10 Siku ya Mndewa yokwiza kamba mbavi. Siku dijo ulanga wosegezigwa
kwa mtigisiko mkulu, vinhu vose vili mumo haviwa baho kabili, nayo isi
yosegezigwa hamoja na kila kinhu kili mgati yake.
11 Kwavija kila kinhu chonangigwa, avo mweye molondeka muwe wanhu
gani? Molondeka mukale kwa kung'ala na kumtegeleza Mulungu,
12 kipindi vimuibeta siku ya Mulungu na kuitenda ize himahima. Siku dijo
ulanga wolukuzigwa kwa moto, na vinhu vose vili mumo volumbuka kwa
joto.
13 Lakini tweye tobetela kija kiyalongile Mulungu, kupata ulanga na isi ya
sambi, kae ya wanhu wotenda goyolonda Mulungu.
14 Avo ndugu zangu, kwavija mobetela vinhu avo, wambeni ng'hani
sekemoneke na chochose kihile, hebu kitala chochose mgameso ga Mulungu
na muwe na tindiwalo kumwake.
15 Molondeka mujuwe kamba Mndewa kofunga umoyo kwavija kolonda
wanhu wakomboligwe, kamba ndugu yetu Paulo vivija viyawandikile kwa
nzewele iyagweleligwe na Mulungu.
16 Paulo kandika mbuli zizija mzibaluwa zake zose, kandika mbuli zino.
Baluwa zake zina mbuli ziyagwe ndala kuzijuwa, na wanhu wayagwe
wabozi na wotanga tanga wofambula vihile kamba viwofambula vihile vi-
fungu viyagwe va Maandiko Gang'alile. Avo woigalila magayo gao wenyego.
17 Avo, ndugu zangu, kwavija muzijuwa mwaka mbuli zino zose, mwinege
sekemuzoligwe na gehile ga wanhu hawamtonga Mulungu na kuleka hanhu
henu hakukalizigwa.
18 Lakini gendeleleni kukula mna ing'hekewa na kumjuwa Mndewa wetu
na Mkombola wetu Yesu Kilisito. Ukulu uwe kumwake, sambi na siku zose!
Ona.

# Baluwa ya Ichanduso yandikigwe na Yohana

## Ulongozi

Baluwa ya ichanduso ya Yohana yandikigwa na mtumigwa Yohana mna ikipindi cha mwaka wa 85-90 toka kuvumbuka kwa Kilisito. Yohana haitambule bule kamba yuyo mwandikaji, lakini sula ya ichanduso yolagusa kamba heyo kawona kwa meso gake ugima wa Yesu hano mwiisi na kuzilibuka kwa Yesu (Sula ya 1:1-3). Vivija wandikaji wa Yohana wa ichanduso uigala na wandikaji wa Mbuli Inogile yandikigwe na Yohana. Wanhu woitogolela kamba Yohana yuyo yandike Mbuli Inogile yandikigwe na Yohana na vivija kandika baluwa ndatu Yohana ichanduso na Yohana wakabili na Yohana wa kadatu kipindi acho kiyakalile kuko Efeso.

Yohana kawandikila baluwa ino wanhu wose wamtogole Yesu mna ikipindi wanhu wamtogole Yesu viwakalile wogazigwa na kibumbila cha wanhu kikemigwe “Ginostiki.” Kibumbila acho kitogola kamba Yesu kakala Mulungu kweli lakini hakalile munhu kweli viyakalile hano mwiisi. Kwa kilamuso acho Yohana kandika kamba heyo kawona kwa meso gake mbuli ya ugima wa Yesu hano mwiisi na makono gake gamkwasa Yesu (Sula ya 1:1-3). Kilamuso cha Yohana kwandika baluwa ino muladi deng'ho jake dimeme (Sula ya 1:4) na kuwagomesa wanhu wamtogole Yesu sambi watende nzambi (Sula ya 2:1) na kuwatenda sekewagoge mafundizo ga uvizi (Sula ya 2:26) na vivija kuwalagusila kamba wakomboligwa (Sula ya 5:13).

**Mbuli zili mkitabu**

Yohana koitambula baluwa yake na kolonga kilamuso cha kuyandika (Sula ya 1:1-4).

Abaho kosimulila Mulungu viyali mulenge na avo tukale kamba Yesu viyakalile (Sula ya 1:5-3:10).

Abaho kotukumbusa lagizo da kuinogela (Sula ya 3:11-5:12).

Komambukiza baluwa yake (Sula ya 5:13-21).

*Mbuli igala ugima*

1 Tuwapetela mweye mbuli ya ayo yokemigwa mbuli ya ugima, yakalile toka mwanduso, tumuhulika na tumona kwa meso getu, tumulola na tumkwasa kwa makono getu.

2 Ugima uno viulawilile tweye tuwona, na sambi tolonga kija kituwone, na towapetela mweye ugima uno wa mazuwa gose, ukalile hamoja na Tata na ulagusigwa kumwetu.

3 Towapetela kija kituwone na kituhulike, muladi na mweye vivija muilumbe na tweye mna ukuilumba kwetu na Tata na Mwanage Yesu Kilisito.

4 Towandikila mweye mbuli zino kutenda deng'ho jetu ditelele.

*Mulungu iyo Mulenge*

5 Tuuhulika usenga uno kulawa kwa Yesu na sambi towapetela mweye kamba, Mulungu iyo mulenge na mgati mmwake mduhu ziza jojose.

6 Kamba twahalonga toilumba nayo kuno tung'hali tokala mdiziza, tolonga uvizi kwa mbuli zetu na kusang'hana kwetu.

7 Lakini kamba tokala mna umulenge kamba heyo viyali mulenge, toilumba tweye kwa tweye, na damu ya mwanage, Yesu yotusunha nzambi zetu zose.

8 Twahalonga hatutenda nzambi toivizila wenyego, na mduhu kweli
mgati mmwetu.
9 Lakini twahatogola kamba tweye twa wene nzambi, Mulungu kota-
maniligwa na kotenda goya, kozigela kumgongo nzambi zetu, na kotusunha
na gose gehile gatutendile.
10 Twahalonga hatutendile nzambi, tomtenda heyo yawe mvizi na imbuli
yake yamduhu mgati mmwetu.

# 2

### *Kilisito iyo mtazaji wetu*

1 Wanangu niwanogela, nowandikila mbuli zino muladi sekemutende
nzambi. Lakini kamba munhu yoyose katenda nzambi, tunayo imoja
yolonga kwa Tata mbuli yetu, nayo ayo Yesu Kilisito, ija yeliduhu kitala
chochose.
2 Kilisito ayo nhosa isegeza nzambi zetu na siyo tweye twiiyeka, lakini
vivija na nzambi za wanhu wose wa mwiisi.
3 Twahagagoga malagizo ga Mulungu, baho todaha kulonga kamba
tumjuwa.
4 Munhu yolonga, “Nimjuwa heyo,” lakini hagagoga malagizo gake,
munhu ayo koviza na kweli yamduhu mgati yake.
5 Lakini munhu yogoga mbuli ya Mulungu, munhu ayo kana unogelwa
wa kweli wa Mulungu mgati yake. Vino avo vitujuwa kamba twa mgati
mmwake,
6 munhu yoyose yolonga kamba kokala mgati ya Mulungu, yakale kamba
viyakalile Yesu.

### *Lagizo da sambi*

7 Ndugu zangu, siwandikila lagizo da sambi lakini lagizo didija dimukalile
najo toka ichanduso. Lagizo dijo da umwaka uwo uja uusenga umuhulike.
8 Hata ivo nowandikila lagizo da sambi, ukweli wake wokoneka mgati
ya Kilisito na mgati yenu. Kwavija ziza dosegela na mulenge wa ukweli
kumwemwesa mwaka.
9 Munhu yoyose yolonga kammulenge na kuno komwihila ndugu yake,
munhu ayo yang'hali kamdiziza.
10 Munhu yoyose yomnogela ndugu yake kammulenge na mgati yake
kuduhu kinhu chonda kimuhonze munhu yatende nzambi.
11 Lakini munhu yoyose yomwihila ndugu yake kamdiziza. Kotem-
bela mdiziza na hajuwa kochola kwahi, kwavija ziza dimtenda yawe
msuwameso.
12 Nowandikila mweye wana, kwavija nzambi zenu zigeligwa kumgongo
kwa kija kiyatendile Yesu Kilisito.
13 Nowandikila mweye kina tata, kwavija mumjuwa heyo yakalile toka
haichanduso. Nowandikila mweye wabwanga kwavija mumuhuma ija
Imdumuka. Nowandikila mweye wana, kwavija mumjuwa Tata.
14 Nowandikila mweye kina tata kwavija mumjuwa heyo yakalile toka
haichanduso. Nowandikila mweye wabwanga kwavija mna nguvu, na
mbuli ya Mulungu yokala mgati mmwenu na mumuhuma ija Imdumuka.
15 Sekemuinogele isi hebu kinhu chochose kili mwiisi. Munhu yoyose
yoinogela isi hadaha kumnogela Tata.
16 Kwavija vinhu vose vili mwiisi ino, kusulukila kwa lukuli, vinhu visu-
lukiligwa na meso ga wanhu, kuitapa kwa munhu kwa kija kiyali nacho na
kija kiyotenda, havilawa kwa Tata, ila volawa mwiisi ino.

17 Isi na vinhu vose visulukiligwa vobita, lakini munhu yotenda viyolonda
Mulungu, kokala siku zose.

### *Ija yomwihila Kilisito*

18 Wanangu, kino kipindi cha uhelelo, kamba vimuhulike kamba ija
yomulema Kilisito kokwiza, hata sambi wengi womulema Kilisito weza, na
avo tojuwa kamba uhelelo wammabehi.
19 Wanhu awo walawa mna ikibumbila chetu lakini hawalawile kweli
mna kibumbila chetu, kwavija maza walawile mkibumbila chetu, wahasi-
gale hamoja na tweye, lakini kusegela kwao kolagusa kamba hawakalile
hamoja na tweye.
20 Lakini mweye mugidiligwa Loho Yang'alile, na mweye mose muujuwa
ukweli.
21 Siwandikila kwavija hamuujuwile ukweli, lakini nowandikila kwavija
muujuwa na kuduhu uvizi ulawa muukweli.
22 Nani yeli mvizi? Iyo ija yolonga kamba Yesu siyo Kilisito mkombola
yasaguligwe na Mulungu. Munhu kamba ayo iyo yomulema Kilisito na
kombela Tata na Mwana.
23 Munhu yoyose yombela Mwana, vivija kombela Tata, na munhu yoyose
yomtogola Mwana, vivija komtogola Tata.
24 Avo, usenga uja umuhulike toka haichanduso ukale mmizoyo yenu. Na
wahakala mmizoyo yenu, vivija mokala kwa kuilumba na Mwana na Tata.
25 Na kino acho kiyatulongele kamba kotugwaa ugima wa mazuwa gose.
26 Niwandikila mbuli zino kuwazuma mbuli ya wanhu waja wolonda
kuwagiza.
27 Lakini kumwenu mweye, Kilisito kawagidila Loho Yang'alile. Na kamba
Loho Yang'alile kokala mgati mmwenu, hamulonda munhu yoyose yawa-
funze. Kwavija Loho Yang'alile kowafunza kila kinhu na kija kiyowafunza
cha ukweli na si uvizi bule. Avo gagogeni mafundizo ga Loho Yang'alile, na
kaleni kwa kuilumba na Kilisito.
28 Na sambi mweye wana, gendeleleni kukala mgati mmwake, muladi
mna isiku yaheza seketudumbe na seketukone kinyala mgameso gake.
29 Kamba mojuwa kuwa Kilisito komnogeza Mulungu, mujuwe kila
munhu yomnogeza Mulungu kaleligwa na heyo.

# 3

### *Wana wa Mulungu*

1 Loleni, Tata viyatunogele ng'hani, mbaka tokemigwa wana wa Mulungu!
Ona vivo vitwili. Lekaavo wanhu wa mwiisi hawatujuwile tweye, kwavija
hawamjuwile heyo.
2 Ndugu zangu, sambi twa wana wa Mulungu, na hatujuwa vondatuwe.
Lakini tojuwa Kilisito yahabwela toigala nayo, kwavija tomona kamba
viyali.
3 Munhu yoyose yomtamanila Kilisito koisunha, kamba vija Kilisito
viyaisunhile.
4 Munhu yoyose yotenda nzambi kobena malagizo ga Mulungu, kwavija
kutenda nzambi kuko kubena malagizo ga Mulungu.
5 Mojuwa kamba Kilisito keza kuzisegeza nzambi zetu, na mgati mmwake
mduhu nzambi yoyose.
6 Avo munhu yoyose yokala kwa kuilumba na Kilisito hatenda nzambi,
lakini munhu yoyose yogendelela kutenda nzambi hamonile na vivija
hamjuwile Kilisito.

7 Avo wanangu, sekemutogole kuviziligwa na munhu yoyose. Munhu
yotenda gaja galondigwa na Mulungu komnogeza heyo kamba vija Kilisito
viyamnogeze heyo.
8 Munhu yoyose yotenda nzambi munhu ayo wa Mwenembago, kwavija
Mwenembago katenda nzambi toka mwanduso. Lakini Mwana wa Mu-
lungu keza mwiisi kukinanga kija kiyatendile Mwenembago.
9 Yeli mwana wa Mulungu hagendelela kutenda nzambi, kwavija kavum-
buka na Mulungu na Mulungu kamgwaa ugima wa sambi, avo hadaha
kugendelela kutenda nzambi.
10 Vino avo vituwajuwa wana wa Mulungu na wana wa Mwenembago,
munhu yoyose hatenda gaja gomnogela Mulungu hebu hamnogela ndugu
yake, munhu ayo hali mwana wa Mulungu.

### *Inogeleni*

11 Na usenga umuuhulike toka hanaichanduso awo uno, tuinogele
wenyego.
12 Sekemuigale na Kaini, yalongozigwe na ija Imdumuka, na kamkoma
ndugu yake Habili. Vino habali kamkoma? Kwavija gaja gayakalile
yosang'hana geha, lakini gaja gayasang'hane ndugu yake gakala ganogile
mgameso ga Mulungu.
13 Avo ndugu zangu, sekemukanganye kamba wanhu wa mwiisi ino
wowehila mweye.
14 Tweye tojuwa kamba tumala kulawa mwiifa na twingila muugima,
kwavija towanogela ndugu zetu. Munhu yoyose yeliduhu unogelwa kosi-
gala mkufa.
15 Munhu yoyose yomwihila ndugu yake mkomaji, na mweye mojuwa
munhu yoyose mkomaji kaduhu ugima wa mazuwa gose mgati mmwake.
16 Vino avo vitujuwa unogelwa viwili, Kilisito kaulava ugima wake mbuli
ya tweye. Vivija na tweye tuulave ugima wetu mbuli ya ndugu zetu!
17 Kamba munhu yoyose kana vinhu va mwiisi ino, abaho kamona ndugu
yake kaduhu kinhu chochose na hamonela bazi bule, vino kodahaze ku-
longa komnogela Mulungu?
18 Wanangu, unogelwa wetu sekeuwe kwa mulomo wiiyeka, ila uwe
unogelwa wa kweli na ulagusigwe kwa kusang'hana.

### *Kugangamala kwetu kwa Mulungu*

19 Vino avo vitujuwa kamba tweye twa mna ikweli, na honda tun-
yawenyawe mgameso ga Mulungu.
20 Hata kamba mizoyo yetu yotutagusa kamba tubananga, Mulungu
mkulu kubanza mizoyo yetu na kojuwa kila kinhu.
21 Ndugu zangu, kamba mizoyo yetu haitutagusa, todaha kugangamala
mgameso ga Mulungu.
22 Kumwake tobokela chochose kitumpula, kwavija togagoga malagizo
gake na kutenda gaja gomnogeza heyo.
23 Lagizo jake dijo dino, tumtogole Mwanage Yesu Kilisito, na tuinogele
wenyego kamba viyatulagize.
24 Munhu yoyose yogagoga malagizo ga Mulungu kokala mgati mmwake.
Tojuwa kamba Mulungu kokala mgati mmwetu, kubitila Loho Yang'alile
iyatugwelele.

## 4

### *Loho wa ukweli na loho wa uvizi*

1 Ndugu zangu, sekemumtogole kila munhu yolonga kana loho wa Mulungu, lakini mgezeni munhu ayo mulole kamba munhu ayo kolongozigwa na Loho wa Mulungu, kwavija watula ndagu wengi wa uvizi walawilila mwiisi.

2 Avo, vino avo vonda mumjuwe munhu yolongozigwa na Loho wa Mulungu. Munhu yolonga kamba Yesu Kilisito keza mna ulukuli, munhu ayo kana Loho wa Mulungu.

3 Lakini munhu yoyose halonga vivo mbuli ya Yesu kaduhu Loho wa Mulungu. Munhu ayo kana loho yomulema Kilisito, na mweye muhulika mwaka kamba kokwiza, na hata sambi keza mwaka mwiisi.

4 Wanangu, lakini mweye mwa wana wa Mulungu na muwahuma watula ndagu wa uvizi, kwavija ija yokala mgati mmwenu kana nguvu kubanza ija yeli mwiisi.

5 Awo wolawa mwiisi ino na walonga vinhu va mwiisi lekaavo wanhu wa mwiisi wowategeleza.

6 Lakini tweye twa wanhu wa Mulungu, munhu yoyose yomjuwa Mulungu kotutegeleza tweye, lakini munhu heli wa Mulungu hatutegeleza. Vivo vitujuwa mbuli ya Loho wa kweli na loho wa uvizi.

*Mulungu ayo unogelwa*

7 Ndugu zangu, tuinogele wenyego, kwavija unogelwa wolawa kwa Mulungu. Munhu yoyose yonogela ka mwana wa Mulungu, na komjuwa Mulungu.

8 Munhu yeliduhu unogelwa hamjuwile Mulungu, kwavija Mulungu ayo unogelwa.

9 Mulungu katulagusila unogelwa wake kumwetu kwa kumtuma Mwanage yaiyeka mwiisi, muladi tuwe wagima kubitila heyo.

10 Unogelwa wa kweli uwo uno, siyo kamba tweye tumnogela Mulungu lakini heyo katunogela tweye na kamtuma Mwanage kamba nhosa ya kusegeza nzambi zetu.

11 Ndugu zangu, kamba Mulungu katunogela vivo, avo na tweye vivija tuinogele wenyego.

12 Kuduhu munhu yoyose yamonile Mulungu, lakini kamba toinogela wenyego, Mulungu kokala mgati mmwetu, na unogelwa wake utelela kumwetu.

